

## **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

### **MAJADILIANO YA BUNGE**

---

### **MKUTANO WA KUMI NA SITA**

---

**Kikao cha Kumi na Saba – Tarehe 30 Juni, 2009**

*(Mkutano Ulianiza Saa Tatuh Asubuhi)*

#### **D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

### **HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

#### **WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:-**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

#### **MHE. STEPHEN J. GALINOMA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):-**

Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa 2008/2009 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

#### **MHE. SHOKA KHAMIS JUMA (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA KATIBA NA SHERIA):-**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

#### **NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:-**

Randama za Makadirio ya Wizara ya Miundombinu kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

#### **NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:-**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 juni, 2007 [The Annual Report and

*Audited Accounts of the Tanzania Industrial Research Development Organisation (TIRDO) for the year ended 30th June, 2007].*

## **MASWALI NA MAJIBU**

Na. 129

### **Kuigawa Wilaya ya Mbozi**

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME aliuliza:-**

Kwa kuwa Wilaya ya Mbozi ina eneo la kilometra za mraba 9,679 na watu wapatao 650,000 na kwa kuwa baadhi ya maeneo katika Wilaya hii hayafikiki kwa urahisi kutokana na miundombinu mibovu na umbali uliopo kutoka Makao Makuu ya Wilaya:-

Je, Serikali ina mipango gani ya kuigawa Wilaya hiyo yenyе majimbo mawili ya uchaguzi hivi sasa ili kufanikisha mipango ya utawala bora?

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Luka Jelas Siyame, Mbunge wa Mbozi Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uundwaji na ugawaji wa maeneo mapya ya kiutawala hapa nchini unatawaliwa na Sheria za Serikali za Mitaa Na. 7 (Mamlaka za Wilaya) na Sheria Na. 8 (Mamlaka za Miji) za mwaka 1982 na Sheria za taratibu za uanzishwaji wa Mikoa na Wilaya Na. 12 ya mwaka 1994.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Wilaya ya Mbozi ni kubwa na ina vigezo muhimu vinavyoifanya istahili kugawanywa kwa lengo la kusogezza huduma za kijamii na kiuchumi kwa wananchi.

Kulingana na hali halisi ilivyo sasa Wilaya nyingi hapa nchini zinastahili kugawanywa katika maeneo mawili au zaidi. Wilaya hii ni moja kati ya Wilaya ambazo ziliwahi kuwasilisha mapendekezo ya kuzigawa Wilaya zao.

Maombi hayo yalichambuliwa na kuandaliwa mapendekezo ambayo yamewasilishwa katika Mamlaka husika kwa maamuzi. NamWomba Mheshimiwa Mbunge avute subira wakati mapendekezo hayo yanafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo naomba Waheshimiwa Wabunge wakumbuke kuwa ugawaji wa Wilaya au maeneo mapya yanategemea Serikali kuwa na uwezo wa kuyajenga Makao Makuu ya Wilaya pamoja na juhudzi za wananchi, gharama za uendeshaji na uwekaji miundombinu muhimu pamoja na kuajiri watumishi wa Wilaya husika.

Kwa ujumla zoezi hili linafanywa kulingana na uwezo wa Serikali kifedha.

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Wilaya ya Mbozi, kwa kuwepo kwake mpakani kunaipa kipaumbele zaidi ya Wilaya zingine baada ya kuwa imetimiza karibu vigezo vyote vya kuweza kugawanywa kuwa Wilaya mbili. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kuwahakikishia wananchi wa Mbozi kwamba pindi itokeapo mgao huo ukakubalika, basi ataipa kipaombele Wilaya hiyo?

Swali la pili, kutokana na matukio ambayo yamekuwa yakijirudiarudia ambayo ni pamoja na tukio la jana la vurugu zilizo tokea na kwa kuelewa Mji wa Tunduma; unakuwa kwa kasi.

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza pia akafikiria wazo la Mji mdogo wa Tunduma kupandishwa hadhi kutoka Mammlaka ya Mji na kuwa Halmashauri ya Mji?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, kwanza nataka nimfahamishe kwamba Wilaya ya Mbozi ina vigezo vyote ambavyo vinatakiwa kuifanya iwe Wilaya mbili. Hili analoliongeza hapa ni la msingi sana. Tunachozungumza hapa ni kwamba, anachosema, anasema kwamba wapo katika maeneo ya mpakani; na maeneo ya mpakani, ni maeneo ambayo kwa kweli tunapashwa tuyatizame kwa karibu sana, ni kama vile tunapokuwa na Longido, unapo kuwa na Siha ile.

Mheshimiwa Spika, unapoangalia maeneo ya Rufiji kule pembedi kule. Haya maeneo ni maeneo ambayo kwa kweli unatakiwa uyatizame kwa karibu na nafikiri Mheshimiwa Mbunge anachozungumza hapa, anazungumza swala la msingi sana. hii ni maeneo ambayo yanahusiana na mambo ya ulinzi na usalama wa maeneo yale na ni moja ya vigezo ambavyo tunaviangalia. Na viro vigezo vingine vingine vingi hata *politics* za maeneo yale tunaliangalia. Kwa hiyo namuomba Mheshimiwa Siyame asiwe na wasiwasi, sisi hapa tunachofanya ni kufanya mapendekezo na kama alivyosema mapendekezo yamefanyika. Na kuna wengi sana hapa, ambao Wilaya zao zimependekezwa, na Mammlaka ile itaangalia, ikiangalia pia na hali ya uwezo wa Serikali katika kuanzisha Mammlaka hizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matatizo yaliyotokea kule Tunduma na swala la kuanzisha Mji mdogo; nilisema hapa jana, kwamba pale Urambo ilipo pale kwa mfano, kama pale ni Makao Mkuu ya Wilaya kauli ishatoka hapa na Serikali kwamba ni kazi ya Halmashauri zile kuanzisha moja kwa moja Mamlaka ya Mji mdogo. Nataka niseme hapa kwamba, huwa sio *automatic*, yani kwamba pale ulipo; Tunduma najua ni eneo la biashara pale ni eneo ambalo limepenuka, nimekwenda pale. Sio *automatic*. Wale ndio wanaotakiwa kuanzisha jambo lile na kusema kwamba sisi tunaona kwamba kuna haja ya kuwa na Mji mdogo. Wakileta, ninataka nikuthibitishie kwamba tutafanya hivyo, wala hakuna wasiwasi kabisa. Wala hili sina haja ya kufanya *consultation* kwa sababu kuna maelekezo ya Serikali tayari ambayo tayari yanaelekeza tufanye hivyo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kabla sijaendelea kumwita Mbunge ambaye anauliza swali linalofuata, nimepewa sasa hivi orodha ya wageni na kwa kutambua uzito wa mgeno mmoja mashuhuri, sitasubiri ule muda wa kawaida.

Waheshimiwa Wabunge, kwa heshima na taadhima, naomba nimtambulisse Jaji Mkuu wa Tanzania, Mheshimiwa Augustino Ramadhani tunathamini sana jinsi ambavyo Mheshimiwa Jaji Mkuu, unavyokuja kushiriki nasi hapa Dodoma kwenye vikao vya Bajeti. Hii ni ishara kubwa ya uwadilifu wako na tutajitahidi kadri itakavyowezekana naona tumechelewa kidogo mwaka huu.

Lakini mwaka ujao, tutajitahidi sana kwamba bajeti ya Mahakama, iwe tofauti kabisa na ilivyo sasa, ili kazi iweze kufanyika vizuri. Ahsante sana. (*Makofi*)

Na. 130

### **Ongezeko la Shule na wanafunzi wa Shule za Msingi**

**MHE. CHARLES N. KEENJA** aliuliza:-

- (a) Je, kumekuwa na ongezeko gani la shule na watoto wa shule za msingi kati ya mwaka 2000 – 2008 katika Jimbo la Ubungo Wilayani Kinondoni?
- (b) Je, mionganoni mwa shule zote zilizopo jimbo la Ubungo ni ngapi zenyen wastani mkubwa wa watoto kwa darasa kuliko wastani uliowekwa na Serikali na wastani mkubwa zaidi uliopo ni watoto wangapi kwa chumba cha darasa?
- (c) Je, Serikali inachukua hatua gani kuondoa tatizo hilo kubwa ambalo linajulikana wazi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Charles Keenja, Mbunge wa Ubungo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, idadi ya shule za msingi zilizokuwepo katika jimbo la Ubungo mwaka 2000 imeongezeka toka shule 29 hadi shule 61 mwaka 2008 sawa na ongezeko la shule 32 au asilimia 110.4. Aidha, mwaka 2000 kulikuwa na wanafunzi 43,197 wa shule za msingi katika jimbo la Ubungo ikilinganishwa na wanafunzi 76,803 waliokuwepo mwaka 2008 sawa na ongezeko la wanafunzi 33,606 au asilimia 77.8.

(b) Mheshimiwa Spika, shule za msingi katika jimbo la Ubungo zenyne wastani mkubwa wa watoto kwa darasa kuliko wastani uliowekwa na Serikali ni shule 51 ambapo wastani mkubwa uliopo ni watoto 163 kwa chumba kimoja cha darasa (1:163).

(c) Mheshimiwa Spika, sababu kubwa zilizosababisha kuwepo kwa tatizo hili ni pamoja na ongezeko kubwa la wakazi wa Jiji la Dar es Salaam lililosababisha ujenzi holela bila kuacha maeneo ya ujenzi wa huduma za jamii kama shule, uhamiaji holela wa watu kutoka vijijini kuja Mijini kutafuta kazi na kufanya biashara. Aidha, aina ya makazi inasababisha kuwa na mlundikano wa wanafunzi mfano, sehemu ambazo zina makazi ya askari polisi.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni na wananchi wa Manispaa ya Kinondoni wakiwemo wananchi wa jimbo la Ubungo imechukua hatua mbalimbali kupunguza tatizo hili ikiwa ni pamoja na hizi zifuatazo:-

(i) Kujenga madarasa mapya katika shule zenyne mlundikano wa wanafunzi katika chumba kimoja cha darasa. Hadi sasa jumla ya madarasa 52 yamejengwa katika Jimbo la Ubungo.

(ii)Kukarabati vyumba vya madarasa vilivyochoakaa katika baadhi ya shule katika jimbo la Ubungo ili viweze kutumika na mpaka sasa vyumba vinane (8) vimefanyiwa ukarabati katika shule ya msingi ya Kiluvya na King'ongo.

(iii)Kwa mwaka 2008/2009 zilitumika shilingi 117,000,000 kwa ajili ya kufanya ukarabati wa majengo ya shule za msingi katika Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni zikiwepo shule za Jimbo la Ubungo.

(vi)Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kuitia Bajeti yake imejenga shule mpya ya Mbezi Kibesa na kukarabati majengo ya baadhi ya shule za msingi za King'ongo, Makoka, Kiluvya, Milenia ya Tatu na Idris Abdul Wakili.

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niuliza maswali mawili ya nyongeza na nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba unapokuwa na watoto wengi kama 163 kwenye chumba cha darasa, ufundishaji unakuwa hauwezekani. Kwa hiyo kuna hitajika mpango maalum wa kushuhulikia tatizo kama hilo. Je, katika Bajeti ya mwaka huu tatizo hili linashughulikiwaje?

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni dhahiri vilevile kwamba kunahitajika mpango wa kudumu utakao hakikisha kupatikana kwa mahitaji ya elimu ya msingi ikiwa ni pamoja na miundombinu walimu na vifaa. Sasa Serikali pamoja Halmashauri zinaelekeza nguvu zake zote kwenye MES, wamesahau shule za msingi. Je mpango wa MEM unaendeleaje?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Charles Keenja, kama ifuatavyo. Kwanza namshukuru kwamba ameshukuru kwamba tumempatia takwimu zote alizokwu anaziitaji.

Hili tatizo analolizingumza hapa, wala siwezi kubishana hapa na wala ambao hawajui mimi *by profession* ni mwalimu. Digri yangu ya kwanza mimi ni ya ualimu, nyingine ndio ya *Public Administration*. Unapokuwa na watoto wengi katika darasa, unapo waweka wale watoto 160 ukafikiri hiyo ni *development*, hiyo sio *development*.

Mheshimiwa Spika, ulaya mwalimu mmoja anafundisha wanafunzi 20. Hiyo ndio *development*, yaani idadi yako inavyozidi kupungua kwa mwalimu mmoja. Kwa maana mwalimu yule anasahihisha, mwalimu yule anaada masomo yale, mwalimu yule ana kazi nyingi za kuangalia wale watoto ambao hawana uwezo wa kwenda haraka na wenzao.

Kwa hiyo, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kwamba anachokizungumza hapa ni jambo ambalo sisi wote tunatakiwa tulifanyie kazi kuona kwamba tunafanya nini.

Mheshimiwa Spika, Bajeti imeshapita, wametenga hela hapa kwajili ya maswala ya shule za msingi. Sikumbuki ile *figure* yenyele, lakini ninajua kwamba tumeelekeza katika maeneo haya na katika *figure* nilizotoa hapa, tumeonesha kwamba tumefanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, lakini ambalo naweza nikalisema hapa, bila kuingiza nguvu ya wananchi katika swali hili la kuhakikisha kwamba tunajenga madarasa, nataka nikuhakikishie kwamba hatutakwenda. Dar es Salaam, lazima waamke wasaidie nguvu za Serikali na nguvu za Halmashauri, waonyeshe moyo wa kujituma kusaidia katika mchango huu. Ndipo tutakapoondoka katika mpango huu.

Mheshimiwa Spika, swalii la pili. Mheshimiwa Keenja anazungumzia suala la walimu, vifaa na vitu vingine. Nakiri hapa mbele yako kwamba katika eneo hili nalo tuna matatizo. Hasa katika pembezoni na maeneo mengine. Hili tunalifanyia mpango. Sasa hivi tunazungumza mpango wa kupanua katika vyuo vyetu vya waalimu kwa upande wa shule za msingi na shule za sekondari. Shule za sekondari ni mbaya zaidi. Lakini nataka nihakikishe na niseme hapa kwamba kuna jitihada za kuangalia, hata wakati mwingine kuangalia walimu ambao wamestaafu na kuwarudisha na kuweka *contract* na wao ili waweze kutusaidia katika mpango huu.

Mheshimiwa Spika, huu mpango wa MEM ambao umezungumzwa hapa ni mpango ambao unasaidiwa pia na wahisani kutoka nje. Wengine hapa wanaita wafadhili, hakuna mfadhili, mfadhili ni Mungu tu. Wahisani ndio wanao tusaidia; hela hizi wakati mwingine zinachelewa kufika, ndio unaona kwamba zinasuasua lakini nataka niseme kwamba kwa sasa hivi zimekuja, na tunauangalia mpango huu tunategemea kwamba tutaendelea nao kama wenzetu wataendelea kutusaidia. (*Makofit*)

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swalii moja la nyongeza. Kwa kuwa tatizo la mlundikano wa wanafunzi uko nchi nzima, ukienda Iramba mashariki, Urambo mashariki, Peramiho, Misungwi, Nzega na kote kwingine. Na wananchi wa Tanzania walishaonyesha nguvu yao na kutambua umuhimu wa wanafunzi kusoma. Wamejenga maboma karibu nchi nzima, Serikali mpaka sasa haijatoa fedha za kuezeka yale maboma. Waziri anasemaje juu ya hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swalii la msingi, nakubaliana nay eye kabisa kwamba nchi nzima kwa kweli kuna mlundikano. Unapokuwa umepiga hatua kubwa ya kimaendeleo, una *create* kitu kinachoitwa mahitaji (*demand*). (*Makofit*)

Wakati mwingine malalamiko yanayokuja hapa, yanatokana na manufaa ambayo tumeyapata katika nchi hii. Yaani yale manufaa sasa, watu wamejua kutumia sukari, wanadai sukari. Elimu, wanadai elimu zaidi. Kwa hiyo, utaona *demand* ni kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nakubaliana nae kabisa kwamba kutokana na sera nzuri za Chama Cha Mapinduzi na Serikali yake, kuna mlundikano. Sasa hapa kinachozungumzwa hapa ni kwamba lazima *u-plan*. Kama wewe umeanzisha madarasa, umeanzisha watoto waende kule, lazima uhakikishe kwamba kuna kuwa kuna walimu, kuna kuwa na madarasa ya kutosha. Ndio raha inayoletwa hapa. Haya majengo anayoyaita maboma, ninayafahamu na nimekwenda Singida nimekuta maboma, kule kwake nimekwenda Iramba nimekuta maboma na tulichosema hapa, tulisema kwamba, wananchi waonyeshe nguvu zao, halafu na Serikali nayo itatoa *bakshish* kwa maana ya kuwasaidia pale walipokuwa wamekwama.

Mheshimiwa Spika, majengo haya tulichosema ni kwamba ni wajibu wa Halmashauri zinazo husika. Kuhakikisha kwamba pale ambapo wananchi ameongeza

nguvu kubwa, wakaenda mpaka kwenye rinta, wakaenda pale mpaka wakapauwa pale. Halmashauri zinatakiwa zisaidie katika mpango huu na sisi hapa tulichofanya na katika Bajeti hii tuliyopitisha hapa, yako maeneo ambao kwa kweli tumeyaona kwamba yapo chini sana na ambayo tumeyawekea kiwango maalum kwa ajili ya kuwasaidia ili kuomdokana na matatizo haya. Kwa hiyo nataka nikubaliane na Msheshimiwa Msindai kwamba yale maboma; ni *obligation* yetu sisi kama Wizara na pamoja na Halmashauri kuhakikisha kwamba tunawasaidia wananchi kwa sababu wananchi wameshatumia nguvu zao pale, tusiache tu ya kabomoka tu hivi hivi.

**SPIKA:** Kwa upendeleo maalum kuzingatia jinsia. Mheshimiwa Rita Mlaki.  
(*Makofi*)

**MHE. RITA L. MLAKI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Naomba kuuliza swali langu la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa wananchi wa Mkoa wa Dar es Salam hususan wa Jimbo langu la Kawe, wako tayari kuchangia maendeleo hasa ya elimu na kwa kuwa kuna maeneo ambayo yalipimwa na Wizara ya Ardhi kwa ajili ya kujenga mashule, lakini yakavamiwa na wananchi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuyachukua hayo maeneo au itawachukulia hatua gani watu ambao wameyavamia maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, Dar es Salaam huko anakozungumzia Mheshimwa Rita Mlaki, ni kweli kwamba kuna maeneo ambayo yamevamiwa vamiwa.

Chombo kinachofanya mipango katika Halmashauri, ni Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, ndicho kinacho *plan* kila kitu, ndicho kinachojua ni nani amevamia eneo, ndicho kinachosimamia na kina Mamlaka ya mae neo hayo ya Kinondoni na Madaraka kamili. (*Makofi*)

Mimi nataka tu nimshauri Mheshimiwa Rita Mlaki na ninajua kwamba ananielewa kwa sababu amewahi kuwa Naibu Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Haya mambo anauliza yeye ni mtaalamu zaidi wa mambo haya kuliko hata mimi ambaye naulizwa hili swali. Sasa naomba tu anisaidie, mimi tutakaa na yeye tuzungumze ili tuweze kupata ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, pale ambapo eneo limevamiwa, kwa mfano *open space*, inafahamika kabisa ramani yake imeonyesha kwamba eneo hili, lilikuwa ni kwa ajili ya watoto kubembea; eneo hili lilikuwa ni kwa ajili ya kujenga shule ya msingi, halafu likavamiwa na sisi kama Mamlaka tuko pale. *No way*. Tutakwenda pale sisi tutasema hapana.

Kwa hiyo, sisi tunachoomba tupate ushirikiano kutoka kwa mamlaka husika. Lakini nataka kusema hapa kwamba chombo kinachosimamia pale ni Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni. Ndiyo ambayo inaweza ikatoka hapa ikasema, Bwana eeeh! Eneo hili hatukukupa, wewe umelivamia, kwa hiyo tukaliingilia pale.

Nadhani ni kitu ambacho kinahitaji kukaa kidogo, nisijibu kwa haraka haraka hapa, watu wakatoka huko wakaenda kuvamia watu kule, tutalifanyia kazi halafu tutaelewana na Mheshimiwa Rita Mlaki kama anavyozungumzia hapa.

Na. 131

### **Hati za Utendaji katika Mashirika**

**MHE. BAHATI ALI ABEID** aliuliza:-

Kwa kuwa Mashirika ya Umma yanaendeshwa na wafanyakazi ambao ni wataalam wa kazi zao ndani ya shirika husika:-

Je, kwa Mashirika yenyeye Hati Chafu wanachukuliwa hatua gani za kinidhamu ili mashirika hayo yaweze kupata Hati Safi na kuendesha shirika kwa faida?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimia Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bahati Ali Abeid (Viti Maalum) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa uwaraka wa msajli wa Hazina Namba Moja wa mwaka 2004, inapotokea hati chafu ya utendaji wa Shirika imesababishwa na watendaji wa Shirika hilo. Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika husika kama mwajiri au mteuzi wa Menejimenti ya Shirika inayo mamlaka ya kuwachukulia hatua za kinidhamu watumishi waliosababisha upatikanaji wa Hati Chafu kufuatana na taratibu na kanuni za kiutendaji wa shirika husika.

Mheshimiwa Spika, hatua zinazochukuliwa ni pamoja na kuachishwa kazi, kufunguliwa mashtaka, kulazimika kufidia hasara ambayo mtumishi huyo amesababisha, kupewa onyo, na kadhalika, kulingana na kosa alilolifanya na kulisababishia shirika kupata Hati Chafu.

**MHE. BAHATI ALI ABEID:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake. Naibu Waziri amejibu kuwa, wapo wafanyakazi ambao wamechukuliwa hatua kwa kuisababishia Shirika hasara au kupata hati chafu. Wamechukuliwa hatua za kufukuzwa kazi au kulipa fidia au kupelekwa Mahakamani. Je, Naibu Waziri ana mifano ya Mashirika ambayo yamefanya hivyo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi. Kama atakumbuka vizuri, katika jibu langu nimetoa mwongozo wa nini kinafanyika pale ambapo

mfanyakazi anasababishia Shirika hasara. Jibu lilikuwa linalenga swali lake mwenyewe kwamba nini kinafanyika, endapo mfanyakazi anasababishia Shirika hasara.

Sasa kwa sababu yapo Mashirika mengi, Wizara yangu ipo tayari kumtaarishia idadi au mifano hiyo ambayo anaisema na tutamkabidhi ama hapa Bungeni, kama atapenda kuifuata Dar es Salaam tutawasiliana kule nitampatia.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa majibu ya Naibu Waziri amekiri kwamba Mashirika ya Umma yanasisimamiwa na Bodi ya Wakurugenzi, na kwasababu nimekuja kwenye Wizara ya Viwanda na Biashara, naomba tu nimwulize, najua Serikali itajibu tu.

Je, utaratibu uliopo ni Mashirika ya Umma, chini ya Wakurugenzi kutengeneza Bajeti na kuhakikisha inapitisha bajeti ya Shirika la Umma. Tofauti na hali iliyopo sasa, Bajeti zimekuwa zikipelekwa kwa ajili ya kuidhinishwa tu nap engine hazipelekwi.

Je , Serikali sasa ina mkakati gani wa dhati wa kuhakikisha kwamba Mashirika yote ambayo yanatengeza hasara sasa yanaanza kutengeneza faida na pili je ina hakikishaje...

**SPIKA:** Swali la nyongeza huwezi kuuliza mawili.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana nae kwamba kwa Mashirika mengi kama sio yote, Bajeti zao zinapotengenezwa na Wakurugenzi ama Wataalamu katika hayo Mashirika, uwa zinapitia katika Wizara husika na Wizara hile inajumuisha pamoja na Bajeti ya Wizara yenyewe, tunaleta hapa Bungeni, Bunge linapitishwa.

Sasa inawezekana kama unavyosema na kama tulivyo shuhudia Mashirika mengine yamepata hasara na iwamuzi wa kubinafsisha Mashirika yetu ya Umma, ultokana na Mashirika hayo kupata hasara.

Sasa kwa sababu ya hasara hiyo ambayo ilipatikana tunachofanya sisi kama Serikali inapotekeea kwamba shirika limekuwa na hasara kwanza tunaangalia namna gani ya kulirekebisha, kuangalia muundo wake na kuangalia kama Serikali inaweza ikafanya lolote.

Inaposhindikana sasa ndiyo tunaliachia kubinafsishwa apatikane mwekezaji ambayo anaweza akaliendesha kwa faida kuzingatia kwamba lakini mwekezaji huyo analiendesha kwa kuzingatia maslahi ya Taifa kwa mujibu wa taratibu na kanuni zetu.

## **Maeneo maalum ya Uwekezaji nchini**

**MHE. ARCHT. FUYA G. KIMBITA** aliuliza:-

Kwa kuwa ni muda mrefu sasa tangu tuzungumzie maeneo mbalimbali ya uwekezaji EPZ na SEZ:-

Je, ni nini kinachoendelea hususani eneo la *KIA* na *Kilimanjaro Machine Tools*?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Fuya Godwin Kimbita, Mbunge wa Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya EPZ yaani *Export Promotion Zone* kwa kushirikiana na uongozi wa Wilaya ya Hai imebainisha eneo la Sanya Stesheni – KIA lenye ukubwa wa ekari 550 kwa ajili ya uwekezaji wa EPZ na SEZ. SEZ hapa ni *Special Economic Zone*.

Mheshimiwa Spika, zoezi la uthamini wa ardhi na mali litaanza mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2009/2010.

Zoezi hili litafuatiwa na ulipaji fidia, Kuandaa *Master Plan* kuweka miundombinu ya msingi kama umeme, maji, mawasiliano kwa kushirikiana na sekta binafsi kabla ya kulitangaza eneo kwa wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kiwanda cha *Kilimanjaro Machine Tools Company (KMT)*, Shirika la Maendeleo la Taifa (*National Development Corporation (NDC)* lilikabidhiwa jukumu la usimamizi wa kiwanda hicho mwaka 2005 baada ya zoezi La kubinafsishwa kushindikana.

Mwezi Januari 2009 NDC imeingia ubia na kampuni binafsi ya *Serengeti Telecom Group Ltd.*, kwa lengo la kufufua kiwanda na kujenga majengo mapya katika maeneo yaliyo wazi kwa ajili ya wawekezaji wenye nia ya kuanzisha viwanda mbalimbali vyta kuzalisha bidhaa za kuuza katika soko la nje na ndani.

Kwa hiyo, natumia fursa hii adimu hapo hapo kuwakaribisha wawekezaji binafsi kwa ajili ya ujenzi na uendelezaji wa viwanda vyta aina zote katika eneo la KMT mara baada ya matayarisho ya awali kukamilika.

**MHE. ARCHT. FUYA G. KIMBITA:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika. Nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mafupi lakini yenye kueleweka. Naomba nimwulize maswali mawili madogo yafutayo:-

La kwanza, kwa kuzingatia umuhimu wa viwanda katika maeneo yote mawili tuliyoyataja ya *KIA* na *Kilimanjaro Machine Tools* na kwa kuzingatia uhaba wa ardhi unaotukabili katika Wilaya ya Hai, Siha, Wilaya ya Moshi Vijijini na Simanjiro. Je, basi ni lini hili zoezi litakamilika ili tuweze kuwapatia wale wananchi wetu ajira kutokana na uhaba wa ardhi mkubwa tulionao?

Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kupitia *NDC* kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Hai ili tuweze kupanga kaeneo kadogo makazi pale Njia Panda kuelekea Machame kutokana na umuhimu unaonekana hivi sasa kuna hitajiko la kuwa na makazi rasmi badala ya vibanda vibanda vilivyopo sasa hivi?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kabisa kwamba eneo hilo alilitaja na jumbo langu linaweza kabisa kunufaika ni eneo ambalo linahitaji sana kuwekezwa ukizingatia kwamba kile kiwanda cha *Kilimanjaro Machine Tools* kilikuwa kinatoa ajira nyingi sana kwa watu wa majimbo hayo yote aliyoyataja.

Nakubaliana naye vile vile kwamba upo uhaba mkubwa wa ardhi katika eneo hilo na hivyo kupelekea watu au watalii ambao wanakuja eneo la Kaskazini pale wakose hata mahali pa kukaa.

Kwa hiyo, ninachopenda kusema tu ni kwamba Wizara yangu kama nilivyosema kwenye jibu la msingi tumeshatenga fedha kwa maana ya mapendekezo kuletwaha Bungeni. Namwomba tu Mheshimiwa Fuya na Waheshimiwa Wabunge wote tusaidie kuitisha Bajeti ya Wizara yetu na mara tu Bajeti kupita tutaanza matayarisho hayo mara moja ili kiwanda hicho na maeneo mengine ambayo yataweza kuwekeza yaweze kuwa tayari kwa ajili ya uwekezaji.

Kuhusu hili la *NDC* kushirikiana na Wilaya ya Hai kuweka makazi ya watu, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Fuya Kimbita kwamba hata pale mwanzo tulipokuwa tunafikiria kubinafsisha eneo lile kulikuwa na mawazo kwamba hekari 100 ambazo zipo upande wa kulia, barabara inaelekea Machame, ziachwe kwa ajili ya ujenzi wa makazi ya watu, nyumba za kisasa, zingine za kukosha zingine za kuishi. Kwa hiyo, napenda kumhakikishia kwamba tunavyoendelea katika mchakato huu tutaongea na wenzetu wa *NDC* kuangalia kama uwezekano wa kulizingatia hilo vile vile katika matayarisho na mazungumzo yatafanyika kama alivyopendekeza kati ya *NDC* na Wilaya yake ya Hai.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipatia nafasi hii kuuliza swali dogo tu la nyongeza. Namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake. Katika mpango wa Serikali tulio hivi sasa ifikapo 2025 *SEZ* utaenea nchi nzima, lakini kwa utaratibu huu tulio nao hivi sasa hazizidi *SEZ* au maeneo hayo matatu au manne, Je, kwa *speed* hii tuliyonayo hata ikifika mwaka huu kweli tuna *SEZ* au maeneo mangapi kulingana na hatua hii au maeneo mengine ambayo tayari yameshaandaliwa kuhakikisha kwamba *SEZ* inaenea nchi nzima. (*Makofit*)

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:**  
Mheshimiwa Spika, kwanza nakubaliana naye kwamba upo umuhimu wa kuharakisha zoezi hili ili ifikapo 2025 kwa kweli tuwe tumefikia yale maeneo yote ambayo tungependa yawe na mpango huu wa EPZ na SEZ. Lakini pili nataka nimtoe wasiwasi kwamba maeneo ni machache. Hapa nilipo nina orodha ya maeneo 14 ambayo yapo katika hatua mbalimbali za matayarisho. Mamlaka yetu ya EPZ inafanyika kazi kubwa katika maeneo hayo.

Napenda nichukue fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru viongozi wa Mikoa na Wilaya na hasa Waheshimiwa Wabunge katika maeneo husika ambaa wamesaidia katika kupatikana maeneo haya wanasadida kuwahamasisha wananchi na vile vile wanasadida katika suala zima la ulipaji wa fidia katika maeneo yale. Naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mzee kwamba akipenda nitampatia orodha ya maeneo hayo 14 ambayo tunayaendeleza na endapo tunapata uwezo mkubwa zaidi tutaendeleza maeneo mengine zaidi. (*Makofi*)

Na. 133

### **Serikali Kuwasaidia Wavuvi Wafugaji**

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE** aliuliza:-

Kwa kuwa Watanzania walio wengi wana hali duni kimaisha na wanajishughulisha na shuguli za kilimo, uvuvi,na mifugo;na kwa kuwa, wananchi hao wanajituma wakijua kuwa mtaji wa masikini ni nguvu zake mwenyewe:-

(a)Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wavuvi zana bora zenye viwango kwa bei nafuu?

(b)Je, Serikali haioni kuwa, wakati umefika kwa wafugaji kutengewa maeneo yao ya ufugaji mapema ili kuondoa usumbufu wa kuwahamisha hamisha?

### **NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Savelina Silvanus Mwijage, kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua matatizo yanayowakabili wavuvi wadogo hususan matumizi ya zana duni za uvuvi hali ambayo inapelekea umaskini kuendelea kukithiri mionganoni mwa jamii ya wavuvi. Kwa kutambua tatizo hilo Serikali, imeweka mikakati ya kuwajengea uwezo wavuvi katika maeneo yao.

Katika ukanda wa Pwani wa Bahari, kupitia Mradi wa MACEMP, jumla ya vikundi 117 vikiwa na washiriki 1,869 vimepewa zana bora za uvuvi zenye thamani ya

shilingi 1,550,459,061. Zana hizo ni pamoja na nyavu za aina mbalimbali, injini na boti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, kupitia Mradi wa Uwiano wa Menejimenti ya Uvuvi katika Ziwa Victoria, Wizara imechukua hatua ya kuboresha na kujenga mialo mipya katika mikoa ya Kagera (3), Mara (5) na Mwanza (3) ili kupata mahali sahihi pa kutunzia zana za uvuvi.

Aidha, Programu ya Maendeleo ya Uwiano ya Bonde la Ziwa Tanganyika kupitia kipengele cha Maendeleo ya Uvuvi na Mazingira kitakachoanza kutekelezwa mwaka 2009/2010, wavuvi watawezesewa kupata zana bora za uvuvi ikiwa ni pamoja na nyavu za dagaa na nyavu za samaki wakubwa zinazokubalika kisheria na mazingira ya mialo kuboreshwa. Aina na idadi ya zana na mialo hiyo, itajulikana baada ya jamii za wavuvi kuibua miradi hiyo. Wizara yangu itaendelea na utaratibu wa kuwasaidia wavuvi kupata zana bora kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, hatua zingine zinazochukuliwa na Serikali, kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki ni kupunguza kodi kwenye malighafi, pembejeo na zana za uvuvi zinazonunuliwa kutoka nje ya nchi. Kulingana na “*East Africa Community Common External Tariff kifungu cha XVII, sura ya 89.*” Malighafi zinazotumika kutengeneza zana za uvuvi zinazonunuliwa kutoka nje ya nchi hupewa punguzo la kodi la asilimia 100 kwa injini za uvuvi na malighafi za kutengeneza zana mbalimbali za uvuvi na viambata vyake.

(c)Mheshimiwa Spika, Serikali, inatambua umuhimu wa kutengeta wafugaji maeneo ya malisho ili kuondoa athari za kuhamahama, ikiwemo mgogoro kati ya wakulima na wafugaji. Hivyo, Wizara inashirikiana na wadau wengine hususan Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Halmashauri kuainisha, kutenga na kupanga matumizi endelevu ya maeneo ya malisho katika mikoa mbalimbali. Hadi kufikia mwezi Machi 2009, jumla ya Hekta 1,391,109.41 ziliikuwa zimepemwa kwa ajili ya ufugaji, katika vijiji 240 kwenye mikoa 13. Mikoa hiyo ni Dodoma (Hekta 50,843.81); Iringa (Hekta 13,841.30); Kagera (Hekta 10,516.62); Kigoma ( Hekta 10,256.93); Lindi ( Hekta 392,067.62); Mbeya (Hekta 295,402.12); Morogoro (Hekta 203,319.02); Mtwara (Hekta 1,098.78); Pwani (Hekta 129,762.65); Ruvuma (Hekta 51.00); Singida (Hekta 19,023.34); Tabora (Hekta 19,165.17); na Tanga (Hekta 14,601.83). Katika mwaka 2009/2010, zoezi hili litaendelea katika mikoa ya Dodoma (vijiji 5); Singida (Vijiji 9), Ruvuma (Vijiji 14) na Rukwa (Vijiji 12) na maeneo mengine ya nchi kulingana na Bajeti itakavyopitishwa hapa Bungeni. (*Makofi*)

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika. Kwa kuwa tatizo hili la wavuvi limekuwa kero kwa muda mrefu na mara kwa mara wanakamatwa na zana haramu na hizo zana haramu zinatengenezwa na viwanda siyo kusema wanajitengezea wenyewe.

Serikali ina mikakati gani ya kufunga viwanda hivyo vinavyotengeneza zana haramu ili kuweza kuwasaidia wavuvi kwa kuwa ni maskini kuwaletea zana halali kuweza kuwasaidia wavuvi hao? (*Makofi*)

Swali la pili, hili tatizo la wakulima na wafugaji Mheshimiwa Spika, limekuwa kero na ni bahati ametangazwa, amenijibu Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba wametengenezwa sehemu ya wafugaji. Lakini kabla hawajakabidhiwa, hizo sehemu, Serikali ina mikakati gani kuwasaidia ili kuondokana na migogoro iliyoko kwa wafugaji waache kuuana mara kwa mara? (*Makofi*)

#### **NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:**

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kufuatana na Sheria ya Uvuvu Na. 22, 2005 na Kanuni zake 2005 zinakataza uvuaji wa samaki kutumia nyavu ambazo ni haramu na tumeoanisha kwa kila aina ya samaki. Tunavyo viwanda viwili, kimoja iko Dar es Salaam na kingine kiko Mwanza.

Viwanda hivyo Wizara yetu huwa inavicheki kuangalia kwamba havitengenezi nyavu za haramu. Pale tutakabaini kwamba vinatengeneza nyavu za haramu ambazo zinaleta uvuvi wa haramu hapa nchini, hatutasita kuzichukulia hatua na mpaka sasa hivi tunachekei hatujapata matatizo. Hizi nyavu zinavyoingia siyo kwamba zinatokea katika viwanda hivyo, lakini kama itabainika wanatengeneza hatutasita kuvichukulia hatua.

Swali la pili, kuhusu matatizo ya wafugaji ni kweli yametokea Kilosa na sehemu zingine. Tatizo hilo limebainika na Mheshimiwa Waziri Mkuu ameunda Tume ambayo inashughulikia suala hilo na mara Tume itakapotoa Ripoti yake Serikali itachukua hatua mahsus ya kuhakikisha kwamba matatizo ya wafugaji na wakulima yanataluliwa, lakini hatungojei hivyo, ndiyo maana tunatenga maeneo na ndiyo maana vile vile tunahamasisha wafugaji waweze kutumia mbegu bora za kuzalisha ili wawe na ng'ombe wachache wanaokua haraka na wanaoweza kutumia maeneo machache.

Kwa hiyo, Serikali inaendelea na vile vile tunahamasisha kwa kupitia *DADIPS* tunaweka miundombinu, malambo majosho ambayo yanafanya watu wasitoke sehemu zingine waweze kukaa sehemu zao ili wasiende sehemu zingine kuwabughudhi watu wengine. Ahsante sana. (*Makofi*)

Na. 134

#### **Matangazo ya Matukio ya Uhalifu**

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE (K.n.y. MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA)** aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwa na matukio mengi ya uhalifu. Je, kwanini matangazo ya matukio hayo ni mengi kuliko taarifa ya hatua zinazochukuliwa dhidi ya makosa hayo?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA (K.n.y. WAZIRI WA MAMABO YA NDANI YA NCHI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jeshi la polisi limekuwa linatoa taarifa kwa wananchi kupitia vyombo vyta habari kuhusu matukio ya uhalifu, maafa, moto, ajali za barabarani na matukio mengine yanayoigusa jamii.

Taarifa hizo kwa kawaida zinatakiwa kutolewa katika ukomo wa:-

- (i) Aina ya kosa lililotendeka.
- (ii) Mahali na muda lilipotendeka.
- (iii) Watuhumiwa waliokamatwa, idadi yao, utaifa wao, jinsia, umri lakini pasipo kutaja majina yao.
- (iv) Majina ya waathirika, anuani na hali zao.
- (v) Majina ya walalamikaji isipokuwa katika makosa ya kubaka na kujamiihana, makosa yanayohusu watoto wadogo na pale ambapo walalamikaji wameomba majina yao yasitajwe.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya kutoa taarifa hizo:-

- (i) Kuiwezesha jamii kuelewa hali ya usalama inavyoendelea katika nchi yao au eneo wanaloishi.
- (ii) Kuwawezesha wananchi kuelewa mbinu zinazotumiwa na wahalifu ili wawe makini zaidi.
- (iii) Kutambua mali zilizoibwa na wahalifu.
- (iv) Kuwapa fursa wananchi kutoa taarita za uhalifu na wahalifu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mwenendo mzima wa matukio yanavyoripotiwa katika vituo vyta Polisi, wahalifu wanavyokamatwa, upelelezi unavyoendeshwa na kesi hizo kufikishwa Mahakamani kusikilizwa hadi kumalizika, ni dhahiri kwamba idadi ya matukio ya uhalifu yanayotangazwa ni mengi kuliko idadi ya kesi zinazohitimishwa Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, hatua ya mwisho ya uhalifu ni kwa Mahakama kutoa hukumu. Kwa mujibu wa Sheria za nchi hukumu hutolewa katika Mahakama ya wazi ambapo wananchi wanaruhusiwa kufika na kusikiliza matokeo ya hukumu hizo. Vyombo

vya habari vina uhuru wa kuchagua na kuamua taarifa ipi ya hukumu iwafikie wananchi kwa mujibu wa utashi wa chombo cha habari husika.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu napenda kutotoa wito kwa vyombo vya habari kuongeza kasi na kutoa msukumo zaidi wa kutoa taarifa kwa Umma juu ya matokeo, mwenendo wa kesi na hitimisho la kesi hizo.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini kwanza nichukue nafasi hii kupongeza jeshi la polisi kwa kazi nzuri wanayofanya na kupunguza matukio ya ujambazi nchini na hasa kwa mbinu wanayoitumia ya *patrol* ya masaa 24 kutumia magari na pikipiki. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kutoa motisha maalum kwa askari wanaojitokeza kupambana ana kwa ana na majambazi wakawekwa kwenye patrol kuwe na motisha maalum kwa ajili hiyo na pengine ni vizuri ikaisema hapa Bungeni ili na sisi tuweze kuridhika na hatua wanazochukua kwa kuwapa motisha askari hawa?

Swali la pili, je Serikali haioni kwamba kuna haja na pengine ituambie katika bajeti hii kwamba imetenga fedha kiasi gani kwa ajili ya motisha kwa askari wanapokuwa katika doria kama malipo ya ziada kwa sababu mishahara yao ni midogo?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI):** Mheshimiwa Spika, upo utaratibu katika Ofisi *IGP* kutoa motisha kwa askari ambao wanapambana na majambazi na kuwakamata ama kuwaua. Hiyo imekwishatoka katika ile kesi ya ujambazi iliyotokea pale Ubungo askari wale walipewa motisha wengine wanapandishwa vyeo, wengine wanapewa pesa taslimu. Kwa hiyo utaratibu huo upo chini ya Ofisi ya *IGP*. Kuhusu Serikali imetenga kiasi gani nitamwomba Mheshimiwa Mbunge asubiri atusikilize bajeti yetu tunavyosema ataona tumetenga kiasi gani kwa ajili hiyo ya kutoa motisha kwa askari wetu.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Nashukuru Mheshimiwa Spika, kwa kuniruhusu kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa polisi ndiyo ambao wanawajibika kulinda usalama wa raia na mali zao na kwa kuwa mtu anapovamiwa na majambazi akaibiwa mali zake inakuwa amepata janga sawasawa na wanaopata majanga mengine kama vile yale mabomu ya Mbagala ama walipitiwa na kimbunga na kwa kuwa watu waliopata majanga Serikali ina utaratibu wa kuwafidia mali zao angalau kupata chochote cha kufuta machozi.

Je, Serikali sasa itakubaliana na mimi kwamba sasa wanaopata matukio ya namna hiyo kwa vile ni janga na wao wafidiwe? (*Makofi*)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI):** Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali huwa inatoa fidia kwa majanga ambayo Serikali yenyewe imesababisha. Kwa mfano huo uliota mambo ya

mabomu yale ya Mbagala pale Serikali ilihusika ni mabomu yake mabomu yameamua kwenda kupata kichaa na kupasuka basi Serikali inahusika lazima itoe fidia kwa walioathirika.

Lakini inapokea kwamba hii sasa binadamu mmoja kamdhulumu binadamu mwingine halafu Serikali iingilie inakuwa vigumu. Ningeshauri tu Mheshimiwa Mnyaa kama inawezekana basi tujitahidi kuweka bima ambapo tutaweza kulipwa matukio kama haya yakinke. (*Makofi*)

Na. 135

### **Utaratibu wa Cash Budget**

**MHE. MBAROUK K. MWANDORO** aliuliza:-

Kwa kuwa utaratibu wa *Cash Budget* mara nyingi unasababisha ucheleweshaji wa fedha kufikishwa zilipopangwa; na kwa kuwa, baadhi ya Watendaji hutumia mwanya huo kuzidi kuchelewesha mtiriko kwa makusudi na mara nyingine wakitarajia wasujidiwe kana kwamba kuzifikisha fedha hizo kunakotakiwa ni hisani na sio wajibu wao:-

(a) Je, vipo vigezo gani mahususi vyta ufanisi wa kufikisha fedha zinazotakiwa kwa kiasi kilichoainishwa kwa muda maalum na hatua za nidhamu kwa wanaokiuka taratibi?

(b) Je, serikali inaweza kubuni utaratibu wa uwazi zaidi na vikwazo kwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya Ofisi za Wabunge Majimboni?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa fedha na uchumi, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mbarouk Kassim Mwandoro, mbunge wa jimbo la Mkinga, lenye sehemu (a) na (b), naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba kulifahamisha Binge lako Tukufu kuwa, madhumuni makubwa ya kutumia utaratibu wa *Cash Budget* ni kuhakikisha inakuwepo nidhamu katika kutekeleza Bajeti ya serikali. Hali hii inaifanya Serikali kutumia kiasi kilichokusanywa kama mapato ya serikali. Kutokana na hali hiyo, utaratibu wa *cash budget* umefanikiwa kuhakikisha matumizi ya serikali hayazidi mapato na hausababishi fedha kuchelewa kufika zilikopangiwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbarouk Kassim Mwandoro, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, kutokana na hali ya kijiografia ya nchi yetu, miundombinu ya sekta ya fedha pamoja na muundo wa malipo, kwa hivi sasa ni vigumu kuweka vigezo, masharti na viwango vinavyofanana au kulingana kwa nchi nzima, hasa katika kuhusisha muda wa kufikisha fedha katika eneo husika. Matarajio yetu ni kuwa fedha iliyoidhishwa kwa malipo ifike inakotakiwa na kwa ukamilifu. Hata hivyo, Wizara yangu ikishirikiana na taasisi za fedha inaliangalia kwa undani zaidi suala hili kwa lengo la kulipatia ufumbuzi wa kudumu.

(b)Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, utaratibu wa Serikali wa kuhudumia Ofisi za Wabunge hautofautiani na ule wa kuhudumia Ofisi nyingine za Serikali. Kwa mujibu wa masharti ya kazi ya Mbunge, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ndiyo yenye dhamana ya kuhakikisha upatikanaji wa Ofisi na vifaa muhimu vinavyohitajika na Mbunge kwa ajili ya kufanikisha shughuli zake za Bunge.

Kutokana na utaratibu huo, tunatarajia huduma kwa Wabunge zitatolewa kwa uwazi na kwa kufuata taratibu zilizopo. Hata hivyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge kama anayo mapendekezo au maoni ambayo yatakayoweza kusaidia kuleta ufanisi na uwazi zaidi katika kuhudumia Ofisi za Wabunge, atupatie ili tuweze kuyafanya kazi.

**MHE. MBAROUK K. MWANDORO:** Nashukuru Mheshimiwa Spika, kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Moja, swali langu hili nililiweka kwa sababu ya utaratibu uliokuwepo zamani wa fedha kupitia Mkoani na Mkoani mara nyingi walikuwa wanachelewesha sana.

Lakini kutokana na Bajeti mpya inaelekea utaratibu huu sasa utabadilika moja kwa moja Wilayani. Napenda niipongeze Serikali kwa hili na ninaamini kwamba utaratibu huu utaleta ufanisi zaidi.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuweka vigezo maalum vya kuhakikisha zile Bajeti zilizowekwa zinapelekwa kwa muda unaostahili?

Pili, sisi Wabunge tunapata matatizo sana kuelewa ni fedha gani halisi zimepelekwa Mikoani kwa ajili ya shughuli mbalimbali za maendeleo.

Je, Serikali itakuwa tayari kutupatia nakala za fedha halisi zilizotolewa kwa maendeleo pamoja na zile ambazo zimetolewa kwa ajili ya matumizi ya Ofisi za Wabunge ili tuweze kujua fedha zilizotolewa na matumizi halisi yanayofanyika? Ahsante sana Mheshimiwa Spika. (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi, kuweka vigezo hasa kwa kuzingatia muda kwa hivi sasa ni vigumu kutokana na miundombinu ya sekta ya fedha tuliyonayo nchini. Lakini nimesema kwamba tutashirikiana na Taasisi za

Fedha kuhakikisha kwamba hili suala linaweza likatatutuliwa katika kipindi kifupi kijacho.

Suala la pili Mheshimiwa Spika, ni kwamba Mheshimiwa Mbunge ametaka kupatiwa taarifa juu ya fedha ya maendeleo na fedha za matumizi kwa ajili ya Ofisi za Wabunge.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie kwamba taarifa hizo akifika kwa Mkuu wa Mkoa atapewa na ninamhakikishia kwamba aende kwa Mkuu wa Mkoa atapewa kwa sababu hakuna utata katika kumpatia taarifa hizo. Namshauri aende akamwone Mkuu wa Mkoa atapatiwa. (*Makofi*)

Na. 136

### **Maombi ya Fedha za Kunasua Nashirika ya Umma Yasifungwe**

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Ofisi ya Msajili wa Hazina imepokea maombi ya kiasi cha Shilingi bilioni 32 na Dola za Kimarekani milioni 21 kwa ajili ya kuokoa Mashirika mbalimbali ya Umma yasifungwe na pia kama mchango kwa baadhi ya mashirika ambayo Serikali ina ubia:-

Je, Serikali imeshatoa fedha kiasi gani kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina ili kutekeleza maombi hayo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI – MHE. OMAR YUSSUF MZEE** Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mbunge wa Jimbo la Wete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli katika mwaka wa mwaka 2008/2009, Ofisi ya Msajili wa Hazina, ilipokea Jumla ya Maombi ya fedha ya Shilingi bilioni 32 na Dola za kimarekani milioni 21 kutoka mashirika mbalimbali kwa ajili ya kuokoa mashirika ya umma na mchango wa Serikali kwa mashirkka hayo. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, hadi kufikia mwezi Juni, 2009, Ofisi ya Msajili wa Hazina ilikuwa imepatiwa kutoka Hazina jumla ya Sh. 46,652,000.66 ambazo ziligawiwa katika mashirkka mbalimbali kama ifuatavyo:-

Kuimarishe mtaji wa *TIB* Shilingi bilioni 21; Mamlaka ya Dhamana na Masoko ya Mtaji, *CMSA* Sh. 1,235,000.2; *Unit Trust of Tanzania* Shilingi milioni 50.0; Kampuni ya Ndege Tanzania, *ATCL* Sh. 11,522,000/=; Kampuni ya Reli Tanzania, *TRL* Sh.

11,522,000/=; Benki ya Posta Tanzania, *TPB* Sh.1,500,000/. Jumla ni Sh. 46,652.66 milioni.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuyasaidia mashirika ya umma ili yaweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na hatimaye kuchangia katika ukuaji wa uchumi wetu.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa haya mashirika ya umma ambayo Serikali inawekeza na ilhali mpaka leo bado yanafanya hasara kubwa kwa Serikali: Je, Serikali ipo tayari kuyauza mashirika haya na kuendelea na kuiondolea Serikali hasara?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI – MHE. OMAR YUSSUF MZEE:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwadini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mwadini kwamba mchakato wa mashirika ambayo yanafanya hasara sio lazima yauzwe, inawezekana mashirika hayo yanafanya hasara kwasababu ya muundo wake. Utakumbuka kwamba mashirkka mengi yalianza wakati hakuna *competition*, hakuna mashirika mengine yaliyojitokeza, kwa hiyo, yakaajiri wafanyakazi wengi sana, ikiwa ni pamoja na Shirika letu la Bima ambalo lilikuwa lina wafanyakazi zaidi ya 400. Sasa hivi kuna Taasisi nyingi sana za Bima, kwa hiyo shirika hili pengine hakuna haja ya kuliiza. Ili liweze kufanya faida kuna haja ya *ku-restructure* tu muundo wake. Lakini kwa yale ambayo yanafanya hasara na hakuna njia nyingine ya kusaidia, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itafanya jitihada zake ili kuweza kuona kwamba yatauzwa au kubinafsishwa kwa Watanzania na wawekezaji wengine kutoka nje.

**SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa. Saa ya maswali imefikia ukomo, lakini tunaweza kuyaangalia haya mawili kwa haraka. Wizara ya Miundombinu sasa. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, wa Moshi Mjini kwa niaba yake Mheshimiwa Said Arfi.

Na. 137

#### **Mtandao wa Reli Katika Afrika mashariki**

**MHE. SAID A. ARFI (K.N.Y. MHE. PHILEMON NDESAMBURO)**  
Aliuliza:-

Kwa kuwa, kabla ya kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1977 kulikuwepo na mtandao wa Reli ulioziunganisha nchi wanachama na kusaidia usafirishaji wa abiria na mizigo na pia kuchangia katika ukuaji wa miji kibashara na kwa kuwa mtandao huo umefungwa:-

(a) Je, ni kwa nini hadi sasa kipande cha reli kutoka Taveta hadi Moshi kimeendelea kufungwa wakati Jumuiya ipo na kuna mtandao wa reli kutoka Mombasa – Voi – Taveta – Moshi?

(b) Je, Serikali haioni kuwa inawanyima haki wafanyabiashara wasio na uwezo kukodi magari kubeba mizigo kutoka Bandari ya Mombasa ambapo wangeweza kuchukulia mizigo yao Moshi?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kutumia mtandao huo na kuepuka uharibifu wa barabara kutokana na magari ya mizigo na pia Serikali haioni kuwa reli hiyo itakuwa kichocheo kikubwa cha ufunguzi wa Bandari kavu ya holili?

#### **NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU Alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mtandao wa miundombinu ya reli kutoka Mombasa – Voi – Taveta hadi Moshi umeendelea kuwepo toka wakati wa Jumuiya ya kwanza ya Afrika Mashariki iliyovunjika mwaka 1977 hadi leo.

Kutokana na kuimarka kwa miundombinu ya barabara hapa nchini, kipande cha Reli cha Taveta hadi Moshi kwa sasa hakitoi huduma ya kusafirisha mizigo kutokana na kukosekena kwa mizigo kwani wasafirishaji wengi huvutika kutumia njia ya barabara.

Mheshimiwa Spika, Serikali haijawanyima haki wafanyabiashara wanaohitaji kusafirisha mizigo yao kwa njia ya reli ila kitendo cha wafanyabiashara wengi kutopendelea kusafirisha mizigo yao kwa njia ya reli ndiko kunakofanya usafirishaji wa mizigo kati ya Taveta na Moshi ukosekane. Serikali inapenda kuwashamasisha na kuwashimiza wafanyabiashara kusafirisha mizigo kupitia njia ya reli kiwango cha mizigo kifikie hatua ya kuwezesha huduma za usafirishaji wa reli kupitia Taveta hadi Moshi. Kwa vile Bandari Kavu ya Holili inahudumia mizigo inayosafirishwa kwa njia ya barabara kutoka na kwenda Mombasa, matumizi ya reli kati ya Kahe na Taveta hayatakuwa na kichocheo cha ufunguzi wa Bandari Kavu ya Holili kwa kuwa upakiaji na upakuaji wa mizigo unapotumia njia ya reli utafanyika Moshi bila kuhitaji tena kupitia Holili.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kulinda na kuimarka miundombinu ya reli ikiwemo hiyo ya Taveta hadi Moshi ili iweze kutumika kusafirisha mizigo hali itakayosaidia kupunguza uharibifu wa barabara unaofanyika hivi sasa kwa kupitisha magari yaliyobeba mizigo mizito. Sambamba na hilo, uharibifu wa barabara kutokana na magari ya mizigo, Wakala wa Barabara, *TANROADS* ambayo inasimamia barabara nchini imeweka taratibu maalum za kisheria za kuhakikisha kuwa magari hayazidishi mizigo na kusababisha uharibifu wa barabara.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, anataka kutushawishi na kuwashawishi Watanzania kwamba tayari kuna maridhiano kati ya nchi mbili za Kenya na Tanzania? Pia mashirika ya reli ya Kenya na Tanzania kwa kuanzisha biashara ya kusafirisha mizigo kati ya nchi hizi mbili? Je, anaweza kulihakikishia Bunge hili kwamba katika mpango wa biashara, *Business Plan* ya *TRL*, wanategemea lini wataanzisha safari za kutoka Moshi kwenda Taveta?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa, ushirikiano wa nchi hizi za Afrika Mashariki, umepelekea Serikali yetu na Serikali ya Rwanda kufanya mazungumzo ya kujenga reli kuanzia Isaka mpaka Kigali: Je, Serikali haiwezi kufikiria pia kujenga reli kati ya Tunduma, Kasanga, Mpanda na Karema kwa ajili ya kuzisaidia nchi zilizo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, swali hili la kwanza kuhusu ni lini *TRL* itaanzisha usafiri kwenda Taveta ni kama nilivyosema tu katika jibu la msingi kwamba tatizo hapa ni wafanyabiashara kuvutika kusafirisha mizigo yao kwa njia ya barabara hasa baada ya kuimarika kwa miundombinu ya barabara nchini. Lakini wakati wowote endapo tutapata mizigo mingi ya kupitia katika njia hii hilo linawezekana, ni wakati wowote. Niseme tu kwamba, katika mpango mzima wa usafirishaji kwa njia ya reli, Serikali ina azma ya kuhamasisha wananchi waweze kutumia njia ya reli kwasababu ni nafuu zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini hili la pili linalohusu ushirikiano wa Afrika Mashariki na ujenzi wa miundombinu ya reli kwa ujumla, niseme tu kwamba kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, kweli sasa hivi upo mpango ambao kwa sasa uko katika mazungumzo ya hali ya juu sana wa kujenga reli kutoka Isaka kwenda mpaka Kigali mpaka Burundi. Kwa hiyo, wazo ama pendekezo la kujenga reli nyingine za kuunganisha hizi Bandari za Kasanga na kwingine kote alikokusema, niseme tu kwamba upo mpango kabambe ambao sasa Jumuiya ya Afrika Mashariki *ime-commission study* ya kuangalia njia zote ambazo zinawenza zikawa na uwezekano wa kuunganisha vituo mbalimbali katika Jumuiya ya Afrika Mashahriki. Hiyo ikishakamilika, suala alilolipendekeza Mheshimiwa Mbunge hapa litazingatiwa. (*Makofî*)

Na. 138

### **Kukarabati Reli ya Kilosa – Kidatu**

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA** Aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati njia ya reli kati ya Kilosa na kidatu ili aianze kutumika tena kusafirisha sukari na mizigo mingine na kupunguza gharama ya usafirishaji kwa kutumia barabara?

(b) Je, Serikali inafahamu wastani wa gharama itakayotolewa kwa kutumia njia ya reli badala ya barabara?

(c) Je, Serikali itatumia njia gani ili gharama itakayookolewa imfaidishe mwananchi wa kawaida?

#### **NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU Alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mbunge wa Mikumi lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kati ya mambo yaliyoifanya Serikali ifikie uamuzi wa kukodisha huduma za reli nchini ni kuzorota kwa huduma za usafirishaji wa abiria na mizigo njia ya reli. Njia ya reli kati ya Kilosa na Kidatu ni moja kati ya njia ambazo huduma zake zilizorota na kushindwa kuendelea. Chini ya reli ya Kilosa – Kidatu imepangwa kufanyiwa ukarabati utakaowezesha kupandisha kiwango cha mwendokasi cha kilometra 35 kwa saa kwenye reli hiyo hadi kufikia mwendokasi wa kilometra 40 kwa saa. Hatua hii itawavutia wasafirishaji kuitumia reli hiyo kwa kusafirisha sukari na mizigo mingine.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu kwamba viwango vya gharama vya usafirishaji wa shehena kwa njia ya reli ni vya chini kuliko usafiri wa barabara. Hata hivyo, gharama za usafiri kwa njia ya reli huwa nafuu kwenye umbali mrefu angalau umbali wa kuanzia kilometra 400 na kuendelea. Kwa mfano, kusafirisha shehena ya kawaida, *general cargo*, kwa njia ya reli kutoka Dar es Salaam hadi Kidatu, wastani wa kusafirisha tani moja kwa kilometra moja ni Shilingi 121 kwa njia ya reli na Shilingi 158 kwa tani moja kwa njia ya barabara, kiasi kinachofanya kuwepo na unafuu wa takribani Shilingi 37 kwa tani moja.

Mheshimiwa Spika, ni kutokana na ukweli huo ndiyo maana serikali imedhamiria kuzifufua huduma za Reli nchini kwa kusimamia mipango yote yenye lengo la kuimarisha miundombinu ya reli ikiwemo ile ya Kilosa hadi Kidatu.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *RAHCO* itaendelea kuweka mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na kusimamia Mkataba wa ukodishwaji ili kuhakikisha usafiri wa reli unaboreshwu kuwezesha wananchi wengi kutumia usafiri huu amba ni nafuu. Aidha, Serikali kupitia *SUMATRA* itahakikisha nauli na gharama za uchukuzi hazipandishwi kiholela na zinawekwa wazi ili mwananchi wa kawaida aweze kunufaika na unafuu huo.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo tu la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize swali hilo kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, sehemu kubwa ya uzalishaji wa sukari ya Kilombero unasambaa katika maeneo ya Bara zaidi ya Kilometra 400 mpaka Dodoma, Urambo, Tabora, Kigoma, Mpanda na kadhalika na hivyo kuwa na umuhimu mkubwa kiuchumi; katika mpango kazi wa ukarabati wa reli nchini; reli ya kilosa – Kidatu imepangwa kuanza lini? Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge ya kwamba miwa inayotoka katika maeneo yale ya Jimbo lake inasafirishwa katika maeneo ya mtandao mpana kidogo mpaka katika maeneo hayo uliyoyataja ya Dodoma mpaka Urambo, Tabora na kadhalika. Katika jibu langu la msingi hapa nimesema, katika ule mpango mkubwa wa kuhakikisha kwamba huduma za reli zinazofufuka nchini, hiyo reli ya Kidatu – Kilosa imo katika mpango huu.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu bado tu ni mpango, ningeomba Mheshimiwa Mbunge, awe na subira. Tutakapokuwa tumeainisha vipande hivi vya ujenzi wa reli hatua kwa hatua tutatoa tarehe rasmi, lakini kwa sasa hivi siko tayari kutoa tarehe hiyo kwa sababu hatujainisha vipande hivi vitaanza kutekelezwa lini na kwa utaratibu upi.

### **MUONGOZO WA SPIKA**

**MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mwongozo wa Spika,

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa Mnyaa. Kanuni?

**MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 68 (7).

**SPIKA:** Kanuni ya 68, naam.

**MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tumetengua Kanuni ya 101 (2) na ninaomba niisome. Kanuni ya 101 (2) inasema: “*Mbunge ye yote anaweza kuomba ufanuzi au maelezo zaidi katika kifungu chochote cha fungu linalohusika wakati wa kifungu hicho kitakapofikiwa na Kamati ya matumizi.*”

Mheshimiwa Spika, katika...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mnyaa, Mwongozo ni lazima uambatane na shughuli inayoendelea; hatuko kwenye Kamati ya Matumizi wala hatuko katika kujadili bajeti. Hivi sasa tuko kwenye kipindi cha Maswali. Sasa huwezi kusimama tu ukaomba mwongozo kuhusu jambo la juzi, lolote, ama sivyo ingekuwa hiyo inaruhusiwa kungekuwa humu hatuna mjadala, ni fujo tu. Mtu anasimama anaomba miongozo. Kwa hiyo, nimekataa huo Mwongozo. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, muda wa Maswali umekwisha. Sasa ni matangazo. Wageni waliopo Bungeni Asubuhi hii ni kama ifuatavyo:-

Wageni wa Mheshimiwa Waziri wetu wa katiba na Sheria - Mheshimiwa Mathias Chikawe. Nilikwishamtambulisha Mheshimiwa Jaji Mkoo, sasa wengine viongozi Waandamizi katika Wizara hiyo ni kama ifuatavyo: Tunaye Bw. Oliver P. J. Mhaiki - Katibu Mkoo wa Wizara, nadhani anakuja; tunaye M. S. Mheshimiwa Shangali - Jaji Mfawidhi Kanda ya Dodoma, yule pale! Ahsante sana. Wengi mnafahamu kwa sababu anashiriki shughuli nyingi sana zinazotuhusu hapa Dodoma, ahsante sana; Mheshimiwa Jaji Shangali kwa ukaribu wako; Mheshimiwa Jaji E. M. E. Mushi - Mkoo wa Chuo cha Mahakama Lushoto, yule pale! Ahsante sana; Mheshimiwa M. H. C. S. Longwe - Jaji Mahakama ya Ardhi, yule pale! Ahsante sana; Mheshimiwa R. V. Makaramba - Jaji Mfawidhi Mahakama ya Biashara, yule pale! Ahsante sana; Jaji A. R. Manento - Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, ahsante sana. Jaji Manento, tunafurahi kukuona tena hapa. (*Makofi*)

Wengine ni Bw. Sazi Salula Naibu Mwanasheria Mkoo wa Serikali, yule pale, ahsante sana; Prof. Ibrahim Juma - Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria, yule pale amefuatana na Katibu Mtendaji wa Tume Nd. Japhet Sagasii. Karibu sana Japheti! Tunashukuru sana kutoka mionganini mwa mazingira haya ya Bunge mtu anapopanda cheo huwa tunashukuru sana. Karibu sana sana, tunakutakia mafanikio katika kazi yako. Pia wapo Makamishna. Kamishna William Mdundo, yule pale! Ahsante sana; Kamishna Jaji Edward Mwesiumo, yule pale na Kamishna Ester Manyesha, yule pale. Ahsante sana. Inawezekana wapo Waheshimiwa wengine, lakini orodha niliyopewa ndio hii. Tunawashukuru sana kwa kuja Dodoma na hususan kuja Ukumbini hapa kusikiliza mjadala wa hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria. Karibuni sana. (*Makofi/Kicheko*)

Wapo wageni wa Mheshimiwa Dr. Emanuel Nchimbi Naibu - Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, ambao ni walimu 72 wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea, Waratibu Elimu Kata 13 na Maafisa Elimu 10. Wageni kutoka Songea tafadhalii. Ahsanteni sana. Nimearifiwa na Wizara kwamba matokeo ya Mtihani wa Darasa la Saba mwaka huu uliopita Songea Mlifanya vizuri. Kwa hiyo, ninyi ndio mnaohusika, tunawapongeza sana kwa kazi yenu njema na tunaomba walimu katika Wilaya nyingine pia waweze kuiga mfano wenu. Ahsante sana na tunawashukuru kwa kutoka Songea hadi hapa. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa John Paul Lwanji, ni Bw. Enock Daniel Anania - ni mjasiria mali mlemau. Anachimba visima virefu na anatoka Rungwe. Yule pale! Ahsante sana. Hii Rungwe au Rungwa? Ni Rungwa ndiyo, ningeshangaa! Rungwa ndiyo. Ahsante sana. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Mohamed Chombo, ambao ni viongozi kutoka Jumuiya ya CCM, Jimbo la Magomeni – Zanzibar, wakiongozwa na Ndugu Hamdani Juma Katibu wa UVCCM Wadi ya Magomeni. Ahsanteni sana. Tunafurahi kila mara kuwaona ndugu zetu kutoka Zanzibar, karibuni sana.

Wageni wa Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, ambao ni familia yake, Getrude Limbu, Neema Robert, Deborah Dickson, Kwandu Andrea, naomba wasimame tafadhali tuwatambue. Wale pale na Bwana na Bibi Kelvin. Ahsante sana na karibuni sana. Wageni wa Mheshimiwa George Simbachawene, ambao ni Wajumbe au Viongozi wa Chama cha Wastaifu Tanzania, Wawakilishi katika Maonyesho ya AZAKI ambao ni Eriot Mzava, yule pale, Ruben Kaduri, Frank Mhando, Zaphresa Mzava na Jackline Ndashau. Ahsante sana, karibuni sana ndugu zetu wa AZAKI. (*Makofi*)

Kuna wanafunzi 40 kutoka shule ya Sekondari ya Msalato, ambao wamekuja kushuhudia Kipindi cha Bunge, kipindi cha Maswali. Vijana wa Msalato nadhani na Walimu, tafadhali. Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyofahamu Shule ya Msalato ni Shule ya wanafunzi wenyewe vipaji maalum, kwa hiyo, hapo mnaowaangalia ndio wenyewe wenyewe bongo zinazochemka kweli kweli. Tunawatachia mafanikio katika masomo yenu, nchi yetu inahitaji watu; mkishafuzu muweze kutusaidia katika maendeleo. Tunawatachia mema. (*Makofi*)

Wako wageni 30 ambao ni washiriki katika AZAKI, wale watu wa AZAKI baadhi yao wako hapa ahsante sana na karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe maonesho ya AZAKI bado yanaendelea katika Ukumbi wetu wa Maonyesho pale jengo la Utawala. Kwa hiyo, mnahimizwa kuweza kuhudhuria mjionee mambo mbalimbali yanayofanywa na asasi hizi zisizo za Serikali. (*Makofi*)

Ooh! Nimefahamishwa kwamba mionganini mwa wageni wetu mashuhuri ni aliyejewa Katibu wetu wa Bunge na Mbunge Mstaifu wa Kalenga, Mheshimiwa George Mlawa, ahsante sana. Ahsante George, tunaendelea kukutakia mema katika maisha na shughuli zako. Ahsante sana. Wageni wa Mheshimiwa George Lubeleje, ni wanafunzi 30 na walimu kutoka Chuo Cha Maafisa Afya Mpwapwa. Sidhani kama, labda wapo katika Ukumbi wa *Basement*. Huo ndio mwisho wa matangazo ya wageni. (*Makofi/Kicheko*)

Sasa matangazo ya kazi, lipo moja tu. Ooh! Yameongezeka! Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, anahitaji Wajumbe wote wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii mkutane saa 7.00 mchana katika Ukumbi Na. 231; Mheshimiwa Abdisalaam Khatib - Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda na Biashara anaomba Wajumbe wote wa Kamati ya Viwanda na Biashara mkutane saa 7.00 mchana katika jengo la Utawala. Ukumbi alioutaja ni ule ule ambao watakuwemo wa Maendeleo ya Jamii. Kwa hiyo, labda itakuwa pale jirani Na. 229; lakini Katibu atawapangia pale.

Waheshimiwa Wabunge, Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara imepokea mwaliko kutoka kwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko kwenda Dar es Salaam kutembelea Maonyesho ya 33 ya Biashara ya Kimataifa. Kwa hiyo, Wajumbe hawa wanaruhusiwa kwenda kwenye maonyesho kuanzia tarehe 01 hadi tarehe 05 kadiri itakavyokuwa imapangwa. Hili ni tangazo kwa Wajumbe wa Kamati ya Viwanda na Biashara. Wanaalikwa kule na Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko kwenye maonesho ya Kimataifa ya Biashara. Kwa hiyo, wanaweza kuwa kule kadiri

watakavyopanga lakini kati ya tarehe 01 hadi 05. Huo ndio mwisho wa matangazo. Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 67, naomba nitoe Mwongozo sasa kuhusu malalamiko ya Mheshimiwa Selelii dhidi ya Wizara ya Miundombinu na Serikali kwa ujumla kwamba Wizara ilianza kutumia fedha bila kuidhinishwa na Bunge kwa sherehe iliyofanyika, Mgeni Rasmi akiwa Makamu wa Rais, kuhusu barabara ya Chalinze – Segera – Tanga. Sasa Waheshimiwa Wabunge, kwa kifupi hii yote nitaigawa kwasababu ni ndefu, inaelezea mambo mengi. Lakini kwa kifupi ni kwamba kuanzia mwaka 2006, zimekuwa zikitengwa fedha za matengenezo ya barabara hii ya Chalinze - Segera. Katika Mwaka wa Fedha 2006/2007 jumla ya Shilingi bilioni 10 zilitengwa na kiasi kikubwa kilitokana na mhisani, *DANIDA*, Shilingi bilioni 10 mwaka 2006/2007 na Shilingi bilioni 17 mwaka 2008/2009 na jumla kwa fedha za ndani ni Shilingi milioni 50 zilikuwa zikitengwa na kuidhinishwa na Bunge. Hatimaye katika Mkutano uliopita, Mkutano wa Kumi na Mbili wa Bajeti, tulipitisha makadirio hayo.

Tatizo lililotokea ni kwamba, Wizara ya Miundombinu ilikuwa na Idara inayoshughulikia barabara ikiitia *Roads Division*, baadaye Wizara hii wamebadili *Roads Division* ikaitwa *Transport Infrastructure Division*. Kwa hiyo, basi tulipokuwa tunaidhinisha miaka yote hii makadirio haya tulikuwa tunaidhinisha kuitia eneo linaitwa *Roads Division*, matokeo yake vitabu vivilvyochapishwa vya mwaka 2009/2010 kwenye Idara ya *Transport Infrastructure Division* ikaonekana kwa miaka iliyopita ni sifuri sifuri kwenye jina hilo, lakini sio kwamba Bunge halijaidhinisha, kwasababu tuliidhinisha chini ya *Roads Division*.

Sasa Waheshimiwa Wabunge, katika bajeti ya mwaka 2007/2008 Wizara ya Miundombinu ilikuwa imeomba bajeti ya Wizara kwa barabara Sh. 332,857,400,000/= kuitia *Roads Division*. Lakini fedha zilizoidhinishwa na Bunge katika mwaka huo wa fedha kwa Idara hiyo, kwa mujibu wa *Hansard* zilikuwa ni Sh. 428,857,400,000/=. Hii kama mtakumbuka inatokana fedha zilizoongezwa baada ya Mkutano wa Dharura tulivyokaa kutokea Kamati ya Miundombinu ikabidi maombi yaongezwe ya fedha za kuelekezwa kwa barabara kwa mwaka huo.

Sasa utata uliojitokeza ni kwamba katika bajeti ya mwaka 2007/2008, Wizara ya Miundombinu ilipokuwa ikiwasilisha makadirio yake kwenye Kamati ya Miundombinu, kulikuwa kumejitokeza hoja ya kuongeza kasima ya ujenzi wa barabara, *subvote 6002*, baada ya wajumbe kuona kwamba fedha zilizotengwa ni kidogo. Serikali ilikubali hoja ya Kamati na Wabunge wengi tu walioongea, kwa hiyo, ndiyo maana fedha hizo zikaongezwa na kwa ajili ya *roads division*, zikitengwa sasa shilingi bilioni 428,857,400,000 badala ya zile zilizokuwa zinaonyeshwa kwenye kitabu, shilingi bilioni 332.

Hivyo, ni uamuzi wangu sasa, baada ya kutazama yote haya pamoja na kuwa kumekuwa na utata baina ya fedha zilizopitishwa na Bunge yaani baina ya fedha

zilizopitishwa hatimaye na zile zilionekana kwenye kitabu, hakuna kasoro yoyote ama uvujanji wa Sheria ama Katiba. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, ila baada ya kupitia maelezo yote haya, ninashauri tu, kwanza naridhika kuwa fedha zilizotumika ni sahihi na zilitengwa na Bunge ingawa hoja ya Mheshimiwa Lucas Selelii ina msingi kwa sababu alipopitia Kitabu cha Miradi ya Maendeleo kwa mwaka huu fedha wa 2009, hivi vitabu tulivyonavyo, ukurasa wa 189, *item 4189*, inaonyesha kuwa miaka ya nyuma hakuna fedha zilizotengwa, ni uchapishaji na kubadilisha hizi kasima ndiyo imeleta tabu. Kwa kuwa utata huu unatokana na mabadiliko ya muundo, naishauri Serikali na Wizara ili tusirudie matatizo kama haya, basi kunapotokea mabadiliko ya miundo ndani ya Wizara hasa mabadiliko yanayohusiana na kutengwa fedha kwa miradi mikubwa, ni vyema basi Bunge likafahamishwa kwamba hiyo ndiyo imetokea ili tunaposoma hivi vitabu sasa tuweze kufanya rejea na kuwa sasa na hakika kwamba fedha zote zilizotengwa zimeidhinishwa na Bunge. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo uamuvi wangu na mtagawiwa na *press* nao watagawiwa kwa sababu jambo hili lilikuwa linashtua kidogo lakini maelezo ni bayana, hakuna utata wowote ila ni suala la mabadiliko ya majina ya Idara ndiyo yaliyoweza kuonyesha sehemu nyingine hakuna fedha zilizotengwa. (*Makofi*)

## **KAULI ZA MAWAZIRI**

### **Taarifa Kuhusu Upangaji Barabara Katika Hadhi Stahili**

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nikushukuru kwa kutoa uteguzi wa kitendawili kilichokuwepo ambacho kilikuwa kinasubiriwa sana na Bunge lako Tukufu. Nakushukuru sana kwa busara ambazo umetumia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, taarifa kuhusu upangaji barabara katika hadhi stahili, kwa mujibu wa kifungu Na.11(1) cha Sheria ya Barabara, Na.13 ya mwaka 2007, Waziri mwenye dhamana ya barabara amepewa mamlaka ya kupanga barabara katika hadhi stahili. Katika kutimiza wajibu huo na kwa kutumia kifungu Na. 48 cha Kanuni za Menejimenti ya Barabara, niliteua Kamati ya Kitaifa itakayonishauri katika kutekeleza wajibu huo niliopewa kisheria. Kazi mojawapo ya Kamati hiyo, ni kupitia na kuchambua maombi yanayohusu kupanga barabara katika hadhi stahili yanayowasilishwa kwangu kutoka Bodi za Barabara za Mikoa na kunishauri ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, sababu za barabara kupangwa katika hadhi mbalimbali, ni pamoa na kuainisha barabara za umma (*public roads*), kupanga umiliki wa barabara na madaraka ya kuzisimamia na kurahisisha utayarishaji wa mipango ya barabara kama vile upembusi usanifu na matengenezo ya barabara.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 12 cha Sheria ya Barabara, Na.13 ya mwaka 2007, barabara zimegawanywa katika makundi mawili ambayo ni barabara za Kitaifa na barabara za Wilaya. Barabara za Kitaifa zinaunganisha Barabara Kuu ama *truck roads* na Barabara za Mikoa. Barabara za Wilaya, zinaunganisha barabara za mkusanyo ama *collector roads* na barabara za mjazio ama *feeder roads* na barabara za vijiji ama mitaa pia zimo katika barabara hizi za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilipitia na kuchambua maombi yote kutoka Mikoa ambayo ina jumla ya barabara 252 zenye urefu wa kilomita 12,708.32 ambazo zimependekezwa na Bodi za Barabara za Mikoa ili zipangiwe hadhi stahili. Jumla ya barabara zilizopendekezwa ni 258.

Mheshimiwa Spika, utaratibu uliotumika, katika kupitia na kuchambua maombi ya kupanga barabara katika hadhi stahili, Kamati iliongozwa na vigezo vilivyomo katika Sheria ya Barabara Na. 13 ya 2007 na Kanuni za Menejimenti ya Barabara za mwaka 2009 ama *The Roads Management Regulations 2009*.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria na Kanuni hizo, Kamati ilitakiwa kutumia vigezo vinavyozingatia, moja, matumizi ya barabara ama *functional criteria* na mbili vigezo vya maeneo ya kiutawala ama *administrative criteria* katika kupanga barabara kwenye hadhi stahili. Kitaalamu vigezo vinavyozingatia matumizi ya barabara, *functional criteria* vinahusisha urahisi wa kusafiri *mobility* na ufikaji *accessibility*, wakati vigezo vinavyozingatia utawala *administrative criteria*, vinahusisha umiliki wa barabara *ownership* na madaraka ya kusimamia barabara, *responsibility*. Vigezo vilivyotumika, vimenyambulishwa katika Kanuni za Menejimenti ya Barabara ya mwaka 2009 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, ili barabara ipande hadhi na kuwa Barabara Kuu, ni lazima ikidhi mojawapo ya vigezo vifuatavyo:-

- (i) Iunganishe Makao Mkuu ya Mkoa na Makao Mkuu ya Mkoa mwingine;
- (ii) Iunganishe Makao Mkuu na Miji ama Bandari Kubwa muhimu zilizopo/iliyopo nje ya nchi yetu; na
- (iii) Iendeleze Barabara Kuu iliyopo na kuunganisha na Barabara Kuu nyingine.

Mheshimiwa Spika, pili, ili barabara iwe na hadhi ya Barabara ya Mkoa, ni lazima ikidhi mojawapo ya vigezo vifuatavyo:-

- (i) Iunganishe Makao Makuu ya Wilaya na Makao Makuu ya Wilaya na Makao Makuu ya Wilaya nyingine;
- (ii) Iunganishe Makao Mkuu ya Wilaya na Barabara Kuu;

- (iii) Iunganishe Makao Makuu ya Mko na Makao Makuu ya Wilaya;
- (iv) Iendeleze Barabara ya Mikoa iliyopo na kuunganisha na Barabara ya Mko nyingine au Barabara Kuu; na
- (v) Iunganishe Barabara Kuu mbili ziendazo sehemu mbili tofauti.

Mheshimiwa Spika, tatu, Ili barabara iwe na hadhi ya Barabara ya Wilaya, *collector ama feeder road*, ni lazima ikidhi mojawapo ya vigezo vifuatavyo:-

- (i) Iunganishe Makao Makuu ya Wilaya na Makao Makuu ya Tarafa.
- (ii) Iunganishe Makao Makuu ya Wilaya na Makao Makuu ya Kata;
- (iii) Iunganishe Makao Makuu ya Tarafa na Makao Makuu ya Tarafa nyingine;
- (iv) Iunganishe Makao Makuu ya Tarafa na Makao Makuu ya Kata; na
- (v) Barabara ianzie mjini na kwenda kuungana na Barabara Kuu au Barabara ya Mko.

Mheshimiwa Spika, nne, ili barabara iwe na hadhi ya mtaa/kijiji, ni lazima ikidhi mojawapo ya vigezo vifuatavyo:-

- (i) Iwe moja ya barabara mionganoni mwa barabara zilizomo ndani ya mji au kijiji; na
- (ii) Iunganishe barabara ya mtaa/kijiji na mtaa/kijiji kingine.

Mheshimiwa Spika, vigezo vya jumla kwa barabara zote ambavyo ni lazima vizingatiwe ni vifuatavyo:-

- (i) Isiwe barabara kitanzi ama *loop*; na
- (ii) Isiende sambamba na barabara yenye hadhi sawa na barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa mapendekezo yake, Kamati hii Kitaifa ilipitia na kuchambua maombi yote yaliyowasilishwa na Bodi za Barabara za Mikoa, barabara kwa barabara na kujiridhisha kuwa barabara zimepangwa katika hadhi stahili na kukidhi matakwa na vigezo vya Sheria.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi, kati ya maombi ya barabara 252, ni maombi 63 ndiyo yaliyokubaliwa. Maombi 50 ni kupandisha hadhi kutoka Barabara za Wilaya kuwa Barabara za Mikoa na maombi 11 ni ya kupandisha hadhi kutoka za

Barabara za Mikoa kuwa Barabara Kuu. Taarifa fupi ya matokeo ya uchambuzi ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara zilizopanda hadhi na kuwa Barabara Kuu, kati ya barabara 25 zenye urefu wa kilomita 2,987.03 zilizokuwa na hadhi ya Barabara za Mikoa zilizoombewa kupangiwa hadhi ya Barabara Kuu, ni barabara 11 zenye urefu wa kilomita 2,141.78, ndizo zimekidhi matakwa na vigezo vya Sheria.

Aidha, katika uchambuzi wa maombi, Kamati ilipendekeza kupandisha barabara mbili ambazo ni Omugakorongo-Kigarama-Murongo (km. 124) na Kigoma Port-Mwanga-Ujiji (km. 7.5) zenye jumla ya kilomita 135.5 kutoka hadhi ya Wilaya hadi Barabara Kuu, zimeruka moja kwa moja zimeenda *truck road*. Hivyo, jumla ya barabara 13 zenye urefu wa kilomita 2272.28 zimepandishwa hadhi kuwa Barabara Kuu na hizi zimeonyeshwa kwenye kiambatanisho namba moja kwenye taarifa hii ambayo Waheshimiwa Wabunge wamesambaziwa.

Mheshimiwa Spika, barabara zilizopanda au kushushwa na kuwa Barabara za Mikoa, kati ya barabara 223 zenye urefu wa kilomita 9,523.79 zilizokuwa na hadhi ya Wilaya ambazo ziliombwa kupangiwa hadhi ya Barabara za Mikoa, ni barabara 50 zenye urefu wa kilomita 3,304.7 ndizo zimekidhi matakwa ya vigezo vya Sheria.

Aidha, katika uchambuzi wa maombi, Kamati ilipendekeza kushusha hadhi barabara mbili zenye urefu wa kilomita 66.0 kutoka Barabara Kuu hadi kuwa Barabara za Mikoa. Barabara zilizoshushwa hadhi kutoka Barabara Kuu na kuwa za Mikoa, ni Nzega, Bokooba katika Mkoa wa Tabora na Bokooba - Kagongwa katika Mkoa wa Shinyanga. Hivyo jumla ya Barbara 52 zenye urefu wa kilomita 3,370.7 zimepangiwa hadhi ya Barabara za Mikoa na hii imenorodheshwa katika kiambatanisho namba mbili.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo haya ya Kamati, nimeyaridhia na hivyo barabara zilizoorodheshwa kwenye kiambatanisho namba moja na zile zilizoorodheshwa katika kiambatanisho namba mbili, zimepangwa katika hadhi stahili.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, zoezi la kuchambua na kupanga barabara katika hadhi stahili ni endelevu, Kamati ya Kitaifa ya Kupanga Barabara katika hadhi stahili, itaendelea kuyachambua maombi yote kadri yatakavyokuwa yanawasilishwa Wizarani.

Mheshimiwa Spika, Barabara zilizopangwa katika hadhi stahili kwa mwaka 2009, zimeorodheshwa katika kiambatanisho namba moja na namba mbili. Kwa ruhusa yako, ningependa nitaje majina ya barabara hizi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, hakuna haja, tumegawiwa, wacha wachambue, ni refu sana, si mmeona viambatanisho?

**WABUNGE:** Ndiyo!!!

**SPIKA:** Nadhani umefanya kazi nzuri, mpaka hapo inatosha, viambatanisho tutachambua wenyewe, ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mimi binafsi napenda nikushukuru sana kwa kazi hii kubwa na hususani kuweza kuipandisha hadhi barabara ya Kigoma - Tabora hadi Singida, ilikuwa inashangaza barabara hiyo inapita Mikoa yote hiyo eti ilikuwa inaitwa Barabara ya Mkoa, inapita Mikoa mitatu. Kwa hiyo, nashukuru sana, hii inadhihirisha sasa hatua ya kuiweka lami barabara hiyo zitaendelea kwa kasi. (*Makofi*)

Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kupandishwa hadhi barabara ya Tutuo - Mole - Ibumba - Urambo na kuwa ya Mkoa. Haya ni mambo mazuri sana ambayo nayaona humu, nawapongeza sana na wengine wote ambao barabara zenu zimepandishwa hadhi, nadhani wanashukuru pia. (*Makofi*)

**SPIKA:** Niseme tu kwamba ile orodha yote ya barabara itaingia kwenye *Hansard* ili kwa historia ziweze kufahamika zilizopo, ingawa Waziri hakuzisoma kwa majina, ahsante sana.

## **HOJA ZA SERIKALI**

### **Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2009/2010 - Wizara ya Katiba na Sheria.**

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala iliyochambua bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili, kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru kwa dhati, Kamati kwa kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2009/2010. Wizara yangu itazingatia na kutekeleza maoni na ushauri uliotolewa na Kamati kwa lengo la kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuungana na Wabunge wenzangu, kuwapongeza viongozi wetu wa Chama na Serikali kwa kazi nzuri waliyofanya tangu wateuliwe kushika nyadhifa mbalimbali. Kipekee nimpongeze Mheshimiwa Lolesia Bukwimba kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mbunge wa Jimbo la Busanda. Ushindi wake ni uthibitisho wa imani kubwa walijonayo wananchi kwa Chama cha Mapinduzi (CCM). Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Charles Mwera kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Tarime. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu, kumpongeza Bw. Oliver P.J. Mhaiki, aliyeeteuliwa na Mheshimiwa Rais hivi karibuni kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria. Namkaribisha Wizarani kwa moyo mkunjufu ili tuiendeleze sekta hii muhimu ya sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza Mawaziri waliotangulia kuwasilisha hoja zao, hususan Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Mashariki, Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Mbunge wa Jimbo la Kilosa, kwa hotuba zao ambazo zimeweka wazi sera, malengo, mwelekeo wa ujumla na mikakati ya Serikali katika kukuza uchumi wa Taifa na kuinua maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ufanisi wa mipango na kazi za Wizara yangu, zinategemea Sekta nyininge, hususan, Wizara na Idara za Serikali zinazojitegemea pamoja na Mahakama, napenda nichukue nafasi hii, kuwashukuru Mawaziri wote walioeleza mikakati ya Wizara zao katika kuleta maendeleo ya wananchi. Mikakati hiyo ni sehemu muhimu katika kufanikisha mipango na shughuli za Wizara yangu kwa ujumla, ikiwa ni pamoja na Maboresho ya Sekta ya Sheria hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge waliochangia hotuba za Waheshimiwa Mawaziri waliotangulia. Maoni ya Wabunge hao, yatasaidia kuboresha mipango ya Serikali katika kutekeleza ahadi zake ilizoahidi kwa wananchi wake ikiwa ni pamoja na zile za Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka 2008/2009, nchi yetu ilishuhudia matukio mbalimbali ya maafa ikiwa ni pamoja na ajali za vyombo vya usafiri katika sehemu mbalimbali za nchi pamoja na milipuko ya mabomu kwa wananchi waishio huko Mbagala na sehemu nyininge za Jiji la Dar es Salaam. Ajali hizo zilisababisha vifo na ulemavu kwa wananchi wengi, uharibifu wa majengo pamoja na mali. Kifo kwa ajali ya gari cha aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Biharamulo Magharibi (TLP), Hayati Phares Kabuye. Aidha, Bunge hili pia lilimpoteza aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Busanda, hayati Faustine Kabuzi Rwilomba (CCM). Kwa niaba ya wafanyakazi wenzangu wa Wizara ya Katiba na Sheria, naomba kutoa pole kwa wale walioathirika na maafa haya kwa njia moja au nyininge.

Pia napenda kutoa pole nyangi kwa BAKWATA na ndugu zangu Waislamu wote hususan wale wa Mkoa Lindi, kwa kumpoteza Kaimu Mufti, ambaye kuwa alikuwa Sheikh Mkuu wa Mkoa wetu wa Lindi, Sheikh Suleiman Gologosi aliyetangulia mbele za haki tarehe 27 Juni, 2009.

Aidha, natoa pole sana kwa Jumuiya ya Wasomi hapa nchini, kwa kuondokewa na Prof. Haroub Othman Miraji, ambaye kwangu binafsi alikuwa ni rafiki yangu wa karibu sana, aliyetutoka hapa tarehe 28 Juni, 2009 mwaka huu.

Kadhalika natoa salamu za pole kwa wananchi wa Wilaya ya Nachingwea na familia ya Hayati Abdurrahman Chowe, aliyekuwa Katibu wa CCM, Wilaya ya Nachingwea, aliyefariki tarehe 27 Juni, 2009.

Ninamwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu wote Mahali Pema Peponi. Amina. Kwa wale majeruhi wa ajali hizi, tunawaombea wapone haraka na wale waliopata ulemavu wa aina yoyote, tunawaombea ustahimilivu.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 ilielekeza Sekta ya Sheria itekeleze maeneo muhimu yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuzifanyia marekebisho Sheria za Mirathi na Sheria zote zinazoonekana kuwakandamiza wanawake. Kama nilivyolitaarifu Bunge lako Tukufu mwaka jana, juu ya marekebisho ya Sheria za Mirathi na zile zinazoonekana kuwakandamiza wanawake, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuzitazama upya Sheria hizi. Aidha, katika kuchambua mapendekezo yaliyofanyiwa utafiti na Tume ya Kurekebisha Sheria, Serikali imebaini kuwa Sheria ya Mirathi na Ndoa zinagusa maeneo muhimu sana mawili, yaani, eneo linalohusu mahusiano ya kijamii na kiutamaduni kwa kuzihusisha mila, desturi na imani za watu na kwa upande mwingine Sheria hizo zinahusisha maendeleo ya kijamii katika dunia ya sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa maeneo yote haya mawili, ni nyeti na muhimu, Serikali imeamua kukusanya maoni ya wananchi juu ya kuwepo mfumo unaofanana wa Sheria inayohusu Mirathi na Urihi kwa kuandaa mapendekezo ya Rasimu ya Sheria. Zoezi la kukamilisha Rasimu hii linaendelea kwa ukusanyaji wa maoni ya wananchi na taasisi mbalimbali. Ninatarajia kuwa zoezi hili litakamilika ndani ya mwaka wa fedha wa 2009/2010. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali inakusudia kufanya marekebisho ya Sheria zingine zinazowakandamiza wanawake kwa kuzingatia mapendekezo yaliyotolewa na Tume ya Kurekebisha Sheria pamoja na wadau mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Sheria zinazohusu makundi mengine ya kijamii hususan walemvu. Aidha, mchakato wa kuboresha Sheria hizi umekwishaanza kwa Sheria ya Kutetea Haki za Watu wenye Ulemavu, Sheria ya Kuhuisha Maslahi na Haki za Watoto na Sheria ya Makosa ya Kujamiihana. Rasimu za awali za Sheria hizi zimeandaliwa na kujadiliwa katika ngazi mbalimbali za kijamii na Serikali. Sheria Jumuishi ya Watoto na ile inayohuisha Sheria ya Makosa ya Kujamiihana, zitasomwa kwa mara ya kwanza katika kikao hiki cha Bunge na kujadiliwa katika kikao cha Bunge cha Novemba mwaka huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la kuundwa au kutokuundwa kwa Mahakama ya Kadhi ndani ya mfumo wa Mahakama ya Tanzania Bara kama eneo mojawapo lililoainishwa na Ilani yetu ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, nililitolea maelezo ya kutosha wakati nawasilisha hotuba yangu ya bajeti mwaka jana. Napenda sasa kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba taarifa ya mapendekezo ya utafiti uliofanywa na Tume ya Kurekebisha Sheria imepokelewa na Serikali na kufanyiwa kazi na Kamati ya Wataalamu wa Sheria

iliyoundwa na Serikali ambayo imetoa mapendekezo kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Hivi sasa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, imeanzisha mchakato wa kukusanya mawazo na maoni kutoka kwa viongozi wa Madhehebu yote za Dini ya Kiislamu kwa nia ya kuorodhesha misingi ya Dini ya Kiislamu yaani *Statements Islamic Principles* hususan ile inayohusu Sheria Binafsi (*Personal Law*) kwa madhumuni ya kuihuisha misingi hiyo katika Sheria za nchi yetu kwa kuzingatia Sheria yetu ya *The Islamic law (Restatement) Act*, Sura ya 375 ya mwaka 1964. Kimsingi, baada ya viongozi hawa wa dini kukubaliana kuhusu misingi hii basi Waziri wa Sheria atatoa tamko kuhusu misingi hiyo na baada ya hapo kwa mujibu wa Ibara ya 3 ya Sheria hii, matamko hayo yatakuwa ni Sheria zitakazotambuliwa na Mahakama zetu zote hapa nchini. Kwa namna hii, ninaamini kuwa zile haki zote binafsi za Waislamu chini ya *Personal Laws* zitakuwa zinalindwa na kusimamiwa na Serikali na kutekelezwa na Mahakama za nchi. Utaratibu huu utalinda haki za waumini wa Kiislamu bila kuathiri misingi ya Katiba ya nchi yetu. Aidha, utaratibu huu unatumika huko Afrika ya Kusini ambako kuna idadi kubwa ya waumini wa dini ya kiislamu bila matatizo yoyote. Kazi hii ya kuihuisha misingi ya Dini ya Kiislam itafanyika kwa umakini mkubwa na ni matarajio yangu kuwa kazi itakamilishwa katika mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, Serikali tayari ilishaanza kutekeleza mpango huu wa kuwa na Mahakama Kuu katika kila Mkoa kwa lengo la kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi. Kama inavyofahamika ujenzi wa Mahakama Kuu umekamilika hususan Mikoa ya Iringa na Rukwa. Ujenzi wa Mahakama Kuu Kanda ya Shinyanga umekwishaanza na upo katika hatua za mwisho kukamilika. Aidha, Ujenzi wa Mahakama Kuu katika Mikoa ya Mara, Singida na Mtwara unatarajiwa kuanza katika mwaka huu wa fedha, kuitia Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria na ule mradi endelevu wa kuboresha Mahakama ambao unagharamiwa na Serikali yetu. Taratibu za kumtafuta Mtaalamu Mshauri kwa miradi hii zinakamilishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na utekelezaji wa mpango wa kuanzisha Kanda za Mahakama Kuu kwa kila Mkoa, Serikali tayari imejenga Mahakama tano (5) za Mwanzo huko Utmini- Singida, Kalenga- Iringa, Bwasi-Musoma, Old Korogwe-Korogwe, Kerege-Bagamoyo na Babati mjini. Aidha, ujenzi wa Mahakama mbili (2) za Lugoba-Bagamoyo na Karabagaine – Bukoba unaendelea. Ukarabati wa Mahakama ya Mwanzo Mwandiga-Kigoma na Mabamba-Kibondo unaendelea. Mahakama kwa kushirikiana na wananchi, imeweza kukarabati Mahakama za Mwanzo Gallapo na Magugu, Lembeni na Ikungi- Singida.

Mheshimiwa Spika, chini ya mradi endelevu wa kuboresha Mahakama zetu, upanuzi wa ofisi katika jengo la Mahakama ya Rufani, Dar es Salaam pamoja na ujenzi wa Mahakama ya Wilaya Mafia na Mahakama ya Hakimu Mkazi Manyara, unaendelea na unatarajiwa kumalizika mwaka wa fedha wa 2009/2010. Kadhalika, ukarabati wa Mahakama za Mwanzo tano (5) za Magugu- Babati, Nyakumbu – Bunda, Kukirango- Musoma, Mwandiga- Kigoma na Tabora mjini - Tabora, umefanyika. Ukarabati wa Mahakama za Mwanzo sita (6) za Tanga mjini - Tanga, Ikungi – Singida, Kitaya-

Mtwara, Lisekesekere – Masasi na Lembeni – Mwanga na Mambamba - Kibondo unaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka ujao wa fedha Mahakama chini ya Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria, itajenga Mahakama za Mwanzo takriban 20 ambazo ni Kawe, Kigamboni, Kibaha Maili moja, Kisarawe, Gairo, Mwanga, Usevya, Mkomazi, Lukuledi, Simanjiro, Makuyuni, Mafinga, Makongorosi, Bunda, Sangabuye kule Mwanza, Uliyankulu, Songea na Mtowisa kule Sumbawanga. Aidha, chini ya mpango wa kudumu wa kuboresha Mahakama, Serikali itajenga Mahakama za Mwanzo za Machame na Katesh. Aidha Serikali itaanza ujenzi wa Mahakama Kuu kule Singida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu, kuwashukuru wananchi wote waliojenga Mahakama kwa nguvu zao, hawa ni wananchi wa Tingi-Mbinga, Mbondo- Nachingwea, Kirando- Nkasi, Sopa na Laela- Sumbawanga na Iguguno-Iramba. Aidha, ukarabati wa Mahakama za Msanzi - Sumbawanga na Mkingo – Songea, umekamilika. Pia napenda nimshukuru kwa dhati ndugu yangu Mheshimiwa Bernard Kamilius Membe, Mbunge wa Jimbo la Mtama na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa kujitolea kujenga Mahakama ya Mwanzo, pale Rondo-Mkoani Lindi pamoja na Uongozi wa Kiwanda cha Sukari Mtibwa kwa kujitolea kujenga Mahakama ya Mwanzo, pale Mtibwa. (*Makofi*)

Mheshimwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi katika Mahakama zote hapa nchini kwa kununua vifaa mbalimbali vya ofisi na vyombo vya usafiri. Jumla ya kompyuta mpakato (*Laptop*) 116 na kompyuta za mezani (*Desktop*) 97 zimenunuliwa na kusambazwa. Magari 60 kati ya hayo, magari 30 aina ya Suzuki *Grand Vitara* yamenunuliwa na Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria ambayo yamesambazwa katika Mahakama Kuu na Mahakama za Wilaya ili kuimarisha ukaguzi na usimamizi wa shughuli za Mahakama. Katika mwaka huu wa fedha, pikipiki 75 zitanunuliwa na kusambazwa katika Mahakama za Mwanzo zilizopo na zinazojengwa zikiwemo zile za Ludewa na kwingine. Aidha, nyumba mbili (2) za Mahakimu katika Mahakama ya Wilaya ya Kongwa na Mahakama ya Mwanzo Kibutuka – Liwale, zimejengwa. Ujenzi wa nyumba ya Hakimu wa Wilaya ya Mafia unaendelea. Serikali katika mwaka huu wa fedha inatarajia kujenga nyumba kumi (10) za Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo katika maeneo ya vijiji ili kupunguza tatizo la ukosefu wa makazi kwa Mahakimu.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kutenganisha jukumu la upelelezi na Mashtaka litaondoa tatizo la haki kucheleva kutendeka kwa kesi kuchukua muda mrefu Mahakamani kwa sababu ya muda mrefu unaotumika katika upelelezi. Utaratibu huu mpya ulianzishwa rasmi kwa Sheria ya “*National Prosecution Service Act*”, 2008 iliyoanza kutumika tarehe 9 Juni, 2008. Chini ya utaratibu huu, Mawakili wa Serikali watahusika na uendeshaji wa kesi za Makosa ya Jinai katika ngazi za Mahakama za Wilaya na Mahakama za Mahakimu Wakazi.

Mheshimiwa Spika, hatua kadhaa zimeanza kuchukuliwa ikiwa ni sehemu ya utekelezaji, uelimishaji na uenezaji wa utaratibu huu katika Wilaya zote za Tanzania

Bara. Hatua hizi ni pamoja na kuajiri Mawakili wa Serikali 47, kwa mwaka 2008/2009 na kuwasambaza katika Mikoa ya awamu ya kwanza, kukamilisha miongozo ya kisheria ya utekelezaji wa mpango huu (*Prosecution General Instructions*), kufungua Ofisi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika Wilaya na Mikoa ya awamu ya kwanza Arusha, Dar- Es Salaam, Mwanza, Ruvuma, Shinyanga na Tanga pamoja na kutayarisha Mpango wa Mafunzo kwa ajili ya Mawakili wa Serikali. Ofisi zilizofunguliwa zimeanza kukarabatiwa na kupatiwa vifaa mbalimbali kama vile, samani za ofisi, kompyuta na magari. Aidha uendashaji wa mashitaka katika Mahakama za Hakimu Mkazi na Mahakama za Wilaya umeanza kutekelezwa katika maeneo ya Kisutu na Ilala kwa jiji la Dar-es- Salaam, Kilimanjaro, Arusha, Mwanza, Tabora, Mbeya na Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi hiki cha mwaka mmoja toka tuanze utaratibu huu, tumeona kuwa, idadi ya wafungwa na mahabusu imepungua kutoka wastani wa takribani 45,000 kwa miaka mitatu iliyopita hadi 38,000 kufikia mwezi Mei mwaka huu. Ni matumaini yangu kuwa tufikapo Desemba mwaka huu, idadi hii itapungua hadi kufikia 33,000. Naamini kuwa, pamoja na mambo mengine, kufikia hapa ni matunda ya utaratibu huu.

Mheshimiwa Spika, katika Kuziainisha, Kuziimarisha na Kuzioanisha Sheria zinazohusiana na Mapambano dhidi ya Rushwa, Wizara yangu imefanya rejea ya Sheria mbalimbali zinazohusiana na Sheria ya Kupambana na Rushwa. Mojawapo ya Sheria hizo, ni Sheria ya Usafirishaji wa Fedha Haramu, Sheria ya Uchaguzi, Sheria ya Mawakili, Sheria ya Vyama vya Siasa pamoja na kutayarishwa kwa Sheria ya wanaotoa msaada wa Kisheria kwa Wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2008/2009, utekelezaji wa Programu ya Mpango wa Uboreshaji wa Mfumo wa Sheria hapa nchini, umekuwa ukihusisha zaidi ya taasisi kumi na tano (15) zikiwemo Wizara saba (7) pamoja na Idara na Taasisi za Serikali na zisizo za Kiserikali zinazotoa huduma za Kisheria. Chini ya mpango huu, Mahakama za Mwanzo tatu (3) za Bereko- Kondoa, Kilolo- Iringa na Basotu- Hanang' zimejengwa, na nne (4) za Shelui – Iramba, Ilolangulu – Tabora, Kirua Vunjo – Moshi, na Ikama Tukuyu, zimekarabatiwa.

Mheshimiwa Spika, chini ya mpango huu, Jeshi la Magereza limewezeshwa kuboresha mfumo wa usafirishaji na usindikizaji wa Mahabusu na wafungwa kwenda kusikiliza kesi zao kwa kununuliwa mabasi matano (5) ya kisasa. Pia, Jeshi la Polisi limepeewa kiasi cha shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Askari. Kadhalika, mfumo wa upelelezi umeimarishwa kwa kuwapatia Polisi vitendea kazi na vyombo vya usafiri na mafunzo ya muda mfupi yaliyohusisha Wakuu wa Vituo vya Wilaya juu ya mbinu za kisasa za upelelezi chini ya mchakato wa kutenganisha upelelezi na mashtaka.

Mheshimiwa Spika, Programu hii katika kipindi cha mwaka 2009/10 imelenga kufanya mambo yafuatayo:-

- (i) Kuimarisha huduma za utoaji haki kwa kujenga Mahakama za Mwanzo 20; kama nilivyokwishazitaja hapo juu;
  - (ii) Kununua mabasi mengine matano 5 kwa ajili ya kusafirisha mahabusu pamoja na kuimarisha shughuli za usimamizi wa mashtaka nchini;
  - (iii) Kuboresha Sheria mbalimbali zinazolenga kuinua uchumi wa nchi pamoja na kuwapatia haki sawa wananchi wote;
  - (iv) Kuimarisha mabaraza ya kata kwa kuwapatia mafunzo wajumbe wote wa mabaraza;
- (v) Kuimarisha utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria kupitia Mashirika yasiyo ya kiserikali na kutoa mafunzo kwa watu wanaotoa msaada wa Kisheria kwa wananchi;
- (vi) Kukarabati Mahabusu ya watoto iliyoko katika Jiji la Dar-es Salaam;
- (vii) Kuzipatia mahabusu zilizoko Moshi na Arusha samani na vifaa vya ofisi, na
- (viii) Kuwapa mafunzo mbalimbali watalaam wanaoratibu Mpango wa Maboresho ya Sekta ya Sheria nchini.

Mheshimiwa Spika, Kuweka Mfumo wa kuwasaidia wananchi wasiojiweza kupata msaada wa Kisheria. Mabadiliko ya muundo mpya wa Wizara yaliyofanywa na Mheshimiwa Rais mwaka jana mwezi Aprili, 2008, yatawezesha Wizara kuanza kutoa msaada wa kisheria kwa wananchi wanaohitaji baada ya Idara mpya ndani ya Wizara kuanzishwa ili ishughulikie malalamiko ya kisheria kutoka kwa wananchi na taasisi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Kuweka Mfumo utakaowezesha kutumika kwa Wanasheria wenye Shahada ya kwanza ya Sheria katika Mahakama za Mwanzo. Ili kukabiliana na upungufu wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na pia kuimarisha dhana nzima ya uwakilishi Mahakamani, Wizara yangu kwa kushirikiana na Mahakama imeandaa mkakati wa kuwatumia wanasheria wanaohitimu Shahada ya kwanza ya Sheria katika Mahakama hizi. Mapendekezo ya muundo mpya wa kutekeleza mkakati huo yamewasilishwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa hatua zaidi. Utaratibu huu utaifanya Mahakama ya Mwanzo kuwa ndiyo ngazi ya kwanza katika kazi ya Uhakimu. Ni imani yangu kuwa, utaratibu huu utakapoanza, Mawakili wa Kujitegemea na Mawakili wa Serikali, wataweza kufanya kazi katika Mahakama hizi na hivyo basi kuimarisha uwakilishi wa wanachi katika vyombo vya utoaji haki nchini na kuwapatia huduma boza zaidi.

Mheshimiwa Spika, atika Kukuza, Kulinda na Kuhifadhi Haki za Binadamu na Utawala Bora katika Jamii, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, kwa kushirikiana na Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa kunakuwepo na uratibu na usimamizi mzuri zaidi wa kupokea kero za wananchi na kuhakikisha kuwa, zinapatiwa ufumbuzi wa haraka kwa kutumia Mamlaka zinazohusika. Tume imeendelea kuharakisha ushughulikiaji wa malalamiko yaliyopo na yanayopokelewa. Katika mwaka 2008/2009, ilipokea malalamiko mapya 1,746 hadi mwezi Juni, 2009 ikilinganishwa na malalamiko 2,660 yaliyopokelewa mwaka 2007/2008.

Aidha, kati ya malalamiko hayo mapya yaliyopokelewa, malalamiko 657 yameshughulikiwa na kuhitimishwa. Tangu kuanzishwa kwa Tume jumla ya malalamiko 24,415 yaliishapokelewa. Kati ya malalamiko hayo, malalamiko 16,898 yalihitimishwa na 7,377 yanaendelea kushughulikiwa. Aidha, utaratibu wa kutumia kompyuta katika kusajili na kutumia maafisa uchunguzi kufuutilia malalamiko mbalimbali utaanza kutumika mwaka wa fedha 2009/10. Utaratibu huu unatarajiwa kurahisisha na kuharakisha ufuutiliaji wa malalamiko na kuyapatia ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza mahitaji ya kupunguza misongamano Magerezani pamoja na kuhakikisha kwamba haki za mahabusu na wafungwa zinakuzwa na kulindwa, Tume imeendelea kufanya ukaguzi wa Magereza nchini na kutoa ushauri kwa mamlaka husika. Katika mwaka 2008/09 jumla ya Magereza 75 katika Wilaya 66 za Tanzania Bara, yalitembelewa na kukaguliwa na taarifa ya awali yenye ushauri imefikishwa kwa mamlaka husika. Hatua za marekebisho zimeanza kuchukuliwa katika kurekebisha mapungufu yaliyoonekana.

Mheshimiwa Spika, kadhalika, katika kuondoa kero za migogoro ya ardhi, hususan, kwa wakulima na wafugaji, Tume ilifanikiwa kufuutilia mgogoro kati ya wananchi na Mwekezaji mwindaji wa wilaya ya Ulanga mkoani Morogoro. Mgogoro huo unaendelea kusuluhishwa na tayari umefikia katika hatua nzuri ya makubaliano. Aidha, Tume imefanya utafiti Zanzibar juu ya usikilizaji hadharani wa vitendo vya ukatili dhidi ya watoto na taarifa ya utafiti huu inakamilishwa. Tume itafanya tafiti tatu za kina zinazohusu watu wenye ulemavu wa akili, mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi, na mimba za utotonii kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari kwa mwaka wa fedha 2009/10 kwa nia ya kupata ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, Tume imekuwa ikitoa elimu kwa wananchi kuhusu haki za binadamu na misingi ya utawala bora katika ngazi za vijiji ili kupanua uelewa wao zaidi juu ya haki zao. Jumla ya wilaya 65 za Tanzania Bara na wilaya moja ya Tanzania Zanzibar zilitembelewa na Tume kwa lengo la kuwaelimisha wananchi na watendaji mbalimbali wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kwamba elimu ya haki za binadamu na utawala bora inaenea sehemu nyingi zaidi nchini, vipeperushi 10,000, mabango 863, vijitabu 8,500 vya Mwananchi Tambua Haki Yako na nakala 3,000 za Jarida la Sauti ya Haki viligawiwa. Pia, Tume ilifanikiwa kuratibu maadhisho ya kitaifa ya Haki za

Binadamu kwa mara ya kwanza hapa nchini. Maadhimisho haya yalifanyika tarehe 10 Desemba, 2008 katika viwanja vya Mnazi Mmoja Dar – es - Salaam. Haya yalifanyika sambamba na adhimisho la miaka sitini ya Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu lililotolewa Duniani kote na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mnamo tarehe 10 Desemba, 1948.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka 2008/2009, Serikali katika kutekeleza matakwa ya Mikataba ya Kimataifa inayohusu Haki za Binadamu ambayo iliridhiwa na Bunge lako Tukufu, kwanza mwezi Machi 2009, Wizara yangu ilihudhuria kikao cha Baraza la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu kilichofanyika Geneva-Uswisi, Pili, mwezi Mei 2009, Wizara yangu iliongoza ujumbe wa Tanzania katika kikao cha Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, huko Banjul Gambia. Lengo la kuhudhuria vikao hivi, ni kuelezea namna ambavyo Serikali yetu inatekeleza mikataba mbalimbali ya Kimataifa inayohusu haki za Binadamu katika kukuza na kulinda haki hizo, kuitetea nchi yetu pale tuhuma za ukiukwaji wa haki za binadamu zinapotolewa dhidi yake na kujifunza uzoefu wa nchi nyingine duniani zinavyotekeliza matakwa ya mikataba hii.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekamilisha na kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa “*International Covenant on Civil and Political Rights*” (ICCPR). Taarifa hii itajadiliwa na Kamati ya Haki za Binadamu (Human Rights Committee) mjini Geneva-Uswisi tarehe 13-14 Julai, 2009.

Mheshimiwa Spika, vile vile, maandalizi ya taarifa ya utekelezaji wa matakwa ya mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni “*International Covenant on Economic, Social and Cultural Rights*” (ICESCR) yamekamilika.

Mheshimiwa Spika, hali ya sekta ya sheria na changamoto zilizopo. Ingawa Wizara yangu imejitahidi kutekeleza dira yetu na majukumu yake kwa ufanisi mkubwa, bado yapo mambo mengi ambayo hayajapata ufumbuzi wa uhakika. Vyombo vyetu vya utoaji haki vinajitahidi lakini havijafikia kiwango cha kuwa kimbilio la wote wanaotafuta haki ambalo ndilo lengo kuu la Dira yetu.

Aidha, mambo yanayoashiria kutofikiwa kwa kiwango hicho ni pamoja na kuwepo kwa mlundikano wa kesi za jinai na za madai, kutokana na ucheleweshaji wa kutatua migogoro, uwezo mdogo wa wananchi walio wengi kuvifikasi vyombo vya kutoa haki na huduma za kisheria, kuwepo kwa matukio ya rushwa na tabia zisizozingatia matakwa ya taaluma kwa baadhi ya watumishi katika Sekta ya Sheria. Mfumo uliopo wa sheria kwa kiasi fulani ni wa kizamani na una taratibu na kanuni zilizopitwa na wakati na ambazo hazikidhi mabadiliko ya kasi katika jamii, kisiasa, kiuchumi na kiteknolojia. Aidha, pamoja na Serikali kujitahidi kuajiri Majaji, Mahakimu, Mawakili pamoja na watendaji wengine katika Sekta ya Sheria, bado upungufu wa watumishi katika sekta hii umeendelea kuwa tatizo sugu.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine zinazokabili wizara yangu ni uelewa mdogo wa wananchi kuhusu mfumo uliopo wa Sheria na Mahakama nchini, uhaba wa ujuzi, utaalamu na kukosekana kwa hamasa ya kazi kwa watumishi wa Sekta ya Sheria nchini, mazingira ya kazi yasiyoridhisha kwa watumishi wengi katika Sekta ya sheria yanayotokana na ujira duni, Uhaba wa vitendea kazi muhimu kama vile, vitabu vyatia sheria, usafiri, nk.

Mheshimiwa Spika, changamoto zilizoainishwa kimsingi zinatokana na ufinyu wa bajeti inayotengwa kwa ajili ya Wizara yangu kila mwaka wa fedha. Mara nyingi kiasi kinachotolewa huwa hakilingani na mahitaji halisi ya Wizara na hata kiasi kidogo kinachotengwa hakitolewi kwa wakati na wala hikitolewi chote, jambo ambalo linaathiri sana Mpango Kazi wa Wizara yangu. Hata hivyo, kwa kulitambua tatizo hili, Serikali imekuwa ikiongeza kiwango cha bajeti kila mwaka kwa kadri uwemo wake wa kifedha unavyoruhusu. Nashukuru sana kwa hili na kuendelea kuwataka wenzangu watambue umuhimu wa sekta hii katika maendeleo ya jamii yetu.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka 2008/09 na malengo ya mwaka 2009/10. Wizara yangu imeendelea kutekeleza ahadi za Chama Tawala zilizomo katika Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2005. Ilani hiyo inaelekeza pamoja na mambo mengine, umuhimu wa kuchukuliwa kwa hatua mbalimbali ili kuiboresha Sekta ya Sheria kwa nia ya kutoa huduma bora zaidi kwa Jamii.

Aidha, Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa huduma za Kisekta zinaimarishwa na kuendelezwa kwa kuzingatia malengo ya kitaifa ambayo ni pamoja na utekelezaji wa maudhui ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, MKUKUTA, Utekelezaji wa Malengo ya Milenia na Maelekezo ya Hotuba za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete.

Hivyo, Wizara katika kutekeleza malengo yake kwa mwaka 2008/09 imezingatia sana ahadi za serikali Bungeni, maswali mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge, hoja binafsi na kauli mbalimbali za Serikali zilizohusu Sekta ya Sheria. Aidha, katika kufanikisha malengo ya utekelezaji, Wizara pia imezingatia ahadi za viongozi wa kitaifa wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu, na hotuba mbalimbali walizozitoa.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa mwaka huu wa fedha imepanga kutekeleza Malengo ya ujumla ya Uratibu wa Mikataba mbalimbali nchini, Uboreshaji wa shughuli za usajili, Ufilisi na Udhamini, Kuongeza ufanisi katika uendeshaji wa Mashauri nchini, Uimarishaji wa utoaji ushauri wa kisheria nchini, Utafiti na mapitio ya sheria mbalimbali kwa madhumuni ya kuziboresha, kuendelea na mchakato wa utenganishaji wa shughuli za upelelezi na uendeshaji wa Mashtaka, Utekelezaji wa Programu ya Mpango wa Uboreshaji wa Mfumo wa Sheria, Uimarishaji wa Mfumo wa kuwasaidia wananchi kupata msaada wa Kisheria, pamoja na Ukuzaji, Ulindaji na Uhifadhi wa Haki za Binadamu na Utawala bora.

Mheshimiwa Spika, Kuratibu Mikataba mbalimbali Nchini. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefanya jitihada za kutoa mafunzo kwa Mawakili wa

Serikali katika eneo la kujadili na kuandaa Mikataba ya kitaifa na kimataifa, hususan, ile ya kibiashara baina ya Mashirika ya Kimataifa na Serikali, pamoja na Mikataba ya ushirikiano kati ya nchi na nchi zingine, zimeendelea.

Aidha, katika kipindi cha mwaka 2008/09 jumla ya Mawakili watano (5) wamepatiwa masomo ya muda mfupi ili kuwajengea uwezo wa kujadili, kuandika na kuhakiki Mikataba. Pia katika mwaka huu wa fedha Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*) limeahidi kutoa Dola za Kimarekani 800,000 kwa ajili ya kutuwezesha kuwapa Mawakili wa Serikali wengi zaidi mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kujadili, kuandika na kuhakiki Mikataba. Mradi huu utahusisha pia wataalam mbalimbali wakiwemo Wahandisi, Wachumi na Wahasibu na Kada nyingine za taaluma kutoka Sekta mbalimbali ambao wanahusika katika majadiliano, uandaaji na usimamizi wa Mikataba. Mradi huu wa “*Capacity Building for Contract Negotiations and Contract Management*” utatekelezwa kwa muda wa mwaka mmoja na kuna uwezekano wa kuongezeka kwa muda huo kulingana na upatikanaji wa fedha zaidi kutoka kwa Wahisani wengine.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kuijengea Uwezo Serikali Kupambana na Rushwa, Serikali kwa kushirikiana na shirika la misaada ya Kimataifa la Uingereza (*DFID*), imeanzisha mradi wa mapambano dhidi ya rushwa kubwa kwa kuzijengea uwezo wa kitaaluma na vifaa taasisi zote za Kitaifa zinazohusika na mapambano dhidi ya rushwa (*Tackling Corruption Project – TCP*). Taasisi hizo ni Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka, Jeshi la Polisi, TAKUKURU, Sekretariati ya Maadili ya Viongozi, Mamlaka ya Kudhibiti Manunuzi katika Sekta ya Umma (*PPRA*) na “*Financial Intelligence Unit*”

Mheshimiwa Spika, chini ya mradi huu Wizara yangu imeandaa Mkakati wa Mawasiliano (*Information Strategy*), ili kujenga uwezo wa Wizara kukabiliana na rushwa na hasa uwekaji wa mifumo imara ya kuwezesha kukamilisha kesi kwa kufuatilia na kusimamia kesi hizo (*Case Docket Management System*). Katika hatua ya awali vifaa vimenunuliwa vikiwemo vitendea kazi kama vile, kompyuta, magari, vitabu vy'a Sheria ili visaidie katika utendaji kazi.

Aidha, katika mwaka ujao wa fedha tutaendeleza mazungumzo na wenzetu wa Sweden na Uingereza, ambayo tayari tumeyaanza kwa nia ya kupata misaada ili tujenge uwezo wa kupambana na changammoto mpya za uharamia katika bahari zetu.

Mheshimiwa Spika, Kutayarisha Miswada ya Sheria na Hati mbalimbali za Serikali. Katika mwaka 2008/2009, miswada 29 imeandaliwa na miswada 22 ilipitishwa na Bunge lako tukufu na kutiwa saini na Mheshimiwa Rais, kuwa Sheria. Aidha, Sheria 53 zilifanyiwa marekebisho, sheria ndogo 500 pamoja na Hati za Serikali, zimeandikwa au kuhakikiwa na baadae kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Spika, kutenganisha shughuli za Wizara na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, ameteuliwa na Ofisi zake zipo katika jengo lililokuwa linatumwiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais. Aidha,

kutenganishwa kwa majukumu ya Katibu Mkuu wa Wizara na yale ya Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kutawezesha wananchi na jamii kwa ujumla kunufaika zaidi na msaada wa ushauri wa kisheria utakaokuwa unatolewa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa wakati. Wizara itashughulikia zaidi masuala ya utungaji na usimamizi wa sera na uongozi na usimamizi wa sekta nzima ya sheria nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), imeendelea kuboresha huduma za Usajili, Ufilisi na Udhamini kwa kuboresha mfumo wa mawasiliano (*Management information System*) ambao utawezesha ukusanyaji wa kumbukumbu zote za Wakala kwa kuunganisha Wilaya zote za Tanzania Bara. Mfumo huu utalinufaisha Taifa kwa kutoa takwimu sahihi kwa ajili ya mipango ya maendeleo ya nchi. Maelezo ya kina kuhusu uboreshaji wa huduma hizi yameanishwa vyema katika Aya ya 39, 40 na 41 ya hotuba yangu. Mpango wa mfumo huu umeanza kutekelezwa katika Makao Makuu ya Wakala pamoja na Wilaya za Temeke, Kinondoni, Kibaha na Dodoma. Wakala pia umepanga kuunganishwa katika mfumo huu kwa, Jiji la Tanga, Jiji la Mwanza, Manispaa ya Arusha, na Manispaa ya Moshi katika mwaka huu wa fedha.

Aidha, Wakala umeendelea kuimarisha mahusiano ya wadau wanaofanya kazi za Wakala hususan, shughuli za Usajili na Mirathi katika ngazi za Wilaya kwa kuwapa mafunzo Makatibu Tawala wa Wilaya, Waganga Wakuu wa Wilaya, Wasaidizi Usajili, Watumishi katika Vituo vya tiba, Maafisa Tarafa pamoja na Maafisa Watendaji wa Kata, Serikali za Mitaa na za Vijiji katika wilaya 13, za Hanang' Kigoma vijijini, Nachingwea, Kasulu, Kibondo, Ngara, Ukerewe, Jiji la Tanga, Manispaa ya Arusha, Siha, Mpanda, na sasa Nyamagana na Illemela za jiji la Mwanza.

Mheshimiwa Spika, katika utoaji wa huduma za usajili, ufilisi na udhamini, taratibu mbalimbali zinazohusu upatikanaji wa huduma hizi zimefanyiwa maboresho. Sheria ya Uandikishaji wa Vizazi na Vifo, Sura ya 108, imefanyiwa marekebisho na kupitishwa na Bunge lako Tukufu Januari, 2009 kwa kumpatia mamlaka ya kisheria Msajili Mkuu kufanya uteuzi wa Wasajili wa Vizazi na Vifo badala ya Waziri mwenye dhamana ya Sheria. Maboresho haya yatamwezesha Msajili Mkuu kuteua Wasajili Wasaidizi katika ngazi za Tarafa na Kata na hivyo kusogezza huduma karibu zaidi na wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, idadi ya vizazi 938,775, vifo 105,482, ndoa 15,345, talaka 73, watoto wa kuasili 39 na miunganisho ya wadhamini 247 vilisajiliwa. Ongezeko la idadi hii limetokana na huduma za usajili, ufilisi na udhamini kufanywa kwa njia ya kampeni ambapo mwananchi hufuatwa alipo ili kupatiwa huduma badala ya utaratibu wa zamani wa wananchi kufuata huduma hii katika Ofisi za Wilaya. Aidha, mirathi kumi na moja (11) hapa Dar es Salaam imeshughulikiwa na kufungwa kwa kuwagawia warithi stahili zao. Huduma ya kutayarisha na kuhifadhi wosia ilianzishwa tangu mwezi Juni, 2008. Huduma hii inasaidia sana kupunguza migogoro katika mirathi kwa kuwa inatarajiwa kuwa mhusika ataweka haki za warithi wake bayana, hususan, watoto wake, watoto wa kuasili na wajane. Hadi sasa jumla ya hati 39 za wosia zimehifadhiwa na juhudzi za kuwaelimisha wananchi zinaendelea kufanywa na

Wakala. Ninawashauri Waheshimiwa wabunge waitumie huduma hii vilivyo na wawahamashe wananchi waitumie huduma hii kwa wingi.

.Mheshimiwa Spika, Hali ya kifedha ya wakala imekuwa ikiimarika mwaka hadi mwaka. Katika mwaka wa fedha 2008/09, wakala umefanikiwa kukusanya maduhuli ya Serikali ya shilingi 1,921,396,837 na mwaka huu wa fedha kiasi cha shilingi 2,211,000,000 kinatarajiwa kukusanya.

Mheshimiwa Spika, uendeshaji wa mashauri Nchini. Katika mwaka wa fedha 2008/09, Serikali imewezesha Mahakama kuimarisha uwezo wake wa kuendesha na kusukuma kesi mbalimbali ili kukabiliana na wingi wa kesi zinazoletwa Mahakamani. Jumla ya vikao kumi na tatu (13) vya Mahakama ya Rufani vilifanyika kati ya vikao 16 vilivyopangwa kwa mwaka uliopita. Katika vikao hivyo, jumla ya maombi na rufaa mia tano sitini (560) yalisikilizwa na kumalizika kati ya mashauri 2,659 yaliyokuwepo. Mahakama Kuu, imefanya vikao mia moja sitini (160) kati ya 208 vilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, katika Mahakama Kuu kulikuwa na jumla ya mashauri 18,805, kati ya hayo, 10,791 ni mapya. Mashauri 9,590 yalisikilizwa na kumalizwa na kubaki mashauri 9,215. Katika Mahakama za mikoa 23 na zile za wilaya 100, kulikuwa na jumla ya mashauri 61,237 na kati ya hayo 46, 282 ni mapya. Mashauri 42,725 yalisikilizwa na kumalizwa na kubaki mashauri 18,512.

Mheshimiwa Spika, Mahakama za Mwanzo zimesikiliza jumla ya mashauri 151,200 kati ya mashauri 213,239 yaliyokuwepo na kubaki mashauri 62,039. Vile vile vikao viwili (2) hadi vitatu (3) vya kusukuma mashauri vimefanyika katika kila kanda kati ya vikao vinne (4) vilivyopangwa kufanyika kwa mwaka uliopita. Kamati za Kusukuma Kesi zimesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza mlundikano wa mashauri ambayo yalikuwa yakikwama. Hali hii ya kuanza kupungua kwa mlundikano wa mashauri Mahakamani imechangiwa na ongezeko la idadi ya Majaji wanaoteuliwa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2009/10, Mahakama inatarajia kuanza kutumia mfumo wa kurekodi mwenendo wa mashauri Mahakamani, hususan, katika Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani Dar-es Salaam, kuitia mpango wa kuboresha huduma zake (*Modernisation of Judiciary Project*), chini ya uhisani wa “*Investment Climate Facility for Africa*”.

Mheshimiwa Spika, pia Mahakama inategemea kuanzisha mfumo wa kusimamia mashauri kwa kutumia tovuti ya Mahakama ili kuboresha mfumo wa kupeana taarifa na utafiti ndani ya Mahakama, chini ya udhamini wa mradi wa MKUMBITA. Mifumo hii mipyä inatarajiwa kurahisisha usimamizi wa mashauri na kuharakisha ukisikilizaji wa mashauri na hivyo kupunguza mlundikano wa kesi.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itaendelea kutekeleza majukumu yake ya kuiwakilisha Serikali katika kesi za Madai kwa kuitetea

Mahakamani pale iliposhtakiwa au kushtaki. Kadhalika, vikao vya kuendesha kesi za makosa ya Jinai katika kanda zote 14 vitafanyika ikiwa ni pamoja na kushughulikia matatizo ya msongamano wa Mahabusu na Wafungwa Magerezani. Mawakili Wafawidhi kwa kushirikiana na Wakuu wa upelelezi wa mikoa na wilaya, Majaji Wafawidhi na Mahakimu Wafawidhi wataendelea kutembelea Magereza yaliyoko hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kupunguza tatizo la matendo maovu dhidi ya watu wenye ulemavu wa ngozi, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali immeanzisha mchakato wa kusimamia mashauri yote yanayohusu suala hili. Hadi mwishoni mwa mwezi Mei, 2009 mashauri 23 yalishapokelewa, na kati ya hayo 6 yameshapelekwa Mahakamani, na 5 yameanza kusikilizwa na 17 yanaendelea kufanyiwa upelelezi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Divisheni ya Biashara ya Mahakama Kuu, ilipokea jumla ya kesi 117 kati ya hizo, kesi 109 zimesikilizwa sawa na asilimia tisini na tatu (93%) ya kesi zilizofunguliwa. Hii ni pamoja na mashauri 4 yaliyofunguliwa masijala ya Mwanza na 8 yaliyofunguliwa masjala ya Arusha. Aidha, divisheni ya biashara iliendelea kusogezza huduma kwa wananchi kwa kufungua masjala ndogo Mwanza. Mchakato wa kufungua masjala Mbeya kwa kufanya upembuzi yakinifu umeanza chini ya mradi wa MKUMBITA. Vile vile, tayari kiwanja cha kujenga ofisi ya divisheni ya biashara Dodoma kimepatikana na uchoraji wa ramani umeanza.

Mheshimiwa Spika, Divisheni ya Biashara immeanzisha Tovuti ([www.com.court.go.tz](http://www.com.court.go.tz)) ili kuitangaza na kutoa taarifa mbalimbali kwa wadau na pia inaendelea na matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano katika kuendesha shughuli zake kwa kutumia mfumo wa kusimamia mashauri ya kurekodi ushahidi kwa kompyuta.

Mheshimiwa Spika, Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi katika utaratibu wake wa kwanza wa usikilizaji wa mashauri ya iliyokuwa Mahakama ya Kazi chini ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana ilikuwa na mashauri 395 yaliyobakia. Kati ya hayo mashauri 188 yalimalizika na kubakia mashauri 207. Katika utaratibu wake wa pili ambaa unahusisha sheria mpya za kazi yalibakia mashauri 177 na mashauri mapya 903 yalipokelewa. Mashauri 224 yalimalizika na kubakia mashauri 856. Katika taratibu zote mbili Divisheni ya Mahakama ya Kazi ilipokea mashauri 1,475 na kumaliza mashauri 412 na kubakia 1,063.

Mheshimiwa Spika, Divisheni ya Ardhi ya Mahakama Kuu, ilipokea jumla ya migogoro ya ardhi 4,859, kati ya hiyo migogoro 1,548 ilisikilizwa na kumalizika, migogoro 3,311 inaendelea kusikilizwa. Vikao 21 vilifanyika katika kanda 12.

Vile vile, ukaguzi katika mabaraza kumi na moja ya wilaya ya Ardhi na nyumba ulifanyika Mtwara, Lindi, Songea, Mbanga, Iringa, Njombe, Mbeya, Tanga, Arusha, Moshi na Manyara. Katika mwaka huu wa fedha, Divisheni ya Ardhi ya Mahakama Kuu itahakikisha migogoro iliyopo ya ardhi na itakayosajiliwa inashughulikiwa kwa kufanya vikao katika masjala ndogo za Kanda kumi na mbili. Pia usimamizi na ukaguzi wa mara kwa mara katika mabaraza ya Ardhi na nyumba ya wilaya utaimarishwa.

Mheshimiwa Spika, Kuimarisha Utoaji wa Ushauri wa Kisheria Nchini. Katika kuimarisha utoaji wa ushauri wa kisheria kwa Serikali na Taasisi zake, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliendelea kutoa ushauri wa mambo ya kisheria yanayohusu masuala ya Katiba na Haki za Binadamu, Uendeshaji wa Kesi za Madai na Jinai, Uandishi wa Sheria, Uandaaji na Uchambuzi wa Mikataba mbalimbali ya kitaifa na kimataifa. Maombi 404 ya ushauri wa mambo mbalimbali ya kisheria yalipokelewa, kati ya hayo 396 yalifanyiwa kazi na maombi 8 yaliyobaki yanaendelea kushughulikiwa. Aidha, ushauri wa kisheria umetolewa katika timu za watalamu zenyenye kuhusisha Sekta mbalimbali (*Government Negotiating Teams*) ambazo zinahusika katika majadiliano ya mikataba mikubwa.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kwamba nchi inatoa huduma bora ya kisheria kwa wananchi wake na kwa wakati, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itaendelea kujengewa uwezo kwa kuajiri watumishi wengine wapya 126 wenye sifa na taaluma mbalimbali katika mwaka huu wa fedha. Vile vile, kwa kutumia Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Na. 4 ya mwaka 2005, utaratibu wa kuwatambua na kuwaorodhesha Mawakili wa Serikali na Wanasheria wengine wanaofanya kazi katika Wizara na Taasisi nyingine za Serikali umeanzishwa. Hatua hii itawezesha Wanasheria wa Serikali kufanya kazi kwa ufanisi zaidi na kwa viwango vinavyostahili kwa ajili ya kulinda maslahi ya Taifa. Ofisi nyingine ya Kanda huko Shinyanga itafunguliwa hivi karibuni na kufanya jumla ya Ofisi za Kanda kuwa kumi na nne.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua uwepo wa taasisi za kiraia ambazo kwa miaka kadhaa zimekuwa zikiwapatia wananchi msaada wa kisheria, kupitia kwa Mhe. Jaji Mkuu wa Tanzania, Ofisi imetayarisha Sheria Ndogo (GN) inayotoa mwongozo kuhusu usimamizi na uendeshaji wa mfumo unaotumika sasa sambamba na kufanyika kwa mapitio ya Sheria yakatayloruhusu uwepo wa mfumo rasmi wa msaada wa Sheria katika jamii.

Mheshimiwa Spika, kutafiti na kupitia Sheria mbalimbali, Tume ya Kurekebisha Sheria imeendelea kupitia na kutoa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ambazo zimepitwa na wakati na zinazokinzana na Katiba ya nchi. Kwa kipindi cha mwaka 2008/09, Tume imekamilisha ripoti tano na kuziwasilisha sehemu husika kwa hatua za utekelezaji. Sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Teknolojia ya Utambuzi wa Vimiminika kwenvye Viumbe Hai (*DNA*) ambayo ilipitishwa na Bunge lako Tukufu katika kikao cha Bunge lililopita. Ripoti ya Sheria ya Haki za watu wenye Ulemavu, Sheria za Mila kwa upande unaofuata nasaba za mama, Ripoti ya mabadiliko juu ya vifungu vya Sheria ya Adhabu ya kifo, viboko na vifungo vya muda mrefu, na Ripoti ya marekebisho ya Sheria ya Makosa ya Kujamiiiana.

Mheshimiwa Spika, Tume iliangalia tathmini ya utekelezaji na utendaji wa sheria ya makosa ya kujamiiiana ya mwaka 1998 na kutoa mapendekezo ya namna Sheria hiyo inavyoweza kurekebisha, kwa lengo la kuondoa dosari za kisheria na za kiutekelezaji zilizojitokeza, ili malengo ya Sheria hiyo yaweze kutekelezwa kwa ufanisi zaidi kama

ilivyotarajiwa. Ninatarajia kwamba, marekebisho ya Sheria hii yatasomwa katika Bunge lako Tukufu, katika kipindi cha mwezi Novembra.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inahakikisha kwamba mfumo wa huduma za Sheria unaboreshw na kuimarishwa kwa kufanya tafiti na mapitio pamoja na kutoa mapendekezo ya kurekebisha na kuhuisha sheria. Tume imeanza kazi ya kuhuisha sheria na kazi hii iko kwenye hatua za awali, pia Tume inaendelea kukamilisha tafsiri ya sheria tano kwa lugha ya Kiswahili na kutoa elimu ya Sheria kwa Umma kuititia vyombo vya habari, vipeperushi na vijarida mbalimbali. Sheria ambazo zimeanza kutafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili ni pamoja na; Kanuni za Adhabu, Sheria ya Ushahidi, Kanuni za Ufanuzi wa Sheria na Mwenendo wa Kesi za Jinai,

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka ujao wa fedha, Tume inatarajia kufanya tafiti na mapitio ya Sheria zinazohusu sekta za Kilimo na Mifugo. Sekta hizi ni muhimu katika maendeleo ya uchumi na jamii yetu kwa ujumla. Lengo la utafiti wa Sheria hizi ni kuweka mazingira endelevu, yenye kuleta tija na yanayochochea ukuaji wa uchumi. Aidha, Tume inaendelea kukamilisha mapitio ya sheria na kanuni za mfumo wa Haki kwa Raia [*Civil Justice Review*], Kanuni za Mahakama ya Rufani [*Court of Appeal Rules*] na kukamilisha awamu ya pili ya Sheria za Mila zinazofuata nasaba za upande wa mama. Katika mwaka huu wa fedha, Tume itaendelea na kazi ya kuhuisha sheria, kutoa elimu ya sheria kwa umma na kutafsiri sheria zingine kwa lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, Maendeleo ya Watumishi. Katika mwaka 2008/09, Wizara imeendelea na jukumu lake la kuwaendeleza na kuwahudumia Watumishi wake kijamii na kitaaluma. Katika mwaka ujao wa fedha, Wizara itaendelea na utaratibu wa kupima utendaji wa kazi kwa njia ya uwazi (*Open Performance Review and Appraisal System – OPNAS*). Aidha, itaendelea na zoezi la kuwapandisha vyeo watumishi na kuwapa mafunzo mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuwaongezea ujuzi na uwezo katika kutenda kazi zao.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hatua za kupeleka huduma za Mahakama karibu na wananchi, Serikali ilitoa nafasi 239 za ajira mpya kwa mwaka wa fedha 2008/09 ili kuongeza watendaji katika Mahakama. Kati ya nafasi hizo mahakama imeweza kujaza nafasi mia mbili na nne (204) kwa kuajiri Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo 111 na kufanya jumla yao kufikia 743 pamoja na watumishi wa kada mbalimbali.

Aidha, jumla ya Majaji 3 wa Mahakama ya Rufani waliteuliwa na kufanya idadi ya Majaji kuwa 49 katika Mahakama Kuu na Majaji 16 kwa Mahakama ya Rufani. Jumla ya Mahakimu Wakazi 46 wameajiriwa na kufanya jumla ya Mahakimu Wakazi na Wilaya kufikia 381. Aidha, ili kuongeza ufanisi kwa Waheshimiwa Majaji Serikali imeidhinisha nafasi 75 za wasaidizi wa sheria wa Majaji ambao wataajiriwa katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, katika kuinua viwango vya utendaji wa watumishi mwaka wa fedha 2008/09, Mahakama chini ya uhisani wa “*Investment Climate Facility for Africa*”

imewapa mafunzo ya kompyuta Waheshimiwa Majaji 33, wasajili 3 wataalamu wa mfumo wa mawasiliano na habari wa kompyuta 6 ndani na nje ya nchi na wasaidizi wa Kumbukumbu 30. Kwa upande mwingine, kupitia bajeti ya Serikali Mahakimu 65 wa Mahakama za Mwanzo na Makarani 80 katika ngazi ya cheti, na stashahada wamepata mafunzo katika Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto na Vyuo vingine.

Mheshimiwa Spika, ili kuiongezea uwezo wa kiutendaji, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa Mwaka 2008/09 imeajiri watumishi 9 katika kada mbalimbali. Aidha, Watumishi na Makamishna wa Tume, walipatiwa mafunzo mbalimbali ya muda mrefu na mfupi. Maafisa Uchunguzi 95, walihudhuria mafunzo ya uchunguzi. Makamishna na Wakuu wa Vitengo 10 wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi nje ya nchi juu ya mbinu za kufanya usuluhishi na upatanishi wa migogoro chini ya Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria. Pia, mafunzo ya matumizi ya mfumo wa kushughulikia malalamiko kwa njia ya Kompyuta yalitolewa kwa watanza kumbukumbu 10. Mafunzo yaliyotolewa yamesaidia kuwajengea uwezo watumishi wa Tume katika utoaji huduma kwa ufanisi na tija.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2008/09, Tume ya Utumishi wa Mahakama ambayo ni taasisi inayojitegemea imefanya vikao vitatu, kati ya vinne vilivyopangwa. Masuala ya ajira, uteuzi, kuthibitishwa kazini au cheo na nidhamu kwa Mahakimu na Maafisa wa Mahakama, yalishughulikiwa. Jumla ya Mahakimu Wakazi 49 wa daraja II na Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo 102 daraja la II wameajiriwa/kubadilishwa /kupandishwa cheo. Mahakimu Wakazi na Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo 127 katika madaraja mbalimbali wamethibitishwa kazini katika cheo, Mahakimu Wakazi na Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo 201 wamepandishwa cheo katika madaraja mbalimbali. Mashauri ya nidhamu kwa Mahakimu 37 yameshughulikiwa. Aidha, Uteuzi wa Wasajili 13 wa Mahakama (*Registrars*) umefanyika.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Utumishi wa Mahakama iliendelea na hatua za kujitangaza kwa kufanya ziara katika mikoa mitatu ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara. Madhumuni ya ziara hizi ni kuwawezesha wananchi, washauri na watumishi wa Mahakama pamoja na Wajumbe wa Kamati za maadili za mikoa na wilaya kuelewa na kutekeleza Sheria Na. 2 ya 2005 iliyoanzisha Tume. Katika mwaka huu wa fedha, Tume itaendelea kushughulikia masuala ya ajira, kupandisha vyeo na mashauri ya maadili na nidhamu ya Mahakimu pamoja na kuelimisha Umma na jamii kuhusu kazi zake. Aidha, mipango ya kuwajengea uwezo watumishi wake kwa kuwapatia mafunzo itaendelezwa.

Mheshimiwa Spika, Vyuo Vya Mafunzo. Wizara ya Katiba na Sheria, inasimamia Vyuo viwili vya Mafunzo vinavyohusika na Sekta ya Sheria. Katika mwaka wa fedha 2008/09, Chuo cha Uongozi wa Mahakama, Lushoto kimeendelea na jukumu lake la kutoa Mafunzo ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na Makarani wa Mahakama.

Aidha, Chuo kimeendelea na ukarabati wa majengo ili kumudu ongezeko la idadi ya wanafunzi 500. Ujenzi wa jengo la madarasa 4 lenye uwezo wa kubeba jumla ya wanachuo 360 kwa mara moja ulikamilika. Ujenzi wa jengo la hosteli ya wanachuo wa

kike lenye gorofa 3 na upanuzi wa jengo la maktaba ya muda uliendelezwa. Katika mwaka wa fedha 2009/10 chuo kinatarajia kudahili jumla ya wanachuo 635. Matumizi ya muda mrefu wa Chuo hiki ni kukifanya kuwa chuo ambacho watumishi wa mahakama kama vile majaji na mahakimu, watakuwa wakienda kupata mafunzo ya muda mfupi kwa madhumuni ya kujifunza mambo mapya yatakayokuwa yanajiri katika sekta ya sheria yanayotokana na mabadilko yanayotokea haraka katika sayansi na teknologia ili siku zote waweze kwenda pamoja na mabadilko yanayotokea katika jamii.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Mafunzo ya sheria kwa Vitendo (*Law School of Tanzania*) ilisajiliwa ikiwa na wanafunzi 800 katika mwaka wa fedha 2008/09. Idadi ya wanafunzi katika mwaka 2009 imeongezeka na kufikia jumla ya wanafunzi 1,074. Kwa hivi sasa mafunzo haya yanafanyika katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, katika Vyuo vyake vya Mlimani na Chang'ombe wakati taasisi hii ikiendelea na taratibu za ujenzi wa majengo yake ya kudumu katika eneo la kiwanja, lenye ekari 23 lililopo mkabala na barabara ya Sam Nujoma. Mchakato wa kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa Chuo hiki unaendelea. Ujenzi unatarajiwa kuanza mara baada ya kupata mkandarasi. Aidha, Ofisi za muda zinazotumiwa na Taasisi hii ziko kwenye jengo la Ubungo Plaza, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka ujao wa fedha, Wizara inakusudia kufanya mabadiliko katika Sheria inayoanzisha Chuo hiki ili sasa watakaolazimika kudahiliwa ni wale tu ambao wanakusudia kuwa Mawakili wa Kujitegemea na si wahitimu wote wa Shahada ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, masuala mtambuka. Utekelezaji wa mkakati wa kitaifa wa utawala bora na kuzuia mianya ya rushwa umekuwa ukifanya kwa njia ya kutoa elimu kwa watumishi juu ya madhara ya rushwa na kuhusu maadili ya kazi. Wizara yangu iliendeleza juhudhi za kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Jeshi la Polisi katika kukamilisha majalada ya kesi za rushwa kwa kuandaa hati za mashtaka na kuzifikisha kesi hizi Mahakamani. Aidha, juhudhi zinaendelea za kufanya uchunguzi na ufuutiliaji pamoja na kuchukua hatua zinazostahili pale ambapo kunakuwa na tuhuma za rushwa dhidi ya watumishi. Vile vile kwa kushirikiana na vyombo vingine mafunzo ya maadili kwa Viongozi na watumishi yamekuwa yakitolewa ili kuepusha watumishi kujiingiza katika vitendo vya rushwa.

Mheshimiwa Spika, katika juhudhi za kupambana na janga la Ukimwi ambalo ni tishio kubwa kwa Taifa letu, Wizara yangu imeendelea kuchukua hatua za kuwapatia elimu na kuwahamasisha watumishi kupima kwa hiari na mbinu za kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huu. Katika kuboresha huduma zitolewazo kwa watumishi wanaoishi na virusi vya ukimwi, wizara yangu imetenga fedha katika Mpango na Bajeti ya Mwaka huu wa fedha ili kuwezesha utoaji wa huduma za kununulia virutubisho na madawa ya kurefusha maisha.

Mheshimiwa Spika, katika kukamilisha ushirikishaji wa jinsia zote katika utendaji kazi wa mwaka huu wa fedha, Wizara yangu imetayarisha Hadidu za Rejea

zitakazotumiwa na mtaalam muelekezi katika kuainisha uwiano wa takwimu mbalimbali zilizopo za utendaji kazi kati ya jinsi ya kike na ya kiume katika Wizara.

Mheshimiwa Spika, shukrani, kwa niaba ya wizara yangu, napenda kuwashukuru kwa dhati wale wote walioshirikiana nasi katika kipindi cha 2008/09 katika kutimiza malengo yetu. Shukrani zetu pia ziwaendee wadau wa maendeleo wanaoshirikiana nasi katika kutelekeza Programu na Mipango yetu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria. Wahisani hao wanajumuisha Mashirika na Taasisi za Kimataifa zinazochangia katika kuboresha utoaji haki sawa kwa wote na kwa wakati. Nchi na Mashirika hayo ni pamoja na; Serikali za Denmark, Sweden, Finland, Canada, Uingereza (DFID), Benki ya Dunia (WB), UNICEF na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) na wengine wengi.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru wananchi na wadau mbalimbali hasa sekta binafsi, wanahabari, na vyuo vya elimu vinavyohusika na mambo ya Sheria kwa ushirikiano wao katika kutelekeza malengo ya Sekta ya Sheria. Shukrani za pekee ziwaendee waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa michango yao ambayo imesaidia sana katika kuboresha huduma zitolewazo na Wizara yangu. Naomba waendelee na ushirikiano huo ili tuweze kuendeleza Sekta hii muhimu katika utoaji haki kwa wananchi wetu. Aidha, niwashukuru sana wananchi wa Jimbo langu la Nachingwea kwa kuendelea kunipa ushirikiano mkubwa katika kuleta maendeleo ya jimbo letu ili kila mmoja wetu awe na maisha bora. Nawaomba wangoje kumsikiliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji akiwaeleza ni jinsi gani serikali yao inavyoshughulikia tatizo lao kubwa la Maji.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru wafanyakazi wenzangu wa Wizara ya Katiba na Sheria, nikianza na Mheshimiwa Jaji Mkuu, Augustino Ramadhani, Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Johnson Paul Mathias Mwanyika, Mheshimiwa Fakihi Abdalla R. Jundu Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu, Katibu Mkuu wa Wizara Bwana Oliver P.J. Mhaiki, Naibu Mwanasheria Mkuu Bwana Sazi Bundala Salula, Msajili wa Mahakama ya Rufani Bwana Ferdinand Wambali, Msajili wa Mahakama Kuu Bibi Eliamani G. Mbise, Msajili wa Mahakama ya Biashara Bwana John R. Kahyoza, Msajili wa Mahakama ya Kazi, Bwana Samuel G. Karua; Msajili wa Mahakama ya Ardhi Bibi Grace K. Mwakipesile, Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama Bibi Celina Wambura, Katibu Mtendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria Bwana Japhet Sagasii, Kaimu Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Bibi Mary Massay na Kaimu Mtendaji Mkuu, wa Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhagini, Bwana Philip Saliboko. Nawashukuru kipekee wataalamu wa Wizara yangu na wote waliota mchango katika kukamilisha Hotuba yangu. Aidha, ushirikiano mzuri wanaonipa unanisaidia sana katika kutimiza majukumu niliyopewa na pia kuniwezesha kutekeleza malengo tuliyojiwekea kwenye Wizara.

Mheshimiwa Spika, ili Wizara iweze kutekeleza malengo yake yaliyoainishwa katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2009/2010, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi Bilioni mia moja na saba,milioni mia sita sabini na nne,laki nne na kumi na mbili, (107,674,812,000) kwa ajili ya matumizi ya wizara

kwa mwaka 2009/10. Kati ya fedha hizi, matumizi ya kawaida ni Shilingi Bilioni sitini na saba, milioni mia mbili thelathini na saba laki tisa sabibini na saba (67,237,977,000) Fedha za miradi ya Maendeleo ni Shilingi Bilioni Arobaini, milioni mia nne thelathini na sita, laki nane thelathini na tano (40,436,835,000). Kati ya hizi, Shilingi Bilioni sita, milioni mia tatu hamsini na sita, laki nane arobaini na tatu (6,356,843,000) ni fedha zetu za ndani na Shilingi Bilioni Thelathini na nne, milioni sabini na tisa laki tisa tisini na mbili.(34,079,992,000) ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe Makadirio hayo ya Fedha za Maendeleo na Matumizi ya kawaida kwa mafungu kumi na moja kama ifuatavyo:-

Fungu 12: Tume ya Utumishi wa Mahakama	
Matumizi ya Kawaida	1,077,670,000.00
Matumizi ya Maendeleo (ndani)	-
Matumizi ya Maendeleo (nje)	146,789,000.00
JUMLA	1,224,459,000.00

Fungu 16: Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali	
Matumizi ya Kawaida	12,052,171,000.00
Matumizi ya Maendeleo (ndani)	-
Matumizi ya Maendeleo (nje)	7,388,358,000.00
JUMLA	19,440,529,000.00

Fundu 18: Mahakama Kuu	
Matumizi ya Kawaida	17,884,425,000.00
Matumizi ya Maendeleo (ndani)	1,679,074,000.00
Matumizi ya Maendeleo (nje)	768,628,000.00
JUMLA	20,332,127,000.00

Fungu 19: Mahakama za Wilaya	
Matumizi ya Kawaida	10,289,826,000.00
Matumizi ya Maendeleo (ndani)	2,020,926,000.00
Matumizi ya Maendeleo (nje)	7,547,481,000.00
JUMLA	19,858,233,000.00

Fungu 40: Mahakama	
Matumizi ya Kawaida	9,680,143,000.00
Matumizi ya Maendeleo (ndani)	1,437,374,000.00
Matumizi ya Maendeleo (nje)	4,594,588,000.00
JUMLA	15,712,105,000.00

Fungu 41: Wizara ya Katiba na Sheria	
Matumizi ya Kawaida	6,876,947,000.00

Matumizi ya Maendeleo (ndani)	1,079,893,000.00
Matumizi ya Maendeleo (nje)	9,571,403,000.00
JUMLA	17,528,243,000.00

Fungu 55: Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora	
Matumizi ya Kawaida	4,603,769,000.00
Matumizi ya Maendeleo (ndani)	-
Matumizi ya Maendeleo (nje)	1,275,134,000.00
JUMLA	5,878,903,000.00

Fungu 59: Tume ya Kurekebisha Sheria	
Matumizi ya Kawaida	1,314,657,000.00
Matumizi ya Maendeleo (ndani)	-
Matumizi ya Maendeleo (nje)	1,160,473,000.00
JUMLA	2,475,130,000.00

Fungu 60: Mahakama ya Kazi	
Matumizi ya Kawaida	1,137,921,000.00
Matumizi ya Maendeleo (ndani)	-
Matumizi ya Maendeleo (nje)	626,410,000.00
JUMLA	1,764,331,000.00

Fungu 64: Mahakama ya Biashara	
Matumizi ya Kawaida	1,176,095,000.00
Matumizi ya Maendeleo (ndani)	139,576,000.00
Matumizi ya Maendeleo (nje)	468,000,000.00
JUMLA	1,783,671,000.00

Fungu 90: Mahakama ya Ardhi	
Matumizi ya Kawaida	1,144,353,000.00
Matumizi ya Maendeleo (ndani)	-
Matumizi ya Maendeleo (nje)	532,728,000.00
JUMLA	1,677,081,000.00

Mheshimwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/10, Wizara yangu, inatarajia kukusanya kiasi cha shilingi 1,930,141,000 kama Maduhuli ya Serikali. Mchanganuo wa Makusanyo kwa kila fungu husika ni kama ifuatavyo:-

- |              |                 |
|--------------|-----------------|
| 1. Fungu 16: | Sh.12,100,000   |
| 2. Fungu 18: | Sh.180,700,000  |
| 3. Fungu 19: | Sh. 805,300,000 |
| 4. Fungu 40: | Sh.183,505,000  |
| 5. Fungu 41: | Sh.22,001,000   |

6. Fungu 55:	Sh.1,532,000
7. Fungu 64:	Sh.650,000,000
8. Fundu 90:	Sh.75,003,000
<b>Jumla</b>	<b>Sh.1,930,141,000</b>

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7), ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2008/2009 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuipatia Kamati yangu kazi ya kujadili Makadirio ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka 2009/2010, Kamati ilikutana na Watendaji wa Ofisi hiyo tarehe 02 Juni, 2009 katika Ofisi Ndogo ya Bunge, Dar es Salaam, kushughulikia Makadirio hayo. Aidha, Kamati ilipokea na Kujadili Taarifa ya Wizara hiyo kuhusu Utekelezaji wa majukumu yaliyofanywa kwa Mwaka 2008/2009 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2009/2010, iliyowasilishwa na Mheshimiwa Mathias Chikawe (Mb), Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria, inahusisha Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria, Fungu 59 – Tume ya Kurekebisha Sheria, Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Fungu 40 – Mahakama, Fungu 18 – Mahakama Kuu, Fungu 12 – Tume ya Utumishi wa Mahakama, Fungu 19 – Mahakama za Wilaya na Mahakama za Mwanzo, Fungu 60 – Mahakama ya Kazi, Fungu 64 – Mahakama ya Biashara na Fungu 90 – Mahakama ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa Majukumu kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009. Katika Mwaka wa Fedha 2008/2009 Mahakama iliidhinishiwa jumla ya Sh.44,079,471,000. Fedha hizo zilitumika kutekeleza majukumu mbalimbali ikiwa ni pamoa na kujizatiti na kuimarisha uwezo wa kuendesha na kusukuma kesi ili kupunguza mrundikano wa kesi Mahakamani na mahabusu Magerezani. Jumla ya vikao 13 vilifanyika kati ya vikao 16 vilivyopangwa kwa Mahakama ya Rufani. Mahakama Kuu imefanya vikao 160 kati ya 208 vilivyopangwa. Aidha vikao vya kila siku katika Mahakama 23 za Mahakamu wakazi na 100 za Mahakama za Wilaya vimendelea kufanyika.

Mheshimiwa Spika, Vikao viwili hadi vitatu vya kusukuma mashauri vimefanyika katika kila Kanda kati ya vikao vinne vilivyopangwa kufanyika kwa mwaka. Vikao hivi vimesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza mrundikano wa mashauri ambayo yalikuwa yakikwama kwa kutokamilika kwa upelelezi wa kesi Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2007/2008 Mahakama ya Rufaa ilikuwa na jumla ya mashauri 1,893, na katika Mwaka 2008/2009 mashauri 766 yalipokelewa na kufanya mashauri hayo kufikia 2,659. Kati ya hayo Mashauri 560 yalisikilizwa na kumalizika na mengine 2,099 yalibaki.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Mahakama Kuu kulikuwa na jumla ya Mashauri 18,805 kati ya hayo 10,791 yalifunguliwa na mashauri 9,590 yalisikilizwa na kubaki 9,215.

Mheshimiwa Spika, Mahakama za Mikoa na Wilaya zilikuwa na jumla ya mashauri 61,237. Kati ya hayo 46,282 yalifunguliwa. Mashauri 42,725 yalisikilizwa na kubakia mashauri 18,512.

Mheshimiwa Spika, Mahakama za Mwanzo zilikuwa na jumla ya mashauri 213,239 ambapo mashauri 14,435 yalipokelewa kwa mwaka 2008/2009, kati ya hayo 151,200 yamesikilizwa na kubakia mashauri 62,039.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu kuwa Mahakama ni chombo kinachohusika na jukumu la kutafsiri, pamoja na kutekeleza Sheria na Haki za Binadamu, kutekeleza jukumu hilo kwa ufanisi, Mahakama ya Tanzania imeendelea kujenga Mahakama katika ngazi zote na kutoa vitendea kazi muhimu pamoja na kuwapatia watumishi wake mafunzo ili kuwajengea uwezo wa kuweza kutoa huduma kama inavyostahili.

Aidha, katika kutekeleza azma hiyo, kwa mwaka 2009/2010 Mahakama imeligawa Fungu 40 na kupata mafungu mengine mawili yaani Fungu 18 Mahakama Kuu, na Fungu 19 Mahakama za Wilaya na Mahakama za Mwanzo. Lengo ni kuongeza nguvu za kiutendaji na kupunguza mrundikano wa kesi Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria, Fungu 41. Katika mwaka 2008/2009 Wizara ya Katiba na Sheria iliidhinishiwa jumla ya Sh. 24,372,455,600. Fedha hizo zilitumika katika kutekeleza majukumu yafuatayo:

(i) Kushirikiana na wadau wa Sekta na Taasisi zilizo chini yake Wizara kwa kutekeleza malengo ya uimarishaji wa mfumo wa utoaji wa haki za Binadamu na Utawala Bora kwa kuimarisha uwezo wa Taasisi na vyombo vyake vya utoaji haki. Aidha Wizara imeimarisha mfumo wa Sheria na uwekaji wa mazingira mazuri kwa makundi yote katika jamii;

(ii) Kutoa mafunzo, semina, makongamano na warsha mbalimbali na kuongeza kiwango cha uelewa kwa wadau na wananchi wote kuhusu Sheria na Haki za Binadamu kwa ujumla;

(iii) Imetoa ushauri wa kisheria, imebuni sera, mikakati na programu za kisekta na kusimamia utekelezaji wake, ikiwa ni pamoja na kuzingatia na kutekeleza masuala mtambuka hususan ya jinsia, mazingira, na kupunguza maambukizi ya UKIMWI;

(iv) Kwa kupitia Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini, Wizara imeendelea kuboresha huduma za Usajili, Ufilisi na Udhamini kwa kuboresha mfumo wa mawasiliano ambao utawezesha ukusanyaji wa kumbukumbu zote za wakala kwa kuunganisha Wilaya zote za Tanzania Bara;

(v) Kwa kupitia Programu ya Maboresho ya Sekta ya sheria, imetekeliza majukumu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuimarisha mfumo wa upelelezi kwa kuwapatia Polisi vitendea kazi, vyombo vyaa safiri, na mafunzo ya muda mfupi ya mbinu za kisasa za upelelezi. Aidha, katika maboresho hayo pia, Wizara imekua na jukumu la kuendesha Taasisi ya Mafunzo ya Wanasheria kwa vitendo ambayo yameendelea vizuri ikiwa ni pamoja na kusajili wanafunzi 1,074; na

(vi) Kutekeleza programu ya kutenganisha shughuli ya Upelelezi na uendeshaji Mashtaka ili kupunguza mrundikano wa kesi na kuharakisha upatikanaji wa haki kwa wakati. Aidha, Elimu na msaada wa kisheria kwa watu wasio na uwezo wa kuwakilishwa Mahakamani vimetolewa chini ya Mtandao wa kutoa huduma za misaada ya kisheria.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Utumishi wa Mahakama, Fungu12. Katika Mwaka 2008/2009, Tume ya Utumishi wa Mahakama iliidhinishiwa jumla ya Sh 703,031,000. Fedha hizo zilitumika kutekeleza majukumu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuendesha vikao vyaa kisheria, kushughulikia masuala ya nidhamu na ajira ambapo jumla ya Mahakimu Wakazi 49, na Mahakimu wa Mahakama za mwanzo 102 wameajiriwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo 201, wamepandishwa vyeo na wengine 127 wamethibitishwa kazini. Tume pia ilishughulikia uteuzi wa maafisa wa Mahakama (*Registers*) 13, pamoja na mapendelekezo ya uteuzi wa Jaji Kiongozi. Sambamba na utekelezaji wa majukumu hayo Tume ilifanya ziara mbalimbali zenyne madhumuni ya kuimarisha Kamati ya Maadili ya Mahakimu, katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara.

Mheshimiwa Spika, mafunzo yalitolewa kwa Makatibu wa Kamati za Maadili katika mikoa ya Tanga, Arusha, na Manyara kwa madhumuni ya kuwaongezaa uwezo katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Fungu 16. Katika Mwaka 2008/2009 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliidhinishiwa jumla ya sh.10,787,601,000 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kushirikiana na Tume ya Kurekebisha Sheria kwa kuzitazama upya sheria zinazokandamiza wanawake na jamii, zikiwemo sheria za mirathi na ndoa na sheria ya makosa ya kujamiana. Aidha, sheria ambazo zimepitwa na wakati na zinazokandamiza jamii ziliendelea kufanyiwa utafiti;

(ii) Vile vile imezifanyia rejea baadhi ya sheria na kuchukua hatua za kufanya Marekebisho ili ziendane na wakati uliopo. Mfano wa sheria hizo ni; Sheria ya Rushwa, Sheria ya Kupambana na Usafirishaji wa Fedha Haramu, Sheria ya Mawakili na sheria ndogo inayotoa mwongozo kuhusu usimamizi na uendeshaji wa mfumo rasmi wa msaada wa sheria katika jamii. Aidha katika utekelezaji wa kazi hii katika Mwaka 2008/2009 miswada 34 imeandaliwa, na mingine 23 ilipitishwa na Bunge na kuwa sheria; na

(iii) Imepeleka Mawakili watano katika masomo ya muda mfupi ili kuwaimarisha na kuwajengea uwezo wa kushauri na kuandika mikataba ya Serikali. Ofisi hiyo pia imeendelea kusikiliza kesi mbalimbali za makosa ya Jinai zilizoendeshwa katika vikao 17 vya Mahakama Kuu na vikao 12 vya Mahakama ya Rufani pamoja na kuiwakilisha Serikali na kuitetea katika kesi za Madai dhidi yake pale inaposhtaki au kushtakiwa.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Fungu 55, katika mwaka 2008/2009, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora iliidhinishiwa jumla ya Sh 4,224,868,000. Kiasi hicho cha Fedha kilitumika kutekeleza majukumu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kusimamia utekelezaji na uangalizi wa masuala ya Haki za Binadamu, utayarishaji wa Programu za Elimu kwa Umma kuhusu Haki za Binadamu, pamoja na uchapishaji na usambazaji wa machapisho ya Sheria yanayohusu Haki za Binadamu.

Mheshimiwa Spika, Tume imeendelea na jukumu lake la kushughulikia malalamiko kutoka kwa Wananchi na kufuatilia matukio yanayotangazwa katika vyombo vya habari kuhusu uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, upo usemi wa sheria usemwao kwamba:-

*“Justice delayed is justice denied” Kucheleweshwa kwa haki ni sawa na kunyimwa haki”.*

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu imeridhika kwani iliripotiwa kuwa, kwa Mwaka 2008/2009, jumla ya malalamiko 1,319 yanayohusu uvunjaji wa haki za Binadamu yamefanyiwa uchunguzi na kupatiwa ufumbuzi na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, licha ya ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, imekuwa ikitoa elimu kwa umma inayohusu Haki za Binadamu na Utawala Bora, katika mkakati wake wa kuelimisha jamii. Vile vile imeendelea kutafsiri sheria mbalimbali kwa lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Kurekebisha Sheria, Fungu 59. Katika mwaka 2008/2009 Tume ya Kurekebisha Sheria iliidhinishiwa jumla ya Sh.1,828,870,000 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na kurekebisha sheria mbalimbali zinazokinzana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sheria

zilizopitwa na wakati, na Sheria zinazogandamiza na kuonea jamii, hususani sheria ya haki za watotona sheria ya ndoa. Aidha, Tume imekuwa ikifanya marekebisho ya mara kwa mara inapolazimika kufanya hivya kwa lengo la kuhakikisha utawala wa sheria unatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Kazi, Fungu 60. Katika Mwaka 2008/2009, Mahakama ya Kazi iliidhinishiwa jumla ya Sh 1,116,651,000. Fedha hizo zilitumika kutekeleza kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupokea na kushughulikia mashauri mbalimbali ambapo katika Mahakama Kuu kitengo cha Kazi kilipokea jumla ya mashauri 356 kati ya hayo mashauri 130 yalisikilizwa na kumalizika na kubakia mashauri 226. Hata hivyo chini ya utaratibu wa kusikiliza Rufaa mapitio/marudio kulingana na uwezo iliyopewa chini ya sheria mpya ya kazi, jumla ya mashauri 1,024 yalipokelewa na kati ya hayo 242 yamesikilizwa na kumalizika na kubakia 782.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Biashara, Fungu 64. Katika mwaka 2008/2009 Mahakama ya Biashara iliidhinishiwa jumla ya Sh 1,505,887,000 kwa ajili ya kutekeleza kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kushughulikia Mashauri yanayohusu biashara, ambapo katika Mwaka 2008/2009 ilipokea jumla ya kesi 108 kati ya hizo 76 zimesikilizwa na kutolewa maamuzi.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Ardhi, Fungu 90. Katika mwaka 2008/2009, Mahakama ya Ardhi iliidhinishiwa jumla ya sh.1,234,289,000 kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuendesha na kuyatolea maamuzi migogoro inayohusu ardhi. Aidha jumla ya migogoro 4,592 ilipokelewa kati ya hiyo 1,398 ilisikilizwa na kumalizika na migogoro 3,194 inaendelea kusikilizwa.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2009/2010, shughuli zilizopangwa kutekelezwa kwa Mwaka 2009/2010. Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na mafungu yake yote itaendelea kutekeleza majukumu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kusimamia utoaji wa haki kwa wananchi, kutoa mafunzo kwa vitendo kwa Mawakili wa Serikali hususan katika eneo la kujadili na kuanda Mikataba, kushirikiana na Wizara nyingine katika uandaaji wa taarifa za Mikataba ya Kimataifa ya Haki za Binadamu, kuratibu shughuli za upelelezi wa Makosa ya Jinai, pamoja na kuendeleza shughuli zilizoanza kutekelezwa katika mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwasilishwa kwa taarifa ya utekelezaji ya Wizara ya Katiba na Sheria na mafungu yake yote na hatimaye kuyachambua na kuyajadili, Kamati iliyapokea maombi hayo na kuyapitisha ili yawasilishwe Bungeni kwa hatua zinazofuata.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati kwa bajeti ya mwaka 2009/2010, wakati wa kujadili utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka 2008/2009 na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2009/2010 Kamati ilitoa maoni na ushauri wa mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Tanzania. Kwa upande wa Mahakama, Kamati imebaini mapungufu mengi katika Mhimili huu, Mahakama zetu katika ngazi zote zinakabiliwa na matatizo mengi hususani upungufu wa fedha za kuendeshea vikao, uchakavu mkubwa wa majengo, upungufu wa Mahakimu hasa katika Mahakama za mwanzo, upungufu wa vitendea kazi unaosababisha ucheleweshaji wa upatikanaji wa nakala za hukumu kwa wafungwa waliopo magerezani, upungufu wa vyombo vyaa usafiri, upungufu wa nyumba za kuishi watumishi hususani majaji, na mahakimu, pamoja na ufinyu wa fungu la fedha za mafunzo na kozi mbali mbali za kuwaongeza watumishi uwezo na ufanisi kazini.

Mheshimiwa Spika, changamoto zote zinazoikabili Idara ya Mahakama zinatokana na ufinyu wa bajeti katika Wizara ya Katiba na Sheria inayoathiri utendaji wa kazi hususan katika idara ya Mahakama. Kamati inaishauri mambo yafuatayo:-

(i) Serikali itafute mbinu itakayoiwezesha kuiongezea fedha Mahakama ili iweze kukabiliana na changamoto hizo;

(ii) Vilevile kamati inaishauri kuwa ni vyema kuwepo na mfuko unaojitegemea wa Uendeshaji wa Mahakama (*Judiciary Fund*) ambao utaipatia Mahakama kipaumbele katika utendaji wake wa kazi;

(iii) Kamati inaishauri Serikali kuongeza wigo wa ajira kwa kuwaajiri Majaji na Mahakimu ili kupunguza msongamano wa kesi na upatikanaji wa haki kwa wakati;

(iv) Kamati inaishauri kwamba Wizara kwa kuzingatia maboresho ya sekta ya sheria iongeze wigo wa ajira na kuwaajiri Wanasheria wengi ili waweze kukabiliana na changamoto hio hususan katika kuweza kufanikisha mchakato wa kutenganisha shughuli ya upelelezi na uendeshaji wa mashtaka ambapo mpaka sasa ipo katika hatua ya majoribio na inahitaji Wanasheria wakutoshua. Aidha, posho na mishahara ya watumishi iboreshwe ili kuwawezesha watumishi hawa kufanya kazi katika mazingira mazuri na kuwaepusha kuijingiza katika wimbi la rushwa;

(v) Kamati inaishauri Serikali kutenga bajeti ya kutosha ili kuiwezesha Tume ya Haki za Binadamu kutekeleza shughuli zake ipasavyo, ikiwa ni pamoja na kuongezea wataalamu wa Sheria; na

(vi) Tume ya Haki za Binadamu iendelee kutafsiri sheria na iongeze kutoa machapisho mengi kwa lugha ya Kiswahili kwa lengo la kuwasaidia Watanzania waweze kutambua haki zao za msingi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii muhimu kuwasilisha maoni ya Kamati yangu.

Pili, napenda kumshukuru kwa dharti Mheshimiwa Mathias B Chikawe, (Mb) Waziri wa Katiba na Sheria, Waheshimiwa wenye viti wa Tume, Makamishna wa Tume, Waheshimiwa Majaji, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Katibu Mkuu, Wakuu

wa Idara, Taasisi na Vitengo na Maafisa wote wa Wizara kwa kushirikiana vyema na kamati wakati wote ilipojadili makadirio ya Wizara hii.

Kipekee, naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati hii, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makisio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria. Uzoefu wao wa muda mrefu katika nyanja mbali mbali za sekta ya sheria ndio uliofanikisha kazi hii. Kwa heshima naomba, niwatambue kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mwenyekiti, Mheshimiwa Ramadhani A. Maneno, Makamu Mwenyekiti.

Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Yussuf R. Makamba, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mheshimiwa Fatma M. Maghimbiri, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Nimrod E. Mkono, Mheshimiwa Rajab H. Juma, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakar, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Salim Yussuf Mohamed, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu na Mheshimiwa Benedict Ngalama Ole-Nangoro.

Aidha napenda kumshukuru, Dr. Thomas D. Kashilillah, Katibu wa Bunge, kwa kufanikisha shughuli za Kamati. Makatibu wa Kamati hii, ndugu Haika Mtui na Ramadhan Abdallah, kwa kuratibu shughuli zote za Kamati na kuhakikisha kuwa maoni ya Kamati yanakamilika kwa wakati uliopangwa. Bila kuwasahau Wakuu wa Idara na Vitengo na watumishi wa Ofisi ya Bunge kwa kufanikisha shughuli za Kamati kama zilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu, liipokee Taarifa hii na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria na mafungu yake yote kwa mwaka 2009/2010, yenye jumla ya Sh. 107,674,812,000/= kati ya hizi shilingi 67,237,977,000/= ni za matumizi ya kawaada na shilingi 40,436,835,000/= ni za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naiunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

**MHE. FATMA M. MAGHIMBI – MSEMAJI WA UPINZANI, WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kwa mujibu wa kanuni zilizowekwa.

Kwanza, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, napenda kutoa maoni kuhusu bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2009/2010, kwa mujibu wa wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 99 (3) na (7), Toleo la mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwenye wingi wa rehema, kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kusimama mbele yenu, ili niweze kutoa maoni kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kuhusu Wizara hii ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuendeleza shukrani zangu kwa wananchi wa Jimbo la Chake Chake, kwa imani yao kwangu na mimi ninawaahidi kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu mkubwa sana, napenda kumshukuru mume wangu, Bwana Mussa Maghimbiri, kwa uvumilivu mkubwa alionao wakati ninapokuwa katika shughuli za siasa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimpe pongezi zangu Mwenyekiti wangu wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa George Malima Lubeleje kwa jinsi anavyoendesha Kamati yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda na mimi kutoa pole kwa wananchi wa Visiwani, kwa kumpoteza Prof. Haroub Othman. Sio Visiwani tu bali Taifa zima tumepata hasara kubwa kwa sababu tuna Maprofesa wachache sana na kumpata mtu mwenye cheo cha Profesa, inachukua miaka mingi.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kumshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa mujibu wa hotuba yake inaelekea ametekeleza mambo mengi ambayo Kambi ya Upinzani imependekeza mwaka jana na mwaka juzi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani katika bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2009/2010 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, bado kuna ucheleweshaji mkubwa wa kesi katika Mahakama zetu na hii inaathiri sana utoaji wa haki. Nanapenda kumnunguu Jaji Mkuu wa Tanzania kwenye hotuba aliyoitoa mwaka jana wakati wa hafla ya kuwaapisha Majaji mwezi Oktoba. Katika hotuba yake Mheshimiwa Jaji Mkuu alisema (naomba kumnunguu kwa lugha ya Kiingereza): -

*“The judicial process in this country was going at a snail’s pace as the number of cases kept piling at the courts, some for over a decade before a judgment is passed.”*

Mheshimiwa Spika, hali hii, inapingana na dira ya Wizara ya Haki sawa kwa wote na kwa wakati (*equal and timely justice for all*).

Mheshimiwa Spika, pamoja na hali ya ucheleweshaji wa kesi kuzidi kuwa sugu, hivi karibuni kumejitokeza hali ambayo imezua utata na migongano ya mawazo kati ya wananchi ambao wengi wao wamejikuta wakihoji iwapo katika nchi yetu, watu wote ni sawa mbele ya sheria. Hii ni kutokana na kuwa kuna watu wengi ambao wamekaa mahabusu kwa muda wa miaka mingi wakisubiri kesi zao kusikilizwa wakati kuna baadhi ya kesi amabazo uendeshaji wake umekuwa ukifanyika kwa kasi ya ajabu (*super-sonic speed*). Watuhumiwa katika kesi hizi hufikishwa Mahakamani karibu kila wiki na mara nyingine zaidi ya mara moja kwa wiki. Watanzania wanauliza je, kasi ya aina hii

inafanyika kwenye kesi za wakubwa tu au ndio kusema kuna *double standards* katika utoaji wa haki?

Mheshimiwa Spika, tatizo la ucheleweshaji wa kesi, linachangiwa sana na idadi ndogo ya Mahakimu na Majaji. Juhudi amabazo zimekuwa zikifanywa kuongeza idadi ya Majaji na Mahakimu, bado ni ndogo ukilinganisha na hali halisi. Kwa Mfano, kwa sasa Mahakama Kuu ina jumla ya Majaji 50 tu ambapo hata kama idadi yao ingekuwa imefikia 100 bado ingekuwa haitoshelezi. Tatizo ni kubwa zaidi katika Mahakama ya Rufaa ambayo ina jumla ya Majaji 16 tu. Cha kusikitisha zaidi ni kuwa Majaji wa Rufaa wanatakiwa kustaafu wanapokuwa na umri wa miaka 65, wengi wao wanakuwa wametumikia Mahakama hii kwa kipindi kifupi tu, maana baadhi huteuliwa wakiwa na umri wa miaka 50 au zaidi na wengine yao huwa wamefikisha miaka 60 hivyo muda wao wa kutumikia Mahakama ya Rufaa huwa ni mfupi sana.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwa muda wa kustaafu kwa Majaji wa Mahakama za Rufaa uangaliwe upya, maana katika utafiti wangu nimegundua kuwa Majaji wanastaafu wakiwa wana nguvu za kufanya kazi na wengi wao wanaishia kutumikia kwa mikataba na baadaye kuteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali za juu Kitaifa ikiwemo ujumbe au uongozi katika Tume.

Mheshimiwa Spika, miundombinu katika Mahakama zetu ni duni. Mahakimu wanafanya kazi katika mazingira magumu sana hali inayohatarisha afya zao na kuathiri shughuli nzima ya utoaji wa haki. Majengo ya Mahakama yaliyopo hayatoshi, baadhi ya Mahakama hazina vyumba vyaya kuhifadhi mahabusu na hivyo mahabusu huwekwa nje huku wakiwa wamefungwa pingu wakati wakisubiri kuanza kwa mashauri yao.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa mfano wa Mahakama ya Kariakoo ambayo binafsi niliitembelea. Mahakama hii ina chumba kimoja tu cha kuhifadhi mahabusu ambacho hutumika kuwahifadhi mahabusu wa kiume huku mahabusu wa kike wakikalishwa nje kwenye uwanja kusubiri mashitaka yao kuanza. Mfano mwengine wa kusikitisha ni Mahakama ya Mwanzo ya Endulen iliyoko Wilayani Ngorongoro ambayo Mheshimiwa hakimu alikuwa akitumia ofisi moja na waendesha mashtaka, ofisi ambayo pia ilitumika kama chumba cha kuhifadhi mahabusu. Hali hii ni vigumu kwa Mahakimu wetu kufanya kazi zao kwa ufanisi na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, hali ya uchakavu wa majengo pia ni tatizio kubwa katika Mahakama/ Mabaraza ya Ardhi na Nyumba, mathalani Baraza la Ardhi la Wilaya ya Kinondoni ambazo ofisi zake ziko kwenye Jengo la Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Mahakama hii ina vyumba vidogo sana kwa ajili ya Mahakimu. Vyumba hivi viko kwenye hali duni sana, sakafu yake imechimbika chimbika hivyo wafanyakazi wa Mahakama hulazimika kumwagia maji kwenye mashimo kila asubuhi ili wanapowasha feni isitimue vumbi. Pia hakuna sehemu ya wadai na wadaifa kuketi wakati wakisubiri mashauri yao kuanza, na badala yake hulazimika kusimama kwenye *corridor*. Mahakimu wa Mahakama hii ya Ardhi hawako katika hali ya Usalama. Tumshukuru Mungu kuwa Watanzania ni watulivu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inafikiria kuwa wakati umefika sasa kwa Halmashauri za Wilaya kuanza kusaidia katika utendaji haki kwa kusaidia ujenzi wa Mahakama na kuboresha miundombinu ya utoaji wa haki kama ambavyo Halmashauri zinavyofanya kwa upande wa elimu na afya, na hii inatokana na ukweli kuwa utoaji wa haki ni huduma kwa jamii kama zilivyo huduma nyingine. Kwa kuchangia katika kuboresha utoaji wa haki ieleweke kuwa kufanya hivyo sio kuingilia uhuru wa mahakama bali ni kuboresha utoaji wa haki nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa shukrani na pongezi za dhati kwa TASAF kwa mchango wake katika kujenga majengo mapya ya Mahakama na kukarabati majengo ambayo yalikuwa katika hali mbaya sana. TASAF inasaidia katika kujenga mambo mengi hapa nchini na pia katika kujenga Mahakama, Wizara hii inatakiwa kuipongeza TASAF kwa mchango wao wa kujenga Mahakama. TASAF ni Mwokozi wa Taifa hili katika kusaidia kutatua matatizo hasa katika huduma za jamii.

Mheshimiwa Spika, uhuru wa Mahakama, ni nguzo muhimu sana katika kuiwezesha Mahakama kutenda haki. Mahakama kama mhimili mkuu wa tatu wa dola inakuwa huru pale tu ambapo utendaji wake hauingiliwi na mihimili mingine. Hii ni pamoja na Majaji na Mahakimu kutokuingiliwa katika utoaji wa maamuzi, ajira zao na mafao yao kulindwa na sheria, pia kuwa na kinga dhidi ya mashitaka na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, moja ya mambo yanayoweza kuathiri uhuru wa Mahakama, ni Mahakama kutokutengewa fungu lake la pesa kama ilivyo mihimili mingine ya dola. Ni kwa mantiki hii, Mahakama ilimuomba Mheshimiwa Rais kuwa itengewe fungu lake kama ilivyo kwa mihimili mingine ya dola, ombi ambalo liliridhiwa na Mheshimiwa Rais katika Mkutano wake na Watendaji Wakuu wa Mahakama huko Bagamoyo. Kambi ya Upinzani inamuomba Mheshimiwa Waziri atoe ufanuzi iwapo fungu lililotolewa kwa Mahakama katika mwaka huu wa fedha ni utekelezaji wa ahadi aliyoitoa Mheshimiwa Rais, au ni mgawo wa kawaida amba Mahakama imekuwa ikipata kama “*idara*” ndani ya Wizara? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mahakama Kufungwa na Taratibu za Kiufundi (*Technicalities*) katika utoaji haki. Sheria ya Mwenendo wa Mashitaka ya Jinai (*Criminal Procedure Act*), Sheria ya Mwenendo wa Madai (*Civil Procedure Code*), Sheria ya Ukomu wa Mashitaka (*The Law of Limitation Act*) ndio zinazotoa taratibu za uendeswaji wa kesi lakini ni taratibu ngumu ambazo sio rahisi kueleweka kwa mwananchi wa kawaida (*lay persons*). Kuna wananchi wengi amba wamepoteza haki zao kwa sababu za kiufundi. Waathirika zaidi ni watu wenye kipato cha chini maana sio tu hawazifahamu sheria bali pia hawana uwezo wa kuajiri wanasheria wa kuwasimamia katika kesi zao. Kambi ya Upinzani inaiomba Wizara ishauriane na mahakama juu ya suala hili ili kuhakikisha kuwa wananchi hawakosi haki zao kwa sababu za kiufundi.

Mheshimiwa Spika, Ripoti za Kesi (*Law Reports*). Uchapishaji wa ripoti za kesi ni muhimu sana katika taaluma ya sheria. Ni kwa kupitia ripoti hizi wanataluma na wananchi wengine huweza kufahamu maamuzi ambayo yametolewa na mahakama katika kutoa tafsiri sahihi ya sheria. Kwa wanafunzi wa sheria, ripoti za sheria ni nyezo muhimu

ya kujifunzia, na kwa wanataaluma wote wa sheria hii ni nyenzo pekee ya kufahamu tafsiri mbalimbali za sheria. Pamoja na umuhimu wa ripoti hizi inashangaza kuona kuwa sasa ni zaidi ya miaka kumi toka kutolewa kwa ripoti ya mwisho mwaka 1998, badala yake wanataaluma wanaishia husoma vipande vya hukumu kwenye magazeti. Kambi ya Upinzani inamuomba Waziri aeleze ni kwa nini machapisho hayo hayajatolewa kwa kipindi hiki chote, na iwapo kuna mkakati wowote wa kuhakikisha kuwa ripoti hizi zinatolewa. Kutotoa Ripoti hizi ni kudidimiza taaluma ya sheria nchini.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inaipongeza Tume ya Kurekebisha Sheria kwa tafiti mabalimbali ambazo imekuwa ikifanya na hatimaye kutoa mapendekezo kwa Serikali juu ya uboreshaji wa sheria ambazo zinaonekana kuwa ni kandamizi au zimepitwa na wakati. Lakini pamoja na rasilimali nyingi zinazotumika kwenye tafiti hizi bado Wizara imeendelea kulipuuza suala la utekelezaji wa mapendekezo ya Tume hali ambayo imepelekea wanachi kuendelea kuumizwa na sheria hizo. Kwa mfano, utafiti wa Sheria ya Watoto Tume iligundua mapungufu makubwa kwenye sheria hizo hasa katika tafsiri ya nani mtoto katika nchi yetu, lakini hadi leo mapendekezo haya hayajafanyiwa kazi na badala yake Wizara imekuwa ikiahidi kuwa marekebisheso yako njiani. Hali ni kama hii kwenye Sheria za mirathi ambazo utafiti wake ulifanyika na kukamilika toka mwaka 1995.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa mwaka jana Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ya bajeti aliliyahidi Bunge lako Tukufu kuwa zoezi la kukamilisha waraka wa Serikali ulikusanya maoni ya wananchi na ya taasisi mbalimbali juu ya sheria za mirathi na sheria ya ndoa na zingekamilika ndani ya mwaka wa fedha 2008/09, na kuwa marekebisheso ya sheria zinazowahusu watoto yangewasilishwa Bungeni mwaka huo wa fedha lakini hadi leo bado hayajaletwa. Kambi ya Upinzani inauliza Je ni lini yataletwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi kubwa inayofanywa na Tume hii, Kambi ya Upinzani imegundua kuwa fungu linalotolewa kwa Tume katika bajeti bado ni dogo sana. Kwa mwaka huu wa fedha Tume imetengewa shilingi 1,314,657,000 tu. Kiasi hiki ni kidogo sana kwa Tume kama hii ambayo ina jukumu la kufanya tafiti juu ya sheria. Kuitengea Tume fungu kidogo ni sawa na kusema kuwa wizara inaitaka tume ipunguze kasi ya kufanya utafiti na hivyo kutoa mwanya kwa sheria kandamizi na zilizopitwa na wakati kuendelea kutumika.

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora sio tu kuliashiria nia njema ya Tanzania katika kulinda na kuheshimu haki za binadamu bali pia kulitoa matumaini kwa wanyonge na wahanga wa uvunjwaji wa haki za binadamu. Hata hivyo inasikitisha kuona kuwa Tume imeendelea kukosa ushirikiano kutoka idara za Serikali hali ambayo imeendelea kuwa kikwazo kikubwa katika ufanisi wa Tume. Idara hizi zimefikia hatua ya kutokeleza maamuzi ya Tume na hivyo kuendelea kuwanyima wananchi haki zao.

Mheshimiwa Spika, Tume imeendelea kutengewa fungu dogo sana katika bajeti, kitu ambacho tunaamini kinaathiri utendaji wa Tume. Katika bajeti ya mwaka huu Tume imetengewa kiasi cha shillingi 4,603,796,000 tu. Kambi ya Upinzani inadhani kuwa kiasi hiki bado ni kidogo sana kuweza kukidhi mahitaji halisi ya Tume. Kambi ya Upinzani

inaona kuwa Serikali imesahau kwamba kwa muda mrefu Tume imekuwa ikipata msaada toka *DANIDA*, msaada ambao sasa umefikia mwisho, hivyo basi jukumu la kuendesha shughuli zote za Tume sasa liko juu ya Serikali hivyo Serikali isiiishie kutoa fedha za za mishahara na mafao ya wafanyakazi tu bila kuiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Marekebisho ya Sekta ya Sheria ilitegemewa kuleta mapinduzi makubwa katika suala la utoaji wa haki. Lakini katika utafiti imeonekana kuwa hivi sasa programu hii ni kama vile imesimama (hii inatokana na kutolewana kati ya Serikali na wafadhili). Baadhi ya Vitu vinavyofanya programu hii isimame ni pamoja na vifuatavyo:-

(i) Serikali kung'ang'ania kuweka masharti tofauti kwa programme zake mabalimbali, kwa mfano, programu ya Utumishi wa Umma na programu ya Serikali za Mitaa (*Local Government Reform Programme*). Programu hizi mbili watendaji wake wanalipwa mafao tofauti (*markert salaries*) ambapo watendaji waliowengi wa Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria wanachukuliwa kama wafanyakazi wa Serikali na hulipwa mishahara ya kawaida. Hii inaleta unyonge mkubwa katika utekelezaji wa shughuli katika programu hii.

Kambi ya Upinzani inapendekeza kwamba Serikali itoe masharti na mafao yanayolingana katika programu zake zote.

(ii) Watendaji wengi wa Serikali kushindwa kuwa makini katika kufuata maelekezo hasa kuhusu manunuzi (*procurement*) kama ilivyoelekezwa katika programu hii, wao hupendelea njia za mkato na hivyo hukuta maombi yao mengi chini ya Programu hii yanakwama kwa sababu tu hawataki kufuata utaratibu.

Kambi ya Upinzani inapendelea kuwa Serikali iwe makini kusimamia Watumishi wake wanaohusika na programu hii na izidi kuonyesha *commitment* yake kwa wafadhili ili wasijiondoe na kuiweka sekta ya sheria gizani.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhampini (*Registration, Insolvency and Trusteeship Agency (RITA)*). Tangu kuanzishwa kwake mengi yamefanyika, baadhi ni: Kuboresha huduma za Usajili, Ufilisi na Udhampini kwa kuboresha mfumo wa mawasiliano (*Management of Information System*) ambao utawezesha ukusanyaji wa kumbukumbu zote za Wakala kwa kuunganisha Wilaya zote za Tanzania Bara. Mfumo huu utalinufaisha Taifa kwa kutoa takwimu sahihi kwa ajili ya mipango ya maendeleo ya nchi. Mfumo huu umeanza kutekelezwa katika makao makuu ya Wakala pamoja na Wilaya za Temeke, Kinondoni, Kibaha na Dodoma na uko mbioni kuunganishwa katika wilaya za Arusha, Tanga na Mwanza.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ina uhakika endapo Serikali itaiwezesha *RITA* kwa kuipa fedha zaidi na kuiimarisha mfumo wa usajili wa *RITA* ili kuweza kukusanya takwimu muhimu zinazohusu maisha ya Mtanzania, *RITA* itakuwa ndiyo chanzo cha takwimu muhimu kwa mifumo mingine kwa maendeleo ya nchi. Mfano;

Daftari la Wapiga Kura, mfumo wa elimu, mfumo wa afya, mfumo wa Taasisi za fedha, na ikiwezekena kuwa mbadala wa Sensa ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa hivi sasa Serikali inatumia mabilioni ya shilingi katika kukusanya takwimu kwenye mifumo hiyo, vitambulisho vya uraia vitahitaji taarifa sahihi za watu kutoka *RITA*. Hivyo *RITA* ikiwezeshwu itaweza kuokoa fedha nyingi zinazotumika na mifumo mengine ya kukusanya taarifa hizo hizo.

Aidha, baada ya kupitia kitabu cha matumizi Vol.II hatujaona bajeti ya Wakala wa *RITA*. Tunamtaka Waziri atuonyeshe ni wapi *RITA* imetengewa Bajeti yake kwa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia njema ya kuanzishwa kwa *Law School*, Taasisi hii imeendelea kukumbwa na matatizo mbalimbali ambayo yanaathiri utendaji wa taasisi na pia taaluma ya sheria nchini. Katika utafiti wangu nimegundua kuwa pamoja na kuendelea kutokuwa na jengo lake, taasisi hii imeendelea kukabiliwa na matatizo mengine makubwa mawili.

(i) Taasisi bado haijapata waajiriwa wake na badala yake imekuwa ikiwategemea mawakili na wanasheria wengine wakiwemo walimu kutoka vitivo vya sheria mbali mbali hapa nchini. Watu wote hawa hufanya kazi kwa muda (on temporary basis) na hivyo utendaji kazi wao kwa kiasi kikubwa hutegemea muda kidogo wanaopata katika shughuli na ajira zao za kudumu. Katika hali hii huwezi kutegemea kuwa taasisi itatekeleza kazi zake kwa ufanisi.

(ii) Suala la mikopo ni kikwazo kwa wanafunzi. Hali ya kutupiana mpira kati ya Bodi ya Mikopo na Wizara inaendelea, huku wanafunzi wakiendelea kuuumia kwa kukosa masomo. Mwaka huu mikopo ilitolewa kwa wanafunzi wachache tu huku wengine wamenyimwa, hali iliyosababisha migomo ya wanafunzi na hata kupelekea wanafunzi kusimamishwa masomo. Kambi ya Upinzani inaiomba serikali iangalie kwa makini suala la mikopo kwa wanafunzi wa Sheria maana mafunzo yanayotolewa na taasisi hii ni ya lazima kwa kila muhitimu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya Lugha ya Kiingereza katika Sheria. Tangu tupate uhuru tumeeendelea kutunga sheria zetu kwa lugha ya kiingereza kama vile sisi hatuna lugha nyingine ambayo inafahamika na Watanzania wote. Kambi ya Upinzani, inasikitishwa na kasi ndogo ya kutafsiri sheria zetu katika lugha ya Kiswahili ambayo ndio inayoelewka na kutumika na watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Spika, Kiswahili sio tu lugha inayotambulika na kutumiwa na Watanzania wengi bali pia ina misamiati mingi ambayo inaweza kukidhi mahitaji. Sheria tunazotunga katika Bunge letu ni kwa ajili ya watanzania. Je serikali haionti kuwa kuendelea na matumizi ya Kiingereza katika sheria inazifanya sheria zetu zioneckana kama sheria za kikoloni.

Mheshimiwa Spika, Matumizi ya Kiingereza katika Sheria zetu yamechangia uelewa mdogo wa sheria mionganii mwa wananchi maana asilimia kubwa ya watanzania hawawezi kusoma au kuielewa lugha ya kiingereza. Ikumbukwe Mheshimiwa Spika kuwa katika sheria zetu “*ignorance of law is no defence.*”

Mheshimiwa Spika, je, Serikali haoni kuwa matumizi ya Kiingereza inawanyima walio wengi haki zao wanapofika mahakamani, ukiondoa mahakama za Mwanzo, Sheria inaelekeza kuwa Kiingereza ndio lugha rasmi inayotakiwa kutumika kuendesha mashauri katika Mahakama za Wilaya, Mahakama Kuu na Mahakama za Rufaa.

Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze Waheshimiwa Mahakimu na Majaji ambao kwa kutambua hali halisi wamekuwa wakitumia lugha ya Kiswahili hasa pale ambapo mdaiwa/mshitaki ni mwananchi wa kawaida ambaye hana Wakili wa kumsimamia. Hata hivyo nyaraka zote zinazowasilishwa katika Mahakama hizi huwa katika lugha ya Kiingereza na hivyo wadai/wadaiwa huwa ni vigumu kwao kuelewa yaliyoandikwa katika nyaraka hizo na jinsi gani ya kuzijibu. Kuna idadi kubwa ya watu wamejikuta wakipoteza haki zao kwa kutokuelewa yaliyoandikwa kwenye hukumu. Wengine wamejikuta wakipoteza fursa ya kukata rufaa kwa sababu taratibu za kukata rufaa zimeelezewa katika lugha ya Kiingereza.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Mahakama ya Kazi kwa kutumia ya Kiswahili katika uendeshaji wa mashauri. Matumizi ya Kiswahili katika mahakama hii sio tu mfano wa kuigwa na mahakama nyingine bali unatufungua macho kuwa Kiswahili kinajitosheleza na kinawenza kikatumika katika utoaji haki.

Mheshimiwa Spika, uwakilishi wa kisheria ni muhimu katika usawa wa kupata haki (*legal representation*) Serikali inao wajibu wa kuhakikisha kuwa wananchi wanapata haki hii bila kujali hali zao za kimaisha maana *watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanayo haki bila ya ubaguzi wowote, kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria.* Kwa mwananchi wa kawaida (*lay person*) fursa ya kusikilizwa na mahakama haimuwezeshi kufaidi haki yake ya kusikilizwa Ili aweze kufaidi haki hii anahitaji kupata uwakilishi wa mtu amabaye anazifahamu sheria na taratibu zinazotumika mahakamani. Kwa kutambua umuhimu wa haki hii, Bunge lilitunga Sheria ya Msaada wa Kisheria katika Mashtaka ya Jinai (*The Legal Aid (Criminal Proceedings) Act, 1969*).

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo kwa sheria hii bado wananchi wa kawaida wameendelea kuumia maana sheria hii haina utekelezaji na wala serikali haijaweka utaratibu wowote wa utekelezaji wa sheria hii. Kambi ya Upinzani inaiomba Wizara kuhakikisha kuwa utaratibu wa utekelezaji pamoja na mpango madhubuti wa utoaji wa msaada wa kisheria unawekwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inatoa pongezi kwa Mashirika yasiyo ya Serikali (NGOs) na Asasi mbali mabali za kiraia kwa kuchukua jukumu la kutoa msaada wa kisheria japo uwezo wa mashirika na asasi hizi bado ni mdogo.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana wakati nikitoa hotuba yangu hapa Bungeni, niliongelea juu ya hoja ya mgombea binafsi na umuhimu wake katika kukuza demokrasia. Kambi ya Upinzani inasikitika kuona Serikali ilikata rufaa dhidi ya uamuvi wa Mahakama wa kuruhusu Mgombea binafsi. Hata baada ya Rufaa ya Serikali kukataliwa bado Serikali inafanya Juhudi ya Rufaa hiyo isikilizwe. Mwezi Mei, 2009 maombi ya Serikali yamekubaliwa na sasa kesi hiyo iko Mahakama ya Rufaa, Kambi ya Upinzani inahoji, kwa nini Serikali bado inaibana Demokrasia?

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kumekuwa na mjadala mkubwa juu ya kinga dhidi ya Mashtaka kwa Marais wastaifu. Pamoja na kuwa katika Ibara ya 46A(10), Ibara ya 46(1) pamoja na Ibara ya 46(2), zinamkinga Rais Mstaifu dhini ya Mashtaka yoyote ya Madai au Jinai kwa kosa alilofanya akiwa madarakani lakini Ibara ya 46(3) inaruhusu Rais Mstaifu kushtakiwa kwa jambo lolote alilofanya wakati akiwa madarakani ambalo halihusiani na kazi yake kama Rais.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, haioni sababu ya kuendelea na mjadala wa kuwa Rais Mstaifu anaweza kushtakiwa au la! Wakati Katiba iko wazi hasa Kifungu cha 46(3).

Mheshimiwa Spika, Sheria yetu ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya Mwaka 2007 Katika kifungu cha 27 inasema kuwa (ninanukuu):-

*27 (1) “Any person commits an offence of who, being or having been a public official:*

*(a) maintains a standard of living above that which is commensurate with his present or past lawful income;*

*(b) owns property disaaproportionate to his present or past lawful income,*

*Unless he gives satisfactory explanation to the court as to how he was able to maintain such a standard of living or how such property came under his ownership.”* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu hiki mtu akikutwa na fedha au mali inayozidi kipato chake halali anachukuliwa kwamba ametenda kosa la kupokea rushwa na inakuwa ni wajibu wake kuthibitisha kuwa mali hiyo aliipata kihalali.

Mheshimiwa Spika, kifungu hiki ni muhimu sana katika kufanikisha mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi. Kambi ya Upinzania inataka kujuwa watu wangapi wameshakamatwa kwa kutumia Kifungu cha Sheria ya Rushwa na hasa ukizingatia kuwa Mzigo wa kuthibitisha (*Burden of Proof*) uko kwa Mdaiwa. TAKUKURU imefumba macho kama vile kifungu hiki hakipo na hivyo kuendelea kulea rushwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inamwomba Mheshimiwa Waziri, awaamshe TAKUKURU na kuwataka wafanye kazi kwa mujibu wa sheria bila uoga wala upendeleo na bila kujali wadhifa alionao au aliokuwa nao mhusika.

Mheshimiwa Spika, wakati naingia kwenye jengo la Bunge leo, nimesimamishwa na watu 7 kutoka Morogoro amba walikuwa na kesi yao, ni Walimu na kesi imehukumiwa walipwe shilingi 166,000,000, lakini hadi sasa hawajapewa kitu chochote na wao waliandikia barua hii, wakampelekea Waziri kutaka kusaidiwa ili wapate mafao yao, lakini mpaka leo tokea mwezi Aprili, 30 hadi leo Mheshimiwa Waziri hata kutoa jibu hajatoa. Tunaomba, tumkumbushe Mheshimiwa Waziri kwamba yeze ndio mshika bendera wa mbele wa kuhifadhi haki za wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo ambayo niliyasema katika hotuba yangu ya mwaka jana lakini utekelezaji wake bado haujafanywa. Na kwa kuwa mambo yenye we ni muhimu, naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge ili wanisaidie kuweka msisitizo:

(1) Hoja ya Katiba Mpya: pamoja na hoja hii kuwa kilio cha Kambi ya Upinzani na watanzania wengi serikali imeendelea kuipuuza na kuifumbia macho licha ya ukweli kuwa suala la Katiba mpya ni la msingi na haliepukiki.

(2) Adhabu ya Kifo: Adhabu hii imeendele a kuwepo ndani ya sheria zetu licha ya upinzani mkubwa unaotolewa na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi.

(3) Matumizi ya teknolojia katika mahakama: mahakama zetu zimeendelea kuwa nyuma katika matumizi ya teknologia hii.

(4) Mauaji ya Maalbino na vikongwe: Pamoja na matatizo haya kuendelea kwa kasi ya ajabu na hivyo kutishia usalama wa makundi haya na jamii kwa ujumla, kasi ya ushughulikiaji hauridhishi.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, narudia kutoa shukrani zangu za dhati kwa kupata fursa hii. Pia nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu amba wamekaa na kunisikiliza.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na kwa heshima na taadhima naomba kuwasilisha. (*Makofifi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimepokea maombi saba ya wachangiaji na sidhani kama wote watapata nafasi kwa sababu hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria na hoja yake, imepangwa tuimalize leo, nitawataja watatu wa mwanzo ambaa ndiyo watapata nafasi ya kuongea. Kwanza, ni Mheshimiwa Manju Msambya, atafuatiwa na Mheshimiwa Rajab Hamad Juma na Mheshimiwa Diana Chilolo ajiandae.

**MHE. MANJU S. MSAMBYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza katika hoja hii muhimu ya Katiba na Sheria. Kabla sijaanza kuchangia, naomba na mimi nitoe rambirambi kwa Sheikh wetu, Sheikh Suleiman Mohamed

Gorogosi, aliyekutwa na maafa kutona na ajali ya gari. Mimi binafsi alikuwa ni Mwalimu wangu wa dini; kwa hiyo kwangu mimi ni pigo.

Lakini vilevile natoa rambirambi kwa Jumuiya ya Wasomi na hasa Wasomi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kwa kuondokewa na Prof. Haroub Othuman, ambaye bahati nzuri kwa miaka mitatu niliyokuwepo pale kama mwanafunzi, alikuwa ni Mwalimu wangu. Lakini Prof. Haroub Othman, amekuwa ni Mwalimu wa Watanzania wengi hasa kwenye vipindi vyake ambavyo alikuwa anashiriki kwenye *television* zetu. Kwa hiyo, naomba Mungu awajalie awaweke mahali pema peponi, amen.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza hayo, nianze kwa kusema kwamba, napata taabu kuunga mkono hoja hii na kinachonipa taabu ni kwenye Ibara ya Tisa ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri lakini nitakuja huko baadaye.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kupata taabu lakini vilevile nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa kazi nzuri anayoifanya kwenye Wizara yake maana mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni. Mheshimiwa Waziri kwa muda wa takriban miaka miwili sasa amekaa pale, amefanya mambo mengi tu. Alipokuwa anasoma hotuba yake, nimemsikitikia kwa jambo moja. Anasema amepewa pesa za bajeti ya maendeleo shilingi bilioni 40.4. Wizara yenye majukumu mazito kama hii, unaipa shilingi bilioni 40, hivi utaleta maendeleo gani ya kisheria kwa wananchi wa Tanzania wenyewe kumtazama yeye kwa shilingi bilioni 40.4? Kwa hiyo, pamoja na kumpongeza kwa kazi nzuri anayofanya, namwonea huruma sana anapewa pesa ambazo ukimfungia inzi anaruka nazo. Hazitoshi!

Mheshimiwa Spika, nizungumize kidogo kwenye masuala ya Jimbo langu. Jimbo langu lina mazingira magumu sana, karibu kila kitu lakini leo nizungumzie suala la Sheria. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri anisaidie kupata ufumbuzi wa majengo ya Mahakama ya Mwanzo. Jimbo langu linapakana na Mkoa wa Rukwa Kata ya Kaja. Kukitokea tatizo la kimahakama kule, inabidi mtu aje Ilagala zaidi ya Km 400 au aje Mahembe Km. 450 au aje Kigoma Mjini Mahakama ya Mwanzo ya Ujiji. Sasa hapo kwa lugha ya hawa wanaosema, *the learned brothers*, haki inakuwa haitendeki kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, vile vile, yako haya Mabaraza ya Ardhi ya Kata, Mheshimiwa Waziri ameyazungumzia vizuri sana katika hotuba yake. Naomba waliopewa dhamana kwenye Mabaraza ya Ardhi ya Kata, wapate mafunzo ya uhakika kama walivyosema na yawe yatakayokwenda kwa undani sana maana kule ndiko ambako migogoro ya ardhi inaweza ikaleta hata mauaji. Kwa hiyo, Wizara kwa malengo iliyoweka, ijitahidi sana itoe mafunzo ya kina kwa wale wanaoendesha shughuli hizo maana kule wengine hata darasani hawakupita, anajua kusoma na kuandika, sasa wapewe mafunzo yanayostahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niipongeze Wizara kwa juhudi inazofanya za kutengenisha masuala ya uendeshaji wa mashauri Mahakamani na upelelezi. Nashukuru Polisi sasa wanaachiwa majukumu yao ya msingi na Mahakama inakwenda awamu kwa awamu kufanya shughuli za uendeshaji kesi Mahakamani, zisimamiwe na Mawakili na Serikali.

Naomba nitoe rai na ombi kwamba basi kwenye Idara ya Mahakama; mafunzo ya Wanasheria yapewe kipaumbele cha juu kama vile ambavyo sasa tumetoa kipaumbele kwenye mafunzo ya Ualimu. Karibu kila Chuo Kikuu sasa hivi kina mtaala unaofundisha Walimu ili shule zetu tangu za msingi, sekondari na vyuo vijitosheleze kwa kuwa na Walimu wa kutosha. Kwa utaratibu huu wa sasa kwamba uendeshaji wa mashauri Mahakamani utaendeshwa na wasomi wa Sheria, basi tufanye vilevile kwamba Wanasheria wasomeshwe kwenye kila Chuo Kikuu ili Mahakama hizi zipate Wataalam haraka sana maana awamu inaweza ikachukua hata miaka ishirini. Tuwaachie Polisi wafanye kazi zao za msingi za usalama wa raia na mali zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka nizungumzie, ni suala la *OIC*. Hili ni suala la Kikatiba na hapa ni mahali pake. Sikumsikia Waziri akizungumzia hatua zozote ambazo pengine Serikali inakusudia kuzifanya, mwaka jana, alitoa kama kurashiarashia tu. Sasa ingekuwa ni vizuri wakati atakapokuwa anajibu hoja zetu atuambie suala hili limefikia wapi.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nilichangia na nikamweleza Waziri, nchi ambazo wala hazina Uislam, hazina chochote, ni wanachama, wengine ni jirani zetu hapa mfano Msumbiji, Uganda na wanafaidika tena kwa kipindi hiki cha mtikisiko wa uchumi, ndio wamefaidika zaidi kuliko hata wakati ule ambaو uchumi ulikuwa mzuri. Hivi kwa nini Tanzania isifaидike kwa hilo?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho yake, atueleze kwa nini mpaka sasa Serikali inashindwa kutoa kauli kuhusu nchi hii kujiunga na *OIC*. Kama nchi ambazo *purely* sio za kiislam, zinajiunga na *OIC* na zinafaيدika, Tanzania ambayo haielekei upande wowote, kwa nini inanyimwa haki hii? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine, Mwalimu aliwahi kusema kwamba *quinin* ni chungu lakini ukiumwa Malaria hakuna namna nyingine ya kupona, kunywa quinin. Sasa hili ambalo nataka kulisema kwa baadhi yetu humu, litakuwa ni chungu.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni umetoka Waraka wa Kichungaji, unaoelekeza Watanzania namna wanavyotakiwa kuchagua viongozi wao. Ndugu zangu Watanzania tunakwenda wapi? Kama leo ma-*Sheikh* watacaa Misikitini, waekelze wapigakura namna ya kuchagua viongozi wao, hebu turejee yaliyotokea Biafra mwaka 1966. Mimi wakati ule nilikuwa Kidato cha Kwanza, tunaelewa yaliyotokea. Matatizo ya Nigeria yanafichwafichwa, mgogoro ulikuwa ni dini. Sasa upo Waraka wa Kichungaji, wa kuelekeza watu namna ya kuchagua tangu wawakilishi, watumishi wengine mpaka viongozi wa kisiasa. Kwa nini Waraka huo unaandaliwa kwa dhehebu moja tu katika madhehebu ya Kikisto? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hili nimesema ni *quinin* na ni chungu. Nimelijadili na Wabunge wenzangu nje, wengine wamenipa hadi jina, mimi sijali jina ninalolitambua zaidi ni lile nililopewa na wazazi wangu, hayo watakayonipa acha wanipe. Tusiifikishe nchi hii mahali ambapo viongozi wa dini ndio wanajaribu kutafuta mstakabili wa

uendeshaji wa nchi yetu. Hao hao mwaka jana walikuwa wanatuambia tusichanganye dini na siasa. Leo wameingia Makanisani wanasesma tuchanganye dini na siasa, wametoa Waraka wa Kichungaji wanapeleka kwa waumini wao. Ukishapeleka Waraka ule, maana yake unamwambia, wewe ukitaka kuchagua, mchague Mkristo mwenzako, Muislamu usimchague. Hii nchi tutaijunjavunja na ndiyo inachukuliwa kama nchi ya mfano, sio tu kwa Afrika, ni kwa dunia nzima.

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya Waraka huu sitaki kumtaja kwa jina Waziri mmoja alikuwa anahojiwa na vyombo vya habari akaungu mkono. Waziri wa Serikali ya Chama cha Mapunduzi, anasema hili halina matatizo, ni watu wanawaelimisha waumini wao. Leo akitokea Sheikh wa madhehebu fulani katika nchi hii naye akasema tukutane kwenye Msikiti wa Mnyamani, tuenze kufundishana namna ya kupiga kura, itakuwa sahihi?

Mheshimiwa Spika, tuache hili. Mimi leo asubuhi nimemsikiliza Kiongozi wa Dini ya Kikristo akiwa amezungumza kwa hekima sana. Sio wa madhehebu yaliyotoa Waraka alikuwa kama anakemea suala hili, namshukuru sana yule kiongozi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa niende kwenye lile la Mahakama ya Kadhi na nitasema kwa nini sikubaliani na Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri anataka kuwapaka wenyewe kuhitaji Mahakama ya Kadhi mafuta kwa mgongo wa chupa.

Mheshimiwa Spika, hatua zote hizi zilizokwishachukuliwa, analipeleka suala hili kwa watalaam, halafu uamuza utakaofikiwa huko mwisho, suala hili liingizwe katika sheria za kawaida. Tatizo liko wapi la kuunda Mahakama inayojitegemea? Iko Mahakama ya Ardhi, mbona haikuungizwa kwenye sheria? Ilionekana haiwezi kushughulikia masuala ya ardhi ikiwa katika mfumo wa sheria tulio nao! Iko Mahakama ya Biashara, iko Mahakama ya Kazi, zote hizi zimetenganishwa kwenye mfumo ule, li kurahisisha utoaji wa haki. Kwa nini Mahakama ya Kadhi ndio tuoanishe sheria ili ziwe zinatolewa hukumu kutokana na sheria zilizopo? Kuna tatizo gani la kuanza Mahakama ya Kadhi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Ardhi, kama nilivyoanza kuzungumza, ipo na Mabaraza ya Ardhi tangu chini. Lakini Mahakama ya Kadhi inaonekana ni kikwazo, kwa nini? Au ndio ile kauli Mheshimiwa Waziri mwaka jana alipokuwa anahojiwa na Vyombo vya Habari akasema hili suala mpaka watu wa upande wa pili wakubali na kwa sababu inaonekana hawajamkulalia, basi anataka kulileta kwa ujanja ujanza tu? Watu wa upande wa pili aliokuwa anamaanisha ni Makanisa.

Mheshimiwa Spika, sasa nchi hii ni yetu wote, hakuna yeoyote kuanzia Rais wa nchi mwenye hati miliki ya nchi hii. Sisi wote tuna haki sawa katika mambo yote ya uendeshaji wa nchi, yaani tunataka kama kuwalainisha watu hivi. Hapana, tufanye mambo ambayo Watanzania wakikaa, wanasesma hili ni la Watanzania wote. Mheshimiwa Waziri alikuwa anazungumzia namna ya kushughulikia masuala ya talaka, masuala ya mirathi, kuna tatizo gani Waislam wakashughulikia masuala yao ya talaka na

miradhi kama ambavyo imani yao inasema? Tatizo liko wapi mpaka tuambwiwe kwamba hizi zitaunganishwa na sheria zingine? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jana Mheshimiwa Waziri alinitania, akaniambia, safari hii naona mambo yamekwenda vizuri, naomba usinikwaruze. Hili sio la Msambya, ni la Waislam. Msambya anaweza hata kesho akaondoka, Mungu apishe mbali, lakini hili ni la Waislam, Waislam ndio wanaomba Mahakama ya Kadhi. Kwa hiyo, Waislam wapewe Mahakama ya Kadhi, sio wawekewe sheria ndani ya sheria zilizopo katika nchi ili waweze kuamua mambo yao.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nilieleza hapa na sitaki kurudia, kazi ya Mahakama ya Kadhi. Sasa tunaambiwa kiujanja ujanja, nchi haiendeshwi kwa ujanja ujanja, hapana! Nchi inaendeshwa kwa muala unaoeleweka na muala ni kufuata sheria. Hii ni Wizara ya Katiba na Sheria, sasa tunaletewa ujanja ujanja? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, napata kigugumizi kuunga mkono hoja hii kama sikupata ufumbuzi wa masuala mawili; Mahakama ya Kadhi na Waraka wa Kichungaji ambao unataka kuwagawa Watanzania. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Msambya kwa mchango wako. Namwita sasa Mheshimwa Rajab Hamad Juma, atafuatiwa na Mheshimiwa Diana Chilolo.

**MHE. RAJAB HAMAD JUMA:** Mheshimkiwa Spika, ahsante sana. Nami namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kupata nafasi hii na nakushukuru wewe ambaye amekuagiza unipe.

Pili, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, kwa hotuba nzuri ambayo nakubaliana na wenzangu, imeendelea kuboresha Wizara hii ukilinganisha na miaka michache iliyopita.

Mheshimiwa Spika, mimi naunga mkono hoja hii na sitakuwa na mengi kwa sababu ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, isipokuwa nitakuwa na machache ya kusisitiza yale ambayo yalikwishakusemwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, kwenye Idara ya Mahakama. Idara hii inafanya kazi vizuri, tunaipongeza sana na inaonekana namna ambavyo inastahili kupata sifa hizo. Lakini inaonekana tatizo liko kwenye Serikali kwa maana ya kuwa haiipi fursa za kutosha ikaendelea kukamilisha yale mapengo ambayo yako kwenye Idara hii.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, hivi karibuni Kamati yetu ilitembelea Mahakama za Mkoa wa Dar es Salaam. Kwa jumla, zinasikitisha sana. Wale Makarani ambao si Mahakimu, kwa baadhi ya Mahakama, hawapati nafasi ya kukaa mpaka Hakimu amalize kesi, ndio wao wapate hicho chumba, ndio wanakuwa wamepata ofisi wakati huo, yaani wanarithishana ofisi kati ya Hakimu na wale *staff*. Kwa kifupi, hakuna majengo ya kutosha katika Mahakama zetu.

Mheshimiwa Spika, kadhalika hakuna vifaa, mpaka leo Mahakama zetu zinapiga ripoti zake kwa chapa zile za zamani (*typewriters*). Hakuna viti vy a kutosha, hakuna meza, watumishi wanabdalishana, anayetoka ndiye atam-leave mwenzake aliyekuwa amesimama, hali sio nzuri kabisa. Pia Mahakimu wanadai sana posho zao. Haki zao za posho haziko katika ukamilifu.

Mheshimiwa Spika, aidha, baadhi ya Mikoa mingine ambako vile vile Kamati yetu ilipata nafasi ya kwenda kutembelea kupitia *TASAF*, lakini tuliziona na Mahakama. Mahakimu wanakwenda masafa marefu, kutoka anakokaa mpaka anakofanya kazi kama kilomita 70, hana balskeli, hana Honda, hana kipando chochote, hali sio nzuri kabisa.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kwa sehemu hii ni *pending case* zimekuwa nyingi mno, kesi ambazo zinakosa kusikilizwa ni nyingi sana. Inawezekana sababu zikawa hizo, lakini vile vile kutokana na ile *quotation* ambayo, mie si bingwa, lakini nampongeza Mama Maghimbi aliitaja, kutoka kwenye *speech* ya Jaji Mkuu, mwaka jana alipozungumza na Majaji, basi inaonekana wazi kuwa haki za wananchi wetu zinachelewa sana. Inawezekana ni nusu tu ya kesi ambazo zinapelekwa Mahakamani ndizo zinazosikilizwa kwa mwaka mzima, zinakutana na mwaka wa pili na wakati mwingine zinaweza zikakaa hata miaka mitatu.

Mheshimiwa Spika, sasa naelekea kwenye Tume ya Haki za Binadamu, nayo naipongeza inafanya kazi vizuri. Juji hapa tumepata kitabu cha ripoti zake kikubwa tu lakini pia nayo ina mapengo mengi ya kazi. Binadamu kwa ujumla wake ana njia nyingi sana na kwa *definition* ya haraka, basi binadamu ni kizazi kinachotokana na Nabii Adamu na Mama Hawa, lakini, haki zao zimejigawa katika njia nyingi sana. Kuna haki za watoto, haki za watu wenyewe ulemavu, haki za akina mama, haki za akina baba, kuna haki za namna nyingi sana katika kuangalia hili suala la haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, wiki iliyopita, uliwapa nafasi Waheshimiwa Wabunge wanne kwenda kuhudhuria semina ya *Child Rights* pale Dar es salaam, mmojawapo nilikuwa mimi. Tulifika pahali tukaona namna ambavyo nchi yetu ilivyo chini kabisa katika hii *level* ya haki za watoto.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile ukiwatizama na walemvu nao wanasema haki zao ziko nyuma sana. Maalbino ndio tunajua hivyo walivyo, akina mama siku zote nao wanadai haki zao humu, ukipita katika Magereza unawakuta Wafungwa na wao wana haki zao. Lakini ukizungumza na Makamishna wa Tume hii, tatizo kubwa wanaloopata ni uchache wa bajeti, wanashindwa kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, namshauri Mheshimiwa Waziri ili tufike mahali pazuri katika kutafuta haki za binadamu kuliko hapa tulipo hivi sasa, basi Tume hii iongeze wigo na ienee katika Mikoa, isibakie katika Makao Makuu ambayo yapo pale Dar es salaam au zile *Head Office* zake nyingine zilizoko Zanzibar na kwingineko. Ishuke zaidi, iwe na watendaji wengi, ili ifanye kazi katika Mikoa, nadhani itakuwa ni njia moja ya kuweza kuzifikia katika kiwango kizuri zaidi hizi haki za binadamu kupitia sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni *Labour Court* (Mahakama ya Kazi). Tunapokuwa na wanachini wetu wanalamikia sana Mahakama hii na wanacho kilalamikia ni kuwa wanasema haina meno, inatoa mamuzi, yanakuwa wazi kabisa, lakini utekelezaji wake haupatikani. Sasa sijui kama inatofautiana na zile Mahakama nyingine au kuna *element* nyingine za rushwa ndio maana labda ikawa hazifanyi kazi, maana hukumu inapotolewa na Jaji, halafu isifanye kazi, hapo kuna kitu, ipo hoja na inaoenekana kama kesi za namna hiyo ni nyingi, zinahukumiwa, zinafikia maamuzi, lakini wanaostahiki kupewa haki, hawapati haki.

Mheshimiwa Spika, nikiondoka hapo, naelekea kwenye *Law Reform Commission*. Sote tunakubali kwamba Tume ya Jaji Nyalali ilifanya kazi nzuri ya ku-*identify cases* ambazo zingeweza kufanyiwa maboresho na Mheshimiwa Waziri ametaja baadhi ya zile ambazo zimefanyiwa maboresho. Lakini Sheria 43 zilizochambuliwa wakati ule, mimi naamini zingekuwa zimeishakamilika, lakini nayo *Commission* hii inakutwa na tatizo lile lile la uhaba wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, tulipokuwa tunazungumza nayo kwenye Kamati zetu, ilifika mahali ikawa Tume hii inatuambia hata watumishi wake sasa wanaondoka, wanahama, wanakwenda kwenye sekta nyingine za kibinagsi. Kwa nini wanakwenda huko, kwa sababu maslahi yao ni madogo mno, kwa hiyo wanakwenda zao *VODACOM* na wengine wanakuja zao kule Kempiski Zanzibar kwenye mahoteli makubwa makubwa ambayo wanapata...

**SPIKA:** Samahani Mheshimiwa, kengele ya pili hiyo.

**MHE. RAJAB HAMAD JUMA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja! (*Makofit*)

**SPIKA:** Ahsante, pole sana! Namwita msemaji wa mwisho kwa mchana huu, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi ya awali kabisa, kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunitia nguvu, afya na uwezo wa kuweza kutoa mchango kwa asubuhi ya leo, juu ya Wizara ya Sheria na Katiba.

Pili, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa jinsi anavyowajalia wanawake wa Mkoa wa Singida, kwa kuendelea kujenga imani na mimi jambo ambalo limekuwa likinitia nguvu na kuendelea kuwa mtumishi mwema kwao pamoja na kutoa michango hapa Bungeni. Nikushukuru na wewe pia kwa kunipa nafasi hii, ili niweze kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizi, sasa nichukue nafasi hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mathias Chikawe, pamoja na Katibu Mkuu na Watendaji wake wote kwa jinsi walivyoandaa bajeti vizuri, bajeti ambayo iko wazi. Ni imani yangu kwamba wataitekeleza vyema kadri walivyoandaa.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizi, sasa nianze kutoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba niongelee suala la ujenzi wa Mahakama Kuu Mkoani Singida. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa kuona umuhimu sasa kutekeleza azma yake ya kujenga Mahakama Kuu Mko wa Singida. Jambo hili amelianisha wazi kwenye hotuba yake ukurasa wa saba, fungu la kwanza. Ni imani kwamba kuazimia ni jambo moja na kutekeleza ni jambo la pili. Lakini, kwa tabia ya Mheshimiwa Chikawe pamoja na timu yake, nina hakika kabisa sasa ajenda hii ya kujenga Mahakama Kuu, Mkoani wa Singida itatekelezwa. Namuombea Mwenyezi Mungu azma hii itimie kwani wananchi wa Mko wa Singida kupitia Mkuu wa Mko wetu Pasko Kone, tuna uchu wa maendeleo na maendeleo ni pamoja na kuwasogezea wananchi huduma hapo walipo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hoja hiyo, sasa niongelee jambo la pili nalo ni ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Iramba. Napenda kuieleza Serikali, Wilaya ya Iramba toka Uhuru mpaka hivi ninavyozungumza haina Mahakama ya Wilaya. Imekuwa ikiendesha kazi zake kwa kutumia Mahakama ya Mwanzo.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba sana Serikali iache tabia ya kupora Mahakama za Mwanzo. Mahakama hizi ndizo Mahakama ambazo ziko karibu na wananchi na kesi nyingi za wananchi huwa zinaishia Mahakama za Mwanzo. Ninaomba sasa Mheshimiwa Waziri aone umuhimu wa kujenga Mahakama ya Wilaya ya Iramba ili waweze kuachia hiyo Mahakama ya Mwanzo iweze kufanya kazi ya kuendesha Mahakama za Mwanzo. Ninaomba sana sana Mheshimiwa Waziri, nina imani na wewe, jambo tu la Mahakama Kuu niliongea na wewe, ukatuma Mtendaji wako, Afisa wa Ngazi ya Juu mpaka Singida na amerudi jana. Nina imani amefika mpaka Iramba kuona jinsi ambavyo hatuna Mahakama. Ninaomba sana Wilaya ya Iramba sasa ifikiriwe kupata Mahakama ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuongea hilo, naomba nizungumzie kuhusu Mahakama ya Wilaya ya Manyoni. Mahakama ya Wilaya ya Manyoni kweli ni Mahakama ya Wilaya, lakini haina hadhi kabisa ya kuwa Mahakama ya Wilaya. Kwanza, ni ndogo sana, wala hajitoshelezi.

Mheshimiwa Spika, naomba tuwajali watendaji wetu, Mahakimu wetu wana elimu zao safi, wamesoma wakiwa wana imani kwamba Serikali itawapa mahali pazuri pa kufanya kazi. Lakini, ukienda kuitizama Mahakama ya Wilaya ya Manyoni, haina hadhi kabisa ya Mahakama ya Wilaya. Ninaomba nayo ifikiriwe kupanuliwa ili iweze kumpa heshima yule Hakimu anayefanya kazi na impe uwezo wa kufanya kazi zake vizuri kama Mahakama zingine zinavyojengwa kwenye Wilaya mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kuhusu gari la Hakimu wa Mko. Ni kweli tulipata gari la Mahakama ya Mko, lakini gari hili hivi ninavyozungumza

limekufa na nina taarifa za kutosha. Magari haya aina ya Honda, yaliyotolewa kwa Mahakama za Mikoa, asilimia 50 yameshakufa. Ni wazi kwamba magari haya ni aina ambayo haina spea hapa Tanzania. Ninaomba niishauri Serikali, pale inapoagiza ama inapotoa tenda kuagiza aina fulani ya magari, basi iwe na utaratibu mzuri wa kutafuta hata gereji moja kuiagiza ilet spea zinazofanana na magari hayo waliyoagiza. Magari haya mengi yamekufa, hayafanyi kazi, hii yote ni uharibifu wa pesa za Serikali.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Mheshimiwa Waziri aangalie namna ya kufufua magari haya kwa sababu sasa hivi Singida tumepata gari la Wilaya, hata kama halitapatikana la Mkoa, ninapata wasiwasi inawezekana gari la Wilaya lisifanye kazi zake vizuri, akalipora Hakimu wa Mkoa, jambo ambalo halitakuwa zuri na halitakuwa lengo lenu kupeleka gari lile la Wilaya. Naomba sana sana gari hili la Mkoa likarabatiwe ili liweze kutoa huduma ipasavyo na magari yote nchini yaliyoharibika kama hilo la Mkoani Singida, yakarabatiwe.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia hilo, naomba kuzungumzia posho za Wazee wa Baraza. Ni kweli Wazee wa Baraza, wanapata posho na kila kesi Mzee wa Baraza anapata shilingi 1500. Hii hela ingeweza kutosha, lakini kesi hiyo moja inaendeshwa kwa muda mrefu sana, inachukua miezi mitatu mpaka sita. Hivi kweli huyu Mzee wa Baraza ataendelea kuisubiri tu hiyo 1500 kwa kipindi chote hicho? Ninaomba sana kama inawezekana kiasi hiki cha pesa kiongezeke na kama hakitaongezezeka, basi tuangalie utaratibu wa kumaliza kesi zetu haraka.

Mheshimiwa Spika, kesi zetu zinachukua muda mrefu kwa sababu hata Mahakimu ni wachache, unakuta Hakimu mmoja anaendesha Mahakama tatu mpaka tano. Kama Hakimu anakuwa na Mahakama tano, unafikiria kesi hizo zitaisha upesi? Hata ufanisi wa uendeshaji wa kesi hautakuwa mzuri. Ninaomba sana sana, tatizo pia la Hakimu linachangia maslahi ya Wazee wa Baraza kuonekana ni hafifu. Hivyo basi, Seikali ijitalidi sana kusomesha Mahakimu wengi ili Mahakama za Mwanzo ziwe na Mahakimu wengi. Kukosekana kwa Mahakimu wengi, kesi nyingi zinalala na Kauli Mbinu ya Serikali ni Kilimo Kwanza lakini ikumbukwe kwamba tunaposema Kilimo Kwanza, mwananchi anapokuwa na kesi, akili yake inachanganyikiwa, anakuwa anaiwaza kesi tu hata ule uwezo wa kulima unakuwa mdogo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba basi tusomeshe Mahakimu wa kutosha ili Mahakama nyingi ziwe na Mahakimu, tuachane na utaratibu wa Mahakama zetu tatu mpaka tano kuwa na Hakimu mmoja, jambo ambalo linachelewesha kesi nyingi sana. Wananchi wanavunjika moyo, wananchi wanashindwa kuzalisha mali, wanashindwa kufanya kazi, wanakuwa watumwa wa kutembea Mahakamani, lakini kesi ni kuahirishwa, ni kuahirishwa, ni kuahirishwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo, naomba kuzungumzia vitendea kazi. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri ametueleza katika hotuba yake kwamba suala la vitendea kazi atalipa kipaumbele. Kwa kweli, suala hili ni kero sana. Kuna maeneo hata mimi mwenyewe nimeweza kujitolea kusaidia Mahakama za Mwanzo kutoa vitendea kazi, hawana hata makaratsasi, hukumu za kesi mbalimbali hazitolewi ama zinatolewa kwa kucheleva kwa sababu vitendea kazi hamna. Sasa hivi ni sayansi na teknolojia,

tunataka kompyuta kwa Mahakama ya Mkoa, Wilaya na Mwanzo ili turahishe kazi za Mahakimu wetu. Ninaomba sana hawa watendaji tuwathamini, tuwajali, tuwawekee vitendea kazi ambavyo vitawafanya waweze kutekeleza kazi zao vizuri na kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kuhusu sheria mbalimbali ambazo zinawalinda wanawake na watoto. Tumeimba sana hapa Bungeni kwamba ziko sheria nyingi ambazo zinawakandamiza wanawake na watoto. Tunaomba basi huo mchakato, hivi hili neno mchakato, upembuzi, itakuwa mpaka lini? Hebu zileteni tuzipitishe ili akina mama na watoto waweze kupata haki zao za msingi. Haya matumizi ya mtoto shilingi 100 yameshaptwa na wakati. Ninaomba sana Serikali iharakishe kutuletea sheria hizi ili tuweze kuzipitisha, ziweze kutenda haki kwa akina mama wanaopata matatizo mbalimbali katika ndoa zao amba wengi wao hawapati haki zao za msingi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia hilo, naomba nizungumzie kuhusu Tume ya Haki za Binadamu pamoja na utawala bora. Naipongeza sana hii Tume inafanya kazi nzuri, inajitahidi kutoa elimu kwa wananchi ili waelewe haki zao za msingi na utawala bora ni nini. Tume hii wanakuwa ni watu wa kukaa Dar es Salaam, hawatembei, Singida hatuwajui, nina amini hata Mikoa mingine hawafiki. Nimejaribu kuongea na Afisa mmoja, hivi shida yenu ni nini mbona hamtembei, wananchi wanahitaji elimu, vipi? Wameniambia Mheshimiwa Chilolo, tatizo letu ni fedha.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali, pamoja na kutoa vipaumbele katika Wizara mbalimbali, naomba pia mzifikirie na Wizara zingine kama Sheria na Katiba, ninaamini Mheshimiwa Chikawe si mchoyo wala hana upendeleo na sekta yoyote katika Wizara yake, lakini fedha ndogo ndio maana taasisi zingine zinakwama. Nina hakika tukiwapa watu hawa hela za kutosha, hata Tume hii itafanya kazi zake vizuri, itafika Singida, itafika Mwangeza, itafika mpaka Rungwa na maeneo yote yaliyoko pembezoni ili wananchi wakiwemo wanawake wapate elimu ya kutosha kujua hazi zao na kuelewa utawala bora wa nchi yetu, unasema nini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo, sasa naomba nitumie nafasi hii, kumshukuru sana Mheshimiwa Chikawe kwa jinsi anavyotujali wana-Singida, anajua kabisa tuna uchu wa maendeleo na taarifa inaonyesha kwamba tayari Mahakama ya Mwanzo Utmini imekamilika. Sasa naamini atatufikiria na Mahakama nyingine za Mwanzo kwa sababu Singida, Kata nyingi hazina Mahakama za Mwanzo na kama zipo, zimechakaa sana. Kwa hiyo, tunaomba sana katika vipaumbele vyako vyta kujenga Mahakama za Mwanzo, Singida usituache.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja na nawataki utekelezaji mwema. Ahsante sana. (*Makofit*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda uliosalia wa dakika mbili/ tatu, kwa mujibu wa Kanuni, hautuwezeshi tena kuendelea ila kabla sijasitisha shughuli za Bunge kwa mchana huu, naomba niwataje wachangiaji wetu wanne na sitegemei zaidi ya hapo kwa sababu ya hatua ya Kamati. Wa kwanza saa 11.00 jioni atakuwa Mheshimiwa Felix

N. Kijiko, Mheshimiwa John Momose Cheyo, Mheshimiwa Dr. Luka Siyame na hatimaye atakayehitimisha mjadala huu wa Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria ni Mheshimiwa John Magalle Shibuda. Baada ya hapo, Mheshimiwa Waziri atakuwa na dakika zisizozidi 30 za kufanya majumuisho, halafu tutaendelea na taratibu zingie zinazofuata.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru kwa ushirikiano wenu na sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka hapo saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.54 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilipokuwa nasitisha shughuli za Bunge pale mchana, nilitangaza kwamba, bado tunao wachangiaji. Jioni hii bado tunao wachangiaji wanenye, niwataje tu wajiandae; tutaanza na Mheshimiwa Felix Kijiko, atafuata Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Dr. Luka Siyame na hatimaye Mheshimiwa Magalle Shibuda. Kwa sasa tunaanza na Mheshimiwa Kijiko.

**MHE. FELIX N. KIJKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu, lakini kabla sijaanza kuzungumza ambayo ninayo, naishukuru familia yangu, kwa matunzo mazuri ninayopata na kuniwezesha kuja hapa Bungeni bila kuugua. Nawashukuru sana Wananchi wa Jimbo langu la Mhambwe, kwa kuniamini na kunipa dhamana hii ya kuja kuwawakilisha katika Bunge Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninawashukuru sana kwa hilo. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijazungumza niseme tu kwamba, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Wizara ya Katiba na Sheria ni chombo muhimu sana katika kuiongoza nchi, kwa sababu bila Sheria, basi nchi itayumba. Kwa hiyo, ni Wizara ambayo ni nyeti sana. Nimejaribu kuipitia Hotuba yake hii, pamoja na kwamba, Mheshimiwa Waziri aliisoma, nimpongeze yeye na wataalamu wake, kwa sababu hii hotuba imeandikwa kitaalamu. Isipokuwa kama Sheria imekupitia pembeni, basi hata ukisoma huwezi kuelewa kitu hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri, kwa anavyoshirikiana na wenzake kufanya hivyo. Sasa labda nije moja kwa moja kuhusu suala la nyenzo zinazowawezesha kufanya kazi vizuri, nimesema ni chombo muhimu sana katika nchi kinachosimamia haki na ndio maana hata kwenye Kitabu cha Hotuba, kuna nembo ambayo inaonesha kwamba, kinatenda haki kwa Wananchi.

Mheshimiwa Spika, bila kuwa na nyenzo ni kwamba, chombo hiki kitashindwa kufanya kazi. Mzungumzaji aliyemaliza kabla hatujapumzika pale mchana, alieleza masikitiko aliyokuwa nayo ya kuwahurumia wale Wazee wa Baraza wanaopata shilingi

1,500 kila wanapohudhuria kesi. Ukisikia shilingi 1,500 ni hela kidogo sana, juzi tumezungumza tukasema tukasema *staff* waongezwe, baada ya kuwaonea huruma kama hawa walivyo. Mimi nadhani tuwaonee huruma hawa Wazee wa Baraza, ambao wanashinda pale kwa shilingi 1,500; huwezi huwezi ukununua kitu chochote kwa shilingi 1500 na siyo huruma itakuwa ni haki kwa sababu wanafanya kazi inayoonekana.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo kubwa sana linalowakabili Watumishi wa Wizara hii; hili nina uhakika nalo kwa sababu kule kwangu Wilaya ya Kibondo, ninaona jinsi ilivyo na Mkoa wa Kigoma kwa ujumla una tatizo hilo. Ninadhani hili linawezekana likawa ni kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, tatizo la usafiri ni kubwa sana kwa Watendaji wa Mahakama. Wana magari madogo, ambayo hayawezi yakawafikisha mahali kama kuna kitu cha dharula. Tuna mahakama ambazo zipo vijiji, mimi kule kwangu kama mvua ikinyesha, huwezi ukatoka Makao Makuu ya Wilaya ukaenda iliko Mahakama ya Mwanzo ukafika, kwa sababu hata gari ambayo ni *four wheel* inashindwa kufika, sasa mtu anapewa gari dogo ni sawa na *saloon* tu ya kutembelea mjini; utakwenda kutoa haki kwa Wananchi namna gani?

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nadhani ni muda muafaka sasa wa kuhakikisha kwamba, Watumishi wa Wizara hii wanakuwa na magari ya kuaminika kwa ajili ya kuwafikisha mahali ambapo wanatakiwa kwenda kutenda haki kwa Wananchi.

Mheshimiwa Spika, tumeona umuhimu wa hawa watu wanavyofanya kazi. Watu muhimu sana, wanatoa hukumu ambazo ni ndogo, kubwa na hata za kuua kabisa, za kunyonga, ni lazima chimbuko lianzie chini Mahakama za Mwanzo mpaka Mahakama Kuu. Sasa watu hawa inasikitisha inapofikia wakati unakwenda kukuta Hakimu anapanga nyumba Uswahlilini kwa watu, lakini huko anakokwenda kupanga nyumba utakuta ndio watu wenye matatizo. Mtu unampangisha nyumba, unakuta wakati mwingine ni jambazi ana kesi, lakini bado Hakimu anakaa humo ndani; je, usalama wa Hakimu ni nini kama sio kuuza maisha yake?

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nadhani Serikali ijikite kujenga nyumba za Mahakimu kote, wawe na nyumba za kuaminika kwa ajili ya usalama wao. Nimelizungumzia hili kwa Mahakimu, lakini Majaji pia wanakaa hotelini. Majaji wanaokaa kwenye nyumba zao usalama wao uko wapi? Kesi wanazosimamia ni kubwa sana kwa Wananchi, kwa hiyo, nilikuwa nadhani kwamba, kwa makusudi mazima, Serikali itafute fedha mahali zijengwe nyumba kwa ajili ya usalama wa Watumishi wa Wizara hii ambao wanafanya kazi nyeti.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo kubwa sana la Mahakama. Nakumbuka mwaka jana wakati nachangia Wizara hii, Mheshimiwa Waziri alisema, utaratibu sasa utawekwa wa kukarabati hizi Mahakama za Mwanzo ambazo nyingi ni mbovu. Alitolea mfano kwenye Mahakama moja ambayo ipo kule kwangu ina hali mbaya sana, lakini nilikuwa napitia hii hotuba ama kitabu kilichoandaliwa, nikakuta kwamba, hiyo kazi haijafanyika kwa Tanzania nzima.

Mheshimiwa Spika, nadhani inawezekana walisahau kufanya hivyo, lakini sasa ni muda muafaka wa kuhakikisha kwamba, Mahakama zinakarabatiwa ili ziweze kurahisisha hizi kesi ambazo zinaweza zikatoka ngazi ya Mahakama za Mwanzo kwenda kwenye Mahakama za Wilaya, kufanyika kwenye maeneo ambayo yanahusika. Kwa hiyo, bado nakumbusha tena nilichokizungumza mwaka jana kwamba, Mahakama zifanyiwe ukarabati zifanye kazi.

Mheshimiwa Spika, usalama kwa Watumishi wa Mahakama ni mdogo sana, kwa sababu mtu huwezi ukaenda kutoa hukumu ya kifo, kunyongwa ama kufungwa maisha kwa mtu, halafu unakwenda unakaa tu kienyejenyeji huko mitaani; bado usalama wa Watumishi wa Wizara hii ni muhimu sana uzingatiwe na kuonesha kwamba kweli wanafanya kazi ama kazi wanazofanya zinathaminiwa.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na msongamano wa wafungwa (mahabusu) kwenye magereza. Nimelifuatilia hili nikagundua kwamba, linatokana na kesi nyingi ambazo zimekaa tu hazifanyiwi kazi. Kukaa ama kuwepo kwa kesi nyingi, ukifuatilia sana utaona kwamba, wakati mwingine ni kutokana na hali iliyoelezwa na wasemaji wa asubuhi kwamba, Watumishi wa Mahakama hawatoshi. Sasa kama Watumishi wa Mahakama hawatoshi ni lazima ufanyike utaratibu wa kufanya *recruitment* upya kutafuta Mahakimu. Watu walioko vyuoni waende kufanya kazi, tupate wafanyakazi wa kutosha. Tukiwatumia hawa, tutapunguza msongamano wa mahabusu ambaa athari zake ni magonjwa ya kuambukiza katika magereza.

Mheshimiwa Spika, hii ni kutowatendea haki watu ambaa wanakaa muda mrefu mahabusu; yaani kesi ndogo ya kuua kuku ama kuiba kuku, mtu unakaa mahabusu mwaka mzima bila kutolewa hukumu. Kwa kweli inasikitisha sana na Serikali inapata gharama kubwa sana ya kuwatunza hawa watu.

Mheshimiwa Spika, kuna hali ambayo pia si kuwatendea haki watu. Mimi nimeshuhudia kwa macho yangu pale Dar es Salaam, nilikwenda kituo fulani cha polisi kipo Kijitonyama; mahabusu wanapotoka pale kupelekwa Mahakama ya Mwanzo Kinondoni, hawapandishwi kwenye karandinga, wanafungwa kamba kutoka njia ya mkato kuja mpaka pale Kinondoni Mahakamani. Sasa hii kusema ukweli, watu wa kushughulikia vizuri ni wa Wizara ya Mambo ya Ndani. Wizara ya Katiba na Sheria nayo, kwa kutafuta haki kwa watu wa namna hiyo, lazima wajikite kwenye suala hili. Huku ni kuwakosea haki Wananchi.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kidogo kuhusu Mahakama Kuu kwa Mkoa wa Kigoma ama Mikoa ya Magharibi. Nashukuru kwamba, tuna Mahakama Kuu iko pale Tabora. Nimekuwa nikiona kunakuwa na usumbufu mkubwa sana wa wale wenye kesi kutoka Kigoma kuja mpaka Tabora.

Mheshimiwa Spika, nadhani ilikuwa ni muda muafaka ama jambo la busara kabisa kusema kwamba, Kigoma inastahili kujengwa Mahakama Kuu. *Records* zilizopo kutokana na mrundikano wa wakimbizi walioko kule, tungeweza kuwa na Mahakama

kule ambayo ingeweza kuwa inatoa uamuzi kwa kesi ambazo nyingine zinashindikana kuamuliwa katika Mahakama za Wilaya zikianzia ngazi ya Mahakama za Mwanzo. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Wizara ifikirie hilo la kujenga Mahakama Kuu kule Kigoma, kwa sababu kuna wahalifu wengi sana na uhalifu mkubwa sana unaotokana na uvamizi wa Wakimbizi wanaotoka nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, udhalilishaji wa akina mama; sheria zinazotumika sasa hivi zimekwishapitwa na wakati. Nadhani sheria sasa zibadilishwe ili ziweze kwenda sambamba na tunachokifanya hivi sasa. Tukiendelea kutumia sheria ambazo zipo, akina mama watakuwa hawatendewi haki hata kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nije kwenye uchache wa Mahakimu ambao nimeshauri kwamba, Mahakama nyingi hazina Mahakimu wa kutosha, hali ambayo imesababisha mrundikano wa kesi. Mrundikano wa kesi unasababisha msongamano wa mahabusu katika magereza na msongamano wa mahabusu ukiwamo katika magereza, ndio maambukizi ya maradhi yanatoka kila upande bila kujua nini kifanyike. Nadhani ni muda muafaka kabisa, Serikali ipambane na hali hii ili kuhakikisha kwamba, haki inatendeka.

Mheshimiwa Spika, kila unapokwenda utasikia Mahakimu wanapokea rushwa. Hii ni lugha ambayo huwa siipendi sana. Ukija kuangalia hawa wenzetu Watumishi wa Mahakama, wanaishi maisha magumu sana. Nadhani hata mshahara hautoshi, wanapambana na vishawishi vingi sana kutoka kwa wahalifu hasa wale wazoefu. Hawa watu waboreshewe maslahi yao. Maslahi wanayopata ni kidogo sana, waboreshewe maslahi; vinginevyo, tutakuwa tunawalaamu tu wanapokea rushwa wakati maisha wanayoishi ni maisha duni sana.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa najaribu kuipitia Bajeti ya Wizara iliyowasilishwa mbele yetu leo, naona kidogo imejipunja sana. Nadhani Waziri hapo na Wataalamu wako, hamkuweza kuona kama Watumishi wenu wana hali ngumu sana.

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye suala la usafiri ni kwamba, hili tulipatie kipaumbele. Msemaji aliyemaliza mchana kabla hatujaondoka humu, alieleza aina ya magari wanayotumia; magari madogo ambayo yakiharibika wanashindwa kupata spea ni sawa sawa na yale magari yaliyonunuliwa na Chama cha Mpinduzi *mahindra*. Magari yale hayana spea, sasa haya yaliyonunuliwa ambayo yanatumika Mahakama na waliyagawa mikoani na baadhi ya Wilaya zina magari hayo. Hayo magari yanaonekana kutokuwa na spea.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nadhani tungekuwa na utaratibu mzuri, akapatikana mtu wa kununua magari hayo kwa ajili ya Mahakama, apewe vigezo kwamba Mahakama ziko kila mahali kama zilivyo shule na Serikali iwape kipaumbele Wizara hiyo ili kuhakikisha kwamba, wanakuwa na nyenzo za usafiri ambazo zinaaminika.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo la Lugha ya Kiingereza inayotumika katika kutoa maamuzi na Sheria zenyewe zimeandikwa kwa Lugha hiyo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofî*)

**MHE. JONH M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, nasikitika leo sauti yangu siyo nzuri sana. Nataka kukushukuru sana kwa kunipa nafasi. Siku moja nilikuwa namsikiliza Spika wa zamani wa Kenya, akizungumzia juu ya Vyama vya Upinzani akasema, sisi kule Kenya tunaviita Vyama Pinga. Sasa nataka kuwaonesha tu kuwa siyo kila mara sisi ni Vyama Pinga, mara nyingine kama kuna kuna vitu vizuri tunavisema.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, nilitaka kusema naipa Serikali A1 kabisa kwa kuweka ruzuku ya pamba; hongera sana Waziri Mkuu. Naipa Serikali mia kwa mia kwa kupandisha hadhi barabara zetu za Bariadi. Leo barabara ya kutoka Bariadi - Gambasini - Meatu, tutakuwa na *Regional Road* halafu tutakuwa na Ngw'igumbi mpaka Ramadi. Hivi ni *positive things, very good*, nawapa A1 kwa mambo kama hayo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sasa niende kwenye hotuba ya leo na hapo lazima nimpe A1 kwa *presentation* ya bajeti yake. Nataka kuchukua nafasi hii, kuwapongeza sana Mheshimiwa Jaji Mkuu, Majaji wenzake na safu yote, kwa kazi nzuri wanayofanya pamoja na mazingira mazuri.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nataka kusema kwamba, baada ya miaka 45 ni vizuri kabisa tukaonesha kuna mahali pa Bunge, Bunge lenye hadhi. Mahakama unayoisema hiyo ni Mahakama ya Tanzania, Mahakama ya Rufaa, jengo lake labda lenye ghorofa 20 au 30, linameremeta; liko wapi? Baada ya miaka 45 leo mmeona kwenye *report* hapa tunaambiwa kwamba, kuna Majaji 16 wa Mahakama ya Rufaa wana *Library*, wana vyumba vya kutosha, wana *stenographers* wa kutosha, wana *Hansard* ambayo badala ya *ku-bend* migongo Waheshimiwa hawa wanaweza wakakaa pale na kusikiliza mambo yetu. Nasema mambo yetu kwa sababu kila mmoja wetu hapa ni mshtakiwa mtarajiwa, hakuna ambaye yupo *above the law*. Je, hawa tunawaangalia vipi?

Mheshimiwa Spika, mimi ningependekeza kwamba, katika Miradi ya Maendeleo, hebu jengeni Mahakama ya Rufaa. Karibu na Karimjee pale kuna viwanja viko *empty* tu watu wanavichezea, kwa nini wasipewe Mahakama wakajenga karibu na Ikulu *Tall Bulding* yenye hadhi inayofanana na utoaji wa haki? Hilo ni pendekezo la bure, naomba ulichukue.

Mheshimiwa Spika, twende kwenye *numbers*, kusema kweli bajeti ni ndogo. Nimejaribu kui-study yote, pamoja na kusema kwamba, umeomba na tutakupa shilingi bilioni 107, ambayo kati ya hizo, shilingi bilioni 40 ni kwa ajili ya maendeleo. Ukiangalia sehemu ya Mahakama kwa zote mbili, Maendeleo na Kawaida ni shilingi bilioni 62 tu, ambayo hii ni sawa sawa na 0.6% ya bajeti nzima. Kusema kweli, hatutoi haki kwa wananchi wanaotegemea mahakama kuwapa haki.

Mheshimiwa Spika, nataka kushauri kwamba, ni vizuri kama tulivyofanya kwa mfano, kwa Mkaguzi na Mdhhibit Mkuu wa Serikali; kwanza, kumwambia kwamba, Bajeti yake haitaandaliwa na Wizara ya Fedha, itaandaliwa na *Public Accounts Committee* na ikishakubaliwa basi imeshakubaliwa hakuna mtu wa kugeuza. Jambo hili lingekuja pia kwa Mahakama na kwa Bunge; ukishakubaliwa Bajeti isichezewe chezewe na mtu, sijui *sealing* ya hapa; naona jambo hilo haliitendei haki mihimili hii miwili.

Mheshimiwa Spika, kama tulivyofanya kwa Vyama vya Siasa tukasema 2% ya *minus debt*, tutaweka kwa ajili ya ruzuku ya Vyama vya Siasa; sioni kwa nini hapa tusifike mahali tukasema kwamba, kwa Bajeti ya Serikali 3% mpaka 4% ya Bajeti yote iende kwa Mahakama na 3% mpaka 4% iende kwa Bunge? Hii iwekwe ndani ya Sheria, isiwe kila siku mihimili hii miwili inakwenda pale kupiga magoti kuwa jamani niongezeeni hapa, mimi ni mnyonge *Chief Justice* yuko hapa, *he is wondering* sijui tutamfanya nini? Tutamwongezea vipi pesa? Habari hii siyo nzuri, hatutamwongezea maana Bajeti imeshafika hapa, tutapiga maneno tu.

Mheshimiwa Spika, ili tufike tunakokwenda, nashauri kila mmoja awe anajua kipande changu ni hiki na atakigawa kufuatana na vipaumbele mbalimbali vilivyopo pale. Kuna kitu kingine kibaya zaidi na ninasema hili kwa sababu mimi ni Mwenyekiti wa *Public Accounts Committee*, kila wakati fedha zinatengwa lakini hazipelekwi au zikipelekwa zinapelekwa mwezi wa tatu au wa nne, katika miezi mitatu minne utaweza kutumia fedha kweli kwa kasi kiasi hicho?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachosema hapa, hizo fedha tunazowapa, kama kuna matatizo Waziri wa Fedha asiende kusema katakata. Mimi naona tukishawapatia fedha kiasi fulani, basi zipelekwe huko.

Mheshimiwa Spika, fedha ya maendeleo, *actually*, inasikitisha sana ukiona Mahakama na Wizara nzima ina shilingi billioni 40, ambazo zimebekwa kwa ajili ya maendeleo, lakini shilingi bilioni 6 tu ambazo ni za ndani; ndio kusema hatuna *ownership* ya maendeleo ya Mahakama. Tusipofanya vizuri na Wafadhili, hakuna maendeleo ya Mahakama. Ninyi mnajisikiaje kama utoaji wa haki ni lazima ukambembeleze Muingereza? Utoaji wa haki ni lazima ukapige magoti kwa Finland na nchi nyingine na bilioni zenyewe unazozungumza ni 40 tu? Ukiangalia Votes nyingine hapa zinapotea potea tu, lakini kwenye *Public Accounts Committee* ninaziona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningeshauri kwamba, kwa upande wa maendeleo, fedha ya ndani ndiyo ikabidhiwe Mahakama na Wizara ya Katiba na Sheria. Nalisema hili kwa sababu tumeona kwamba, fedha ya ndani katika miaka kama minne hivi tumefanya vizuri sana. Ukiangalia matokeo, unakuta *perfomance* ni 99%, kama tumetoa fedha kiasi fulani 99%, lakini fedha za kutoka nje haijazidi 50%. Kwa hiyo, yote haya umetuambia hapa wengine tunaweza kusema ni hadithi ya *Alfa Ulela* tu, kumpigia sabuni Mheshimiwa *Chief Justice* kwamba, amepata hela lakini mimi sioni uhakika wa fedha hizi. Ninashauri kuwa, lazima maendeleo ya Mahakama yawe yetu, kutoa haki ni jambo ambalo ni haki ya msingi kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napendekeza kwa dhati, tuweke fedha za ndani. Nataka kuzungumzia kidogo juu ya Mahakama ya Ardhi; nimeona hapa kuwa kuna Majaji watano. Mahakama hii pia inapanga haina ofisi. Siyo hivyo tu, ukiangalia bajeti yake, shilingi bilioni 1.1, kwa ajili ya maendeleo ni shilingi milioni 500, hawana vyumba watafanya nini na hizi hela ambazo mmeweka hapa?

Mheshimiwa Spika, tumeelezwa kuwa hapa kuna kesi zaidi ya 4,889, wameweza kumaliza kesi 1,546, bado kuna kesi 3,311 na bado nyingine zinakuja. Ninasema zitakuja tu, kwa sababu baada ya kumhoji Afsa Mhasibu wa Vote ya 90, tunaanza kujiuliza hivi mwanzo wa kesi zote hizi ni sheria yenye au vipi? Mimi nakwambia mwanzo wa kesi za mauaji katika Kanda ya Ziwa ni ardhi.

Mheshimiwa Spika, mtu anakwenda kutembea huko, akirudi anakuta ardhi imegawiwa hana mahali pa kwenda. Hii ni sehemu ambayo ningeshauri kwamba, Wanasheria na Wizara yako muangalie upya mambo ya Sheria Namba tano, tuachane na Sheria Namba Nne, tuwe na Sheria moja tu ya Ardhi ambayo inaangalia pia haki za kila mmoja.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa huu siyo wakati wake, nitakuja kulizungumza wakati wa Ardhi. Naona sasa hivi mtu anayeleta migogoro mikubwa sana ni Serikali yenye, kwa kuchukua ardhi za watu mbalimbali. Kwa hiyo, hii ni sehemu ambayo ninashauri tuiangalie vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, jambo la tano ninalotaka kulizungumza ni juu ya mahabusu na hili mitasemea zaidi kwa Bariadi. Jamani mimi nimechoka, kila siku kazi yangu kama Mbunge ni kujaribu kumtoa mtu mahabusu. Nikitoka hapo mchana tu napigiwa simu fulani yuko ndani; sasa labda tuangalie hii sheria kwanza ya kuweka watu ndani halafu tutathibitisha baadae. Mimi naona labda lingeangaliwa upya, tunawaonea watu wengi sana na tunajaza mahabusu; watoto wadogo, akina mama, kila mmoja yumo mle ndani, baadae unaambiwa kwamba hamna kesi, hali hii haikubaliki hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, nimefurahishwa angalau sasa Mkurugenzi wa Mashtaka atafunga Ofisi kule Shinyanga. Hili ni jambo jema sana. Ninapenda pia kusema kwamba, kwa Bariadi atuharakishie huu mtindo wa Wanasheria, waje haraka ili wasaidie watu ambaa wanakaa mahabusu. Taasisi hii labda ingefikiriwa, badala ya kama ilivyo TAKUKURU na sehemu nyingine. Imetajwa ndani ya Katiba kwamba, *The DPP will be an independent person*. Kwa nini tusifanye iwe Taasisi Maalumu ambayo ina uhuru? Waziri alifikirie hili kwa baadae, labda anaweza akatuboreshea hali halisi ya mambo hayo.

Mheshimiwa Spika, kabla sijamaliza, nataka kuzungumzia jambo moja tu ambalo kidogo ni gumu. Hili la dini jamani, najua ukurasa wa sita umejaribu kutafuta njia ya ku-incorporate Islamic Laws ndani ya Sheria nyingine, ziangaliwe na Mahakama kwa

ujumla. Mimi naona hili tunadanganyana, tuache dini iendeshe sheria zake huko, sisi Wakristo tuna *Canon Law*, tuachenii tuendeshe mambo yetu huko. Sisi kwa Sheria ya Ndoa hatuachani mpaka kufa, lakini Mahakama mara nyingine inatutenganisha, ndio hali halisi.

Mheshimiwa Spika, tukiingiza kwa njia yoyote ile, tunachezea amani na mkichezea amani nchi hii tumekwisha. Miaka 45 tulivoishi, tuishi hivyo hivyo. Mimi siyo Hatibu na hata sifirii kama ni Muislamu, najua ni Hatibu tu na sidhani kama anavyoniita John ana Ukristo au ana Ukatoliki anajua ni John tu. Kwa hiyo, huu ndio udugu tuliojenga Tanzania, tukileta haya mambo humu *we are finished*.

Mheshimiwa Spika, mwisho, haki za binadamu; wengine wamezungumzia Idara hii na Tume hii ingeongezewa nyenzo. Tunaona mara nyingi wafugaji wanaporwa ardhi na Serikali, kila mahali kuna matatizo makubwa sana. Nawaomba tuongeze mkate kidogo ili haki za binadamu zitusaidie katika migogoro mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, Bariadi Mahakama yetu imechakaa ile mbaya tusaidieni.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa John Cheyo, kwa mchango wako mzuri. Sasa namwita Mheshimiwa Dr. Luka Siyame na hatimaye atakayehitimisha ni Mheshimiwa Magalle Shibuda.

**MHE. LUKE J. SIYAME:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia kidogo kwenye Hotuba hii ya Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nikushukuru sana kwani jana baada ya kunipa nafasi, niliweza kutoa kauli moja kuhusu tukio la kule Tunduma. Nashukuru ile nafasi uliyonipa, iliweza kuzaa matunda, kwani toka wakati ule nilikuwa napigiwa simu na wananchi wakiwa wamefarijika sana na hii leo wametoa taarifa kwamba, wamelala salama, kwa amani na kila kitu kinakwenda salama. Katika hali hiyo, naomba tena niwashukuru wao wananchi, kwa jinsi walivyokuwa watulivu na pia vyombo vya dola, kwani baada ya tukio lile la vurugu, ilitokea uharibifu mkubwa kwa magari ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, pamoja na Polisi na hata Viongozi waliokuwa kwenye Mwenge, ikiwa ni pamoja na kujeruhija Katibu wetu wa Mkoa wa CCM; waliweza wote kuwa wavumilivu na leo mambo yanaenda vizuri. Hii yote ni kwa busara yako, kwa sababu uliweza kunivumilia nikaweza kuongea kitu nje ya lile liliokusudiwa kuongelewa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, naomba niseme kwamba, ninaunga mkono hoja ya Waziri wa Katiba na Sheria na nampongeza yeze pamoja na timu yake yote ya Wizara ya Katiba na Sheria. Nawashukuru pia wote wale aliowataja kama wafanyakazi wenzie wa Wizara hiyo ya Katiba na Sheria, kwa sababu mlolongo wa majina ni mrefu, naomba niishie hapo ila niingie katika mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema, mimi nimeanzia zile kurasa za mwisho; nimeanza na michoro kwa maana ya *graphs*, ambayo inahusiana na mrundikano wa kesi kwenye Mahakama ya Rufaa na Mahakama Kuu, ukurasa wa 47.

Mheshimiwa Spika, tukiangalia jedwali la 2(a), ambalo linahusiana na mrundikano wa kesi kwenye Mahakama ya Rufaa, inaonekana kati ya mwaka 2004/05, kulikuwa na upungufu wa mrundikano huo hadi mwaka 2006/07 na baada ya hapo, kumekuwa na kasi ya ongezeko hadi kufikia asilimia 79. Hii kwa namna nyingine, inaonekana kazi inayofanywa haiishi na inawezekana ni kwa kutotosheleza idadi ya Majaji wa Mahakam ya Rufani ama hizo kesi zinazoletwa kama za rufani ni kesi ambazo zina utata mkubwa, ambao wanashindwa kutoa maamuzi kwa wakati kuliko ilivyokuwa hapo nyuma.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, labda tumwombe Mheshimiwa Mtukufu Rais, ambaye ndiye mwenye mamlaka ya kuweza kuteua Majaji wa Mahakama ya Rufani, aongeze idadi yao ili hizi kesi zipungue, maana zikianza kuongezeka, hautaonekana ufanisi wa uwepo wa Waheshimiwa Majaji wa Mahakam ya Rufani.

Niwapongeze Majaji wa Mahakama Kuu, kwani katika hii miaka niliyoiona ni kwamba, kumekuwa na kupungua kwa mrundikano wa hizi kesi. Kwa mfano, kati ya mwaka 2007/2008, ambapo mrundikano ulikuwa asilimia 83, hivi sasa tunavyoongea mrundikano huo umepungua umefika asilimia 49. Hiki ni kitu ambacho kinastahili kupongezwa, kwa maana hawa Waheshimiwa wamefanya kazi kubwa na kuweza kupunguza huo mrundikano kwa karibu asilimia 50. Naamini huenda ni kwa sababu Mheshimiwa Rais, aliteua Majaji wengi mwaka jana na hivyo, kuweza kuongeza ile idadi ya Waheshimiwa Majaji wanaoshughulikia kesi hizi.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, naomba nije ukurasa wa 22, ambao unahusiana na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (*RITA*). Natoa pongozi kwani hapo nyuma shughuli hii ilikuwa lazima iishie kwa Kabidhi Wasii, Makao Makuu ya Dar es Salaam; lakini hivi sasa wameweza kupoleta hizi huduma hadi kwenye Kata na siku za hivi karibuni linaloonekana ni usajili kufanyika ndani ya muda mfupi. Kwa hiyo, tunaomba na kuwatachia kila la kheri kwa kazi hiyo wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye Mahakama Kuu Divisheni ya Ardhi. Tukiangalia kwenye hizo *graphs* za ukurasa wa 48, tunaona kwamba, Mahakama hii baada ya kuwepo kisheria na kuhudumia hizi kesi, pamoja na kwamba, hakuna lililopungua kuanzia ilipoanzishwa hadi hivi sasa, tunaomba pengine ile idadi yao iongezwe ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi, maana hivi sasa pamoja na kueleza kwamba, wamefanya kazi, wameweza kusuluhisha ama kumaliza hizo kesi, lakini ile idadi bado ni kubwa. Hivyo, tunamwomba Mheshimiwa Rais, kwa mamlaka yake aliyonayo, awateue ili wawe wengi maana hizi kesi ni nyingi na za kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukija kwenye changamoto katika Sekta ya Sheria, kumeelezwa sababu za uelewa mdogo wa sheria. Kwa upande wa wananchi,

tumeambiwa uwepo wa hamasa ndogo kazini kwa watumishi wa Sekta ya Sheria na pia katika hali hiyo, kuna suala la msongamano wa wafungwa magerezani. Ningeshauri kwa upande wa wananchi, pamoja na hali yetu kuwa ngumu na kwamba hakuna semina au vipi, kuwe na dhamaira ya makusudi ya kuwafikia wananchi na kuwaelewesha juu ya sheria za nchi hii na taratibu za Mahakama. Katika hali hii tunaweza kufanya wananchi kwa namna moja wakaielewa sheria yetu na namna zipi waifikie mahakama kwa ajili ya kupata haki yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa hamasa kwa wafanyakazi wa Sekta hii ya Sheria, nashauri Serikali iweze kuwapa motisha kwa namna moja au nyingine. Tumeshuhudia Waheshimiwa Mahakimu hususan wale wa maeneo ya pembezoni, wakiishi katika mazingira magumu kiasi cha kukatishwa tamaa na hiyo hali na wengine hadi kuondoka ama kuanza kuingia kwenye taratibu nyingine kama kuomba rushwa ndogondogo kwa wale watuhumiwa wao. Hivyo basi, Serikali iwaangalie kwa namna ya pekee ya kuweza kuwapa kipaumbele, kuwapatia nyumba, usafiri na zile nyenzo nyingine ambazo zitawawezesha wafanye kazi katika mazingira mazuri.

Mheshimiwa Spika, napenda niseme kwamba, wiki chache zilizopita, tukiwa kwenye vile vikao nya Kamati za Bunge, nilikuwa immojawapo wa Wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, lakini kwa wakati ule tukawa tumekwenda kwenye masuala ya UKIMWI, kwenye Gereza la Keko; kile tulichoshuhudia kilikuwa ni cha kukatisha tamaa, juu ya msongamano katika hivyo vyumba wanavyolala hao wafungwa. Kile chumba ambacho kilikuwa kimekusudiwa kuchukua wafungwa watatu, tulikuwa tunakuta wako wafungwa kati ya 15 na 20. Katika hali hii, thamani ya binadamu inakuwa imevunjwa kabisa, maana yake walikuwa wanalala kwa namna ambayo wao wenyewe walikuwa na jina lao ambalo ilikumbuki; tulikuta wengine vichwa viko upande huu na wengine upande ule, ilimradi tu ni kama magunia yaliyowekwa si binadamu.

Mheshimiwa Spika, katika hali hiyo, hali katika magereza iangaliwe tukichukulia kwamba, wale watu wapo pale, wengine makosa yao ni ya kutuhumiwa tu na wala hawahusiki nayo.

Mheshimiwa Spika, tukija kwenye mfumo wa kuwasaidia wananchi wasiojiweza kisheria, nashukuru Wizara imesema inachukua hatua ya kuweza kuhakikisha wanasheria waliopata Shahada ya Kwanza, wanakwenda kwenye Mahakama za Mwanzo. Naamini litakuwa ni suala jema kabisa kwa wananchi, lakini Serikali iwapatie mazingira mazuri ya kufanya kazi kwa sababu siamini kama kuna Mwanasheria ataamua kwenda kwangu kule Kamsamba ama Ndalambo ambako hatapata hata mahali pa kuweka mzigo wake. Kwa hiyo, kwanza, wawekewe mazingira mazuri ndiyo washawishiwe kwenda huko.

Mheshimiwa Spika, napenda niongelee tena juu ya Mahakama ya Kadhi. Nimesoma mstari kwa mstari, yale yaliyoelezwa na Mheshimiwa Waziri, kwa hakika kila kinachoonekana pale ni kizuri, lakini kama walivyosema wenzangu, masuala ya dini tungeacha yashughulikiwe na wenyewe dini wenyewe, badala ya sisi kama Serikali kubeba mzigo na kuanza kuratibu hayo masuala. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Sheria za Mirathi, nadhani muda umepita, tungependa mchakato huu uletwe haraka ili sheria ikishatungwa, ianze kutekelezwa maana yake nina hakika wanawake, wajane na watoto, ndio wanaoumia kupita kiasi kwa hivi sasa. Hivyo, hiyo Sheria ikiletwa kwa wakati muafaka tukaipitisha, basi itakuwa ni jambo jema.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nilipoangalia katika hiki Kitabu cha Waziri, katika ugawaji wa Mahakimu na Mahakama, kwa kweli Wilaya ya Mbozi haijatendewa haki, kwa sababu sijaona popote katika Wilaya nzima yenye Kata 26. Mahakama moja na ambayo inajengwa kwa nguvu kazi za wananchi, nadhani wangetufikiria vizuri zaidi. Mbaya zaidi ni kwa Jimbo langu la Mbozi Magharibi, ambalo lina Kata 11, lakini kuna Mahakama Mbili tu za Mwanzo, moja ikiwa umbali wa kilomita zisizopungua 200 kutoka ile nyingine ilipo. Kwa hiyo, wananchi wote ama waende hizi mahakama mbili au waende kwenye Makao Makuu ya Wilaya, ambayo nayo wengi wao ni karibu kilomita hizo 200 kutoka pale walipo.

Mheshimiwa Spika, naomba watendewe haki siku za usoni huko na wao wafikiriwe angalau kwa kila Kata kuwa na Mahakama, kama ilivyokuwa hapo mwanzo kabla hazijafutwa zile mahakama zilizokuwepo kila Tarafa katika Jimbo lile.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, ninakushukuru na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Siyame, tunamalizia na Ustaadhi Magalle John Shibuda.

**MHE. MAGALLE J. SHIBUDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata fursa hii ili na mimi niweze kuchangia hoja ya Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nampongeza sana Waziri wa Sheria na Katiba, Mwanasheria Mkuu, Jaji Mkuu na Watumishi wote waliopo katika Wizara hii na Taasisi zake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kutumia fursa hii, kukupongeza Spika, hasa Wazazi wa Urambo kwa kutuzalia mtoto ambaye ana maadili na hatimaye akafikia fursa ya kuwa Spika. Kwa hiyo, nawaomba Wazazi na Wananchi wa Urambo, wahakikishe ya kwamba, wanamrejesha kwa kishindo Mheshimiwa Samwel Sitta katika Jimbo lake ili tuendelee kuwa naye, msije mkakosea mkaambiwa maneneo ya ovyo japo Manabii na Mitume pia walipata mitihani. (*Makofi*)

**SPIKA:** Amina! (*Kicheko*)

**MHE. MAGALLE J. SHIBUDA:** Mheshimiwa Spika, kila mwamba ngoma huvutia upande wake; ninaiomba kauli ya Serikali kama Wizara inaweza ikaandaa kikosi kazi ambacho kitakuja Maswa kuhakikisha ya kwamba, mahabusu waliochelewa kupata

haki zao kwa muda mrefu wanatendewa haki. Naomba kikosi kazi cha Mwanashereria, Hakimu na Polisi, mtembelee mahabusu na Magereza ya Maswa, Malya, vile vile mje Maswa msaidie kutenda haki.

Mheshimiwa Spika, dhuluma ni kubwa sana Maswa hata Mkoa wa Shinyanga, kwa sababu sisi hatukupata bahati ya kupata elimu. Elimu yetu ni matambiko na kupiga ramli, kwa hiyo, ninaomba sana mje mtuokoe tuondokane na dhuluma hii. Naomba kikosi kazi na kauli ya Serikali kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali italeta *Administrative Law*? Wapo baadhi ya watu wanafikiria ya kwamba, kupata dhamana ya uongozi au cheo basi wamekuwa ni watu wa peponi; eti kwamba, hawastahili kushtakiwa. Ninaomba *Administrative Law* ya kusimamia watu wanaotumia madaraka vibaya ihmizwe na iletwe, tukabiliane na DCs, OCDs na RPCs au ofisa ye yote anayetumia madaraka yake kunyanyasa wananchi. Wananchi wanabaguliwa, hawana fursa ya kwenda kujieleza, akienda anaambiwa wewe unakuja hapa kuuliza kama nani, nitakuweka ndani ondoka, basi wanaondoka kwa unyonge wao. Tilitafuta uhuru ili haki kwa Watanzania ipatikane, tulipigania Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ili haki ipatikane. Naomba haki hizi zilindwe na sheria na kanuni.

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba kusema kwamba, mahusiano kati ya Bunge au kati ya mihimili yote mitatu, wakati umefika sasa yaimarishwe. Ninaomba Waziri wa Wizara hii, pamoja na Jaji Mkuu, mtoe mwongozo elekezi ya kwamba Kitaifa, viongozi mnaheshimiana. Tunapokwenda Mikoani, kuwatembelea Mahakimu, wasifikirie kwamba, Wabunge tunapeleka siasa kwao, bali ni mhimili wa Mahakama unaowakilishwa na Hakimu na mhimili wa Bunge unaowakilishwa na Mbunge, hivyo, wanakutana kujadiliana kwa azma ya mustakabali wa kunawirisha ustawi na maendeleo ya jamii na haki za jamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, viongozi wote tunahitajiana, hivyo ninaomba sana, kauli elekezi au mwongozo ujengwe hivi sasa. Hii ni kwa sababu ya tafrani zinazotokea kwamba, Wabunge tunapokwenda unaambiwa analeta siasa, hapana! Sisi tunawakilisha mhimili, tuheshimiane, tuthaminiane na tupendane, kwa sababu sote tupo hapa kwa maslahi ya kuhakikisha kwamba, Tanzania inasonga mbele kwa umoja na mshikamano na haki sawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kuzungumzia kwamba, pana dhana potofu kwa masuala ya *private prosecution*. Naiomba Serikali kwamba, kama tunataka kuhimiza Utawala Bora, basi *private prosecution* iruhusiwe. Mimi sijaona mfuko wa suruali unaweza ukaficha kaa la moto, kwa hiyo, kama ninyi mnazuia *private prosecution*; sielewi mnamsizia nani na mnamsitiri nani! Ninaomba iruhusiwe.

Mheshimiwa Spika, vile vile neno Mtumishi wa Serikali, Kiongozi wa Serikali, lisitumike vibaya kwa sababu udhaifu wa Sheikh ama Askofu siyo udhaifu wa Msahafu ama Biblia; kila binadamu ana hulka na silka yake, kwa hiyo, tunapokosoa udhaifu binafsi, naomba usilindwe na mfumo ukiitwa Kiongozi wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niishauri Serikali kwamba, tuna tatizo moja nalo ni kuhusu masuala ya dhamana. Dhamana vijijini hasa kwangu Maswa, mtu yupo kilomita mia moja kutoka Maswa Mjini palipo na studio, je, mtu huyu akiambiwa na Hakimu kwamba lete kitambulisho chenye picha na yeze asili yake ni ufugaji na ukulima atapata wapi picha? Je, hizi siyo nyenzo za rushwa? Naomba busara na hekima zitumike, kuhakikisha kwamba, panakuwa na maangalizo ya watu wa vijijini, kwa sababu wanatambuliwa na Mwenyekiti wa Kijiji au Kiongozi wa Kijiji, basi ithaminike kupewa dhamana.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanateseka sana vijijini na kwa sababu ya uduni wa elimu na uduni wa kufahamu haki zao wanateseka, hivyo inabidi mara nyingine wauze ng'ombe ili kununua haki zao. Niliona niliseme hilo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, wananchi wanakuwa hawana hati za nyumba lakini wana ofa. Mradi wa kurasisimisha mali za maskini bado haujakamilika, naiomba Wizara hii ikae na kubuni kwamba tutatimiza vipi kuwapa watu haki ya dhamana walio na ofa wakati hawana hati za nyumba, si kwa sababu hawapaswi kuwa na hati bali mfumo bado haujakamilika. Naomba Serikali itathmini na ione jinsi gani itawatendea haki watu wenye ofa ili waweze kupata haki zao za dhamana.

Mheshimiwa Spika, mdidimio wa haki za binadamu ni mkubwa sana katika maeneo yetu ya Mkoa wa Shinyanga. Sisi kule tunategemea kwamba, sura na mantiki ya haki za binadamu ni pale tu itakapotokezea kwamba, Tume ya Haki za Binadamu itakuja kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme machache kuhusu kunawirisha mhimili wa Mahakama Kuu. Wakati umefika sasa, Serikali muwatengenezee nembo ya bendera ya kutambulisha kwamba, huo ni mhimili kama tulivyo na nembo ya bendera yetu sisi hapa Bungeni. Nitashukuru sana kama hilo litafanyika na Serikali ikaleta hoja hiyo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kusema kwamba, Majaji Vijana wasaidiwe kupata uunganifu wa Majaji Wastaafu kwa kupewa hata kazi za muda. Tunaweza kubuni na kugundua cheo mkawapa labda *Advisor Retired Judges*, hii ni kwa sababu tunahitaji kuvuna misimu mbalimbali ya uzoefu wa Majaji ili waweze hawa Vijana kunawirishwa maarifa yao na elimu. Hivi sasa wana upungufu; watasadikishwa na kuthaminishwa vipi kama hawana masimulizi au majadiliano? Kwa hiyo, inabidi wachelewe hata kutoa hukumu wakijitahidi kutafuta waelewe wapi wanawenza kupata ushahidi ama kumbukumbu za Hakimu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ni muhimu sana leo nikalizungumzia, wakale wanasema ya kwamba, kila binadamu kaumbwa na viwango vyake vya uelewa na mara nyingine binadamu anaposema jambo, anaomba asaidiwe kupata ujazo kwa upungufu alionao.

Mheshimiwa Spika, Bungeni ni mahali pa kunawirisha na kusadikisha na kuthaminisha jamii kwamba, hapo wapo viongozi na mhimili. Bunge linazungumza kwa maslahi yao. Napenda hapa nitoe tafakari moja nzuri sana, napenda kupongeza kwamba, Zanzibar ni chuo ambacho kwa kweli kisiasa na kwa ustawi wa maendeleo na kwa maana ya kuvumiliana, sisi Afrika tunapaswa kwenda kujifunza Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema hilo kwa sababu Ukristo Zanzibar uliruhusiwa na Sultani aliyekuwa Muislamu, akawapatia kiwanja cha kujenga na Waislamu na Wakristo Zanzibar wanaishi kwa amani na mustakabali wao ni upendo, umoja na mshikamano. Kwa hiyo, Tanzania Bara ni vyema Wakristo na Waislamu tukaenda kujifunza Zanzibar huko panafanyika nini.

Mheshimiwa Spika, naomba kuipongeza BAKWATA, kwa juhudzi zake za kupiga vita Ugonjwa wa UKIMWI. UKIMWI ni sawa na ujinga, kwa hiyo, binadamu anahitaji kuelimishwa. Vile vile Maaskofu wameungana katika vita dhidi ya UKIMWI. Nawaomba Baraza la Wakristo, ambalo sasa hivi wanatoa elimu ya uraia, liendelee kutoa elimu ya uraia, tupate viongozi bora dhidi ya wanasiisa uchwara, Madiwani na Wabunge dhoofu. Vilevile BAKWATA, waunge mkono. Naomba kutahadharisha ya kwamba, dhana hii ya kanisa kutoa elimu ya uraia, isipokelewe vibaya. Natambua kwamba, mwegemeo wa tafsiri ya binadamu uko katika dhamira binafsi, kila binadamu ana mwegemeo wake.

Mheshimiwa Spika, hoja hii ni muhimu sana ikatazamwa, kwa sababu mficha maradhi hufichuliwa na kifo. Hivi sisi viongozi tunahisi ya kwamba ndiyo tuna haki miliki? Sisi ni waja wa Mwenyezi Mungu, tunaelewa na ukweli ni kwamba, kila binadamu ana hulka na silka yake. Wapo viongozi walaghai; hivi kweli hatufahamiani lakini wananchi wanaelewa? Je, elimu ya uraia sote tunaifahamu? Tuachie Baraza la Wakristo watoe elimu hiyo.

Mheshimiwa Spika, Wasukuma wangu dini yao ni ramli. Sasa hawa dini yao na kanisa lao ni Tume ya Haki za Binadamu. Ninaomba Tume ya Haki za Binadamu, ifungue Misikiti na Makanisa ya kuja kutuelimisha Wasukuma Watanzania kule hawajui haki zao. Wakinishwa kidogo, hata mifupa ya mafuvu ya kichwa cha ng'ombe wakiambiwa ni kichwa cha binadamu ulimuua anauza ng'ombe. Ninaomba mje kutukomboa. Kwa hiyo, mimi napongeza juhudzi za kanisa kutoa elimu ya uraia.

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kwamba, waumini wa kikristo si wa chama kimoja. Waumini wa kikristo ni wa vyama mbalimbali. Sasa panakuwaje na hofu? Mimi BAKWATA naipongeza sana na vilevile wanaendesha elimu ya uraia. Kwa hiyo, ninaomba sana, mwegemeo wa tafsiri usiwe wa hila na visa au uwe na upungufu, omnia ujazwe kabla hujatoa kauli kwani mnena ya Mwenyezi Mungu, ukiwa na dhamana ya uongozi unasadikisha jamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niliona hili niliseme kwa sababu ulimi na meno ukigombana, dhahama yake ulimi hutoka damu. Sasa nilipenda nitahadhalishe hilo. Aidha, napenda kusema kwamba, angalieni sana Rwanda na Burundi kwa nini ilitokea hivyo? Umoja wa

Tanzania, unazungumzwa sana na Katiba yetu na napenda ninukuu ibara ya 18 inasema: "Haki ya uhuru wa mawazo: kila mtu ana uhuru wa kuwa na maoni na kueleza fikra zake na haki ya kutafuta na kupokea habari bila kujali mipaka ya nchi; ana uhuru wa kufanya mawasiliano na haki ya kutoingiliwa katika mawasiliano yake; anayo haki ya kutoa taarifa wakati wowote kuhusu matukio mbalimbali muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na pia kuhusu masuala muhimu kwa jamii."

Mheshimiwa Spika, viongozi wa madhehebu washirikiane na Serikali. Hivi ni nani anayeweza kusema ya kwamba, kanisa linataka kuihujumu Serikali; hivi Usalama wa Taifa umekufa? Rais Kikwete atakubali? Waziri Mkuu atakubali? Ninaomba tusizushe hila kwa mwegemeo wa tafsiri zenye upungufu. Mwenyezi Mungu, atatuepusha na mitihani mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi/Kicheko*)

**SPIKA:** Nakushukuru Mheshimiwa Shibuda.

## **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri kwa Kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, je, kwa nini watoto wadogo wanawekwa gereza moja na watu wazima?

Sheria inasemaje kama mtoto wa shule anapofanya kosa na hakimu kumhukumu na huyo kijana amefaulu kwenda Kidato cha kwanza? Je, nchi hii haioni kuwa inamnyima kijana elimu na kumfikisha mahali akawa mtukutu zaidi?

Sheria ya kulipa mama ambaye amezaa mtoto nje ya ndoa na kulipwa Sh. 100 italetwa lini?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Naungana na wenzangu, kutoa rambirambi zangu kwa Marehemu Sheikh Suleiman Gorogosi, pamoja na Profesa Haroub Othman. Zaidi hatuna ila Mungu awape mapumziko mema. Amen.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu katika Wizara hii, kwanza, napendekeza Wizara hii iwe ya Muungano kwa sababu maudhui ya Wizara hizi ni moja. Hivyo, nahisi kuziunganisha Wizara hizi ni kutanua haki za binadamu ndani ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mtazamo wangu ni mbaya sana kwa Wizara hii kutokupewa fedha, kwa sababu inasimamia haki za watu na usalama wao. Hata ukitazama mtiririko

tu wa uwasilishaji wa hotuba, imechukua nafasi za Mwanzo kabisa, lakini kwa kweli Wizara hii hatujaitazama vizuri.

Mheshimiwa Spika, vijana wetu wanaohitimu shahada mbalimbali hata ikiwa sheria, mwishoni huangalia waende wapi kiajira na mtazamo huwa wanafuata mvuto. Leo taasisi hii ni muhimu, lakini haina mvuto; hakuna magari, hakuna samani bora, hakuna nyumba kwa mahakimu, hata *computer* tu shida tena za kazi, kusema kweli Wizara hii ni yatima.

Mheshimiwa Spika, bado Mahakama zetu henzieleweki katika maamuzi ya haraka, hata pale ushahidi unapokuwa wazi na hii tayari imejenga mazoea katika Mahakama zetu; mfano, maamuzi katika kesi ya samaki (uvuvi), kesi za Albino ambapo wauwaji wana vielelezo vyote. Suala hili limalizwe.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi, naomba wale vijana (wanafunzi), waliofungwa kwa sababu tu ya maji ya kunyweshea, waangaliwe ili waendelee na masomo na ubabe wa matajiri usiharibu maisha ya vijana wadogo. Ahsante.

**MHE. MOHAMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kutoa salamu zangu za dhati kwako. Aidha, napenda kutoa salamu zangu za rambirambi kwa vifo vya wapendwa wetu; Sheikh Suleiman Gorogosi na Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Profesa Haroub Othman. Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi. Amen.

Mheshimiwa Spika, Mahakama zetu nyingi hapa nchini ziko katika hali duni sana, kwa majengo na vitendea kazi. Kutokana na hali hiyo, ufanisi wa kazi unashuka zaidi na kusababisha usumbufu usio wa lazima, kwa wale wote wanaohitaji kuzitumia Mahakama kwa kutafuta haki zao, kwani Mahakama ni sehemu pekee pa kupata haki yako.

Mheshimiwa Spika, upungufu wa mahakimu kwenye Mahakama zetu, unasababisha ucheleweshaji wa maamuzi katika kesi ambazo ushahidi wake uko wazi na zina uwezo wa kusikilizwa na zikaisha kwa kipindi kifupi sana. Upungufu huo wa mahakimu unasababisha ucheleweshaji na wakati mwingine unachangia kuongeza mahabusu magerezani.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache, naunga mkono hoja hii.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Waziri, Mheshimiwa Chikawe, kwa kazi nzuri na kwa hotuba yenye utashi mkubwa wa kuziendeleza Mahakama. Hata hivyo, bajeti hiyo ni ndogo mno kwa shughuli za Wizara hiyo. Ninachukua fursa hii pia, kumpongeza Katibu Mkuu, Mheshimiwa Mhaiki na Wataalam wake. Pia ninawapongeza Mheshimiwa Jaji Mkuu, Agustino Ramadhani, Majaji wote na Mahakimu wa ngazi zote, kwa kazi nzuri. Ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Serikali kwa kukamilisha ujenzi wa Mahakama ya Kibutuka Liwale na nyumba za Mahakimu. Pia ninaipongeza Serikali kwa jitihada za kusomesha vijana wengi ili kujaza nafasi za mahakimu wa ngazi zote. Hata hivyo, bado patakuwa na upungufu mkubwa wa mahakimu wa ngazi zote, kwani idadi ya wanaostaafu na kadhalika ni kubwa. Ninashauri baadhi ya mahakimu wanaostaafu, kama wapo wanaofaa na kupenda kuendelea, ni vyema wakapewa nafasi hiyo bila vikwazo visivyo na sababu. Haiwezekani mstaafu aliyefanya kazi ya uhakimu vizuri, kwa zaidi ya miaka 15 au 20, awe hafai kwa *contract* ya miaka miwili. Haiji akilini mwangu; hivyo, ninashauri hilo liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru Serikali kwa kutupatia gari Mahakama ya Wilaya ya Liwale. Ninaomba sasa iboreshwe Mahakama yenewe ya Wilaya ambayo jengo lake ni la Mjerumani limepitwa na wakati na lililojitokeza ni kwamba, Mahakama ya Mwazo ya Kibutuka ina mvuto zaidi kuliko Mahakama hiyo ya Wilaya.

Ahsante, ninaunga tena mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo mazuri aliyyoyatoa Mheshimiwa Waziri. Napenda kuchangia yafuatayo, ambayo hayakupewa mkazo kwenye taarifa yake:-

Jimbo la Kilwa Kaskazini halina mahakimu na pia vitendea kazi na miundombinu ni duni sana. Nadiriki kusema kuwa, tunajisikia kama hatupo kwenye Karne ya 21, kwa mfano, Mahakimu ni wachache sana na hawana ulinzi wa kutosha, hasa wa Mahakama ya Mwanzo/kiiji. Vitendea kazi hakuna kabisa, kiasi kwamba, mahakimu huwaomba wenyewe kesi karatasi, peni na kadhalika.

Watuhumiwa hupelekwa kwenye gereza lililopo Kilwa Masoko, kwa kusindikizwa na mgambo au Mtendaji wa Kata na wanatembea kwa miguu umbali wa zaidi ya kilomita 80 wakiwa wamefungwa kamba badala ya pingu. Hivyo, huhatarisha wapelekaji endapo wale watuhumiwa wataverageukia njiani.

Ni lini Kilwa Kaskazini itapata magereza yake yenewe wakati ardhi tupu za kujenga si tatizo kabisa? Kutokana na hali ya maendeleo, makosa ni mengi mno. Tungejengewa japo mahabusu kwa ajili ya watuhumiwa tungejiona tumejaliwa.

Katika Kata ya Kipatimu kuna majengo ya *mission*, ambayo yangetumika kuwekwa watuhumiwa bila wasiwasi wowote, lakini askari magereza hawapo.

Je, unafahamu kwamba kuna Kata ya Kandawale isiyotawalika katika Jimbo la Kilwa Kaskazini? Wavunjaji wa sheria na haki za binadamu wapo wengi sana na ni rahisi kukimbilia kwenye Wilaya nyingine au mbuga za Selous kujificha.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. MWAJUMA HASSAN KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa afaya njema na kuniwezesha kuchangia hotuba hii. Nakushukuru na wewe kwa kuliongoza Bunge hili, kwa umakini na umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Spika, ningependa nianze kwa kuzungumzia kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza Waziri wa Wizara hii, kwa kuweka wazi kwamba, mnamo mwaka 2009/10, anategemea kuanzisha Mahakama ya Kadhi Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mahakama hii ni muhimu sana na pia ni kilio cha muda mrefu kwa Watanzania, kwa hiyo, ninaiomba Wizara isicheleweshe suala hili ili wale wanaoshindwa kupata haki zao kwa kupitia Mahakama hii, waweze kupata haki zao bila usumbufu wa aina yoyote.

Mheshimiwa Spika, ningependa kumshukuru tena Mheshimiwa Waziri, kwa kuweza kukamilisha mchakato wa kutenganisha shughuli za upelelezi na uendeshaji mashtaka.

Mheshimiwa Spika, ningependa kumwomba Mheshimiwa Waziri kwamba, hao Mawakili 47 ambao aliwaajiri mwaka 2008/09, bado ni kidogo sana kwani kuna baadhi ya Mahakama bado kesi zinazidi kulimbikizwa kwa uchache wa wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningemwomba Waziri aongeze tena kuajiri Mawakili wengine ili kesi ziweze kuhukumiwa kwa urahisi na utaratibu mzuri.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mungu, kwa ulinzi wake. Nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Jaji Mkuu na Watendaji wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nichangie maeneo yafuatayo:-

Naishukuru Serikali kwa kufungua Mahakama ya Wilaya, ambayo imeondoa tatizo la wananchi kufuata haki yao Kahama.

Serikali itupatie gari la Mahakama ya Wilaya. Hata hivyo, namshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa kuahidi upatikanaji wa gari hilo.

Waheshimiwa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ni vizuri tuwapatie pikipiki.

Serikali ijenge mahabusu katika Mahakama ya Wilaya.

Mtumishi katika Mahakama (W), Ndugu Luhaga Mwandum, ni tatizo kubwa sana, anataka kutuharibia Mahakama. Naomba Serikali imwondoe haraka sana, pengine amekaa muda mrefu sana Bukombe. Yeye alikuwa Mahakama ya Mwanzo, baadaye amepelekwa Wilayani. Naomba huyu mtumishi aondolewe, asiendelee kuvuruga Mahakama na wananchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ichukue jukumu la kuharakisha utoaji haki kwa wananchi. Katika Wilaya ya Bukombe, zipo kesi nyingi sana za mauaji ambazo hazifiki mwisho. Mfano, Kesi MC 19/2008 – USH/695/2008 ya Anthony d/o Julius na wenzake. Hawa vijana kwa uthibitisho wa Uongozi ngazi ya Kijiji, wanasema hawana hatia ila tu ni ugomvi waliokuwa nao vijana na polisi, ndiyo maana wakabambikizwa kesi. Naiomba Serikali iwasaidie kuwapatia haki yao.

Mheshimiwa Spika, Wazee wa Mabaraza ni vizuri walipwe madai yao. Hata hivyo, nampongeza Mheshimiwa Waziri, alipotembelea Bukombe alipatiwa taarifa hizi na alizipokea.

Mheshimiwa Spika, katika nchi isiyo na dini ni vizuri Serikali iache madhehebu kufanya utaratibu wake bila kuhusisha Bunge. Haifai tena haipendezi, kuanza kulazimisha Watanzania tujunge na mfumo wa Mahakama ya Kadhi.

Mheshimiwa Spika, kimsingi, Mahakama ya Kadhi kutumia fedha za Watanzania suingi mkono suala hili, kwani tusipokuwa makini, tutaleta mpasuko katika nchi wa Wakristo na Waislam.

Mheshimiwa Spika, ni afadhali Serikali ilauwiwe kuwa haikutekeleza Ilani ya 2005, kuliko kuruhusu suala hili litakalopasua na kuwagawa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kuwa, wanaohitaji Mahakama hii, watengeneze utaratibu wao nje ya Bunge tena nje ya fedha za wananchi.

Baada ya mchango huo, naunga mkono hoja kwa hali zote.

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuanzisha utaratibu wa uendeshaji mashauri Mahakamani kwa kutuma Mawakili badala ya ilivyo sasa, ambapo tunatumia Polisi. Utaratibu huu wa kutumia Mawakili wa Serikali kuonesha mashauri Mahakamani, utawezesha Polisi kushughulikia majukumu yake ya msingi, ambayo ni pamoja na ulinzi na usalama wa raia na mali zao.

Kwa kuwa zoezi hili limeanza kwa awamu, nashauri Serikali na Wizara kwa ujumla, kuanzisha utaratibu wa kusambaza kwa kusomesha wanasheria wengi ili kukidhi mahitaji. Hili linawezekana kama lilivyowezekana na kufanyika na linavyoendelea kufanyika katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya ufundi. Elimu wamefundisha na kuandaa walimu ili kutatua tatizo la uhaba wa walimu; hivyo basi, ni jambo lisilohitaji mjadala kwa Wizara kusomesha wanasheria wengi ili waweze kusimamia uendeshaji wa mashauri.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara itazame uwezekano wa kuwa na Mahakama za Mwanzo karibu na sana na wananchi hususan eneo la Jimbo la Kigoma Kusini, lenye Kata 12 ambazo toka Makao Makuu ya Kata hadi nyingine ni takriban kilomita 250. Utoaji wa haki katika Mahakama za Mwanzo unakuwa ni sumbu. Nashauri sana Wizara ione uwezekano wa uhakika wa kuwa na Mahakama maeneo kama Kahu, Buhingu, Sunuka, Kandaga na Simbo. Tunahitaji kufikisha huduma hizi karibu sana na wananchi. Hivyo, kuwa na Mahakama au Ofisi za Mahakama za Mwanzo katika maeneo nilioainisha.

Mheshimiwa Spika, Mabaraza ya Ardhi ya Kata, nashauri watu watakaoendesha na wanaoendelea kusimamia Mabaraza ya Ardhi ya Kata wapatiwe mafunzo yatakayoingia kwa undani ili kuwapa upeo wa kuamua kwa haki mashauri yanayofikishwa mbele yao, elimu isiwe ya kurashia rashia.

Mheshimiwa Spika, hivi tatizo liko wapi kwa Tanzania kujiunga na OIC? Hii hofu ya Wakristo kuwa nchi hii itafanywa ya Kiislamu mbona Msumbiji, Uganda, Ivory Coast na nyingine ambazo sio za Kiislam na ni za Kikristo kiutawala hazijaweza kubadilika na kuwa za Kiislamu?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Waraka wa Wachungaji; hivi Kanisa Katoliki linataka kuipeleka wapi nchi hii? Hivi unapotoa Waraka wa kuelekeza waumini wa madhehebu ya Kikatoliki wajifunze namna ya kumchagua kiongozi wa nchi; Waraka huu mantiki yake ni kuleta vurugu nchini. Tena baya zaidi ni kwamba, Maaskofu hao sio wa Wakristo wote, bali ni Kanisa Katoliki. Kwa nini hali ya kutoridhika na uongozi iwe inajitokeza wakati Rais wa nchi akiwa Muislam?

Nchi hii ni yetu sote, hakuna haja ya dini fulani kudhani kuwa ina haki na masuala ya nchi kuliko nyingine. Kama wanadhani ipo haja ya kusaidia uongozi au kusimika uongozi bora kuliko uliopo, hivi isingekuwa vyema dini zote na madhababu yote; Waislamu kwa Wakristo wakakutana ili kuishauri Serikali namna ya kuondoa ujisadi?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mahakama ya Kadhi, binafsi sikubaliani na Wizara jinsi inavyopiga dana dana suala hili. Kwa nini Wizara ikae na kukubaliana na Viongozi wa Kidini wa Waislam ili waamrishe mambo yatakayoingizwa kufikia uamuzi katika masuala ya Waislamu?

Mheshimiwa Spika, tatizo la kuruhusu Mahakama ya Kadhi kama vile Mahakama ya Kazi, Ardhi na Biashara lipo wapi? Kwa nini Serikali ishindwe kuanzisha Mahakama ya Kadhi ambayo itasimamia masuala ya Waislam tu na Mahakama nyingine au mfumo wa Mahakama uliopo ushughulikie matatizo yanayowahusu wote bila kujali imani zao? Yapo mambo ambayo ni ya jumla bila kujali imani zetu, lakini yapo mambo ya ndoa, mirathi na talaka. Hivi kupata Mahakama ya Kadhi ni mpaka watu wa upande wa pili wakubali?

Mheshimiwa Spika, hivi hofu ya kupata uanachama wa OIC inasababishwa na nini au ndio hadi wale wa upande wa pili (Wakristo) wakubali kama Mheshimiwa Waziri alipokuwa anahojiwa na TBC mwaka jana alivyosema? OIC siyo chombo cha kidini na ndio maana uanachama hauhitaji dini ya nchi husika. Ni wakati muafaka sasa Serikali ione umuhimu wa kuijunga na Taasisi hii ili nchi na wananchi waweze kupata faida wanazopata nchi nyingine za Kiislam na zisizo za Kiislam na za Kikristo.

**MHE. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Mathias Chikawe, Waziri wa Katiba na Sheria kwa yafuatayo:-

Kwanza, kunisaidia kwa moyo alipokuwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria na nampongeza kwa kuongoza Wizara ya Katiba na Sheria, baada ya kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri wa Katiba na Sheria.

Pili, kwa kuipa Wilaya ya Hanang' na Mkoa wa Manyara, kipaumbele kwa kujengewa Mahakama. Wananchi wa Hanang na Manyara, wanamshukuru kwa dhati.

Tatu, kwa kutembelea Mkoa na Wilaya yangu ya Hanang, kuona maendeleo na changamoto zilizopo za Sekta ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa aweze kuona Baraza la Ardhi la Wilaya ya Hanang linaanzishwa ili Wananchi wa Jimbo la Hanang, wasiendelee kusumbuka kufuatilia huduma za Baraza hilo Babati. Naomba hilo lifanyike mapema.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, Mwanasheria Mkuu, Jaji Mkuu, Naibu Mwanasheria, Katibu Mkuu, pamoja na Majaji, Mahakimu na Watumishi wote.

**MHE. ZAYNAB MATITU VULU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii, nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, kwa kazi nzuri anayoifanya. Naipongeza Hotuba yake ya Bajeti. Hali kadhalika, nampongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Katibu Mkuu na Watendaji wote.

Mheshimiwa Spika, kilio cha Serikali ni kupunguza au kuondoa kabisa tatizo la watoto wanaoishi katika mazingira magumu, ambapo hata jamii nayo inasikitishwa kwa kuona jinsi watoto hao wanavyoishi. Chanzo cha tatizo hili huenda ni watoto kufuata makundi ya rika au malezi. Vile vile kuna tatizo la Sheria ya Matunzo ya Watoto waliozaliwa nje ya ndoa au hata watoto ambao wazazi wao wameachana.

Mheshimiwa Spika, Sheria hiyo imepitwa na wakati kwa maana Sh. 100 haina thamani tena na taifa linazidi kupoteza nguvu kazi ya watoto amba ni taifa la kesho.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali inapata kigugumizi kipi cha kuchelewesha kufanya marekebisho ya Sheria hiyo; na kama kufanya marekebisho inabidi zipitiwe/vipitiwe vifungu vyote ambavyo vitachukua muda mrefu; kwani nini Serikali

isilet kipengele cha Sheria hiyo tu ili kuweza kuwasaidia na kuwalinda mama na mtoto atakayeathirika?

Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali italeta hapa Bungeni Marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 kwani nayo imepitwa na wakati? Vile vile Sheria ya Mirathi. Hizi zote zinamkandamiza mwanamke na mtoto.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza idadi ya Mahakimu ambao watafanya kazi katika Mahakama za Mwanzo zilizopo kwenye Wilaya na Kata nchini?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kuchukua fursa hii, kumpongeza Waziri wa Sheria na Katiba, pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa hotuba nzuri iliyotolewa leo.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa leo ni kuhusu masuala mawili yafuatayo:-

Kwanza, kwa muda mrefu sasa Serikali imekuwa ikishindwa katika kesi nyingi ambazo imekuwa nazo katika Mahakama. Ninachojua ni kwamba, kesi inapita katika taratibu nyingi kutayarishwa. Kwanza, polisi wanapitia katika utaratibu wao, lakini baadaye inapitia kwa mwendesha mashtaka. Je, ni kwa nini Serikali haijawahi kuangalia suala hili na kufanya utafiti ili kuangalia tatizo liko wapi?

Serikali imekuwa ikipoteza pesa nyingi kwa ajili ya fidia kwa wadai, kwa kesi ambazo huonekana wazi kuwa Serikali imezidiwa ujanja. Je, ni tatizo la Waendesha Mashtaka, Mahakimu au Majaji?

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni ujenzi wa Mahakama katikati ya miji. Nashauri Mahakama zilizopo mijini katikati kama vile Mahakama ya Kisutu, zihamishwe zipelekwe nje ya mji, kwani zinasababisha foleni kutokana na msongamano mkubwa wa magari yaliyopo, unaotokana na msafara wa watuhumiwa hasa pale zinaposikilizwa kesi kubwa. Aidha, kunakuwa pia na msongamano watu wanaokuja kushuhudia kesi hizo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HERBERT JAMES MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria na Watendaji wote, kwa kuwasilisha hotuba nzuri na mpango mzuri wa maendeleo ya Mahakama.

Napenda pia kuhoji na kutoa ushauri katika maeneo yafuatayo:-

Hakimu katika ngazi mbalimbali kutoka Mahakama Kuu hadi Mahakama za Mwanzo, hurekodi maelezo kwa kuandika kwa mkono. Kazi hii ni ngumu na inachosha

sana na pia inatoa mwanya kwa hakimu kutoandika kwa usahihi yanayoelezwa na wakati mwingine kutosikia au kuelewa kwa usahihi yaliyosemwa. Je, hakuna utaratibu bora wa kisayansi unaoweza kuanza kutumiwa na Mahakama wetu kurekodi maelezo Mahakamani. Kwa mfano, kuna uwezekano gani wa kutumia mfumo kama wa Bunge (*Hansard*), katika Mahakama zetu hatua kwa hatua.

Taafira ya Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Matumizi ya Fedha 2009/10, inaonesha jitihada za ujenzi wa Mahakama Kuu za Mikoa na Wilaya; nawapongeza. Hata hivyo, uwiano wa kazi za ukarabati hauridhishi sana. Baadhi ya Mahakama za Mwanzo katika Wilaya ya Muheza zimesahauliwa kabisa. Licha ya kukumbusha katika Hotuba ya Bajeti mwaka 2008/09, bado hata Wilaya ya Muheza ambayo ipo katika hali mbaya imesahauliwa. Majengo ya Mahakama za Mwanzo niliyoainisha mwaka uliopita ni pamoja na Kilulu (Kata ya Kilulu), Kicheba (Kata ya Kicheba) na Nkumba (Kata ya Nkumba). Pamoja na hali hiyo, Mahakimu huenda katika maeneo hayo ya kazi mara chache kwa wiki wakiwa hawana usafiri na hivyo kuchelewa au kutofika kabisa na pia kuhatarisha maisha yao. Pikipiki zilizokadirwa kutolewa katika bajeti hii, hazijaelekezwa huko hata moja! Ningombwa sana moja kati ya nyumba 10 za Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo katika maeneo ya vijiji ielekewe Muheza.

Mfumo wa kisheria na kuzuia utekelezaji wa amri za Mahakama au maamuzi muhimu, umekuwa ukitoa mwanya wa ucheleweshaji wa makusudi wa amri zinazotolewa kihalali na Mahakama. Mfano, Amri ya Mahakama inapotolewa kuza nyumba ya mshtakiwa, inawekewa pingamizi dalali asiuze nyumba hiyo. Upo mgongano hapa, licha ya sheria kuruhusu! Kwamba; amri ya kuza nyumba imetolewa na Mahakama! Matokeo ya migongano hiyo ni ucheleweshwaji wa haki na kuongeza malalamiko dhidi ya utendaji wa Mahakama.

Baadhi ya kesi zinachukua muda mrefu sana kutajwa na hata kupangwa kusikilizwa. Mfano: Kampuni ya BP Tanzania Ltd., ambapo Serikali inamiliki hisa asilimia 50, imefungua mashtaka dhidi ya mwendeshaji wa kituo chake cha mafuta eneo la Upanga (karibu na Hospitali ya Agakhan), ambapo mwendeshaji huyo amekiuka mkataba wa uendeshaji kwa kuacha kununua mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa kutoka kwa mmiliki wa kituo hicho BP (T) Ltd. na kutaka arejeshe kituo hicho. Shauri hilo sasa limechukua takriban miaka miwili bila kutajwa wala kusikilizwa! Kwa msingi huo, mwenye Kituo; BP (T) Ltd, aliyewekeza katika ujenzi, anakosa haki na Nembo yake BP (T) Ltd kuendelea kutumiwa na mwendeshaji bila kujali sheria na haki! Kimsingi, Kampuni kubwa kama hiyo ambapo Serikali ina hisa asilimia 50, inakandamizwa bila kupewa nafasi ya kusikilizwa! Ni vyema hali kama hii niliyoitolea mfano, ikaangaliwa na kurekebishwa hata kama itabidi kuangalia upya mfumo wetu wa Sheria unaopelekea mambo kama hayo kutokee bila kuhojiwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mwanasheria Mkuu na Katibu Mkuu, Ndugu

Oliver Mhaiki na Maofisa wote wa Wizara, kwa kujumuisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Mwaka 2009/2010 na kuyawasilisha vyema katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya Waziri aliyoitoa akiwasilisha hoja alisema katika bullet ya 17; Wizara imefanya rejea ya sheria mbalimbali zinazohusiana na Sheria ya Kupambana na Rushwa na kuziimarisha na kuzioanisha. Naipongeza sana kwa hatua hiyo.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa hatua mbalimbali ilizozichukua katika Programu ya Mpango wa Uboreshaji wa Mfumo wa Sheria. Lakini nina ushauri katika uboreshwaji wa mfumo wa usafirishaji na usindikizaji mahabusu na wafungwa kwenda kusikiliza kesi zao.

Mheshimiwa Spika, Serikali isitizame mijini tu, itazame na Wilaya zilizo pembezoni mwa miji, ambazo zinahudumia maelfu ya vijiji na kata za nchi yetu kwenye asilimia 74.3 ya wananchi wa nchi yetu. Hivyo, kuna kesi nyingi huko lakini mtuhumu anawekewa masharti ya kumhudumia mtuhumiwa, hasa gharama za usafiri kwenda mahabusu na kuja Mahakamani. Naomba uwewe utaratibu unaoeleweka katika kesi za Mwanzo ngazi ya kata, utakaowezesha haki kutendeka. Dola itimize wajibu wake wa kuwahudumia watuhumiwa, kwani mtuhumiwa anaposhindwa kutoa huduma hiyo ya usafiri, inafikia wakati huachiwa kwa visingizio mbalimbali; sababu kubwa ni kushindwa kutopelekwa Mahakamani. Sasa hii inaongeza uhalifu au uvunjwaji wa sheria wa mara kwa mara vijijini na kuwapa unyonge wananchi wema na wanaofuata sheria katika maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri pia amesema katika ukurasa wa 12, bullet 20(iv); kuimarisha Mabaraza ya Kata kwa kuwapatia mafunzo Wajumbe wote wa Mabaraza. Nawapongeza kwa hatua hii, kwani Mabaraza ya Kata yalikuwa yanafanya kazi bila mafunzo, ambapo kumekuwa matokeo mengi yasiyowaridhisha katika maamuzi na hivyo kesi nyingi zinakatiwa rufaa katika Mahakama za Wilaya na hivyo kufanya mrundikano wa kesi.

Naomba tusiishie katika mafunzo tu, tuwapangie na posho za uendeshaji kesi, kwani itawaondolea mawazo tofauti kwa wanyonge kutokuwa na imani na Baraza, kama unatenda haki pale unapotoa maamuzi kwa kesi iliyokuwa baina ya mtu asiyе na uwezo na yule mwenye uwezo wa kipesa. Kuna baadhi ya maeneo, wenye kesi huwa wanawagharimia Wajumbe kwenda sehemu ya mbali, yenye mgogoro, kuona wenywewe kinacholalamikiwa. Naomba Serikali wawekewe posho pia.

Naomba pia katika uboreshwaji wa sheria na kuimarishwa kwa kufanya tafiti, Serikali isisahau kuona ni jinsi gani ya kutunga sheria itakayohusu Usafirishaji Haramu Binadamu (*Illegal Human Trafic*), ulioshamiri siku za karibuni.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda niwashukuru Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria na Wataalam wake wote, kwa kuandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ni mhimili muhimu sana hapa nchini katika kutafuta na kutoa haki, lakini kwa bahati mbaya ni moja katika sehemu inayolaumiwa sana kuwa haitekelezi majukumu yake ipasavyo; ama kwa kukosa nyenzo muhimu za kufanya kazi au kwa kutawaliwa na rushwa; hivyo basi, pamoja na maboresho yote iliyoyafanya, bado kuna umuhimu kubadilisha mtazamo wa Watanzania walio wengi kuwa hiki ni chombo chao ambacho haki itapatikana kwa kila mtu.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005, ilieleza wazi kuwa, itaananza Mahakama ya Kadhi. Inaonekana kuwa, CCM iligundua kuwa kura za Waislam wapatao asilimia 60 ya Watanzania wote ni muhimu na kwamba, njia pekee ya kuwapata ni kuvuta hisia zao kwa kuwaambia wataundiwa Mahakama ya Kadhi, lakini kumbe hiyo ilikuwa ni kiini macho tu! Iweje hadi leo, Serikali inakuja na maelezo kuwa itaorodhesha misingi ya kiislam (*Islamic Principles*) katika Mahakama zote nchini. Kwanza, Serikali ya CCM ikiri kuwa, imeshindwa kutekekeza ahadi yake, labda kwa kuogopa vitisho kutoka kwa watu wa dini nyingine. Inawezekanaje Sheria za Kiislam zihukumiwe na Hakimu asiye Muislam?

Serikali itamke wazi kuwa, imeshindwa kutafuta ufumbuzi wa kuunda Mahakama ya Kadhi. Kwa nini Serikali itoe mfano wa Afrika Kusini badala ya kutoa mfano wa Zanzibar au Kenya? Kinachoonekana, Kanisa Katoliki halijakubali iundwe Mahakama ya Kadhi na hili ni kosa kubwa kwa Serikali kuwa mpaka kanisa likubali.

Mheshimiwa Spika, sambamba na Mahakama ya Kadhi, Serikali imepata kigugumizi kuijunga na IOC. Pamoja na maelezo mengi yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge na wadau mbalimbali, faida za kiuchumi zitakazopatikana na kutoa mifano ya nchi kama Uganda, zinavyofaidika hata kama si za Kiislamu, bado hadithi ndio ile ile; Kanisa Katoliki bado halijakubali, hivyo Serikali nayo haijakubali.

Mheshimiwa Spika, naomba niitahadharishe Serikali kuwa, isichezee amani ya nchi iliyopo sasa. Kuna mifano mingi ya nchi ambazo amani ilivurugika kwa sababu ya dini.

Mheshimiwa Spika, tunatambua ufinyu wa bajeti, kuiendeleza Wizara ya Sheria kuanzisha majengo, vifaa vya ofisi ni vichache na vingine vimepitwa na wakati. Jambo hili linakaribisha rushwa kwenye Wizara hii ya Sheria, ambayo ndio inategemewa kutoa haki kwa wote.

**MHE. SIRAJU JUMA KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Waziri, Jaji Mkuu, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Katibu Mkuu na Watendaji wote, chini ya Wizara hii, kwa matayarisho mazuri ya bajeti inayojadiliwa. Pamoja na hatua nzuri za utekelezaji wa hatua mbalimbali, kwa madhumuni ya kuboresha ufanisi wa

utoaji wa huduma za sheria hapa nchini, napenda kuainisha hapa chini, baadhi ya maeneo ambayo yanahitaji kushughulikiwa haraka.

Mahakama Kuu Kanda ya Tabora inajumlisha Mikoa ya Tabora, Kigoma na Shinyanga. Kanda hii ina Majaji wawili tu badala ya watano, kwa mujibu wa mahitaji ya *establishment*. Kwa hiyo, kuna upungufu wa Majaji watatu. Upungufu huu unaathiri ufanisi wa kazi za Mahakama Kuu Tabora; kuna haja ya haraka ya kuliziba pengo hili.

Zipo nyumba mbili za Serikali kwa ajili ya matumizi ya Majaji Mjini Tabora. Hivyo, Serikali inalazimika kutumia fedha nyingi kulipia gharama za hoteli na nyumba za kupangisha. Viwanja viro, tatizo ni uhaba wa fedha za kujengea.

Jengo linalotumika hivi sasa kwa shughuli za Mahakama Kuu Tabora halina hadhi inayostahili. Jengo hili hapo awali lilikuwa ni Ofisi za Manispaa. Kwa hiyo, hata bwalo la kusikilizia kesi ni dogo na pia hutumika kama maktaba. Hakuna nafasi ya kufanya marekebisho ya ziada. Kwa kuwa Tabora ndiyo Makao Makuu ya Kanda, nilitarajia kuwa Serikali ingelianza ujenzi wa jengo la kisasa la Mahakama Kuu Tabora, badala yake ujenzi umeanza Shinyanga! Ni dhahiri kwamba, kuna haja ya kuanza ujenzi wa jengo la kisasa, linalokidhi mahitaji ya Mahakama Kuu Tabora haraka iwezekanavyo. Kiwanja kipo, tatizo ni fedha. Nashauri zitafutwe fedha kwa utaratibu wa mikopo toka Mashirika ya Hifadhi ya Jamii (NSSF, PSPF na kadhalika).

Mkoaa wa Tabora na Wilaya ya Tabora, hazina majengo yake yanayokidhi mahitaji ya shughuli za kimahakama. Taasisi zote hizi zimerundikana katika eneo moja, kwa kutumia nyumba ndogo ndogo ambazo hazina hadhi ya Mahakama. Ufumbuzi wa tatizo hili, unafanana na ule wa Mahakama Kuu, yaani Serikali ijenge majengo mahususi kwa ajili ya Mahakama hizi. Viwanja si tatizo; tatizo ni fedha, zitafutwe kwa lengo maalumu kuititia bajeti na mikopo toka Taasisi za Hifadhi ya Jamii.

Wizara imejitahidi kuongeza idadi ya magari kwa ajili ya matumizi ya Majaji, Mahakimu na Watendaji wengine. Vitendea kazi vya maofisini kama vile kompyuta, mitandao ya *internet* bado ni tatizo. Ukosefu wa mitandao ya *internet* kwa utaratibu wa *Local Area Network (LAN)* katika ofisi mbalimbali za Mahakama, unaathiri ufanisi wa Watendaji mbalimbali. Aidha, kasoro hii itaathiri utafiti wa haraka kuhusu masuala ya kisheria na kadhalika na hasa kwa vile maktaba zetu nazo hazina vitabu na vijarida vya kutosha kwa ajili ya rejea za haraka. Wizara irekebishe kasoro hii haraka ili kuwawezesha watendaji kupata taarifa za karibuni zaidi (*more recent information*), katika masuala mbalimbali ya kisheria na kadhalika.

Pamoja na uwepo wa utaratibu wa kuwapatia Wafanyakazi wa Sekta ya Sheria, mikopo ya ujenzi wa nyumba kuititia Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, upatikanaji wa mikopo hii huchukua muda mrefu sana. Serikali iangalie uwezekano wa kuwawezesha wafanyakazi wa sekta hii, kupata mikopo ya nyumba kwa haraka zaidi.

Wafanyakazi wa Sekta hii ya Sheria, wanastahili kupata mishahara mizuri zaidi, kulingana na unyeti wa kazi waliyokabidhiwa ili wasiweze kurubuniwa kwa urahisi na watoa rushwa.

Matatizo ya ardhi ni mengi na yametapakaa nchi nzima. Mahakama Kuu ya Ardhi ina Majaji watano tu na wapo Dar es Salaam. Upungufu huu wa Majaji, unaathiri sana utekelezaji wa majukumu ya Mahakama hii. Kesi zinachukua muda mrefu sana kukamilika, kuna haja ya kurekebisha upungufu huu haraka.

Pamoja na kasoro nilizozieleza hapo juu, naiunga mkono hoja hii.

**MHE. DKT. GUIDO GOROGOLIO SIGONDA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu upungufu wa Mahakimu Mahakama ya Mwanzo; kwenye Jimbo la Songwe lenye kata 10, yupo Hakimu mmoja tu, ambaye Kituo chake ni Mji Mdogo wa Mkwajuni.

Matokeo yake, haki ya kisheria haitolewi ipasavyo kwenye Jimbo hilo. Tatizo ni umbali kati ya maeneo husika hadi hakimu anakofanya kazi. Kesi nyingi humalizwa kienyeji huko vijijini. Hali hiyo pia hushawishi rushwa mionganoni mwa Watendaji.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliahidi kuwakopesha Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo; ni lini Hakimu wa Jimbo la Songwe atakopeshwa pikipiki?

Mheshimiwa Spika, je, Wizara ina mpango wowote wa kuwapatia makazi ya kuishi (nyumba), Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo?

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Jimbo la Songwe, wangeshukuru sana kama ungefanya ziara ya kikazi kwenye Jimbo hilo. Tunakukaribisha kwa mikono yote.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, natoa pongezi kwa Wizara kufanya kazi zake vizuri.

Tunaomba Wizara ijipange vyema kusambaza Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo vijijini hasa katika Jimbo langu la Kalambo lenye Mahakimu wachache. Tujengeeni Mahakama za kisasa Makao Makuu ya Jimbo, Kijiji cha Matai, Kasanga, Mwambi, Mwarye na Legeza Mwendo, Makao Makuu ya Kata na Tarafa.

Usimamizi wa karibu kwa Mahakimu wasio na maadili, wanaokula rushwa na kuwakosesha haki wananchi, hivyo kufanya watu kukosa imani na Mahakama zetu. Nashukuru kwa kumwondosha Hakimu Mzee Issa, aliyepelekwa Chunya. Mumwangalie sana, anavuruga haki za watu Mahakamani.

Vijana wengi wamekwama kwa matatizo ya kushindwa kupatiwa fedha kujiunga na Law School of Tanzania, basi hawa vijana wapatiwe fedha za kurudishwa makwao wakatafute njia nyingine ya maisha.

Haki za Binadamu wadhibitiwe wasitumie vibaya chombo hiki, wamegeuka sasa kuwa haki za ng'ombe, kutetea uharibifu wa mazingira na nchi yote inateketezwa na wafugaji wanaotegemea kitengo hiki kutangatanga nchi nzima kwa kisingizio cha haki za binadamu. Pesa inayokusanywa na wafugaji, kuwapa watu mbalimbali ndani ya kitengo hiki sasa imekuwa kero kwa wananchi Wakulima wa Tanzania, kunyang'anywa ardhi yao nzuri kwa kilimo ili iharibiwe na mifugo. Waziri fuatilia rushwa hii ndani ya chombo hiki; wizi mtupu kwani wakulima siyo binadamu; wakati hao ndio wanaonusuru wala rushwa hao na njaa? Inasikitisha.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Nampongeza sana Waziri, hana Naibu Waziri, lakini anajitahidi sana kushughulikia haki za Kikatiba za Watanzania. Nampongeza Katibu Mkuu. Wizara hii ni mpya, kwa maana ya Sheria inayoipa mamlaka ya kujitegemea. Tunamfahamu Katibu Mkuu huyu ni mtu makini na ni msikivu, anatosha kusimamia shughuli hii muhimu ya eneo la haki.

Mheshimiwa Spika, Mahakama za Mwanzo ni kiungo muhimu cha Mwanzo wa upatikanaji wa haki. Ninaomba Serikali ichukue nafasi ya kutoa mwelekeo ili wananchi wahamasike kujenga Mahakama za Mwanzo kwa kushirikiana na Serikali (zana shirikishi).

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa msongamano wa kesi ni budi chuo cha Mahakama Lushoto kiongezewe uwezo hasa kifedha ili kiongeze udahili na kutoa wataalamu wengi kukidhi mahitaji ya Mahakama zetu.

Mheshimiwa Spika, Mahakimu wanaishi katika nyumba hafifu katika mitaa. Hivi hawawezi kuleta dhana ya haki ya KiKatiba na hasa haijengi uadilifu machoni pa jamii. Tunahitaji kutambua hili ili kusaidia Watumishi hawa wa Mahakama wawe na maisha yenye mwonekano wa utoaji haki.

Mheshimiwa Spika, suala ya usajili wa vizazi na vifo kwa wakati huu ni ajenda muhimu sana. Tumeona jinsi RITA wanavyofanya kazi katika kutatua tatizo hili la usajili. Kwa kuwa kwa sasa kuna umuhimu mkubwa wa kuhakikisha Tanzania wanapata vyeti hivyo kwa wepesi na kwa muda unaofaa, tunashauri Serikali iamue kuiwezesha RITA ili ifanye kazi maalumu ya usajili kuliko kusubiri katika maeneo au matukio muhimu tu.

Naomba sana suala la usajili wa vizazi na vifo liwekewe mpango mkakati ili Watanzania wengi wanufaikie.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RUTH BLASIO MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naunga mkono hoja. Pili, nimpongeze Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana, Ndugu Mathias Chikawe (Mb), kwa uwasilishaji wa hoja yake.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia yafuatayo:-

Naomba Mahakama ya Mwanzo Muhutwe iwe kwenye orodha. Vile vile Mahakama ya Rushwa iangaliwe, ipatiwe majengo na huduma zinazostahili. Hadi sasa Mahakama za Mwanzo za Muhutwe na Kamachumu zinahudumiwa na Hakimu mmoja. Hali hii inafanya kesi ziende kwa kasi ndogo. Naomba Serikali, itupatie Hakimu wa pili ili kila Mahakama iwe na Hakimu wake. Pia Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wana shida ya usafiri, hali hii inafanya kesi zichelewe na haki ichelewe vile vile.

Mheshimiwa Spika, Mahakimu hawana nyumba kila Mahakama, mfano ni Mahakama ya Mwanzo Muhutwe. Mahakimu wanapopangwa pale, hupata shida ya makazi.

Mrundikano wa mahabusu nchini na wafungwa ni tatizo sugu. Mojawapo ya sababu ni kesi kuchelewa. Pili ni kila kosa kufikishwa polisi.

Mheshimiwa Spika, napendekeza vianzishwe vikundi vyatupanishi vyenye sura ya uwakilishi wa jinsia na rika zote ili kesi ndogo ndogo kama za wizi wa kuku zimalizwe katika jamii.

Mheshimiwa Spika, taratibu zitafutwe ili kesi zisiwe zinachelewa kufanyiwa upelelezi.

Mheshimiwa Spika, mauaji ya maalbino; imekuwa ni aibu na fedheha kwa watu kuamini utajiri kwa ushirikina hadi karne hii. Hata hivyo, naipongeza Serikali kwa hatua ilizochukua. Hatua hizi ziwe ni za kudumu, watu wasionewe tena kwa maumbile, jinsia, ulemavu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia uzima na afya.

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe, Naibu Spika, Wenyeiti wa Bunge, pamoja na Viongozi wa Kambi ya Upinzani, kwa kutuongoza vizuri. Pia nampongeza Waziri.

Mheshimiwa Spika, majengo mengi ya Mahakama ni mabovu, kiasi kwamba inaponyesha mvua yanavuja na hivyo kuwa vigumu kuweza kufanya kazi zao kwa ufanisi. Ni vyema Serikali ikalionia hilo na kulipatia ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, kesi zinachukua muda mrefu kutohana na uchache wa Mahakimu na vitendea kazi na hivyo, kusababisha mrundikano wa mahabusu na watuhumiwa wengine mbalimbali. Serikali itafute njia ya kuondoa tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, maslahi ya Mahakimu yanapaswa kuangaliwa vizuri ili utendaji kazi wao uwe wa haki na ufanisi na hivyo, kuwafanya waepukane na rushwa ya aina yoyote.

Mheshimiwa Spika, wakati umefika kuwa na Katiba mpya badala ya ile ya 1977, ambayo ni *rigid* (habadiliki), ili iwe *flexible* (ibadilike), kuendana na wakati. Hii ni kutokana na mabadiliko ya kiuchumi, kisiasa na kijamii. Vile vile mabadiliko ya kutoka mfumo wa chama kimoja kwenda mfumo wa vyama vingi vya siasa. Pia hali ya ukweli na uwazi (*Truth and Transparency*).

Mheshimiwa Spika, wakati umefika wa kuanzisha Mahakama ya Kadhi bila pingamizi lolote, kwani hii ni haki ya Waislam katika utendaji wa shughuli zao zinazohusiana na dini yao.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa sheria ni muhimu sana katika utoaji haki za binadamu kwa wananchi wote. Sheria pia inapaswa kutekelezwa na Jeshi la Polisi, wanapofanya upelelezi kutokana na tuhuma au kesi zinazowakabili watu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, elimu kuhusiana na mambo ya kisheria inapaswa kutolewa kwa wananchi ili wasiingie katika makosa kwa sababu hawajui sheria kutokana na matendo yao mbalimbali kila ya siku.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kumekuwepo na migogoro kadhaa inayohusiana na ardhi, haki na sheria inapaswa kupewa kipaumbele ili kusiwe na uonevu wa aina yoyote hasa kwa wale watu ambao ni wanyonge.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Spika, msongamano wa mahabusu gerezani unachangiwa na ucheleweshwaji wa kesi. Nashauri Mahakama zimalize kesi mapema pindi ushahidi ukamilikapo ili kumpunguzia adha Mkuu wa Magereza ya matumizi ya bajeti ya ziada yasiyo na sababu yoyote.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru kwa Mahakimu kupata usafiri (magari), ndani ya Wilaya. Magari haya hayaendani na nyumba wanazoishi; ni sawa na kuoga kisha ukavaa nguo iliyovurugwa ndani ya tope. Naomba suala la makazi ya Mahakimu, lipewe nafasi kubwa katika Wilaya zote. Watumieni NSSF, PPP na kadhalika.

Shria nyingi zimepitwa na wakati na hata faini ndani ya Mahakama kadhalika; hivyo basi, yawepo marekebisho ya sheria zote zilizopitwa na wakati. Tunasubiri utekelezaji wa Mahakama ya Kadhi kama ilivyozungumzwa ndani ya hotuba hii.

Kwa ujumla, pongozi kwa hotuba nzuri.

**MHE. SEVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia Wizara hii kwa masikitiko makubwa sana. Mara kwa mara naiuliza maswali mengi Wizara na kulalamikia tatizo la majengo ya Mahakama; ubovu wake na madhara yake

hasa Mkao wangu wa Kagera; Maruku, Katelero, Katoro, Ibwera na si hapo tu; Karagwe inaongoza.

Pamoja na majengo ya Mahakimu, nafikiri taarifa unayo; juzi Hakimu wetu kauawa kwa kukatwa mapanga. Si hayo tu, kuna mengi sana yanayosababisha madhara makubwa sana; rushwa, mrundikano wa kesi kuchukua muda mrefu, ubambikizwaji wa kesi ovyo, unyanyasaji wa kila aina hasa Mkao wangu.

Tatizo la pikipiki na baiskeli ambalo ni kero mpaka leo naomba kusaidiwa sana; kuna siku italeta mgogoro kama tunaousikia kwenye mikoa mingine. Unaweza ukakisia mambo mengine kuhusu suala hili, sehemu nyingine zinaendeshwa Bukoba wanazuiwa; je, hiyo ni haki; sheria inazuia Bukoba tu sehemu nyingine zinafanya kazi? Naomba nipatiwe majibu kwa niaba ya Wananchi wa Bukoba na wale ambao wameshakamatwa na baiskeli na pikipiki basi wapelekwe Mahakamani kuliko kukaa polisi. Huo ni uharibifu na inasababisha rushwa kwa mapolisi ni kero ya miaka minne sasa. Litolewe tamko tupate kupumua sio kudanganyana. Chonde chonde, hili tatizo tusaidiwe kisheria.

Tanzania tulitangaziwa wananchi wote kupiga kura za maoni ya mauaji ya wale mavu wa ngozi (Albino); je, matokeo mbona hayatangazwi? Kuwaficha ni kulea mauaji na ukataji wa viganja utaendelea. Wananchi wanalamika eti Serikali inawalinda. Je, Jengo la Mahakama Bukoba Mjini hasa la Mkao mbona haliishi linasuasua? Kwa nini maofisi yarudi kwenye jengo hili tukizingatia Mahakama ziko kwenye ofisi finyu sana, hakuna sehemu ya kutunzia makabrasha, hakuna parking ya wateja sehemu ya mahabusu wananyanyasika sana? Naomba kupatiwa majibu niweze kujiridhisha.

Mheshimiwa Spika, nakutania bajeti njema.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Wilaya ya Kasulu ni mbaya sana na wakati mwingine kuhatarisha maisha ya Watumishi wa Mahakama. Ninapendekeza kwa udharura yafuatayo yafanyike:-

- a) Wizara ipeleke fedha haraka kwa udharura ili likarabatiwe Jengo la Ofisi ya Mahakama.
- b) Kwa kuwa eneo la Mahakama lipo na kuna jengo kongwe sana, basi harakati za kujenga jengo jipya uandaliwe.
- c) Eneo la Kata ya Buhoro halina Mahakama, basi harakati za ujenzi zianze. Mimi na Serikali ya Kijiji cha Buhoro tutashiriki.

Katika ujenzi huo, vifaa kama matofali, mawe na mchanga, vitaandaliwa na Ofisi ya Mbunge na Viongozi wa Kata wa Kijiji cha Buhoro. Wizara ituletee mabati, saruji, chokaa, misumari na mbaao. Aidha, jengo hili la Mahakama liende sambamba na ujenzi wa nyumba ya Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo.

Mheshimiwa Spika, wananchi kuzuiliwa kuingia Mahakamani eti kwa ajili ya usalama. Baada ya tukio la mabomu kurushwa Mahakama ya Wilaya ya Kasulu, mwaka jana, Jeshi la Polisi na Uongozi wa Mahakama, wanazuia wananchi kuingia Mahakamani kusikiliza kesi. Hii inafanya kesi kuendeshwa kimya kimya, bila wananchi kufuatilia mienendo ya kesi Mahakamani. Ninaomba Waziri atoe msimamo wa jambo hili, Mahakama lazima ziwe wazi (*Open Court*) na sababu ya usalama isichukuliwe kisingizio cha kufanya Mahakama yetu kuwa siri (*Closed Court*). Polisi wabuni njia mbadala ya kuhakikisha usalama unadumishwa Mahakamani na vitendo vya mabomu havitokei tena. Jambo la kuzuia wananchi kuingia Mahakamani ni kero kubwa sana na lazima lifikie mwisho.

Wilaya ya Kasulu ni kubwa sana katika Mkoa wa Kigoma. Mwaka 2006 lililetwa gari dogo aina ya Suzuki – Vitala. Gari hili halifai, ni bovu na sasa Mahakama ya Wilaya inahitaji gari kubwa, imara na linalokidhi jiografia ya Wilaya. Tuleteeni Land Cruiser Hardtop mpya mapema. Ninashauri Wilaya za pembezoni kama Kasulu, zipewe kipaumbele wakati wa kugawa vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu motisha kwa wafanyakazi, nashauri *strongly* Watumishi wa Mahakama za Wilaya na hata zile za Mwanzo, wapewe motisha maalumu ya kufanya kazi katika mazingira magumu, hasa katika maeneo ya Mikoa ya Kigoma, Rukwa, Lindi na Mtwara. *Special Package*, iandaliwe kwa kada za aina hii.

Mheshimiwa Spika, napendekeza ukaguzi wa mara kwa mara ufanyike ili kukabiliana na baadhi ya vitendo vya baadhi ya Mahakimu ambaao ni wala rushwa, waonevu na wasio waadilifu; wale watakaobainika basi hatua za haraka zichukuliwe. Katika baadhi ya maeneo ya Wilaya ya Kasulu, vitendo vya uonevu na uadilifu viliripotiwa kwangu na mimi kuwasilisha kwa Uongozi wa Wilaya hasa kwa *District Magistrate*. Hakimu mpya wa Wilaya aliyefika Kasulu ni kijana safi, apewe nguvu na Wizara yako ili atekeleze majukumu yake kikamilifu. Ameanza vizuri, Uongozi wa Wilaya tunampa ushirikiano unaofaa. Wizara tekelezeni yaliyo ndani ya uwezo wenu ili kujenga taswira nzuri ya Mahakama zetu katika Wilaya ya Kasulu.

**MHE. RITA L. MLAKI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nachukua nafasi hii, kuwapongeza Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote na Wizara yako, kwa kazi nzuri mnayoifanya. Pia nawapongeza kwa *Budget Speech* nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, ningependa kwa niaba ya Wakazi/Wananchi wa Jimbo la Kawe, nitoe shukrani kwa kuiweka Mahakama ya Kawe katika Mpango/Programu ya Uboreshaji wa Sekta ya Sheria, kwa kuamua kujenga Mahakama ya Kawe. Tunaahidi ushirikiano mkubwa. Ningependa kuchangia Bajeti hii kama ifuatavyo:-

Tunaomba Mahakama zitazame upya mfumo mzima wa uendeshaji wa kesi katika Mahakama za Mwanzo. Kesi ndogo sana ambazo upelelezi au ushahidi upo wazi, zinachukua mwaka mzima. Kuna kesi nyingi sana ambazo ni za wizi au watu wamepigana na kadhalika na mashahidi wapo, lakini kesi inapigwa tarehe na inapoanza kusikilizwa inachukua muda mrefu sana, wakati mwingine mshtakiwa anakosekana Mahakamani kwa makusudi ilimradiacheleweshe kesi na Mahakama haimchukulii hatua yoyote. Tungeomba serikali ilitizame hili ili iweze kuondoa kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali izitazame Mahakama za Ardhi. Wilaya ya Kinondoni ina kesi nyingi sana za Ardhi, lakini mpaka sasa Kitengo hicho hakina ofisi za kudumu, wamejibanza pale Ofisi ya DC katika chumba kimoja. Tafadhali naomba wapatiwe jengo linalokidhi mahitaji yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa uzima ili nami niweze kutoa mchango wangu. Naomba nimpongeze Waziri wa Katiba na Sheria, kwa hotuba yake nzuri. Vilevile nampongeza Naibu Waziri na Wataalam wote.

Mheshimiwa Spika, mimi ninawakilisha Wananchi wa Manyara, hususan Wananchi wa Simanjiro katika Mji Mdogo wa Mererani.

Mheshimiwa Spika, Mji huu una Mahakama ndogo ya Mwanzo, ambapo Hakimu anafanya kazi zake katika mazingira magumu sana. Nyumba anayoendeshea kesi ni mbovu, ya udongo na pia inavuja wakati wa mvua na wakati mwingine mafaili yanallowana.

Mheshimiwa Spika, Mji Mdogo kama Mererani, una wakazi 48,000. Kuna kesi nyingi za mauaji, wizi, ujambazi, ubakaji na kadhalika, kesi hizi zinapelekwa Babati Makao Makuu ya Mkoa; hivyo mwananchi lazima aende Mahakamani Babati.

Mheshimiwa Spika, kutoka Mererani kwenda Babati kupitia Arusha; nauli, kulala na chakula kwa siku tatu hadi kurudi nyumbani ni Sh. 100,000.

Mheshimiwa Spika, gharama hizi kwa mwananchi wa kawaida ni kubwa sana. Binti mmoja alibakwa na mshtakiwa alipelekwa Babati, lakini mama yake alishindwa kuhudhuria kesi Mahakamani na baadaye ilifutiliwa mbali. Wananchi wengi wanaachilia mbali.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kesi kama hizi haziwezi kuendeshwa katika Mahakama ya Mwanzo, naomba Serikali iangalie uwezekano wa kujenga Mahakama ya Wilaya ili kupunguza adha wanazopata Wananchi wa Mererani.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa pia Serikali inatumia gharama kubwa kuwatoa washtakiwa Mererani kwenda Babati; je, haioni kuwa kuna hatari ya kutorosha washtakiwa? Hivi mshtakiwa akitoroka ni hasara ya nani? Je, wale wananchi wanaoshindwa kufuatilia kesi zao kwa kukosa nauli ya kwenda Babati Serikali inasemaje?

Naomba Serikali iangalie hilo na kuweza kujenga Mahakama yenyé hadhi ya Wilaya katika Mji wa Mererani.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii, kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Mathias Chikawe, Waziri wa Katiba na Sheria; Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Johnson Paulo Mwanyika; Mheshimiwa Jaji Mkuu, Agustino Ramadhani; na Watendaji wote wa Taasisi, zinazohusu Wizara hii, kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya hasa kwa kusimamia sheria na haki na hivyo kufanya nchi yetu kuwa nchi inayoendeshwa kwa kutii Sheria na Katiba ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni nyeti sana, kwani ndiyo Wizara pekee inayotengeneza mienendo na utaratibu wa uendeshaji wa nchi kisheria. Aidha, Wizara kupitia Taasisi ya Mahakama, ndiyo inayosikiliza na kusimamia haki, hivyo umakini katika uendeshaji wa Wizara hii ni kitu muhimu sana. Aidha, uadilifu ni kipengele kimojawapo katika majukumu yake ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, Katiba ya Nchi hii ndiyo Sheria Mama katika uendeshaji wa shughuli za nchi, kwa masuala ya kila siku. Ni wajibu wa Wizara hii, kuona namna inayofaa kufanya marekebisho ya mara kwa mara katika vipengele ambavyo vimepitwa na wakati na pengine vile vinavyonung'unikiwa zaidi na wananchi ama vile vinavyokwamisha utekelezaji wa mambo muhimu ya kimaendeleo. Kitengo cha Law Reform (Kurekebisha Sheria), kisijikite zaidi katika kuona ama kurekebisha sheria ambazo zimepitwa na wakati na kutoa maoni ya kurekebisha kabla ya kuzileta Bungeni na kupitishwa kwa sheria. Kituo kifanye utafiti wa masuala yote ya Katiba ili kitoe maoni yake na hivyo maboresho yaendane na wakati.

Juhudi za makusudi zichukuliwe na Wizara, kuhakikisha wananchi wanaielewa Katiba yao ya nchi. Hatua za elimu ni vyema zikaanzia kwenye ngazi ya shule za msingi na kadhalika. Wizara ihakikishe nakala za kutosha za Katiba zinapatikana mikoa yote ili wananchi waweze kuipata kwa urahisi, tofauti na hali ya sasa, Katiba kusatikana mahali pamoa (Duka la Vitabu vya Serikali). Pawepo na Mawakala wa kuuza nyaraka za Serikali kwa kila Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Wizara kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, kwa namna ilivyojishugulisha kukusanya taarifa mbalimbali za ukiukwaji wa haki za binadamu na Utawala Bora. Aidha, nashukuru pia namna ya uendeshaji wa shughuli zake, hasa pale wanapofanya mihadhara juu ya kukuza, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu na Utawala Bora katika jamii. Mihiadhara hii imesisitiza eneo hilo kupewa kipaumbele katika kukuza, kuzingatia, kutekelezwa na kuhifadhiwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Tume hii, nashauri ukusanyaji wa taarifa kupitia mikutano ya hadhara, isiwe ndiyo njia pekee bali Tume inapotembelea katika Wilaya fulani itoe nafasi ya Wajumbe wa Tume kuonana na wananchi mmoja na kumsikiliza akiwa peke yake.

Mheshimiwa Spika, yapo mambo mengi yanayobainika kwa Tume, ambayo yanakiuka haki za bianadamu na Utawala Bora, kadhalika Tume hutoa maoni yake na hatua za kuchukuliwa. Je, ni kwa nini maoni mengi ya Tume hayatekelezwi? Pengine kupitia mhimili wa Utawala, huiponda Tume waziwazi.

Mheshimiwa Spika, vitendo hivi ni vya kudharau Tume na kufifiisha utendaji wa kazi nzuri inayofanywa na Tume.

Mheshimiwa Spika, 2008/09 wakati Waziri akiwasilisha, alilieza Bunge lako Tukufu juu ya namna Wizara ilivyojipanga, kwa kushirikiana na kada nyingine, kutoa mafunzo kwa wataalamu wanaoshughulikia utaratibu wa mikataba mbalimbali nchini. Naamimi dhamira ya Mheshimiwa Waziri na Serikali ilikuwa nzuri kabisa, katika kuhakikisha suala la umakini linapewa kipaumbele na kuhakikisha Taifa haliingii katika hasara ya mikataba mibovu, ikiwemo ulaghai ambao unaambatana na rushwa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri, atueleze ni kwa jinsi gani mafanikio yamefikiwa kutokana na mikakati aliyojipangia. Kutoa ufanuzi huu, kutasaidia kuondoa hofu ambayo ipo hadi sasa mionganini mwa wananchi, hususan suala zima lihusulo mikataba.

Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kutangaza utaratibu wa kupata mafunzo ya sheria kwa vitendo, hasa pale wahitimu wa Shahada ya Sheria wanapohitimu kabla ya kupata kazi ni lazima kupitia mafunzo hayo (*Law School*); utaratibu wa Serikali ulikuwa mzuri lakini iweje wanafunzi hawa wanaendelea kusumbuliwa ama kusimamishwa kutokana na kukosa mikopo? Naomba Serikali kupita Waziri, tatizo hili likomeshwe.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kutupatia Hakimu wa Wilaya ya Iramba, lakini naomba Serikali ituongezee wa pili li kuharakisha usikilizaji wa kesi nyingi. Vile vile kwa kupeana zamu, Hakimu anaweza kutembelea maeneo yaliyo mbali na Wilaya na kusikiliza kesi nyingine huko huko kama wafanyakyo Majaji kwenda Mahakama za Mkoa na kadhalika. Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, wapatiwe vitendea kazi hasa usafiri. Wizara ikamilishe ahadi yake ya kujenga Mahakama ya Wilaya ya Iramba.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KHADIJA SALUM AL-QASSMY:** Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia kuwa mzima wa afya njema na kuweza kuchangia hoja iliyoko mbele yetu ya Katiba, Sheria na Utawala.

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe binafsi, pamoja na Naibu Spika na Wenyeviti wako wote, kwa jinsi mnavyoliendesha Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kumpongeza Waziri na Watendaji wake wote, kwa jinsi walivyoandaa Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, naanza kuchangia bajeti hii kwa kuiomba serikali ijenge majengo ambayo yana hadhi ya Mahakama, pamoja na kuweka samani ambazo ni nzuri na kuondosha ile aibu tulioiona karibuni katika vyombo vya habari, ambavyo ni aibu kwa taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa hali ya samani zilivyo kwenye Mahakama zetu, basi si rahisi kwa binadamu kuweza kufanya kazi kwa uadilifu mzuri. Tunawapongeza Majaji na Mahakimu, kuweza kwa kiasi fulani kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, ili kuzidi kupunguza rushwa katika Mahakama zetu, serikali izidi kuwaboreshea maslahi yao wafanyakazi hao.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana kuona serikali mpaka leo bado jambo hili inalipiga danadana, kwani karibu tutamaliza miaka mitano, lakini inaonekana jambo hili la Mahakama ya Kadhi limewekwa kwenye Ilani ya CCM kijanjanja. Kwa maoni yangu, naona serikali haikuwa *serious* katika suala hili.

Mheshimiwa Spika, suala hili lipo upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, yaani Zanzibar, lakini la kusikitisha, serikali imekwenda kuchukua mfano kutoka Afrika Kusini; kulikoni au Zanzibar hakuna haki ya kuwa kigezo cha Tanzania Bara?

Mheshimiwa Spika, imefika wakati sasa kwa Katiba yetu kufanyiwa marekebisho, kwani mpaka sasa bado ni ya Chama kimoja. Kwa ushahidi wa hilo, mpaka leo Katiba haioneshi mfumo wa vyama vingi na kuna malalamiko mengi ya watu kuhusu Katiba. Serikali ina wasiwasi wa nini kubadilisha Katiba? Wakati sasa umefika wa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, naipongeza serikali kwa kuchukua jitihada za kufanya kura za maoni na kutambulika watu ambao wanawaua albinos na vikongwe. Sasa tunaomba serikali ichukue hatua za haraka ili kukomesha hali hii.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**MHE. DKT. MAUA ABEID DAFTARI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Naomba kuchangia ifuatavyo:-

- (i) Ucheleweshaji wa kesi mbalimbali umekithiri na watuhumiwa wananyimwa haki yao kwa wakati. Hakimu anasikiliza kezi na kukaa miaka miwili bila kutoa *judgment*. Je, kweli atakumbuka kila kitu? Hasa wale ambao afya zao sio nzuri; *how can we judge them?*

Wapo wenye uwezo ambao kesi zao huchukua wiki moja au mbili na *judgment* zinatoka. *Why double standard?*

- (ii) Mahakimu wengi wenye afya mbaya wanahamishiwa Dar es Salaam; je, hii ni kufanya shughuli za Mahakama kuzorota? Kazi nyingi za Majaji zinawafanya Majaji wachoke kimwili na kiakili; hivyo uwepo utaratibu maalumu wa kupima afya za majaji wetu kila mwaka. Bado tunahitaji taaluma na busara zao.
- (iii) Makarani wa Mahakama (baadhi), hukosa uaminifu na kuvujisha siri za Mahakama. Wapo wanaopewa taarifa za kila linaloendelea katika kesi zao na hata kujua *judgement* mapema kuliko wenzao kwenye mashtaka. Hii sio *healthy*. Vyema sasa makarani wa Mahakama wawe *vetted* na wachunguzwe kwa kina kabla ya ajira zao.
- (iv) Matapeli wengi wana mbinu za kujua vyema Mahakama na watu wake, hivyo wanaposhtakiwa wanajua mbinu za kupita za kulaghai na kushinda. Watu kama hawa ni mahasidi wa wenzao.
- (v) Bado hali ya maslahi ya Mahakimu/Majaji wetu sio nzuri, tuwalipe vizuri na kuwapa marupurupu ili wasiingie katika mitego ya wenye fedha. Sehemu nyingi wanazofanya kazi haziko katika hali ya kuridhisha; ni vyema ziangaliwe kwa majengo, *furniture* na vitendea kazi.

Nimefurahi kusikia kuwa utaratibu huu wa *ku-record* (Hansard) unaotumika Bungeni sasa utafika katika Mahakama zetu. Hiki ni kitu kizuri kwani ubongo hauna uwezo wa *ku-record* yote unayoyasikia na mara nyingine hata *uki-record* mengine yatakupita. Hongera sana kwa hilo

Mahakimu kukaa eneo moja la kazi kwa miaka mingi sio vizuri, kwani inajenga mazoea.

Waendesha mashtaka waelimishwe umuhimu wa uadilifu wako katika utoaji haki kwa washtakiwa na washtaki.

Majaji wasitoe nafasi ya washtaki/washtakiwa kuwatemebelea majumbani kwao. Kuwepo na *system* kama ile ambayo sasa *TRA* wameianzisha ya maofisa kutokuonana na wafanyabiashara katika masuala ya kodi, bali *system* ya *information* (ya kupata taarifa) iko wazi kwa ufuatiliaji.

Kuwepo na mfumo wa kupata *feedback* ya namna Mahakama inavyofanya kazi na wenye matatizo, wala rushwa, waiba nyaraka na wenye kupotosha Mahakama zetu.

Watu watoe taarifa na taarifa hizo zifanyiwe kazi na marekebisho yafanyike pale dosari inapogundulika.

Majaji wawe macho na matapeli wenyewe uwezo wa kujieleza, kulia na kujigaragaza, huku nyuma wakiendelea kula haki za wenzaao. Kujionesha ni watu safi kumbe ni mbwa mwitu aliyeava ngozi ya kondoo. Hivyo basi, lazima matapeli hao wanaposhtaki basi Majaji wafanye *analysis* ya kutaka kupata taarifa toka Mahakama nyingine juu ya kesi mbalimbali zinazowagusa washtaki hao (matapeli). Iweje mtu awe safi huku ana kesi za jinai na mada kwenye Mahakama tatu au nne?

Hongera sana Waziri, Majaji na Watendaji wote, kazi yenu ni ngumu. Mwenye uadilifu atashinda.

**MHE. DIANA MKUMBO CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii, kwa njia ya maandishi, kumpongeza Waziri wa Sheria na Katiba, Mheshimiwa Chikawe, kwa hotuba yake nzuri sana na ambayo ameiwasilisha kwa umahiri wa kiwango cha juu. Ninatambua uchapakazi wake pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara hii; ni imani yangu kuwa, hata Watendaji wote wa Wizara hii hufuata nyayo za Waziri wao.

Mheshimiwa Spika, kwa mtazamo wangu, sina budi kuunga mkono bajeti hii mia kwa mia na niwaombee Mwenyezi Mungu, awape afya, nguvu na maisha mrefu ili waweze kutekeleza azma yao barabara.

Mheshimiwa Spika, napenda kuikumbusha serikali, maombi yangu kwa niaba ya Wananchi wa Mkoa wa Singida, kujenga Mahakama Kuu Singida. Pia napenda kuikumbusha serikali, ahadi yake ya kutoa kipaumbele kujenga Mahakama Kuu, kauli aliyoitoa Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, alipokuwa Waziri wa Wizara hii. Kwa kuwa Uongozi wa Mkoa wa Singida chini ya Mkuu wa Mkoa, Mheshimiwa Parseko Kone, akisaidiwa na Mheshimiwa Masamu, Hakimu wa Mahakama ya Mkoa wa Singida, ambao tayari walishaandaa kiwanja pamoja na mikakati mbalimbali ya ujenzi huu. Ninapenda kujua mikakati ya serikali, juu ya ujenzi wa Mahakama Kuu kuititia bajeti hii zimetengwa shilingi ngapi kwa kuanzia? Nategemea majibu ya Waziri, najua hawezikutuangusha Wanasingida.

Mheshimiwa Spika, ninayo faraja ya pekee sana, kwani serikali tayari imetupagari kwa ajili ya Mahakama ya Wilaya. Nina imani gari hili litafanya kazi nzuri ya kutembelea Mahakama za Mwanzo ili kuona ufanisi na kero zilizoko huko.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizi, vilevile nina kilio cha gari la Mahakama ya Mkoa aina ya Honda, ambalo limekufa na vifaa vya kutengenezea hapa nchini hakuna. Nina ushahidi wa kutosha kuwa, nusu ya magari haya yaliyoko mikoani yamekufa na hayatengenezeki, kwani hakuna *spare* nchini.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri serikali, pale inapotoa tenda ya kuagiza magari ni vyema kuagiza magari ambayo yana *spare* hapa nchini, kuliko ilivyoagiza magari aina ya Honda ambayo hayana *spare*. Hivyo basi, ninamwomba Waziri mwenye dhamana, atoe ufumbuzi wa gari hili la Singida ili Mahakama ya Mkoa iweze kuwa na gari. Wakati wa majumuisho nipate majibu.

Mheshimiwa Spika, ninayo masikitiko makubwa kuwa, Wilaya ya Iramba toka uhuru haijawahi kufikiriwa kujenga Mahakama ya Wilaya. Jengo linalotumika kama Mahakama ya Wilaya ni la Mahakama ya Mwanzo ya Kiomboi Bomanı.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri serikali, iache tabia ya kupora majengo ya Mahakama za Mwanzo na kuyafanya kuwa Mahakama za Wilaya. Serikali itambue kuwa, wananchi wengi kezi zao huwa ni za kusikilizwa Mahakama za Mwanzo. Ninaomba Mheshimiwa Waziri anipe maelezo ujenzi huu utanza lini.

Mheshimiwa Spika, napenda kukiri kuwa, natambua wazi kuwa, Mahakama iliyopo sasa ya Wilaya ya Manyoni ndiyo Mahakama ya Wilaya, bali ni ndogo sana ambayo inafanana sana na Mahakama za Mwanzo. Ninaiomba serikali iangalie uwezekano wa kutoa fedha za upanuzi wa jengo la Mahakama hii ili ilete hadhi ya Wilaya.

Mheshimwa Spika, ninaamini hata Hakimu wa Mahakama hiyo, hujisikia mnyonge anapofanyia kazi kwenye jengo lenye mazingira magumu ukizingatia hadhi, elimu na usalama wa Hakimu huyo. Endapo Bajeti ya Serikali haijaweka, basi bajeti ijayo ikumbuke kutenga fedha za kupanua jengo hili la Mahakama ya Wilaya lenye hadhi ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza serikali kwani inajitahidi kusomesha Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, ingawa hadi sasa upungufu huo bado ni mkubwa sana kwa Mkoa wa Singida, kwani mpaka sasa HakimU mmoja bado anaendesha Mahakama tatu hadi tano.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika kuwa, upungufu huu wa Mahakimu hauleti tija katika kupunguza uwingi wa kesi katika Mahakama zetu za Mwanzo. Ingawa kaulimbili ya serikali ni Kilimo Kwanza, napenda serikali ielete kuwa, mambo mengi yanategemeana sana. Kwa mfano, mwananchi anapokuwa na kesi, mawazo yake huvurugika hata ari ya kazi hupungua kama sio kwisha.

Mheshimiwa Spika, naishauri serikali iendelee kuibua vyanzo mbalimbali vya mapato, pamoja na kuboresha vyanzo vilivyopo ili Wizara hii nayo iongezewe fedha bajeti ijayo. Ufanisi wa Wizara hii, utakuwa mgumu hata kama watakuwa na jitihada na tija katika uwajibikaji. Nitaishukuru serikali ikitoa maelezo ya tatizo la Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuikumbusha serikali kuwa, Wazee wa Mahakama ni kiungo kikubwa sana cha Hakimu katika kutenda haki kwa watuhumiwa

wanaofikishwa Mahakamani. Vile vile ninatambua posho wanaoyopata kwa kesi moja ni Sh. 1,500. Posho hii inaweza ikawa na manufaa kwa Mzee wa Mahakama, endapo kesi hiyo itachukua muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa upungufu wa Mahakimu ni mkubwa na kusababisha kesi moja kuchukua muda mrefu hadi miezi mitano, utaratibu unaofanya posho hii isiwe na thamani; ninaionba serikali ione utaratibu mzuri ili posho hii ipate thamani kama sio kuongeza kiwango cha posho kwa kesi moja.

Mheshimiwa Spika, napenda kuikumbusha serikali kuwa, bado tuna kero ya vitendea kazi katika Mahakama zetu zote, kuanzia Mahakama za Mwanzo hadi Mahakama Kuu. Suala hili ni kero sana kwa watendaji wetu, ambao walisoma kwa juhudhi kubwa wakitegemea watatumia taaluma zao vizuri, wakiwa na mazingira mazuri ya kazi bali hata karatasi ni tatizo. Ninaionba serikali iondoe kero ndogo ndogo. Hii italeta tija ya kazi hata hati za hukumu zitatolewa mapema.

Mheshimiwa Spika, ninatambua umuhimu wa Tume ya Haki za Binadamu, ingawa inasahaaulika sana kutengewa fedha za kutosha ili iweze kwenda mikoani kuwafikia wananchi kutoa elimu na Watanzania wajue haki zao.

Mheshimiwa Spika, mwisho, baada ya mchango wangu ambao ninasubiri majibu ya Mheshimiwa Waziri, napenda kutamka kuwa, ninaunga mkono mia kwa mia. Nawatakia utekelezaji wenye tija.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, natoa shukrani kwa Waziri na Wataalam wake wote, kwa kuandaa Hotuba na kuileta hapa Bungeni tuweze kuijadili. Pongezi kwa Hotuba nzuri sana ya Kambi ya Upinzani, yenye maoni na mapendekezo mengi ya kuwezesha Wizara hii muhimu kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ni Taasisi muhimu sana, inayosaidia wananchi kufuatilia haki zao. Wananchi wengi wamejenga imani na Tume hii, hasa kwa kuona jinsi inavyotenda kazi zake kwa haki. Hii ni sehemu au kimbilio la mwisho kwa mwananchi ambaye ameonewa, amedhulumiwa na kuteseka bila kutendewa haki.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, inatakiwa kujengewa uwezo wa kiutendaji, kuongezewa watumishi, wataalam, vitendea kazi na mafungu ya pesa.

Tume inachukua muda mrefu sana kufuatilia malalamiko huko vijijini, kwa sababu ya kukosa fedha za kutosha. Pia wanashindwa kukaa vijijini muda mrefu ili waweze kuchunguza kwa makini madai ya walalamikaji, kwa sababu ya kukosa fedha. Inasikitisha, malalamiko ya wananchi yanaweza kuchukua miezi 6 hadi 12 hayajafuatiliwa. Serikali lazima itambue majukumu makubwa ya Taasisi hii muhimu sana na hivyo, kutengewa fedha za kutosha ili wafanye kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, serikali ihakikishe inaainisha Kamati za Haki za Binadamu kuanzia ngazi za vijiji hadi wilayani ili kusaidia wananchi kupata haki zao kwa karibu na kwa muda mfupi. Kamati hizi zitakuwa zina mahusiano ya moja kwa moja na Tume ya Haki za Binadamu. Matatizo mengine yanaweza kuishia kwenye kamati hii, yale malalamiko makubwa yawasilishwe kwenye Tume kwa hatua zaidi.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii muhimu kwa kumpatia Mtanzania haki ya Kikatiba, ni muhimu sana iwezeshwe kwa fedha za kutosha ili kujenga uwezo wa watumishi (wanasheria), kujenga miundombinu yenyenye hadhi na kuwepo na vitenda kazi nya kutosha.

Mheshimiwa Spika, Mahakama zetu hapa nchini, kwanza, zipo chache sana kazikidhi mahitaji, pia hazina vitenda kazi nya kutosha. Ni jambo la kawaida, Mahakama kukosa hata karatasi za kuandika *charges* za watuhumiwa; hii ni aibu kubwa.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya Mahakama kushindwa kufanya kazi kwa ufanisi ni kusababisha msongamano wa mahabusu kwenye magereza yetu machache. Tumeshuhudia mara nyingi, mahabusi wanagoma na wengine wanapoteza maisha, kwa sababu ya kutopewa nafasi ya kusikilizwa mapema.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu sasa Mahakama ipatiwe Bajeti yake peke yake kama mihimili mingine ili iweze kujipangia mipango yao na kazi zao, bila kuomba kwa serikali. Hili litasaidia kuboresha Mahakama ambazo ziko kwenye hali mbaya, kupata watumishi wa kutosha na kwa ujumla kuleta ufanisi kwenye Taasisi hizi muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, tatizo la Viongozi wa Kata, Vijiji, VEO na WEO, kunyanya wananchi na hasa wale wa Kambi ya Upinzani, kuwabambika kesi mbalimbali ilimradi kuwadhoofisha, bado inaendelea maeneo mengi hapa nchini. Viongozi hawa wanalindwa na Madiwani, DEDs, Wakurugenzi wa Wilaya na Wakuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Urambo, Jimbo la Urambo Magharibi, matatizo haya nimeyasemea sana bado yanaendelea. Mwananchi akihoji lolote la msingi kwenye mkutano wa hadhara, hasa mapato na matumizi, wataanza kumwandama kwa kila njia ilimradi kumfunga mdomo.

Mheshimiwa Spika, Kata ya Usinge, Kijiji cha Usinge, Kitongoji cha Luhanjo Mtoni, yupo mwananchi ambaye alihoji kwenye mkutano; sababu za serikali kutowapeleka wananchi wa pale kituo cha kupigia kura za maoni kufichua wauaji wa maalbino na vikongwe? Viongozi wa Wilaya walikwenda pale wakawaahidi, lakini siku hiyo ya kura za maoni kituo hakikuwepo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuhoji hilo, Viongozi wa Kijiji hicho, wakiwepo VEO na WEO, wameana kumwandama na hivsi sasa wamemtafutia kesi mwananchi huyo kwamba, amehusika na kumuua mbwa na kumtupa kwenye kisima cha maji ya kunywa. Mwezi Mei na Juni, wamekuwa wanamfuata wanamwambia ahame kwenye

kijiji hicho haraka, vinginevyo kesi hiyo watamfunga. Serikali ifuatlie masuala haya, vinginevyo tutapelekea amani ya nchi kuvunjika.

**MHE. CHARLES N. MWERA**, Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Waziri wa Katiba na Sheria, kwa hotuba nzuri. Nawapongeza wote walio katika Wizara hiyo.

Nianze kwa upungufu mkubwa wa Mahakimu, Majaji na Mawakili. Serikali iongeze watendaji kwa chombo muhimu cha sheria ili wananchi waweze kupata haki zao mapema. Kuna kesi nyingi sana, hasa Mahakama ya Tarime, ambapo wananchi wengi wamebambikiwa kesi za mauaji. Zipo kesi nyingi zinahitaji Majaji wa Mahakama Kuu wapange ili kusilikiza kesi hizo na kumaliza kero kwa watuhumiwa, maana nao ni binadamu na wana haki ya kusikilizwa mapema.

Naomba serikali iunde Tume kuangalia hali ya Gereza la Tarime, maana watuhumiwa wengi wa mauaji (*Marder Case*), wapo katika Gereza hilo. Kwa wakati mmoja, watu kumi wametuhumiwa kumuua mtu mmoja. Wananchi wanaonewa sana na maaskari wasiokuwa waaminifu, wanatumia vibaya madaraka waliyopewa na serikali. Kwa hiyo, naishauri serikali iunde Tume ya kuchunguza hali isiyokuwa ya kawaida, ambayo inanyima haki na ukiukwaji wa haki za binadamu.

Hali ya Mahakama zetu si nzuri, zipo kwenye hali duni, serikali iwe inafanya ukarabati wa mara kwa mara, sambamba na kukarabati Mahakama. Mahakama zipewe vitendea kazi mafaili, ream, si vizuri mlalamikaji au mshtakiwa kununua makaratasi au mafaili. Mahakimu wapewe usafiri kama vile magari au pikipiki ili waweze kuleta ufanisi. Vilevile wapewe mafunzo ya mara kwa mara ili kuboresha utendaji wa kazi kwa Mahakimu.

Kuna tatizo kubwa la rushwa kwa Idara hii ya Mahakama. Mahakimu na Makarani katika Mahakama zetu, wanatuhumiwa kwa kupokea rushwa. Mahakama ni chombo muhimu cha kuzuia rushwa na kutoa haki kwa wananchi, lakini kinapogeuka na kushindwa kusimamia haki, Mahakama wakati wote imekuwa inalalamikiwa sana na wananchi kwa kupokea rushwa na kuchelewa kutoa hukumu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Spika, nami napenda kuchangia katika hoja iliyopo mbele yetu. Kwanza kabisa, napenda kuiomba Wizara iitangaze Sheria ya Uchaguzi mara kwa mara ili wananchi waweze kuifahamu. Sasa hivi tunaelekea Chaguzi za Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji na hapa ndipo hasa sheria zinapopinda.

Wizara kama mama wa sheria, itoe mafunzo ya kutosha na isifumbie macho wale wote wanaovunja sheria. Wavunjaji wakubwa ni Watendaji wa Kata wakati wa Uchaguzi wa Mitaa, Vitongoji na Vijiji. Mfano katika Kata ya Bugogwa, Wilaya ya Ilemela, eneo la Kabangaja; mtaa ulimteua Mwenyekiti kutoka Chama cha CUF na

alitangazwa, anaitwa Mnyemo. Cha ajabu, baada ya siku saba alifika Mtendaji wa Kata na kutengua uchaguzi na kumtoa Mwenyekiti huyo na kuitisha uchaguzi tena baada ya siku zisizozidi saba. Je, ni nani anayepaswa kutengua matokea hayo kisheria?

Je, watendaji hao mnaaminije kama sheria wanaitambua au la? Tunaiomba Wizara, uvunjaji huu wa sheria ndio chanzo cha vurugu. Nina imani hata baadhi ya Wakurugenzi wa Halmashauri, hawajui sheria hizo. Hasa Mkurugenzi aliyeruhusu utengulwaji wa Mwenyekiti Mnyemu.

Pili, Sheria za Tathmini zimeandikwa kwa Luga ya Kiingereza, hasa pale ambapo uthamini huo unafanyika vijijini ambako hata elimu yao ni ndogo na kutilishwa saini katika lugha ambayo hawaijui; tunaomba Kiswahili kiwe ndiyo dira na si lugha nyingine ili kuokoa malalamiko hapo baadee. Pia kuna hasara gani kama sheria zetu zitaandikwa kwa Kiswahili? Tunasema Kiswahili ni Luga ya Taifa; je, ni Taifa la akina nani? Nadhani tubadilike sasa, tuachane na lugha ya wafahamu wachache. Tujali lugha yetu na tupunguze malalamiko yaliyo mengi.

Tatu, hivi kweli serikali kupitia Wizara ya Sheria hamwoni kuwa matunzo ya mtoto wa nje ya ndoa ya Sh.100 inawanyanyasa sana watoto na akina baba kupeta tu? Hiki ndicho chanzo kikuu cha ongezeko la watoto wa mitaani. Tunaomba serikali kupitia Wizara ya Sheria, ilitilie mkazo na kutunga sheria kali. Tangu tuliongee, sasa yapata mwaka wa tatu, lakini mabadiliko hayapo. Si watoto wa nje ya ndoa tu hata wa ndani ya ndoa; akina baba walio wengi wanakimbia majukumu yao na kumtelekezea mama watoto. Pale mama anapokuwa mtazamo wake ni mdogo au hana wazo la kujishughulisha, ndiyo watoto wanaingia mitaani. Tunaomba sheria kali iletwe hapa Bungeni kuhusu suala la watoto. Ukizingaitia sasa kuna kipimo cha DNA, hivyo haina ubishi tena.

Tusaidie watoto kwa sheria kali ili kuepuka ongezeko la watoto wa mitaani. Ahsante.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Watendaji wake, kwa hotuba yao nzuri na niwape pole namna wanavyofanya kazi katika mazingira ya ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, Mahakama zetu nyingi ni mbovu, hazikidhi haja, majengo hayafai, baadhi yanavuja sana, samani ni mbovu na hata uhifadhi wa nyaraka unakuwa dhaifu kutohana na hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ucheleweshaji wa kesi ambao unachangiwa kwa kiasi kikubwa na upungufu wa Mahakimu katika Mahakama zetu za Wilaya na Mahakama za Mwanzo. Tunaomba sana serikali ifanye kila juhudhi, kuhakikisha Mahakimu wanaongezeka katika Mahakama zetu. Kesi zinapcheleweshwa ndiyo kunapokuwa na mrundikano wa mahabusu.

Mheshimiwa Spika, kurundikana kwa mahabusu zaidi kunasababishwa na kuweka mahabusu, hata wale ambao wana kesi ndogo ndogo kama vile wanaoiba kuku, nazi na kadhalika. Watu ambao wangeweza kupewa dhamana na inapofikia hukumu zao, basi hata vifungo vya nje vitumike zaidi kwa wahalifu kama hao.

Mheshimiwa Spika, kuwaweka mahabusu wengi katika chumba kimoja ni kuwavunjia haki za binadamu na hivyo nashauri kwamba, serikali pamoja na mambo mengine, basi pia ifikirie kutanua majengo ya magereza ili waweze kuishi kama wanadamu wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, ukienda magerezani kunatisha, ukiwaona binadamu jinsi wanavyodhalilika. Hivyo, tusiwape adhabu kabla ya kuhukumiwa.

Mheshimiwa Spika, zaidi naomba Bajeti ya Mahakama iongezwe, kwani fedha wanayotengewa ni ndogo sana ukilinganisha na majukumu na hiyo wanayoomba hawapewi.

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida, sheria zinaandikwa kiingereza na asilimia kubwa ya Watanzania wako vijijini, hawana elimu na kwa maana hiyo hawajui Kiingereza. Kwa nini serikali haichukui hatua ya kutafsiri sheria ziandikwe kwa Luga yetu ya Taifa ili Watanzania walio wengi waelewe na waweze kudai haki zao kwa uhakika na wasidhulumiwe ama kudanyangwa kwa kutokuelewa?

**MHE. MICHAEL LEKULE LAIZER:** Mheshimiwa Spika, napenda kutanguliza kuunga mkono hoja ya Waziri wa Sheria na Katiba. Katiba na Sheria ni muhimu sana, kwani ni chombo cha ulinzi wa haki za binadanu. Bila sheria, nchi yoyote ile haikaliki. Katiba ndiyo mwongozo wa sheria, kwa vile sheria inasimamiwa na Mahakama ni muhimu watoa sheria Mahakamani wawe wa kwanza kutoa haki bila upendeleo, chombo hiki kiwe cha kutoa huduma bila upendeleo.

Ni muhimu kuwe na usawa wa kutoa haki bila upendeleo wa matajiri na wasio na uwezo. Chombo hiki kilinde wananchi wa hali ya chini, ambao hawawezi kuweka Mawakili ambao wanawatetea wenye uwezo huku wale wasio na uwezo wanategemea Mahakama tu.

Pamoja na utoaji haki, inafaa huduma ya Mahakama iwepo karibu na wananchi ili wale ambao hawana uwezo wa kusafiri kufuata Mahakama mbali, nao waweze kupeleka kero zao Mahakamani.

Kwa hiyo basi, Wilaya ya Longido haina Mahakama ya Wilaya, wanatumia Mahakama ya Monduli ambayo iko mbali zaidi hata ya Mahakama Kuu ya Mkoo. Kutoka baadhi ya Kata za Wilaya ya Longido mpaka Mahakama ya Wilaya ya Monduli ni kilometra 300, jambo ambalo wananchi wanakaa bila kwenda kutafuta haki kwa ajili ya umbali. Tuna miji kama Namanga na Longido, ambayo kuna shughuli nyingi za kero na kesi ambazo zinahitaji Mahakama ya Wilaya.

Wilaya ya Longido haina hata Jengo la Mahakama ya Mwanzo. Jengo ambalo linatumika limejengwa zamani na Wakoloni wa Kijerumani Mwaka 1945. Jengo hilo litaanguka wakati wowote, kwani lina nyufa kila ukuta pamoja na udongo wake.

Inafaa serikali itoe kipaumbele kwa Watumishi wa Mahakama ili wasiwe na tamaa ya kudai rushwa, kwani shida ni kishawishi cha watumishi kutaka kitu kidogo. Mahakimu wanahitaji kuwa na nyumba nzuri, tena zenyе ulinzi, kwani ni watu ambao wanatoa adhabu kwa watu wa aina mbalimbali. Wawe na mishahara mizuri ili waweze kuwa na hali inayofanana na hadhi yake. Wananchi wengi wanategemea kupata haki, kwani wengi hawajui haki ya kisheria. Naomba Wizara hii isaidie kutoa elimu kwenye Mabaraza ya Kata ili waweze kumaliza kero nyingi vijijini.

Naomba Mheshimiwa Waziri, ukumbuke Wilaya ya Longido ni kubwa kwa eneo, mwanachi kutoka mpaka wa Rombo kwenda Mahakama ya Wilaya ya Monduli, anapita Mahakama tano za Wilaya nyingine na Mahakama mbili za Mikoa. Moshi na Arusha mpaka Monduli ni kilometra 240. Toka Gilay karibu na Lake Natron mpaka Monduli ni kilometra 260. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba, wananchi hawawezi kwenda kutoa ushahidi wanapotakiwa.

Tangu ukoloni watu wakiwa wachache mpaka leo watu wamekuwa wengi, bado wanatumia Mahakama ile ya Monduli. Wananchi wameamua kutumia vikao vyta mila ambazo hazifuati sheria na kusababisha baadhi ya wananchi kunyanyaswa.

Pamoja na matatizo hayo, ieleteke kwamba, Longido ni Wilaya ya pembezoni, inahitaji kuwe na usafiri. Hakimu hawezi kufanya kazi bila kuwa na usafiri kwa kuwa ni wilaya kubwa. Bado kunahitajika Mahakama ya Mwanzo kwenye Tarafa ya Enduimet West Kilimanjaro ili wananchi wapate huduma huko, kwani hata Longido yenye bado ni mbali.

Mheshimiwa Waziri, naomba wakati wa kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, nami nipate majibu kwani kuna kero nyingi. Kwenye Jimbo langu, haki haipatikani kwa urahisi mpaka ugharimie kwa gharama kubwa, kufuata chombo cha kutoa haki. Ahsante.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, hongera sana kwa Hotuba yako nzuri. Ninayo matatizo yafuatayo katika Wilaya ya Ngorongoro, yanayohusu Wizara yako ambayo kwa heshima kubwa, naomba uniangularie kwa jicho la huruma:-

Mazingira ya Wilaya ile ni magumu sana na kwamba, haivutii watumishi kukaa na kufanya kazi. Ndiyo maana TAMISEMI imetupa fedha ya ziada ya kujenga nyumba kumi za wafanyakazi, hususan walimu na wale wa Idara ya Afya. Naomba Ofisi ya Mahakama ya Wilaya na Nyumba ya Hakimu. Ofisi iliyopo ni ya mabati (*full suite*) na ilijengwa miaka ya 1970's. Hakuna choo, ubunifu haupo kwa sababu watumishi hawakai.

Ngorongoro ni Wilaya ya mpakani; jirani sana na Kenya Wilaya ya Narok. Wakati wa vikao vya ujirani mwema ni aibu tupu; wahalifu wa nchi jirani nao wanaletwa kuhojiwa katika Mahakama ya Wilaya. Hawaamini kuwa ile ni Mahakama ya Wilaya ambapo haki inatolewa!

Kama nilivyomwomba Mheshimiwa Waziri kwa maandishi tarehe 18 Juni, 2009, tafadhalii atutembelee ili ajionee haya. Ahsante.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii, kumpungeza Mheshimiwa Waziri, Ndugu Chikawe na Wasaidizi wake, akiwemo Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara hii, ambao kwa mwaka mzima wamefanya kazi nzuri ya kuiweka nchi yetu katika hali ya utulivu na amani, kwa misingi inayosimamia haki, uhuru na usawa. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, mimi nina maeneo machache, ambayo ninaiomba serikali ione namna ya kuiwezesha Wizara hii itekeleze majukumu yake vizuri. Yapo maeneo yanayohusu usafiri wa Mahakimu wa ngazi za Kata na baadhi ya Wilaya. Nyumba za Mahakimu na hata za Mahakama zenyewe bado ni duni sana. Hili ni tatizo kwa nchi nzima na siyo kwa jimbo langu tu.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, atusaidie kulieleza Bunge lako Tukufu kuhusu suala la adhabu ya kunyonga imefikia wapi; mbona mpaka sasa serikali haisemi lolote kuhusu maombi ya baadhi ya Wabunge kutaka Mheshimiwa Rais aidha awasamehe wale wote waliohukumiwa kunyongwa? Kwa msingi huo huo, ndiyo maana Wabunge wanahoji kwa nini sheria ya kunyongwa isifutwe?

Mheshimiwa Spika, hatua ya Mheshimiwa Waziri kutaka Kamati ya Wataalamu iifanyie kazi, suala la kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi Tanzania Bara si ya kuchukuliwa kirahisi; ni la kitaifa na la maslahi ya watu wote siyo kwa waislamu tu, bali kwa wote hata wasioamini dini yoyote. Hatua inayochukuliwa na serikali ndiyo sahihi, wala tusiyumbe kwa jazba zinazotolewa humu ndani ya jengo hili.

Mheshimiwa Spika, mimi nashauri ili tuweze kufanikiwa katika suala la rushwa, ni budi kwanza tukahakikisha maslahi ya Watumishi wa Mahakama yanapewa kipaumbele ili waishi maisha ya kutokuwa omba omba kwa vitu vidogo vidogo.

Mheshimiwa Spika, hivi sheria 43 ambazo zilipewa jukumu la kuzirekebisha zimefikia wapi mbona hakuna taarifa ambazo hata angalau kila mwaka Waziri akawa anatoa taarifa ya utekelezaji kama kuna maeneo ya sheria ambayo yanaonekana hayana utata wowote na kuoanishi na upande mwagine wa sheria zenye matatizo kuyatekeleza? Nashauri hili lipewe uzito, maana wananchi hawaelewi kwa nini hili linasuasua.

Mwisho, Mheshimiwa Waziri, atusaidie kuelezea kwa nini Wazee wa Baraza hawajaongezewa posho zao na malimbikizo ya madai yao yamefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa nguvu zangu zote.

**MHE. ANIA SAID CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kwa maandishi, Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria. Nawapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wa Wizara. Wizara hii imetekeleza na kuendelea kupanga mambo mbalimbali ya kurekebisha matatizo ya ujenzi wa Mahakama nchini.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Haki za Watoto na Walemaavu ipewe kipaumbele. Jamii hii hivi sasa angalau ndio inaanza kutambulika kwa kasi hapa nchini. Mfano, Sheria ya Kulea au Kutunza Watoto, kiwango cha Sh.100 kimepitwa na wakati.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi kubwa inayofanywa ya kupunguza kesi, mahabusu wengi wanadai kesi zao hazitajwi, mfano, Gereza la Keko, uchunguzi ukifanywa utakuta mtu anakaa miaka bila kwenda Mahakamani na akiulizia faili halionekani; naomba lifuatiliwe jambo hili.

Mheshimiwa Spika, pia kuna tatizo la kesi zikiisha, mtu akitakiwa kulipa fidia, hulipwa na mhusika, lakini fidia hiyo kufika kwa mhusika ni tatizo. Inachukua muda mrefu kupata haki hiyo, kwa sababu ya ukiritimba wa Watendaji wa Mahakama. Hili ni tatizo; ni vema lifanyiwe kazi ili wananchi wapate haki zao kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na maombi ya watu wazima na inakuwa ngumu kusajiliwa ili kupata vyeti vya kuzaliwa, RITA iboreshwe ili haki ipatikane kwa kila mwananchi.

Mheshimiwa Spika, Waziri ametoa maelezo jinsi mapendekezo ya Mahakama ya Kadhi yatakavyotolewa na Masheikh na Wanazuoni. Napenda kutoa angalizo, chombo hiki kina uhusiano mkubwa na Qurani Tukufu, taratibu za jambo hili la Sheria ya Ndoa na Mirathi, sio mawazo ya mtu ni agizo la maneno ya dini; katika kupokea mawazo hayo, jambo hili lizingatiwe ili lisije likaleta madhara katika jamii.

**MHE. OMAR YUSSUF MZEE (NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI):** Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake. Ilikuwa na mwangaza mkubwa, licha ya matatizo ya kibajeti aliyonayo, ambayo ni yetu sote na yanatokana na mapato madogo ya serikali, ukilinganisha na mahitaji yetu.

Hata hivyo, tatizo langu la msingi ndani ya Wizara hii ni kuchelewa kwa malipo ya mirathi. Wakati Hazina hutoa malipo hayo kwa wakati kupitia Mahakama zilizofunguliwa mirathi, lakini watu wako wanachelewesha malipo hayo na baadhi ya wakati hudiriki kusema hata faili halionekani. Tunaomba sana, tusaidiane kwa hilo ili tuweze kuondosha usumbufu huu kwa wananchi wetu. Ahsante.

**MHE. HEMED MOHAMMED HEMED:** Mheshimiwa Spika, ni vyema nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia siku ya leo kuliona jua la tarehe ya leo 30 Juni, 2009. Pia kuwapa mkono wa hongera wewe Spika, Naibu wako, pamoja na

Wenyeviti wote wa Bunge, kwa umakini wenu katika kutuongoza kwa imani Wabunge wako.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hotuba iliyio mbele yetu, utajua ipo hoja Wizara iwe tayari kufanikisha mahitaji muhimu ya kisheria kwa wananchi wote.

Mheshimiwa Spika, Chombo cha Mahakama ni eneo muhimu, kwani ni maeneo yanayotoa haki. Kuna upungufu mkubwa wa Mahakimu na Majaji, jambo ambalo hupelekeaa ucheleweshaji wa kesi zao. Ipo haja serikali izidumishe Mahakama zetu ili zikidhi haja ya kuwa Mahakama kuanzia majengo na vitendea kazi; hali zake ni mbaya sana. Hii ni dhahiri ni ufinyu wa bajeti yenyeewe. Ni vyema serikali iiongezee fedha Wizara ili iweze kujikwamua katika kazi zake.

Mheshimiwa Spika, upungufu mkubwa wa Mawakili katika nchi yetu hii, unasababisha watu kukosa haki zao za msingi. Kwa kuzingatia jiografia ya nchi yetu, utaona Mawakili wanabaki katika miji tu na kule vijijini kweupe. Hii ni haki ya msingi kwa kila raia. Mrundiko wa Mawakili mijini, unasababishwa na kukosekana huduma muhimu huko vijijini. Je, serikali imejipanga vipi kuweza kuwapatia watu wa vijijini Mawakili huku tukijua miundombinu ni michafu huko na hata vivutio hakuna?

Mheshimiwa Spika, ieleweke wajibu wa Mahakama ya Kadhi; ni eneo litakalotoa haki kwa Waislam kupita Qurani Tukufu ama Hadithi za Mtume Muhammad (SAW) na hakuna anayeweza kuongeza lake katika hili. Mirathi, ndoa, haki, misingi ya hukumu yake imewekwa katika Qurani. Kwa kujali Qurani ni maelezo ya Mwenyezi Mungu, sidhani kama eneo hili linahitaji kupatiwa maoni. Ni Muislam gani awezaye kutoa maoni yake akafuta neno la Mwenyezi Mungu? Hukumu za Kiislamu hazihitaji marekebisho, bali kama utatekeleza ni kheri kwako na kama hukutekeleza ni shari kwako. Kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi, ilibaini umuhimu wa kuwepo Mahakama ya Kadhi Tanzania Bara; ni wazi ni kutoa haki kwa Waislam.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi ya Muungano, ndani ya Muungano wetu, Zanzibar ina Mahakama ya Kadhi na zinafanya kazi zake kama kawaada. Napata wasiwaso kwa maneno yaliyomo katika kitabu hiki cha hotuba, ukurasa wa sita, eneo lisemalo: “Aidha, utaratibu huu unatumika huko Afrika ya Kusini, ambako kuna idadi kubwa ya Waumini wa Dini ya Kiisalam.”

Kwa nini tusiangularie utaratibu uliopo hapo Unguja; juu ya Waislam na sheria zao? Afrika Kusini tutarithi nini?

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika, ipo haja muhimu ya kuwepo Mahakama ya Kadhi nchini. Mimi nahisi kuna kigugumizi tu, ndio ikiwa kila leo ni lugha ya jiandiko inayotoa jibu kuwepo kwa Mahakama ya Kadhi nchini na siyo vitendo. Naiomba serikali ifanikishe azma yake, kama Ilani ya CCM ilivyotoa nia yake nzuri ya kuwepo kwa Mahakama ya Kadhi nchini. Naitakia kheri Wizara ili iweze kufanikisha mchakato wake.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia nchi yetu imo katika Mfumo wa Vyama vingi vya Siasa, napata wasiwasi mkubwa, mfumo huu haumo katika Katiba yetu. Je, serikali haionti umefika wakati Mfumo huu uwemo katika Katiba zetu? Ahsante.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, sheria ni msingi thabiti katika kutoa haki kwa wananchi kama itatumika vizuri, lakini italeta kutokuaminiana na kudhalilisha kama haitatumika vizuri. Hapa Tanzania, wananchi wengi wamekuwa wakilalamika jinsi ambavyo watuhumiwa wa makosa mbalimbali wamekuwa wakinyimwa haki zao. Lakini jinsi ambayo wananchi wamekuwa wakijichukulia sheria mikononi kwa kile kiitwacho dola kushindwa kuwachukulia sheria wahalifu.

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni kawaida kwa wahalifu kufikishwa katika vyombo vya sheria, lakini huachiwa.

Mheshimiwa Spika, suala la Mahakama ya Kadhi limeongelewa kwa muda mrefu na inavyoolekea ufumbuzi unakaribia kupatikana, kama Hotuba ya Waziri inavyosema. Ni wazi kuwa, nchi yetu haina dini ila wananchi wana dini mbalimbali zikiwemo za Kikristu, Kiislam, Kimila na Wapagani. Ni jambo la kushangaza, kuona dini moja inapatiwa Mahakama yao. Kama ni suala la *personal law*, basi kila mtu ana sheria binafsi; iweje Waislam ndio hii *personal law* izingatiwe na si kwa wote?

Mahakama ya Kadhi kuwa kwenye Ilani ya CCM, haina maana itekelezwe hata kama italeta madhara kwa nchi. Kuna ahadi nyingi tu ambazo hazitekelezeki; hivyo ya Kadhi kutotekelizwa haitakuwa na athari yoyote. Tujiulize ni sababu zipelekeza Mahakama hii ifutwe? Je, sababu zile sasa hivi hazina msingi tena? Vile vile tujiulize kwa kipindi hiki chote cha kutokuwa na Mahakama hii, Waislam wameathirika vipi na ikirejeshwa dini nyingine zitaathirika vipi?

Ni vyema serikali ipime na kuona *advantages* na *disadvantages* za Mahakama hii, lakini pia madhehebu mengine, wakiwemo wadau mbalimbali au kwa maana nyingine kuwe na *public hearing* kwa kuwa ni suala lenye maslahi ya kitaifa.

Mheshimiwa Spika, Mahakimu wetu wanaishi sehemu zisizo na staha, hasa tukizingatia shughuli nyeti wanazozifanya, ikiwa ni pamoja na kusikiliza kesi za mabilioni ya fedha, ufisadi na nyingine nyingi. Watu hawa wanastahili kupatiwa nyenzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupatiwa nyumba, ulinzi, gari na kadhalika. Hivi vitawasaidia sana kutokushawishika au kurubuniwa na wenye kesi hasa mafisadi, wauwaji na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Mahakama za Mwanzo bado ni chache na Mahakimu pia ni wachache sana, wakati watuhumiwa ni wengi sana; hivyo kufanya kesi kuwa nyingi na kutomalizika kwa wakati na gharama kuwa kubwa kwa kuwa mahabusu wanapaswa kugharimiwa chakula.

Mheshimiwa Spika, zipo sheria nyingi ambazo zimepitwa na wakati, mfano, Sheria ya Kutunza Mtoto. Bado fedha inayotolewa (Sh.100), ni ndogo mno na haina maana yoyote. Tunaomba Muswada uletwe ili kiasi hicho kitenguliwe na kiendane na hali halisi ya maisha ya leo.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Mafunzo ya Sheria kwa Vitendo (*Law School of Tanzania*), ilianzishwa 2008/09. Toka kusajiliwa kwake, wanafunzi wamekuwa na matatizo makubwa sana, ikiwemo kutokupata fedha kwa wakati na hivyo kuwaweka katika hali mbaya sana. Wakati Waziri Mkuu akijibu swali la Mheshimiwa Killimbah alisema, shilingi bilioni moja zilipelekwa ila baadhi ya fedha hizo zililipwa kwa wanafunzi waliokuwa hawastahili. Maelezo haya yanashangaza, kwani Uongozi wa *Law School* unajua wahitaji wa fedha hizo. Suala la kujuliza ni kweli katika ulimwengu huu wa Sayansi na Teknolojia hatuna *database* ya kujua vijana hao na mahitaji yao?

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kutekeleza mambo mbalimbali aliyowaahidi wananchi kupitia Wizara hii.

Pia nimpungeze Mheshimiwa Mathias Chikawe, kwa kuwasilisha bajeti yake vizuri na pia utendaji wake na jinsi anavyoshirikiana vizuri na Wabunge wenzake.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizi, napenda kufahamu yafuatayo:-

Je, hii Wizara inapiga vita sera ya jinsia ambayo imekuwa mstari wa mbele katika kupata haki na usawa na pia kuleta ustawi wa jamii?

Mheshimiwa Spika, nasema hayo kwa sababu Tume ya Kurekebisha Sheria ipo kwenu. Mara kwa mara wanawake nchini, wamekuwa wakiilalamikia Sheria ya Ndoa ya 1970 na Sheria ya Mirathi na Matunzo ya Watoto wa Nje ya Ndoa, ambayo inatoza Sh.100 tu kwa ajili ya matunzo ya mtoto. Je, ninyi mnaishi japo kwa shilingi 10,000 kwa mwezi?

Kama sheria nyingine zinaleta utata kwa nini msianze na zile ambazo hazina utata? Kwa nini ninyi bajeti yenu ipite wakati wengine wamekuwa watoto wa mitaani kwa kukosa matunzo? Haki za binadamu zipo katika Wizara hii, zote zimeshindwa kusaidia?

Mara ya mwisho niliuliza swali kwamba je, ni kweli dhamana za barua kutoka Serikali za Mtaa/Kata hazitambuliki Mahakamani? Lazima anayedhaminiwa awe na mdhamini ambaye ni mtumishi wa kudumu wa serikali? Kama ndivyo; je, wote wana ndugu watumishi serikalini?

Serikali iiongezee Wizara hii pesa za kutosha ili wapate nafasi ya kutosha (ofisi), kwa kujenga majengo yake pamoja na vitendea kazi vingine.

Kuhusu madhehebu ya dini kuelimisha waumini wao, mimi pia sioni tatizo labda kama katika mahubiri yao watasema kuwa mtu wa imani nyingine asichaguliwe. Kama kweli tunapiga vita ubaguzi au udini mbona sasa tunajichanganya tunapodai mambo mengine ya kiimani wakati mengine tunapinga? Mimi nadhani tuwe na subira. Wakristu watulie, Waislam watulie na watu wa imani zote tutulie, kwani Waraka huo haujaingia hata kwenye serikali bali ni starehe zao tu za kiimani, kiasi kwamba serikali inaweza kuingilia. Serikali acheni dini, shughulikieni ndoa za serikali tu na mambo yenu mengine. Hili suala la Mahakama kuvunja ndoa za Kikristu, Wakristu wanasisitika sana, lakini bado kuna ukweli mazingira mengine ni vigumu kudumu katika ndoa sasa sijui itakuwaje?

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na Wakuu wote wa Vitengo walioko chini ya Wizara hii, kwa kazi nzuri wanazofanya. Pamoja na uhaba wa Watendaji na vitendea kazi, endeleeni na moyo huo huo wa kulitumikia Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kutujengea Mahakama Iguguno, naomba fedha zikipatikana ijengwe na nyumba ya kuishi Hakimu.

Mheshimiwa Spika,, Iramba Mashariki tuna Mahakama za Mwanzo Iguguno, Kinyangiri, Iambi, Nduguti, Gumanga, Ibaga na Kirumi. Nasikitika kuandika kwamba, Mahakimu wote isipokuwa wawili wamestaafu.

Mheshimiwa Spika, nafahamu kabisa kwamba, tuna upungufu wa Mahakimu, naomba sana tuongezewe hata Mahakimu watatu na kati yao, mmoja apangiwe Nduguti, ambapo ni Makao Makuu ya Jimbo.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni nilitembelea Wilaya ya Sikonge, nilisikitika sana kwani Wilaya hiyo haina Hakimu wa Wilaya. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, Hakimu wa Wilaya apelekwe huko mapema sana.

Mheshimiwa Spika, Mahakama za Mwanzo zote zimechakaa sana, ukiacha ya Iguguno, ambayo ni mpya. Naomba sana kwa kuanzia, Mahakama za Nduguti, Ibaga na Kirumi, zikarabatiwe au zijengwe mpya.

Mheshimiwa Spika, naomba sana vitendea kazi vipelekwe kwenye Mahakama zote za Mwanzo na Mahakama ya Wilaya, kwani hali yao si nzuri na ni aibu kwa Watumishi wa Mahakama, kuomba vitendea kazi toka kwa wenye kesi au ofisi nyingine.

Mheshimiwa Spika, naomba sana sheria mpya zinazopitishwa na Bunge na sheria zote zinazofanyiwa marekebisho, ziwe zinapelekwa mapema kwenye Mahakama zote za Mwanzo.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ardhi, imebadilisha na kuelekeza kwamba, sheria zote zinazohusu migogoro ya ardhi, zisiendeshwe na Mahakama za kawaida bali

Mahakama zilizoteuliwa. Naomba sana Wizara ipeleke Waraka wa Kuagiza Mahakama za Mwanzo, ziache kuingilia migogoro ya ardhi, kule kwangu Mahakama ya Mwanzo Nduguti inawavuruga sana wananchi.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Naomba niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na asasi zilizo chini yake hasa Jaji Mkuu, kwa usimamizi mzuri wa Mahakama zetu.

Nidhamu Mahakamani kwa Mahakimu inaonekana na tuhuma za rushwa Idara za Mahakama zinaendelea kupungua. Naomba nidhamu na maadili ya kazi za wasimamizi wa haki ziendelee ili kulinda heshima ya Mahakama zetu.

Katika Bajeti ya Mwaka 2008/2009, niliiomba serikali usafiri kwa Hakimu wa Mahakama ya Nyambiti, ambapo nilisema kuwa Hakimu huyu mwanamke anahudumia zaidi ya Mahakama nne. Serikali (Waziri), aliniahidi kutoa usafiri wa pikipiki, hadi leo anasoma tena bajeti yake, hakuna dalili yoyote ya kupatiwa usafiri wa pikipiki kwa Hakimu huyu. Je, leo ananiambia nini kuhusu usafiri huo?

Serikali miaka ya nyuma ilisema itajenga na kukarabati Mahakama za Mwanzo ikiwemo na Mahakama ya Mwanzo ya Nyamikoma iliyoko wilaya ya Kwimba ningependa kujua mpango huo uliishia wapi?

Pamoja na ufinyu wa bajeti, vitendea kazi ni vitu vya msingi sana katika Mahakama hasa za Mwanzo. Sehemu ambapo kuna wananchi wengi ambaao hukosa huduma kwa ukosefu wa karatasi, Mahakimu, posho za Wazee wa Mahakama na kadhalika, tunaiomba serikali kupitia Mahakama Kuu, Idara ya Mahakama za Mwanzo, ifanye utaratibu wa kupeleka fungu kwa ajili ya vitendea kazi.

Naomba nimalizie kwa kuomba kupata majibu ni lini serikali itapeleka pikipiki kwa Hakimu wa Nyambiti? Mpango wa kujenga au kukarabati Mahakama ya Mwanzo ya Nyamikoma utafanyika lini?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Nitoe pongezi kwa Waziri, kwa kazi nzuri inayofanywa na Wizara yake. Pongezi kwa Katibu Mkuu, ambaye tunafahamu utendaji wake, tuwaombe Watendaji walio chini yake, wampe ushirikiano ili kazi iendelee kuwa nzuri.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Mahakama Lushoto ni Chuo kinachotoa kozi ambazo zitapunguza kero za upungufu wa Mahakimu hapa nchini. Pesa zinazotolewa kwa chuo hiki ni kidogo sana, serikali itoe kipaumbele kwa Chuo hiki pia Watendaji wake, Walimu na Watumishi kwa ujumla, wapewe au waboreshewe mishahara na posho zao.

Mheshimiwa Spika, Mahakama za Wilaya zipo nyingi, ambazo hali yake si nzuri. Wilaya ya Misungwi haina majengo yenye hadhi ya Wilaya. Tayari Hakimu wa Wilaya ameletwa, tunaipongeza serikali lakini hana gari la kutumia ili aweze kuzifikia Mahakama za Mwanzo. Naiomba sana serikali ilifikirie suala hili upesi na katika magari yatakayonunuliwa, Misungwi ipangiwe ili Mheshimiwa Hakimu wa Wilaya aweze kutenda kazi zake kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, Mahakama za Mwanzo, bado zina hali mbaya kwa majengo yake, lakini pia nyumba za watumishi. Serikali ieleze ni lini itakarabati au kujenga nyumba za watumishi kwa Mahakama za Mwanzo Wilayani Misungwi?

Mheshimiwa Spika, kiasi cha Sh. 35,000,000 kilitakiwa ili kukarabati Mahakama iliyopo Misungwi ili itumike kama ya Wilaya wakati taratibu nyingine zinaendelea; hizi ni za 2008/2009; je, pesa hizo zimetumwa ili kazi hiyo iendelee?

Mheshimiwa Spika, serikali kwa ujumla wake, hajatoa kipaumbele kwa Wizara hii. Hili ni figa la tatu, lakini pesa zinazotengwa si sahihi. Uangaliwe mkakati ili kazi zake ziboroke na haki ipatikane. Sisi Waheshimiwa Wabunge, hatufurahishwi na kiasi kinachotengwa, inakuwa vigumu kuzigawa kutokana na wingi wa matatizo wakati pesa kidogo.

Mheshimiwa Spika, wewe ni mwanasheria, unajua umuhimu wa Mahakama katika kutoa haki, tushirikiane kuona bajeti zijazo zinaongezwa ili Mahakama iwe na hadhi yake.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja ili kazi za 2009/10 zifanyike.

**MHE. MERYCE MUSSA EMMANUEL:** Mheshimiwa Spika, nami pia naomba nichukue nafasi hii, kumpongeza Waziri wa Katiba na Sheria, Katibu Mkuu wake, pamoja na Wizara nzima kwa ujumla, kwa Hotuba ya Bajeti, ambayo inaonesha dira na mwelekeo mzima wa Wizara hii muhimu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuchangia machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mahakama nyingi hapa nchini, hazina ubora unaotakiwa na nyingine hazifai hata kutumika kabisa; hazina hata vitendea kazi mfano karatasi na kadhalika. Hii inazorotesha kabisa utendaji mzima wa kazi. Naiomba Wizara hii ifikie mahali sasa ione umuhimu wa kuleta mabadiliko ya haraka ili watumishi hawa waweze kufanya kazi kwa ubora zaidi na wapatiwe vifaa vyaa kisasa zaidi.

Mheshimiwa Spika, Mahakama haina watumishi wa kutosha, unakuta Hakimu mmoja anahudumia Mahakama zaidi ya mbili. Hii inasababisha mrundikano wa kesi na kusababisha kesi nyingi kuchelewa kuhukumiwa na watuhumiwa wana haki ya msingi ya kusikilizwa kesi zao kwa muda unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie ucheleweshaji wa kesi hasa zile za mauaji. Ni kweli kwamba, kesi hizi zinahitaji muda ili kubaini ukweli na kuhakikisha haki inatendeka bila kuonea mtu yelete. Si kweli kwamba, kesi hizi lazima zizidi zaidi ya miaka mitano hadi tisa.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, watuhumiwa hawa wanakaa muda mrefu kupita kiasi kama vile wamesahaulika, na wengine hypoteza maisha. Kwa kuwa Serikali hii ya Awamu ya Nne ni ya kasi mpya, nguvu mpya na ari mpya; utendaji pia ufanane na kasi hiyo. Wizara iangalie upya eneo hili ili tuweze kuleta tija zaidi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. JOHN PAUL LWANJI:** Mheshimiwa Spika, natoa shukrani kwa kupeleka Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo za Ukimbu na Mwamagemebe.

Naomba Mahakama hizo za Ukimbu na Mwamagemebe, zifanyiwe ukarabati kwa sababu ziko katika hali mbaya sana. Hakimu wa Wilaya ya Manyoni aliomba Sh.40m kwa bajeti iliyopita kwa ajili ya ukarabati wa Mahakama ya Ukimba, lakini hazikupatikana. Tunaomba jumla ya Sh.80m kwa ajili ya ukarabati wa Mahakama hizo mbili @ Sh.40m x 2 = Sh.80m.

Mwakani Bajeti ya Wizara hii iongezwe, hususan kwa Chuo cha Sheria cha Lushoto ili *training* zaidi ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo zifanyike, sambamba na ujenzi wa Mahakama mpya za Mwanzo. Jimbo langu linahitaji Mahakama mpya zifuatazo:-

KATA	KITUO/MAKAO
(a) Rungwa	Rungwa
(b) Idodyandole	Idodyandole
(c) Sanjaranda	Gurungu
(d) Aghondi	Kamenyanga
(e) Ipande	Ipande
(f) Itigi	Kitaraka

Tunaomba ombi hili lifanyiwe kazi ili kuwapunguzia wananchi gharama kubwa za kusafiri kwenda mbali kufuata Mahakama Itigi, Ukimbu na Mwamagemebe. Kuna upungufu mkubwa wa Mahakama za Mwanzo. Bajeti hii walau Mahakama mbili za Rungwa na Idodyandole, zitengewe posho maalum ili zijengwe na mwakani nyingine zifuatie.

Kwa kuwa vita dhidi ya rushwa haiwezi kupiganwa kwa maneno ya wanasiwa pekee, mhimili wa Mahakama ni muhimu sana katika kupambana na tatizo sugu la rushwa. Napendekeza mishahara na maslahi mengine ya Mahakimu yaboreshwe ili kuwaondolea vishawishi vinavyowafanya wapindishe sheria na kuwanyima haki wale wanaostahili lakini ni maskini.

Napendekeza kuwa Hakimu au Mahakimu wasikae kituo kimoja muda mrefu (usiozidi miaka mitano). *Rotation System* itasaidia kupunguza tatizo la rushwa na mambo mengine ya utemi.

Makarani wa Mahakama ndiyo viota vya rushwa. Wamekuwa daraja kati ya Mahakimu na washtakiwa/washtaki. Makarani waliopo wastaafishwe na wapya wenye elimu waajiriwe, baada ya kufanyiwa *training* maalum na usaili maalum, na walipwe vizuri ili kuepuka vishawishi. *Trafficking* ya rushwa hufanywa na Makarani wa Mahakama, japokuwa mlengwa huwa ni Hakimu, inakuwa vigumu kumkamata Hakimu kwa sababu yeye siye anayepewa mzigo, anapelekewa na mtu mwingine ambaye ni karani wake.

Posho ya Wazee wa Baraza iboreshwe ili kuwaepushia vishawishi vya kitu kidogo.

**MHE. JANETH MAURICE MASSABURI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kuwapongeza wahusika wote waliohusika kuandaa Bajeti ya Wizara ya Sheria na Katiba, wakiongozwa na Waziri, Mheshimiwa Mathias Chikawe na Katibu Mkuu wake.

Kama ilivyo kwa Bunge letu ambapo lina bajeti yake, ingekuwa vyema na Idara hii ya Mahakama ipewe fungu lake ili iweze kukidhi mahitaji na hasa katika suala zima la kuharakisha kesi ili kupunguza mrundikano wa wafungwa katika magereza yetu. Itasaidia kuipunguzia serikali matumizi ya chakula kwa mahabusu. Katika hali ya unyeti wa idara hii, itawasaidia kununua magari, nyumba za Majaji na Mahakimu, kuboresha majengo yao na kadhalika.

Mahakimu wasitumie kifungo kwa watuhumiwa kwa kila kosa, wazingatie ukubwa wa kesi na kwa makosa madogo madogo, Mahakimu watoe hukumu ya kifungo cha nje kwa adhabu ya kupanda miti na kuihudumia miti hiyo kwa muda uliopangwa na Hakimu.

Mwisho, nawapongeza sana Watendaji wote katika mhimili huu muhimu na pia nawatakia kheri katika kazi zao za kila siku.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na kazi nzuri inayofanywa na Wizara yake na taasisi zake. Namwomba Mheshimiwa Waziri anifafanulie maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, Mahakama za Mwanzo. Wakazi wa Kata za Ngweloo, Makanya, Malibwi, Kwai, Gare na Ubiri, wako tayari kushiriki katika ujenzi wa Mahakama za Mwanzo katika Kata zao. Wanaomba Serikali iwapatie ramani sahihi na

kubainisha aina na kiasi cha mchango wa Serikali kusaidia ujenzi wa Mahakama zinazojengwa na wananchi wenyewe.

Chuo cha Mahakama, Lushoto (IJA), kimesaidia sana upatikanaji wa Mahakimu. Je, Serikali iko tayari kufuta ada kwa wanafunzi ambao watakuwa tayari kuingia mkatuba wa kufanya kazi Serikalini baada ya kufaulu ili kudahili Mahakimu wengi zaidi?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Mathias Chikawe, Waziri wa Katiba na Sheria kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru Serikali kwa kutuletea Mahakimu katika Mahakama za Mwanzo za Ufana, Bashanet na Dareda. Kwa hali hii, sasa huduma za Mahakama zimekuwa karibu na wananchi. Hata hivyo, tunaomba Mahakama ya Mwanzo kwa wananchi wa Gidas kilometa 45 kutoka Babati, Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwengine, naishukuru Serikali na kuipongeza kwa kushirikiana na wananchi kukarabati Mahakama ya Gallapo.

Mheshimiwa Spika, suala la Mabaraza ya Kata, ni la siku nyingi na tukifikiri lingengeza ufanisi katika “*administration of justice and rule of law*” lakini bado hili halijawa dhahiri vya kutosha kwani bado kesi nyingi zinaenda Mahakamani. Swali pia ni kwamba ni jinsi gani Mabaraza haya na masuala ya ardhi yanavyohusiana?

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na ucheleweshwaji wa kesi nyingi vijijini kwa kisingizio cha uchunguzi kuendelea kwa muda mrefu. Je, Mahakama na Polisi wanashirikiana vipi kupunguza uchelewesho huu? Je, Serikali inafahamu kwamba Mahakama na Polisi, ni maeneo yanayolalamikiwa sana na wananchi kwa rushwa?

Mheshimiwa Spika, je, Serikali inaridhika na posho ya Wazee wa Baraza kwenye Mahakama zetu? Je, Sh.1,500 zinatosha nini? Hata *Lunch Allowance* siyo hiyo!

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, katika kufuatilia kwangu, nimegundua baadhi ya Halmashauri za Wilaya hazina Wanasheria katika utendaji wao wa kazi za kila siku. Ikiwa kama Waziri wa Sheria, unaweza ukaeleza nini kuhusu suala hilo? Je, utendaji wao ukoje hasa pale Halmashauri inaposhitakiwa au inaposhtaki?

Mheshimiwa Spika, pia nimegundua baadhi ya Halmashauri za Wilaya, hufanya au hutengeneza rasimu (*draft*) ya Sheria Ndogo zinazohusiana na kutaka wananchi kwa mwelekeo wa Sheria Ndogo waweze kuchangia na kufanya kazi za kujenga Taifa. Kuweka sheria inayohusiana na uchangishaji au ujengaji wa Taifa, dhahiri ni njia mojawapo kisheria ya kuwalazimisha watu wachangie na wajenge Taifa kwa nguvu iwapo hawakuchangia au kujenga Taifa wachukuliwe hatua. Kwa mtazamo wangu,

Sheria hizo ni za uonevu kwa mfano Sheria ya Kodi ya Maendeleo au Kodi ya Kichwa. Je, msimamo wa Wizara yako ukoje kama sheria hizo zitatungwa?

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Chama chenu cha CCM, ilisema itahakikisha inawapatia Waislamu Mahakama ya Kadhi. Je, ni hatua gani imefikiwa mpaka sasa katika kulifanikisha suala hili?

Mheshimiwa Spika, licha ya kuwa Tanzania haina dini, lakini ielewe kuwa Watanzania wana dini. Dini ya Kiislamu, sheria ya mirathi haina mjadala wala marekebisho. Kwa hiyo, katika marekebisho yenu mchukue tahadhari kubwa ili msijeingilia mirathi ambayo maamuzi yake yamefanyika na Mwenyezi Mungu mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, ieleweke kuwa baadhi ya sheria kutokana na muda wake na mabadiliko hapa nchini zimepitwa na wakati. Kwa hivyo, Wizara ni lazima waweke mkakati madhubuti kuzifanyia marekebisho sheria hizo. Katika suala hili, Wizara ya Katiba na Sheria ihimize sheria hizi nazo zifanyiwe marekebisho kwa sababu zimeshapitwa na wakati.

Mheshimiwa Spika, ipo haja Mahakama kuongeza kasi katika kuzishughulikia kesi kwani kuichelewesha haki ni sawa na kunyimwa haki hiyo. Yako malalamiko mengi juu ya usheleweshaji wa kesi.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, mwanzoni mwa kikao hiki cha Bunge, niliwasilisha kwako maombi ya mwananchi (mpiga kura) wangu wa Makonde (Ludewa), ya kutaka kesi yake ambayo imekuwa ikiendeshwa pole pole sana (bila tija) katika Wilaya ya Kyela (Mbeya) ihamishiwe nyumbani Ludewa (Iringa). Naomba kujua kama kuna uamuzi wowote uliofikiwa kuhusu maombi hayo.

Mheshimiwa Spika, nashukuru Wizara yako kuzingatia upatikanaji wa pikipiki mbili kwa ajili ya Mahakama za Mwanzo Wilayani Ludewa. Bila shaka, mwaka huu pikipiki hizo zitapatikana baada ya kuzikosa mwaka 2008/2009 licha ya ahadi iliyokuwepo. Hata hivyo, naomba Wilaya ya Ludewa tufikiriwe kupata gari moja kwa ajili ya kuboresha mawasiliano na usafiri kwa ajili ya maafisa wetu wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, sisi katika Wilaya ya Ludewa, hatujafikiriwa kupata vifaa vyovoyote vya ofisi ikiwa ni pamoja na kompyuta kwa ajili ya Mahakama zetu. Naomba tufikiriwe kama bado vipo.

Mheshimiwa Spika, kadhalika, naomba Ludewa tupatiwe (tujengewe) nyumba moja kati ya kumi (10) kwa ajili ya Hakimu wetu wa Mahakama ya Mwanzo.

Mheshimiwa Spika, nitashukuru iwapo katika mpango wa Wizara yako wa kuimarisha Mabaraza ya Kata, kwa kuwapatia mafunzo wajumbe wa Mabaraza hayo, wajumbe wa Wilaya ya Ludewa, watafikiriwa katika kipindi cha mwanzo.

**MHE. ARCHT. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wengine wote hapo Wizarani kwa kutuletea hotuba nzuri pamoja na changamoto zilizopo, hongera sana.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kushukuru kwa jengo la Mahakama ya Wilaya ya Hai, tunashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, nitoe rai ya kutuboreshea Mahakama zetu za Mwanzo pamoja na kuongezewa idadi ya Mahakimu.

Mheshimiwa Spika, nitoe mapendekezo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, iwe ni lazima kwa watu kuandika wosia (*will*) ili kuepuka migogoro mingi inayotokea pale mmojawapo wa wanandoa anapotwaliwa na hivyo kusababisha matatizo kwa anayebakia haswa wanawake na watoto.

Mheshimiwa Spika, kuangalia muundo/utaratibu mzuri zaidi katika Mabaraza yetu ya Ardhi kuanzia ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, kubainisha maboresho yatakayosaidia kupunguza kama sio kuondoa kabisa rushwa kwenye Mahakama zetu ikiwa ni pamoja na kuongeza mishahara pamoja na maslahi mengine.

Mheshimiwa Spika, kuangalia uwezekano wa kujenga Gereza kwa ajili ya Wilaya za Hai na Siha ili kupunguza msongamano uliopo katika Gereza la Karanga.

Mheshimiwa Spika, kuongeza idadi ya Majaji na Mahakimu ili kupunguza msongamano wa kesi na haki kwa wananchi zipatikane mapema na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na malalamiko mengi kutoka kwa wananchi, wanaharakati, wanasiasa na hata makala katika vyombo vya habari, nadhani jambo hili lisipuuzwe, kwa maoni yangu ipo haja ya kuendesha mjadala wa kitaifa ili kubaini kama lipo hitajio la kuwepo au kubadili mambo wanayopigia kelele katika Katiba ya sasa.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo wananchi wanapiga kelele, ni muda mrefu wa kusikilizwa kwa kesi mbalimbali na hasa unapopata fursa ya kuongea na washtakiwa wa kesi za mauaji, wanalalamikia muda mrefu ambao kesi zao zinachukua na kukaa mahabusu kwa muda mirefu.

Mheshimiwa Spika, lakini napenda kupongeza hatua zinazochukuliwa za kusogeza huduma za Mahakama Kuu hadi katika ngazi ya Mikoa kwa mfano Sumbawanga na kuongezwa kwa idadi ya Majaji. Lakini pia jitahada ya makusudi inahitajika kuongeza Mahakimu katika ngazi ya R.M. na Mahakama za Wilaya na Mahakama ya Mwanzo, pia kuboresha huduma mbalimbali ikiwemo majengo, vitendea kazi, samani na kadhalika katika Mahakama zetu.

Mheshimiwa Spika, aidha, ni lazima makazi ya Majaji na Mahakimu yapewe kipaumbele na yawe na hadhi kwa mujibu wa ngazi na mamlaka yao pamoja na kuboresha maslahi yao ili wasiwe katika ushawishi pia haipendezi kuona Jiji au Hakimu hana gari.

Mheshimiwa Spika, sasa niombe Wizara iangalie hadhi ya Mahakama ya Wilaya ya Mpanda ambayo inatumia jengo lililokuwa *Liwali Court* na baadaye Mahakama ya Mwanzo, hebu fikiria jengo hili ndilo ambalo hata Vikao vya Mahakama Kuu vinafanyikia; ni aibu isiyo na mfano. Eneo la kutosha la kujenga Mahakama yenyе hadhi katika mji wa Mpanda, pia kwa makazi ya Mahakimu lipo tayari kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kwa mujibu wa sheria za nchi yetu za ndoa na mirathi, zinatambua haki za imani za wananchi wake, hata za kimila zinatambulika, sasa iweje sheria inatambua haki ya ndoa za Kiislam na za dini nyingine, Serikali hiyo hiyo haitambui Shahada za Ndoa za Kiislam zinazotolewa na BAKWATA, kwa watumishi wa Serikali hadi wawe na vyeti ambavyo vinatolewa na *RITA* ambayo imeanza hvi karibuni na kutaka hata wale waliofunga ndoa kabla ya *RITA* wapate vyetu toka *RITA*. Naomba haki za wananchi za kuabudu zisiingiliwe na Serikali isiyokuwa na dini. Vyeti vyote vinavyotolewa na Makanisa na BAKWATA, viheshimiwe na kukubalika kama hati halali.

**MHE. MARTHA M. MLATA**, Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote, kwa hotuba nzuri aliyoitoa Mheshimiwa Waziri. Pia napenda kutoa pongezi kwa Mahakama Kuu hadi za chini, kwa utendaji mzuri wa kazi zake, japo ni katika mazingira magumu sana.

Mheshimiwa Spika, sote tunatambua kuwa, ili nchi yetu iweze kuwa na watu waadilifu na kuwa na amani, ni vema sheria zetu zikatekelezwa kwa haki na uangalifu. Hivyo, kwa hali hiyo, wenzetu hawa wametusaidia sana kwa utendaji wao mzuri. Nipende tu kuiomba Serikali, itoe kipaumbele pia katika Wizara hii kwa kuwatengea fedha za kutosha ili wawexe kufanya kazi zao vizuri. Pia naomba Mahakimu na Majaji, waongezewa mishahara na marupurupu mengine, ili kuwawezesha kutenda kazi yao kwa haki. Kwani, kuna baadhi ya Mahakimu hulalamikiwa kuwa hukumu zao ziko katika mazingira ya rushwa. Yote haya yanatokana na hali ngumu walizo nazo Mahakimu wetu, hiyo inasababisha kutoaminika kwa jamii. Kwa kuwaongeza fedha, heshima na uaminifu kwa jamii itakuja.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni suala la Sheria ya Ndoa. Bado ina upungufu, naomba iletwe hapa ili tuibadilishe ili kuleta haki kwa wanawake ambao tayari wengi wao wameshaathirika, pamoja na watoto.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, ni kwa nini kesi za za uchaguzi huchukua muda mrefu? Naomba kuwe na Kitengo Maalumu cha Kuzungumzia suala la Kesi za Waheshimiwa Wabunge Majimboni ili ziishe haraka na kuleta haki kwa wananchi wanaoishi katika Jimbo lile. Kwani kuchelewesha kesi hizo kunawanyima haki wananchi wa Jimbo husika kupata uwakilishi kamili ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, pia naomba Mahakimu wetu wajengewe nyumba.

**MHE. MARIAM REUBEN KASEMBE:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii, kuishukuru Wizara hii kwa kuandaa Hotuba yao kwa ufanisi mkubwa unaoeleweka.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi ya pekee, kumpongeza Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mathias Chikawe, kwa utendaji wake mzuri wa kazi na usikivu pale unapomwomba ushauri au utekelezaji wa shughuli mbalimbali katika majimbo yetu.

Mheshimiwa Spika, binafsi katika mwaka wa fedha wa 2008/2009, nilipochangia katika Wizara hii, nilielezea uchakavu wa Mahakama ya Mwanzo ya Lusekese – Masasi. Ninashukuru na natumaini hata Wananchi wa Masasi wataona jinsi serikali ilivyo sikuvi, kwani katika Hotuba hii inaonesha Mahakama hii imeshakarabatiwa.

Mheshimiwa Spika, si hilo tu, kwa niaba ya Wananchi wa Kata ya Lukuledi na Masasi kwa ujumla, niliomba mchango katika Wizara hii, kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo Lukuledi. Baada ya Wananchi hawa kuandaa mpango wa ujenzi wa Mahakama na nyumba ya Hakimu ili kuondokana na kero kubwa ya kufanya kesi katika Ofisi ya Kata au Ofisi ya Kijiji na mara nyingi kesi kuhamishiwa Mahakama ya Mwanzo ya Lusekese, leo nashukusru sana kupokea taarifa inayoonesha ombi hili limekubaliwa na serikali imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo Lukuledi. Kwa niaba ya wananchi, ninasema ahsante sana na tupo tayari kushirikiana na serikali katika shughuli ya ujenzi huu ili kukamilisha kwa wakati na wananchi wawe na mahali pao pa kupatia haki zao.

Mheshimiwa Spika, hadi hivi sasa, bado akina mama wengi hapa nchini, wamekuwa wakikosa haki za urithi na mirathi pale wanapofiya na waume zao au wazazi wao. Kwa kuwa nchi yetu ina makabila mengi; hivyo kutofautiana katika mila na desturi; na kwa kuwa Wizara inaandaa rasimu ya marekebisho ya Sheria za Mirathi na Sheria zote zinazoonesha kukandamiza wanawake; ninaishauri serikali kushirikisha kikamilifu, wadau wote kutoka mikoa yote yenye mila hizi zinazokandamiza akina mama ili kuwa na mjadala wa pamoja na kutoa elimu ya kutosha ili sheria hii itakapopitishwa, iwe yenye nguvu kwa kumaliza ukandamizaji huu unaoendelea hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, naiomba pia Wizara hii, wawe wasimamizi wazuri katika kutatua suala la mirathi, ambalo kwa hivi sasa kumekuwa na ucheleweshaji mkubwa wa malipo haya; hivyo, kuwa kero kubwa kwa wananchi wanaopata tatizo la kufiwa. Ninaamini Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, wataliondoa tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kurudia tena, kuipongeza Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya ya kuboresha Mahakama zetu hapa nchini, ingawa katika mazingira magumu ya hali ya fedha, kwani *budget* yao hailingani na huduma wanazotakiwa kutoa. Serikali ione umuhimu wa kuongeza kiasi cha fedha kwa *budget* zijazo. Inawezekana, tutimize wajibu wetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii, kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri iifanyazo na ninaipongeza kwa uwasilishaji mzuri wa Hotuba yenu Bungeni.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara isaidie matatizo ya uhaba wa Mahakama za Mwanzo kwenye Wilaya ya Sikunge. Wilaya ina Mahakama moja tu ya Mwanzo. Kutokana na ukubwa wa eneo la Wilaya ya Sikunge, wananchi wengi wanashindwa kufika Makao Makuu ya Wilaya, wanapokuwa na mashauri Mahakamani. Naiomba Mahakama kuititia Wizara, iongeze maeneo ya Mahakama katika Kata hasa za Tutuo, Kitunda, Kipiri na Kiloleli.

Aidha, naiomba Wizara ikishirikiana na Idara ya Mahakama, ianzishe kwa haraka Mahakama ya Wilaya kwa kuleta Mahakimu au Hakimu wa Wilaya ili kesi zinazosikilizwa Tabora (kilimita 71 toka Sikunge), zinazostahili kwa Mahakama hiyo ziweze kufanyika Sikunge ili kuwapunguzia adha ya kusafiri kwenda Tabora kufuata mashauri ya kesi zao hapo Tabora.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**SPIKA:** Katika hatua hii, tumehitimisha uchangiaji wa Waheshimiwa Wabunge na ni kawaida sasa kumwita mtoa hoja ambaye ni Waziri, aweze kufanya majumuisho. Kwa hiyo, namwita Waziri wa Katiba na Sheria, afanye majumuisho kwa dadika zisizozidi 30. Tutaondoa ile sehemu ambayo utakuwa anataaja wachangiaji na vitu vingine kama hivyo.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia na mimi kufika wakati huu. Aidha, nakushukuru sana wewe binafsi, kwa kusimamia vizuri mjadala huu na pia kwa kunipa fursa ya kuhitimisha hoja hii niliyoitoa leo asubuhi, kwa kutoa maelezo kuhusu masuala mbalimbali yaliyojitokeza na yaliyozungumzwa na

Waheshimiwa Wabunge. Kwa kuzingatia kuwa Waheshimiwa Wabunge ni Wawakilishi wa Wananchi; ni wazi kuwa yote waliyoyasema ni kwa niaba ya wananchi wanaowawakilisha. Hivyo, nafasi hii niliyoipata ni sawa na nafasi ya kutoa majibu kwa hoja za Wananchi.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa maelezo kuhusu hoja mbalimbali ni vyema niwatambue wote waliochangia, ambao wapo katika makundi makubwa matatu: Wapo wale waliochangia masuala ya Katiba na Sheria wakati wakichangia Hotuba ya Waziri Mkuu; wapo waliochangia kwa kuzungumza humu Bungeni; na waliochangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, waliochangia masuala ya Katiba na Sheria wakati wa Hotuba ya Waziri Mkuu walikuwa wawili nao ni Mheshimiwa Sijapata Fadhili Nkayamba na Mheshimiwa Shoka Khamis Juma.

Waliochangia kwa kuzungumza ni Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbiri, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Rajabu Hamad Juma, Mheshimiwa Sipata Fadhili Nkayamba, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Manju Msambya, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Dr. Luka Siyame na mwisho kabisa, ndugu yangu Mheshimiwa Magalle John Shibuda.

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa maandishi ni wengi kidogo nao ni Mheshimiwa Jacob Shibili, Mheshimiwa Meryce Emmanuel, Mheshimiwa Zaynab Matitu Vulu, Mheshimiwa Mary Michael Nagu, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Janeth Mourice Massaburi, Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, Mheshimiwa Suzan Lyimo, Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Profesa Mwalyosi, Mheshimiwa Archt. Fuya Kimbita, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Khadija Al-Qassmy, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Dorah Mushi na Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Rita Mlaki, Mheshimiwa Charles Mwera, Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Salum Hemed Khamis, Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda,

Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula na Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis.

Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia. Kimsingi, wametoa hoja nzuri sana, zenyé malengo ya kuimarisha utekelezaji wa majukumu katika Wizara yangu. Hii inaonesha ni namna gani Waheshimiwa Wabunge, wako tayari kutoa michango yao ya kimawazo kwa minajili ya kuendeleza sekta hii muhimu ya sheria.

Mheshimiwa Spika, michango ambayo Waheshimiwa Wabunge wameitoa ni mingi. Ni wazi kuwa, muda huu tulionao si rahisi kutoa maelezo ya kujibu kila hoja iliyotolewa. Nieleze tu kwamba, michango yetu yote iliyotolewa tunaithamini sana na kwamba, kama Wizara tutaifanyia kazi kikamilifu, kama ilivyo ada, tutawaandalia majibu ya hoja zote kwa kina na tutawasambazia Waheshimiwa Wabunge, kabrasha lenye majibu ya hoja zote zilizotolewa leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kujibu hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, ni vyema basi nikaanza kujibu hoja za jumla ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge, pamoja na zile hoja zilizotolewa na Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua na kuheshimu umuhimu wa mhimili wa Mahakama katika kujenga taifa imara kijamii, kisasa na kiuchumi. Mahakama ina jukumu kubwa katika kukuza na kulinda demokrasi katika jamii iliyostaarabika kama ya kwetu hapa nchini. Kwa kutambua ukweli huu, Serikali siku zote imekuwa ikiheshimu na kulinda uhuru wa mahakama.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majukumu mazito ya mahakama, mhimili huo umekuwa ukikabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo Waheshimiwa Wabunge katika michango yao, wamezielea kwa kina. Moja ya changamoto hizo ni upungufu wa majengo ya Mahakama na idadi ndogo ya Mahakimu na Majaji. Kama nilivyolieze Bunge lako Tukufu katika hotuba yangu, Serikali inalitambua tatizo la upungufu wa majengo ya mahakama na idadi ndogo ya watumishi wa mahakama wakiwemo Mahakimu na Majaji. Hivyo basi, Serikali imekuwa ikichukua hatua madhubuti na za makusudi za kuongeza idadi ya Watumishi wa Mahakama.

Kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009, Serikali iliajiri Mahakimu 101 wa Mahakama za Mwanzo, Mahakimu wa Kazi tuliajiri 47 na kuteua Majaji wa Rufaa watatu, kujaza nafasi zilizoachwa wazi na Majaji waliostaafu. Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2009/2010, Serikali inakusudia kuajiri Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo 100 na Mahakimu wa Kazi 50. Hii yote ni katika kuboresha huduma hii kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyolieza katika hotuba yangu leo asubuhi, Serikali kwa kushirikiana na Program ya Maboresho ya Sekta ya Sheria, imeendelea kujenga Mahakama na kukarabati zilizopo kadiri uwezo wa fedha ulivyokuwa unaruhusu. Mathalani katika mwaka ujao wa fedha, jumla ya Mahakama 20 za Mwanzo zitajengwa na ujenzi wa Mahakama Kuu Shinyanga utaanza na ikiwezekana utakamilika. (*Makofi*)

Aidha, ujenzi wa Mahakama Kuu Singida utaanza mwaka huu. Hii inadhihirisha nia ya dhati ya Serikali ya kukabili ana na uhaba wa watumishi, pamoja na kuongeza idadi ya majengo ya Mahakama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko ya ucheleweshaji wa kesi mahakamani. Ucheleweshaji huu, kwa kiasi kikubwa unachangiwa na uhaba wa Majaji, uhaba wa Mahakimu, mazingira ya upeletezi na upungufu wa vitendea kazi na miundombinu duni. Kwa kutambua tatizo hilo, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ili kulitatu tatizo hili. Moja ya hatua hizo ni kuendelea kuongeza idadi ya Mahakimu, kuongeza idadi ya Majaji na watumishi wengine, kama nilivyoeleza hapo nyuma. Aidha, kupitia Program ya Maboresho ya Sekta ya Sheria, wapelelezi wa Jeshi la Polisi, wamekuwa wakipatiwa mafunzo katika medani ya upeletezi ili kuimarisha uwezo wao na hivyo kuharakisha upeletezi. Kadhalika, Program hiyo imekuwa ikitoa kwa Jeshi la Polisi, vifaa mbalimbali kama vile pikipiki na vyombo vingine vya mawasiliano kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa upeletezi ili kesi zisichelewe sana. Katika ngazi za Mikoa na Wilaya, kumekuwa na vikao vya kusukuma kesi ambavyo huchangia kwa kiasi kikubwa, kupunguza mrundikano wa kesi katika Mahakama zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais, alikubali kuanzishwa kwa Mfuko wa Mahakama (*Judicially Fund*), kama ilivyo kwa mhimili wa Bunge. Mchakato wa kuanzisha Mfuko umeanza na tayari Waraka wa Baraza la Mawaziri, umeandaliwa na utawasilishwa katika Baraza la Mawaziri, kwa ajili ya kupata baraka ya Baraza wakati wowote kuanzia sasa. Hivyo basi, pamoja na Mahakama kuendelea kupata mgao wa fedha kutoka Hazina, kama ilivyo kwa Wizara nyingine za Serikali, katika mwaka huu wa fedha kumekuwa na mabadiliko kidogo kwa maana kuwa sasa Mahakama ya Rufaa, Mahakamu Kuu na Mahakama za Wilaya na za Mwanzo, zitakuwa na mafungu tofauti. Huko nyuma kulikuwa na Fungu moja tu Fungu la 40, lakini sasa kutakuwa na fungu la 40 kwa ajili ya Mahakama ya Rufaa, Fungu la 19 kwa Mahakama za Wilaya na za Mwanzo na Fungu la 18 kwa ajili ya Mahakama Kuu. Hatua hii ya Serikali itaongeza ufanisi katika shughuli za Mahakama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa hivi karibuni kumekuwa na mjadala juu ya kinga dhidi ya mashtaka kwa Marais Wastaafu. Ibara ya 46(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inatumika kwa mtu aliyekuwa anashika madaraka ya Urais, ambaye madaraka yake ya Urais yameondolewa kwa mujibu wa ibara ya 46(a)(10). Hivyo basi, ibara ya 46(3) haitumiki kwa Rais aliyestaafu kwa mujibu wa Katiba.

Mheshimiwa Spika, kwa mfumo wa utoaji haki wa Tanzania, hakuna ubaguzi wa aina yoyote, kwa lugha nyingine hakuna *Double Standards*. Mashauri yote yanayofikishwa mahakamani, husikilizwa na kuamuliwa kwa mujibu wa sheria za nchi yetu. Ni ukweli usiopingika kuwa, baadhi ya kesi huchukua muda mrefu kutokana na upeletezi wa kesi hizo kutokukamilika kwa wakati, kunakosababishwa na ukosefu wa vitendea kazi, kutopatikana kwa mashahidi na ugumu wa upeletezi unaosababishwa na aina ya kesi zenyewe. Kuna kesi mpya siku hizi zinahitaji teknolojia ya aina ya hali ya juu kuweza kupata ushahidi wake, mambo ya TEKNOHAMA na kadhalika ni magumu.

Ni kweli zipo baadhi ya kesi ambazo usikilizaji wake umekuwa ukienda kwa kasi, lakini hii inachangiwa na upelelezi wa kesi hizo kuwa rahisi na pia baadhi ya kesi hizo kuwa na maslahi ya umma (*Public Interest*). Mtakumbuka kuwa, hivi karibuni wananchi wamekuwa wakitoa maoni yao, kutaka kuundwa kwa Mahakama maalum ya kushughulikia kesi za wauaji wa Maalbino. Hii peke yake, inadhihirisha wazi kuwa, hata wananchi wenyewe wanaona umuhimu wa baadhi ya kesi kuendeshwa kwa haraka. Katika hili niseme tu, zipo kesi nyingi za watu wa kawaida tu, ambazo zimeendeshwa kwa kasi na kumalizika. Kutokana na kuwa wahusika wa kesi hizo siyo watu maarufu, zimekuwa hazitangazwi kabisa kwenye vyombo vya habari. Kwa hiyo, kinyume na zile za watu maarufu ambazo zinatangazwa, ingawa watu wanasema zipo kesi za watu maarufu wanapendelewa labda kesi zao zinasikilizwa haraka lakini si kweli. Zipo za watu ambao hawajulikani kabisa zinasikilizwa haraka, ila kwa sababu ya kutokujulikana kwao basi na kesi hazitangazwi.

Mheshimiwa Spika, kwa maendeleo ya taaluma ya sheria, ripoti za kesi ni muhimu sana. Nakubaliana na Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwamba, ripoti za kesi ni vitu muhimu sana katika kazi yetu ya uanasheria. Ripoti hizi husaidia Mahakimu kutoa tafsiri sahihi za sheria kwa kurejea Hukumu za Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, chini ya Mpango wa *Business Environment Strengthening for Tanzania*, mchakato wa kuchapisha *Law Reports* za kuanzia mwaka 1996 hadi 2006 umeanza na itakapofika Desemba, 2009, *Law Reports* hizo zitakuwa tayari zinapatikana. Kwa hiyo, tutakuwa tumepiga hatua mpaka angalau mwaka 2006. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Katiba Mpya, suala hili limezungumzwa katika karibu Mabunge yote. Wizara yangu ilitoa maelezo ya kina katika Bunge la Bajeti la Mwaka 2007/2008 na 2008/2009. Katika maelezo hayo, tulieleza kwa nini Serikali haiwezi kwa sasa kuwa na Katiba Mpya. Napenda kusisitiza kuwa, sababu tulizozieleza wakati ule ni za msingi na msimamo wa Serikali haujabadilika kuhusu hoja hii hadi hivi sasa.

Niseme tu hapa kwamba, hata mimi mwenyewe nimeshawahi kuwaauliza wanaotaka Katiba Mpya walete tu kwa maandishi nini hasa wanakitaka. Mpaka sasa bado sijapokea mapendekezo yoyote kutoka kwa mtu yejote; ni kitu gani kinatakiwa kwenye Katiba Mpya, ambacho wanadhani Katiba hii ya sasa haikidhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mgombea binafsi, sote tunafahamu kuwa si vyema kulizungumzia kwa kuwa kuna kesi mahakamani kuhusu suala hili. Niseme tu kuwa, uamuzi wa kukata rufaa hauna nia ya kuibana demokrasia kama anavyozungumzia Msemaji wa Upinzani, bali ni kutaka kujiridhisha kama sheria na taratibu zilifuatwa katika kufikia uamuzi wa kuwa na mgombea binafsi.

Uamuzi mkubwa kama huu, unapaswa vile vile ungetolewa na mahakama yetu ya juu kabisa; Mahakama ya Rufani. Kwa hiyo, tunalipeleka huko ili tupate uamuzi huo na pindi uamuzi ukitolewa, basi tutauzingatia ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuendelea kuwepo kwa adhabu ya kifo katika sheria zetu, hili pia limezungumzwa na wachangiaji wengi wameliandika. Kwa sasa nalo pia siwezi kusema lolote, kwa kuwa Chama cha Wanasheria Tanzania kikishirikiana na Taasisi Zisizo za Kiserikali, kimefungua kesi Mahakama Kuu dhidi ya Serikali, kikihoji uhalali wa adhabu ya kifo. Kwa kuwa kesi hiyo haijatolewa uamuvi, si sahihi kujadili suala hili hapa Bungeni na taratibu zetu zinatukataza kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, sasa nijaribu kujibu hoja mahususi moja moja, baada kuzizungumza ambazo zilikuwa ni za jumla.

Naomba nilitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, pengine sitaweza kuzimaliza zote kwa sababu hoja ni nyingi. Nitajaribu kwenda kasi kwa kadiri ninavyoweza ili angalau kila Mbunge asikie majibu ya hoja zake. Kama nilivyosema mwanzo, kwa wale ambao hoja zao nitakuwa sijaweza kuzizungumzia, tutatengeneza kitabu cha majibu ya hoja zote na kila Mbunge atapatiwa nakala.

Msemaji wa Kambi ya Upinzani, amezungumzia kwamba, miundombinu katika Mahakama ni duni, hakuna pa kuhifadhi mahabusu na akatoa mfano wa Mahakama ya Kariakoo na Mahakama ya Endulen kule Ngorongoro. Nami nataka nikubaliane naye kwamba, ni kweli miundombinu katika Mahakama zetu ni duni, lakini hii inatokana na ufinyu wa bajeti. Mahakama ya Mwanzo ya Nduleni, kwa sasa imefungwa wala haifanya kazi, hata mimi mwenyewe nilipita juzi kule Machame, nilikuta Mahakama ambayo ipo kwenye hali mbaya, tukaamua nayo pia ifungwe, kwa sababu ilikuwa inahatarisha hata usalama wa wale wanaokwenda kwenye Mahakama hizo. Hivi sasa shughuli za Mahakama hii ya Nduleni, zinafanyika kwenye Mahakama ya Mwanzo Ngorongoro.

Mheshimiwa Mgana Msindai, alizungumzia kuhusu nyumba ya Hakimu Iguguno na uhaba wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo Iramba Mashariki, Mahakimu Wilaya ya Sikonge, Nduguti, Ibaga na Kirumi, uhaba wa vitendea kazi na Mahakama ya Mwanzo kusikiliza kesi za ardhi. Napenda nimwambie Mheshimiwa Mgana Msindai kwamba, nyumba ya Hakimu Iguguno itajengwa kulingana na upatikanaji wa Fedha. Kama wenyewe mlivyoona, hata katika hotuba yangu hii tumejitahidi sana kujenga na kukarabati nyumba na Mahakama kwa kadiri fedha zilivyokuwa zinaruhusu. Nataka niwaeleze kwamba, tutaendelea na zoezi hili kwa nguvu zetu zote na hivi mnavyozi kutuombea dua na kutuombea tupate fedha nyingi, nataka niwahakikishie kwamba, kazi hizi ndiyo tunazokusudia kuzifanya. (*Makofi*)

Mahakama ya Mwanzo ya Nduguti ina Hakimu na hizo nyingine alizozitaja, tutawapelekeea Mahakimu kadiri tunavyowapata. Sasa hivi tuna *shortage* ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo hizi wasiopungua 500. Hii ni *shortage* kubwa, lakini tunajaribu ku-*train* vijana wetu zaidi pale Lushoto na pindi kila wanapotoka, tunawagawa katika Mahakama hizi ili waweze kukidhi haja. Kama tulivyokuwa tumezungumza pia katika kitabu chetu cha bajeti ni kwamba, tunakusudia kuziboresha hizi Mahakama za Mwanzo na kadiri itakavyowezekana, kuzipatia Mahakimu ambao watakuwa wana shahada ya sheria.

Hawa ni wengi; hivi sasa nchini tuna hizi *Faculty* za sheria karibu 10 na zote kila mwaka zinatoa wahitimu wa sheria. Kwa hiyo, tunadhani hatutapata tabu ya kuwapata wahitimu. Sisi tunadhani tukiwapeleka kule, tutapata huduma nzuri zaidi na pia tutawenza kuwapa wananchi wetu ile huduma ya uwakilishi ya kupata *advocate* wa kututetea. Maana wakati mwingine mtu anakwenda mahakamani si kwa sababu amekosa anaweza kufungwa, lakini anaweza kufungwa kwa sababu anashindwa kusema anaogopa anatetemeka, lakini akipata mtu wa kumsemea, anaweza akaipata haki yake. Tunataka tufikishe huduma hii mpaka kule kwenye Mahakama za Mwanzo. Tunajua itakuwa ni ngumu kwa kuanzia, lakini tunasema tutaanza kidogo kidogo; tutaanza kwenye *urban areas* halafu tutakwenda jinsi tunavyoweza *kuzi-improve* zile *facilities* kule nje tutapeleka na huko pia.

Napenda nimjibu Mheshimiwa Msindai, kuhusu Wilaya ya Sikonge kwamba, kweli hawana Hakimu na pia hawana Jengo la Mahakama ya Wilaya. Hoja hii ililetwa pia na Mbunge wa Sikonge. Jitihada za kupata jengo zinaendelea na mara likipatikana, nataka niwahakikishie kwamba, tutawapatia Hakimu wa Wilaya mara moja.

Mahakama za Mwanzo za Nduguti, Ibaga na Kirumu, zitakarabatiwa mara tutakopata fedha katika bajeti. Nafikiri siyo Bajeti hii, ni bajeti ijayo. Kuna uhaba wa vitendea kazi katika Mahakama za Mwanzo na hii ni sawa. Kuna uhaba mkubwa na hili nimelizingumza, hata mimi mwenyewe kila ninapotembelea. Hili linaanza kule mahabusu; unakuta mahabusu wengi, ukiuliza wanasema sisi tumefungwa na Mahamama ya Mwanzo tunataka kukata rufaa, lakini hatuna nakala ya *judgement*. Kwa nini huna nakala ya *judgement*? Anasema kwa sababu haijachapwa. Ukienda Mahakamani ukiwaliza kwa nini nakala ya *judgement* haijachapwa, wanakwambia kwa sababu *typewriter* labda tunazo lakini hatuna mchapaji. Kwa hiyo, kuna matatizo mengi madogo, ambayo sasa hivi tunayashughulikia na nafikiri utafika wakati hivi karibuni, tutatoa maamuzi ya kimsingi kabisa ambayo tunadhani yatarekebisha hali hii.

Msemaji wa Upinzani pia alizungumzia Sheria ya Misaada ya Kisheria, yaani *Legal Aiding Criminal Proceedings*. Alisema hakuna utaratibu wowote wa kuitekeleza Sheria hiyo na aliomba Wizara ihakikishe kuna utaratibu uliowekwa na mpango madhubuti wa utoaji wa msaada uwekwe. Nataka nimweleze Mheshimiwa Maghimbi kwamba, kwa mujibu wa Sheria hiyo, Sura ya 21, *Revised Addition 2002*, kifungu cha tatu; pale ambapo mamlaka inayohusika inaona kuwa katika shauri la jinai lililopo mbele yake katika mahakama, mshtakiwa anahitaji msaada wa kisheria, lakini hana uwezo wa kuweka, mamlaka hiyo itaelekeza mshtakiwa apewe wakili wa kumteteta.

Kwa sasa mchakato wa kuweka taratibu za jinai za kuendesha mpango huo chini ya kifungu cha pili unaandaliwa. Hata hivyo, wakati huu mamlaka ya kuelekeza kupewa wakili yametolewa kwa Mheshimiwa Jaji Mkuu, Mheshimiwa Jaji Kiongozi na Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu katika kanda kwa Mahakama zilizo chini yake, Mahakama ya Hakimu Mkazi na Mahakimu wa Wilaya. (*Makofî*)

Mheshimiwa John Lwanji, Mbunge wa Manyoni Mashariki, alizungumza kuhusu kufanya ukarabati katika Mahakama za Mwanzo za Ikumbi na Mwanagembe. Kwa mujibu wa taratibu za matumizi ya fedha za umma, Hakimu husika ametakiwa kuwakilisha makadirio ya ukarabati ili kazi husika iweze kufanyika. Kwa hiyo, pindi Hakimu huyu atakapoweza kuleta makadirio ya ukarabati huo, basi kazi ya ukarabati utafanyika.

Mheshimiwa Lwanji, aliomba Bajeti ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama ya Lushoto iongezwe ili mafunzo zaidi kwa Mahakama za Mwanzo yatolewe, sambamba na ujenzi wa Mahakama. Ushauri huu tunauzingatia na kila mwaka huwa tunaomba bajeti iongezwe, lakini tunajua pia bajeti ni ndogo kwa sababu makusanyo ya Serikali ni madogo, hayawezi kutosheleza kwa kila idara inayoomba.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ludovick Mwananza, Mbunge wa Jimbo la Kalambo, yeche aliwa na hoja kwamba, Wizara isambaze Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo hasa katika Jimbo lake la Kalambo hana Mahakimu pale. Nasema tumelipokea ombi hili na tutajitahidi kusambaza Mahakimu hao katika Mahakama hizo, pindi tutakapowapata kutoka chuoni. Alisema pia kwamba, tuwajengee Mahakama za Kisasa Makao Makuu ya Jimbo Kijiji cha Matai Kasanga, Mhombi, Mwanzie na Legeza Mwendo. Pia nataka niseme, tumepokea ombi hili tatalishughulikia na tutajenga mahakama za kisasa. Tuna-*design* nzuri sana kwa Mahakama za Mwanzo, ambazo tumezijenga kwa mfano kule Kalenga na kwingineko; watu wamezipenda sana, ni nzuri na ni za kisasa. Kwa hiyo, namwambia Mheshimiwa Mwananza kwamba, tutakapopata uwezo wa kujenga, basi tutajenga Mahakama nzuri zaidi.

Ningemwomba naye kama anaweza, awahamasithe wananchi wa sehemu za Matai, Kasanga, Legeza Mwendo na kadhalika, waweze kuchangia kiasi fulani katika ujenzi wa Mahakama hizi au wazijenge kama walivyojenga wananchi wa sehemu nyininge.

Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mbunge wa Kasulu Mashariki, alizungumzia kuhusu hali mbaya Mahakama ya Wilaya ya Kasulu. Anasema, ofisi inahitaji ukarabati lakini pia tuandae mpango wa kujenga ofisi mpya. Mahakama ya Wilaya ya Kasulu itawekwa katika mpango wa kujengwa, hali ya fedha itakaporuhusu. Aidha, ukarabati utafanywa hali ya fedha itakaporuhusu. Nasema haya kwa sababu bajeti ni mpango wa mwaka mmoja tu, lakini miaka inaendelea na jinsi tunavyokwenda, mipango hii tutaiweka ili angalau basi tutimize maombi hayo ambayo ni mengi kutoka karibu kwa kila Mbunge kwamba, mahakama inahitajika mpya au inahitaji kukarabatiwa. Nataka niseme kwamba, maombi haya tumeyapokea na tutakuweka katika *priority* pindi tutakapopata fedha ili kuzijenga na kuzikarabati Mahakama hizo.

Ameomba pia apewe gari, yaani kununua gari kubwa *Land Cruiser Hardtop* hali ya fedha ikituhusu. Najua kwa sasa una gari ndogo, lakini hiyo ni hatua kubwa mwanzo kabisa, tulikuwa hatuna hata pilipiki tukapata hizo ndogo, sasa anaomba *Land Cruiser* basi tungojee tu neema ikishuka, nina hakika na *Land Cruiser* pia atapata.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ole-Telele anasema, pale Ngorongoro kuna Mahakama ambayo ni *full suit*, yaani mabati tu. Kwa vile yeye yuko mpakani na wale watu wa Kenya wakija pale huwa hawaamini kama ile ni Mahakama; mimi mwenyewe nitachukua muda kutembelea huko pamoja na Longido, nikaone matatizo haya halafu tutaona ni kitu gani tunaweza kukifanya. Hatuwezi kuruhusu mahakama zetu zikafanye kazi katika sehemu ambazo hazina hadhi hata kidogo. Hii inatushushia hadhi sisi kama Mahakama, lakini pia kama nchi.

Kwa hiyo, nilitaka niwaambie tu kwamba, ombi hili nimelisikia na nitalifanya kazi kadiri uwezo utakavyoruhusu.

Mheshimiwa Suzan Lyimo, alizungumzia kuhusu Mahakimu kukosa nyumba na ulinzi. Kwa sasa hivi nataka nimweleze kwamba, kila tunapojenga Mahakama mpya, tunahakikisha tunajenga na nyumba ya Hakimu. Kila mahali tutakapojenga Mahakama, tutaweka na nyumba angalau moja ya Hakimu. Tumejaribu kupeleka magari katika Mahakama za Wilaya na pikipiki katika Mahakama za Mwanzo, kadiri uwezo unavyoongezeka.

Mheshimiwa Martha Mlata, alizungumza kuhusu maslahi ya Majaji na Mahakama yaboreshwe. Nasema ushauri huu tumeupokea na tutaufanyia kazi.

Mheshimiwa Paul Kimiti, amezungumzia nyumba na usafiri kwa Mahakimu. Nasema ni mkakati wa Serikali kujenga Mahakama, pamoja na nyumba za Mahakama. Serikali kuitia Wizara ya Miundombinu, inajenga nyumba za Mahakama. Mwaka huu nafikiri tumepata fedha za kujenga miundombinu, watatujengea nyumba za Majaji kama 14. Mahakama Kuu mwaka huu wa fedha, kiasi kitatengwa kwa ajili hiyo.

Ujenzi wa Mahakama katikati ya Miji, hili lililetwa na Mheshimiwa Lucy Mayenga; alikuwa anasema ujenzi wa Mahakama katika Miji inasababisha msongamano wa magari, msafara unapopita na msongamano wa watu wanaokuja kushuhudia kesi hizo, kwa mfano Kisutu. Anasema Mahakama hizi zijengwe sasa nje ya Mji. Ushauri ni mzuri na wazo hili tumelipokea tatalitafakari. (*Makofî*)

Msemaji wa Kambi ya Upinzani, alizungumzia kuhusu muda wa kustaaifu Majaji. Alisema muda huu uangaliwe upya, kwani wengi wanastaifu wakiwa na uwezo wa kuendelea kufanya kazi za Mahakama. Tunasema Mahakama na Serikali kwa ujumla tumelipokea wazo hili na ni wazo zuri tatalifanyia kazi, labda mwakani tukija tunaweza kuja na maelezo tofauti na ya sasa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mbunge wa Nzega, anazungumza kwamba, mshahara na maslahi ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo yaboreshwe. Mimi nasema ni kweli na tayari mchakato wa kuangalia na kuboresha maslahi ya watumishi hawa umekwishaanza. Alizungumzia pia kuhusu mahitaji ya teknolojia ya kisasa kutumika katika Mahakama za Wilaya na Mwanzo, pamoja na kuboresha ofisi zao. Utaratibu wa matumizi ya kiteknolojia ya kisasa katika Mahakama hizi umeanza kwa

awamu. Mahakama za Mwanzo 15 zimeshapata *computer*, Mahakama za Wilaya zote zina *computer* na Mahakama ya Mwanzo ina kipaza sauti pia.

Msemaji wa Upinzani pia alizungumzia kuhusu matumizi ya teknolojia katika Mahakama na nimelieleza kama nilivyoeleza hivi punde. Kama nilivyosema, watoa hoja ni wengi na hoja ni nyingi, siwezi kuzisoma zote.

Sasa naomba tu nimalizie kwa kuzungumzia hoja ambayo Serikali imeitolea maelekezo; hoja ya kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi. Hoja hii imezungumzwa na watu wengi kwa pande zote mbili; wapo waliosema kwamba, Serikali iko katika njia sahihi na tunachokifanya sasa ni sahihi. Mimi naomba kuwashukuru wao kwa kututia nguvu. Wapo waliosema kwamba, wao hawatakubali kitu chochote mpaka ipatikane Mahakama ya Kadhi, nao pia ni mawazo yao.

Niseme tu kwamba, kama Serikali ya nchi ambayo haina dini, Serikali inaheshimu dini zote. Katiba yetu imeunda Mahakama, ambayo inatoa haki kwa watu wote; haibagi dini wala wa rangi.

Kwa hiyo, tunaamini utaratibu huu ambao tumeuleta hapa Bungeni, ambao ndiyo Serikali imeamua kuufanya, utatoa haki kwa watu wote; kwa Wakristo na kwa Waislam wa Madhehebu yote. Utaratibu huu utakachofanya ni kwamba, wale wataalam wa madhehebu mbalimbali ya dini ya Kiislam, wataaka wakubaliane ile misingi ambayo iko kwenye Quran na kwenye hadithi, kote kule yanakusanywa yale yanaandikwa tu katika sheria, hayabadilishwi hata kidogo yanaandikwa tu katika *Government Notice* yanatangazwa, ukienda mahakamani unaikuta hiyo. Haitabadilishwa na haitapinda. Huwezi kubadilisha Quran, hata kama unataka haibadiliki. Kwa hiyo, tunachofanya hapa ni kutafuta tu njia ambazo Muislam akienda pale, ataipata haki yake kwa dini yake. (*Makofi*)

Kwa hiyo, naomba ndugu zangu Wabunge, jambo hili tulipokee vizuri na tushirikiane. *Actually*, niseme tu wenzetu wa Madhehebu ya Shia, walishakuja na wamekwishaandika vizuri sana tena Kiingereza. *Islamic Principles* zote za mirathi, ndoa na matunda ya watoto, zimeandikwa vizuri na zinaweza kutumika. Tunakusudia hizi tuzitazame upya, tukikaa na wao wenyewe tutazi-gazette na zitatumika katika Mahakama zetu kama sheria za nchi. Huu ni utaratibu mzuri, ambao haumletei mtu ye yote matatizo. Sheria za Nchi na Mahakama zetu ambazo ziko tayari zikiendeshwa na Jaji Mkuu, zitasimamia haki ikitendeka.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema yote haya, naomba sasa niwashukuru Wabunge kwa kuniunga mkono na naomba sasa nitoe hoja kwamba, bajeti yangu ipitishwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria ya kilitaka Bunge likubali kupidisha makadirio ya Wizara yake ya Katiba na Sheria kwa Mwaka Fedha 2009/2010, imetolewa na imeungwa mkono.

Utaratibu wetu ni kuiamua kwa mtiririko ulioelezwa katika Kanuni ya 100 ya Kanuni za Bunge. Kwa hiyo, nitamwomba Katibu, atutajie utaratibu unaofuata sasa.

## KAMATI YA MATUMIZI

**MWENYEKITU:** Tafadhali tuketi. Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea, tumegundua kwamba, Vitabu vya Pili vya rangi kama nyeupe hivi, vina makosa; Vote 64 haionekani. Kwa hiyo, nimeagiza na mtakuwa mmegawiwa sasa. Bado? Aah! ndiyo hiyo inagawiwa. Inagawiwa karatasi ambayo inaonesha Vote ambayo ingawa imeandikwa kwenye kitabu, lakini ilikuwa inaonesha hakuna fedha. Yaani ukurasa ule unakuwa hauna tarakimu zozote; ni kosa la uchapaji na linarekebishwa.

Cha pili, ili tuendelee vizuri, naomba niwakumbushe utaratibu ambao tulikuwa tumekubaliana kwenye Kamati ya Matumizi; tunaifuata Kanuni ya 100, kwa hiyo, kila tunapofikia kasma au kifungu ambacho Mheshimiwa Mbunge anataka ufanuzi, nitamtambua ataongea kwa muda usiozidi dakika tatu na ataruhusiwa kuuliza mara moja tu na baada ya hapo basi tutakuwa tunapitisha kifungu; isitoshe ye yeyote atakayesimama kwenye Kamati ya Matumizi, hataruhusiwa kuzungumzia masuala mawili tofauti. Kwa hiyo, huwezi kusema ni hili na la pili ni hili, hapana ni moja. Baada ya ufanuzi huo, sasa Katibu utupitishe kwenye vifungu.

## MATUMIZI YA KAWAIDA

### Fungu 12 – Tume ya Utumishi wa Mahakama

Kif. 1001 - <i>Administration and General</i> ... .. ....	Sh. 570,673,000
Kif. 1002 - <i>Finance and Accounts</i> ... .. ....	Sh. 80,941,000
Kif. 1003 - <i>Procurement Management Unit</i> .....	Sh. 16,462,000
Kif. 1004 - <i>Internal Audit Unit</i> .....	Sh. 9,076,000
Kif. 1005 - <i>Recruitment, Appointment and Confirmation</i> .....	Sh. 182,443,000
Kif. 1006 - <i>Ethics and Discipline Section</i> .. ....	Sh. 218,075,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

### Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Kif.1001 - <i>Admini &amp; Human Resource Mngt</i> ...	Sh. 2,105,749,000
Kif.1002 - <i>Finance and Accounts Units</i> ... .. ....	Sh. 245,112,000
Kif.1003 - <i>Planning Division</i> .. .. ....	Sh. 371,239,000
Kif.1004 - <i>Internal Audit Unit</i> ... .. ....	Sh. 126,871,000
Kif.1005 - <i>Inf, Edu and Communication</i> .. .. ....	Sh. 107,504,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif.1006 - *Legal Registry Unit*..... Sh. 236,301,000

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 1006, *item* ya *Communication and Information*. Naomba ufanuzi kuhusiana na hali ilivyo hasa kwenye *Library* ya *AG Chamber's* kwamba hali ni duni sana. Matarajio ilikuwa nione *figure* inayolinganalingana na dhamira ya kurekebisha hali hiyo, lakini hali ya *figure* hii inatia wasiwasi kidogo. Naomba ufanuzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, nadhani umewahi tu, kwa sababu hapo ni masijala sio maktaba, maktaba inakuja 1008. Nitakutambua wakati huo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif.1007 - *Procurement Management Unit* ..... Sh. 2,355,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif.1008 - *Research and Library Service Unit*..... Sh.370,350,000

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kaboyonga.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakushukuru kwa msaada wako wa kunielekeza kifungu halisi cha kuzungumzia hoja ninayotaka ufanuzi. Ufanuzi ninaouhitji hapa kama nilivosema hapo awali ni kwamba, hali ya *Library* ya *Ofisi* ya *AG Chamber's* ni duni sana na kiwango kilichowekwa hapa; hakioneshi kama kuna dhamira ya makusudi ya kutatua tatizo hili. Naomba ufanuzi.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hali ya maktaba yetu tunaitambua na ndio maana utaona kuna nyongeza hapo ya zaidi ya shilingi milioni 70. Niseme tu kwamba, sasa hivi kulingana na teknolojia, tunatumia sana MCD na mtandao katika kupata *data* hizi, hasa kule *Library*.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif.1009 - *Management Information System Unit* Sh 173,023,000  
 Kif.2002 - *Public Prosecution*..... Sh. 2,633,863,000  
 Kif. 2003 - *Legislative Drafting*..... Sh. 821,838,000  
 Kif.2004 - *Zonal Office- Arusha*..... Sh. 304,439,000  
 Kif.2005 - *Zonal Office-Dodoma*.....Sh. 166,046,000  
 Kif.2006 - *Zonal Office-Dar es Salaam*..... Sh. 506,452,000  
 Kif.2007 - *Zonal Office-Iringa*..... Sh. 132,374,000  
 Kif.2008 - *Zonal Office-Moshi*.....Sh. 221,206,000  
 Kif.2009 - *Zonal Office-Kagera*..... Sh. 129,084,000  
 Kif.2010 - *Zonal Office-Mbeya*.....Sh. 218,795,000  
 Kif. 2011 - *Zonal Office-Mtwara* .....Sh. 130,992,000  
 Kif.2012 - *Zonal Office-Mwanza*.....Sh. 465,251,000  
 Kif.2013 - *Zonal Office-Ruvuma*.....Sh. 135,695,000  
 Kif.2014 - *Zonal Office-Sumbawanga*.....Sh. 118,568,000  
 Kif.2015 - *Zonal Office-Tabora*.....Sh. 399,483,000  
 Kif.2016 - *Zonal Office-Tanga*.....Sh. 252,013,000  
 Kif.3001 - *Civil and International Law Division*..... Sh. 862,589,000  
 Kif.4001 - *Constitutional Affairs and Human Rights* Sh.04,979,000

*(Vifungu viliyyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati  
 ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 18 - Mahakama Kuu**

Kif.1001 - *Administration and a General (RHC)*....Sh.3,100,463,000  
 Kif.1002 - *Arusha Zone* ..... Sh. 999,448,000  
 Kif.1003 - *Dar es Salaam Zone*.....Sh. 2,269,624,000  
 Kif.1004 - *Dodoma Zone*.....Sh. 853,126,000  
 Kif.1005 - *Mbeya Zone*.....Sh. 524, 751,000  
 Kif.1006 - *Iringa Zone*.....Sh. 202,130,000  
 Kif.1007 - *Mtwara Zone*..... Sh. 792,258,000  
 Kif.1008 - *Mwanza Zone*.....Sh. 1,445,378,000  
 Kif.1009 - *Songea Zone* .....Sh. 893,880,000

*(Vifungu viliyyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati  
 ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif.1010 - *Tabora Zone*.....Sh. 1,764,180,000

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki cha 1010, naomba ufanuzi kwenye eneo la *Rental Expenses*. Kwa hali ilivyo hapa, *rental expenses* zinazooneshwa ni shilingi 1,500,000; wakati tunaelewa kwamba, Majaji wetu hawana nyumba za Serikali pale, wanatumia nyumba za kukodisha. Kweli kwa fedha hizo tutawakodisha nyumba hawa Majaji? Naomba ufanuzi.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Majaji wa Kanda ya Tabora, wanakaa kwenye nyumba za Serikali.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif.1011 - <i>Sumbawanga Zone</i> .....	Sh. 224,890,000
Kif.1012 - <i>Bukoba Zone</i> .....	Sh. 764,553,000
Kif.1013 - <i>Tanga Zone</i> .....	Sh. 635,586,000
Kif.1014 - <i>Moshi Zone</i> .....	Sh. 904,598,000
Kif.1016 - <i>Resident Magistrate Courts</i> .....	Sh. 2,512,560,000

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

#### **Fungu 19 - Mahakama za Wilaya na za Msingi**

Kif. 1001 - <i>Administration and General</i> .....	Sh. 1,209,653,000
Kif. 1002 - <i>Districts Courts</i> .....	Sh. 3,222,382,000
Kif. 1003 - <i>Primary Courts</i> .....	Sh. 5,857,791,000

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

#### **Fungu 40 - Mahakama ya Rufa**

Kif. 1001 - <i>Administration and General</i> .....	Sh. 6,756,238,000
Kif. 1002 - <i>Finance and Accounts Unit</i> .....	Sh. 386,889,000
Kif. 1003 - <i>Internal Audit Unit</i> .....	Sh. 186,530,000
Kif. 2001 - <i>High Court</i> .....	Sh. 0
Kif. 2002 - <i>Court of Appeal Dar es Salaam</i> .....	Sh. 2,350,486,000
Kif. 2003 - <i>Arusha Zone</i> .....	Sh. 0
Kif. 2004 - <i>Dar es Salaam Zone</i> .....	Sh. 0
Kif. 2005 - <i>Dodoma Zone</i> .....	Sh. 0
Kif. 2006 - <i>Mbeya Zone</i> .....	Sh. 0
Kif. 2007 - <i>MtWARA Zone</i> .....	Sh. 0
Kif. 2008 - <i>Mwanza Zone</i> .....	Sh. 0
Kif. 2009 - <i>Tabora Zone</i> .....	Sh. 0
Kif. 2010 - <i>Tanga Zone</i> .....	Sh. 0
Kif. 2011 - <i>Primary Courts</i> .....	Sh. 0
Kif. 2012 - <i>District Courts</i> .....	Sh. 0
Kif. 2013 - <i>Kagera Zone</i> .....	Sh. 0

Kif. 2014 - <i>Ruvuma Zone</i> .....	Sh. 0
Kif. 2015 - <i>Moshi Zone</i> .....	Sh. 0

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri labda usaidie tu, maana yake sasa tunapita sifuri, sifuri, watu wasidhani kwamba mwaka huu shughuli yoyote katika vifungu hivyo vidogo?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, sasa hivi tumegawanya *Votes* hizi. Zamani zote zilikuwa zinakwenda kwenye *Vote 40*, sasa tumezigawa shughuli hizi ziko kwenye *Votesya High Court*.

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

#### **Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria**

Kif. 1001 - *Administration and General* ... ... ... Sh. 4,043,278,000

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Katika mchango wangu wa maandishi na mashauriano na Mheshimiwa Waziri, nilimweleza tatizo ambalo limejitokeza kwenye Mahakama ya Wilaya ya Kasulu, ambapo mwaka jana Mahakama ile ilivamiwa na majambazi likapigwa bomu na tangu wakati huo, Mahakama hiyo ya Wilaya imekuwa ya siri, wananchi wamezuiwa kuingia Mahakamani. Nimezungumza na Waziri, nimezungumza na District Magistrate wa Kasulu, jambo hili halipendezi. Naomba ufanuzi, kwa sababu jambo hili linakera sana na nafikiri ni jukumu la vyombo vinavyohusika; Polisi na Mahakama, kuhakikisha kwamba, Mahakama ile inaendelea kuwa ni Mahakama ya wazi na si Mahakama ya siri. Naomba ufanuzi.

**MWENYEKITI:** Nisamehe kidogo, kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri, nataka na mimi mwenyewe nielewe; unasema lilipigwa bomu halafu sasa imekuwa ya siri yanahusiana vipi?

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lilitokea tukio la aina yake kwamba, majambazi wenye mabomu ya kutupa kwa mkono, walikwenda Mahakamani wakati Mahakama inaendelea. Waziri analifahamu vizuri jambo hili, lilikuwa *very unique*. Tokea tukio lile; bahati nzuri mimi mwenyewe nilikuwa Kasulu, nilikawenda kushuhudia tukio kwa macho yangu. Tangu wakati ule, wananchi wamezuiwa kuingia Mahakama ya Wilaya ya Kasulu, kwa sababu ya tukio hilo na Mheshimiwa Waziri analifahamu kwa kirefu. Naomba ufanuzi; kwa nini wananchi wanaendelea kuzuiliwa kuingia Mahakamani?

**MWENYEKITI:** Nimekuelewa ni kwa sababu ya tishio la usalama. Mheshimiwa Waziri ufanuzi.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nimezungumza suala hili na Mheshimiwa Mbunge. Ushauri ambao mimi na yeye tulikubaliana ni kwamba, pengine sasa tuwashauri wenzetu wa Polisi katika zile Mahakama ambazo zipo kwenye sehemu hizi za mipakani, ambazo usalama wake upo tete, basi kabla ya watu kuingia Mahakamani, angalau basi wafanye upekuzi kwa ajili ya kuangalia kama hawaingii na silaha hizi za kutisha. Hili ni jambo ambalo nimelizingumza pia hata kwenye ziara zangu, baada ya kusikia tukio hili. Kwa hiyo, ni jambo ambalo tunalifanyia kazi.

**MHE LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kwa bahati mbaya, Mheshimiwa Waziri alipokuwa anajibu mchango wangu wa maandishi, hakueleza niliyokuwa nimemuuliza. Nilimwuliza kwamba, tunayo makubaliano ya kufungua Ofisi ya Wanasheria wa Serikali pale Nzega. Mwanzoni, Wizara ilisema tutafute kiwanja ili wajenge tukatafuta, wakasema pesa hawana; lakini baadae wakasema tutafute Ofisi ili Wanasheria hao, Mawakili wa Serikali waweze kuhamia pale Nzega; tumetafuta hiyo Ofisi, sasa hivi tuna mwaka mzima, Ofisi ipo tayari na tunawaomba waje. Pengine kwa sababu ya muda hakuweza kujibu; aniambie wanakuja lini hawa Wanasheria wa Serikali?

**MWENYEKITI:** Nyumba mnazo lakini sio za kuishi?

**MHE LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba na ofisi zipo.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utaratibu huu wa kufanya Mradi wa *Civilazation*, tumekwenda mpaka kwenye mikoa ambayo hatukupanga, lakini zinapojitokeza fursa kama hizo huwa tunakwenda Kahama. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Selelii kwamba, tutakwenda kwake Nzega mapema iwezekanavyo. Wanasheria wapo, tulikuwa hatuna hizo *facilities*, kwa kuwa zipo tutawapeleka tu waende wakafanye hiyo kazi.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wanawake ni kiwanda kikuu cha kuangulia wapiga kura; na kwa kuwa muda mrefu kumekuwa na Sheria zile ambazo ni kandamizi dhidi ya wanawake, ikiwemo ya mirathi na watoto kupewa Sh. 100 kama matunzo yao; tunaziomba kila wakati ziletwe Bungeni ili ziwezwe kufanyiwa marekebisho; na kwa kuwa Wizara hii ndio ambayo ina Tume ya Kurekebisha Sheria na mambo yote ya msingi katika kushughulikia Sheria; je, Wizara hii haikuweka *gender sensitive* au kuna jambo gani linaloendelea? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, Sheria kandamizi dhidi ya viwanda vyetu hivyo vilivyotajwa. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nikubaliane na utangulizi wake huo wa viwanda kandamizi, lakini pia niseme hata kwenye Ilani ya CCM, tumezungumzia kukarabati hizi Sheria kandamizi. Hizi za wanawake, ndoa na mirathi ni Sheria ambazo tunakusudia kuzikarabati. Utararibu tunaofuata kwa hivi sasa, tumeandika *Cabinet Paper* ambayo itatupa kibali cha kwenda

kukusanya maoni na mahojiano na wananchi na sababu kubwa ni kwamba, Sheria hizi zinagusa mila, dini na imani za watu mbalimbali. Ni vitu *sensitive* vinavyoguswa na ukisema umri wa kuoa au kuolewa kwa jamii yetu ni imani nzito sana kuhusu hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nilikuwa nasikiliza redio, kuna mtu amekamatwa na Polisi huko Tanga, alikuwa anataka kuoa mtoto wa miaka 17; kule ilikuwa *normal*, jamii ilishakubali na ndoa ilikuwa inafanyika. Seikali imeingilia kati, kuna mtafaruku mkubwa unaendelea kule. Nasema ni vitu *sensitive*, lazima tuvichukue kwa makini. Kwa hiyo, tunakwenda kwa wananchi, kutafuta maoni yao. Mwaka huu tutafanya *White Paper*.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, nipate ufanuzi wa jambo hili ambalo nataka kulisema. Inaonekana katika hili ambalo nataka kulisema, tayari kuna msimamo wa Serikali, kwa jinsi Waziri alivyokuwa analizungumzia. Hata hivyo, naomba nipate ufanuzi.

Katika ukurasa wa nne wa Kitabu hiki cha Bajeti cha Mheshimiwa Waziri, ameeleza juu ya marekebisho ya Sheria ya Mirathi na Ndoa na kadhalika. Katika hili amesema kuna pande mbili; kuna upande wa mila na utamaduni na kuna upande wa imani za kidini. Mimi nakubaliana naye sana kuhusu hili; lakini niongeze tu katika upande wa imani; chombo kinachohusika na suala hilo hilo wakati nazungumzia Mahakama ya Kadhi kimesema kwamba, kinaorodhesha zile Sheria na Taratibu za Dini mbalimbali za madhehebu mbalimbali za Kiislamu halafu mnapeleka Mahakamani. Kwa hiyo, inapokuja kesi, Mahakama itakuwa ina kitu kilichoandikwa. Ninapata wasiwasi, labda nichukue mfano wa South Afrika, kuchukua mfano wa Zanzibar na Kenya ambazo ni nchi moja.

Mtu akija na kesi. kwa mfano, atakayehukumu ni yule yule Jaji wa kawaida au ni Jaji, wa Kidini au Hakimu wa Kidini? Kwa sababu mambo haya siyo rahisi kama mnavyofikiria, nichukue mfano mmoja; tuseme mtu kamwacha mke wake, akasema nimekuacha talaka tatu, kwa mujibu wa Dini ya Kiislamu, talaka tatu maana yake huwezi kumuoja tena yule mpaka aolewe na mtu mwengine; lakini inategemea mazingira gani; ya ulevi, ya chuki au ya nini. Mwanachuoni peke yake ndiyo anayeweza kujua kwamba, tatalaka tatu hizi zimethibiti au hazikuthibiti. Sasa unieleze hapa huyo atakayehukumu.

**MWENYEKITI:** Kwa sababu nakueleweni vizuri, naomba Mheshimiwa Alhaj Msambya akandamize humu humo, maana yake nadhani hoja yake inafanana fanana ili Waziri aweze kuyajibu kwa pamoja. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu yeye kalizungumza hilo na kalizungumza kwa ufasaha, mimi nitakwenda sehemu nyingine. Kazungumza kwa ufasaha tu.

**MWENYEKITI:** Mradi umesimama basi, kwa hiyo, lijibiwe hili kwanza. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tuliyoyaeleza hapa ndiyo msimamo wa Serikali, lakini Mheshimiwa Mbunge asilifanye likaonekana kama ni gumu haliwezekani, si kweli. Sasa hivi pale RITA kwa mfano, wanasimamia Mirathi ya Kiislamu na anayesimamia pale si lazima awe Mwislamu, si lazima awe mwanaume, inafanyika kisheria. Sheria iko wazi, Mirathi ya Kiislamu inasimamiwa pale RITA, sasa hivi ninavyozungumza na ile ni Idara ya Serikali iko chini ya Wizara yangu. Wanasimamiwa na Sheria, wanasoma zilivyoandikwa kama dini inavyotaka, wanafanya kazi hiyo. Msilifanye likaonekana kama lina uchawi fulani, halina. (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa kuna Mbunge yejote anataka kuchangia kwenye hili? Likae hivyo kwanza. Anayependa labda alete hoja mahsususi tutaizingatia.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nilipokuwa nachangia kwa maandishi, nilielezea ukiukwaji wa haki za binadamu na Utawala Bora, ambao wanafanyiwa wananchi unaofanywa na viongozi mbalimbali kuanzia ngazi ya Vijiji mpaka Wilaya na nikaelezea ni jinsi gani ambavyo wananchi hawa wanavyoteseka hasa kupata haki zao na kwamba, Tume ya Haki za Binadamu inafanya kazi nzuri, lakini haina matawi kwenye vijiji.

Kwa hiyo, inakuwa ngumu sana mpaka mwananchi aje apate haki inachukua hata mwaka mpaka miaka miwili. Kwa hiyo, nikaiuliza Serikali kwamba, je, ina mpango wowote mahususi wa kuweza kuwa na Kamati za Haki za Binadamu kuanzia ngazi za Vijiji mpaka Wilaya angalau wananchi wapate mahali pa kupeleka matatizo yao ili kuwepo na mahusiano mazuri kati ya hiyo Kamati pamoja na Tume ya Haki za Binadamu kurahisisha utendaji wananchi waweze kupatiwa haki kirahisi na kwa muda mfupi? Ni hilo fupi, naomba ufanuzi. Ahsante.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, inafungua Matawi katika Mikoa mbalimbali. Kasi ya ufunguaji wa Matawi haya siyo nzuri. Wazo alilolitoa kwa kutumia hizo Kamati Vijijini na Wilayani, mwisho wafike kwenye Tume ya Haki za Binadamu ni zuri, nafikiri tutalichukua tukalifanyie kazi.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Wakati nachangia kwa maandishi, nilizungumzia suala zima la *Law School*. Najua kabisa kwamba, lengo la kuwepo kwa *Law School* lilikuwa ni kuwapa Shahada ya Kwanza wanafunzi wote wanaomaliza Sheria ili waweze kupata mafunzo kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule hii imeanzishwa mwaka jana, lakini katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri anasema kwamba, wanategemea kuleta Sheria hapa Bungeni ili watakaoingia katika Chuo hicho au Shule hiyo wawe ni wale Mawakili wa kujitegemea tu. Sasa suala langu ni kwamba, je, Mheshimiwa Waziri, haoni kwamba kutakuwa na *double standard* wale Mawakili wa Serikali kwa mfano kama hawatapata mafunzo hayo watakuwa tofauti kabisa na wale wa kujitegemea? Vile vile kwa mawazo

yangu, nadhani labda Waziri atufafanulie lengo la uanzishwaji wa shule hii ilikuwa ni nini na kama imeanzishwa mwaka jana tu leo tunataka kubadilisha maana yake ni nini? Kwa hiyo, nilikuwa naomba ufanuzi kwa hilo.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natumaini sitachukua muda mrefu kulieleza. Niseme kwamba, *Law Shool* ilipoanzishwa ilikuwa ni mwendelezo wa wazo la zamani la *internship*, baada ya kumaliza Digrii ya Kwanza ya Sheria. *Internship* tulianzisha mwaka 1974, bila Sheria, ilikuwa ni utaratibu wa kawaida tu wa *Administrative*, tukaifanya wakati ule wanafunzi waliokuwa wanamaliza ni kati ya 30 au 40. Kwa hiyo, ilikuwa inawezekana tukawaweka *Tanzania Legal Corporation, Judiciary* na kwa *Attorney General*; wanapitia mle, wakimaliza wote walikuwa wanaajiriwa ama na Serikali au Mashirika ya Serikali. Tumekwenda na utaratibu huo, kwa hiyo, tulipoanzisha *Law School concept* ilikuwa ni hiyo.

Tumejifunza, tumekwenda kwa wenzetu, tumepita Kenya, Uganda, Namibia na South Afrika, tumeona *Law Schools* za kule; *actually*, ni shule za ku-train *Advocates* wanaokwenda ku-practice kwenye *High Courts*. Hapa kwetu pia nimeongea hata na Jaji Mkuu anasema, ye ye kuajiri Hakimu hahitaji apitie *Law School*. Nimeongea na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, naye anasema mimi kuajiri pale *State Attorney* sihitaji apitie *Law School*, nitam-train mwenyewe katika namna yangu.

Kwa hiyo, wanaohitaji kupitia *Law School* ni wale ambao wanataka wakitoka pale waka-practice waingie kwenye soko hilo la biashara ya sheria.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchango wangu wa maandishi, nilielezea hali ya Mahakama katika Wilaya ya Longido kwamba, Wilaya ya Longido iko pembezoni, hatuna Mahakama ya Mwanzo, hatuna Mahakama ya Wilaya, katika Tarafa ya Enduimet, ambayo inapakana na Rombo. Wananchi wanapita Wilaya tano na kupita Mahakama Kuu ya Mkoa mpaka waende Monduli. Imeshindikana, wananchi siku hizi hawaendi kwa ajili ya gherama. Wanatumia mila kwa ajili ya kuamua kesi zao. Mila ambayo inagandamiza kwa upande mmoja, haitumii haki. Bajeti iliyopita nilielezea jambo hili na maana ya kuwa na Wilaya ni kuleta huduma karibu na wananchi. Sasa hatuna kabisa huduma hii ya Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kujuu Serikali inachukua hatua gani ili Wananchi wa Longido nao wapate haki, wapate Mahakama kama Wilaya nyingine kwa sababu ni shida, hatuna Mahakama za Mwanzo wala Mahakama ya Wilaya. Nataka ufanuzi.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, Mheshimiwa Laizer ameandika katika maelezo yake. Mimi nimezungumza na nimeahidi vitu viwili; nimemuhidi kwamba, kwanza, nitakwenda Longido, lakini pili, tutatafuta kwa kila namna ili tuweze kujenga Mahakama ya Wilaya pale Longido. (*Makofit*)

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, nilielezea kwamba, hali ya Jengo la Mahakama Kuu Tabora hairidhishi kabisa na hailingani na hadhi ya Mahakama Kuu. Aidha, Jengo hilo lilitirithiwa kutoka kwenye Manispaa ya Tabora, ilikuwa ni Ofisi za Manispaa. Kwa hiyo, Wizara ya Sheria ikachukua na kufanya fanya mabadiliko ili iwe Mahakama. Jengo lile halikidhi kabisa mahitaji ya shughuli za Mahakama.

Katika mchango huo nilitoa rai kwamba, ukiangalia bajeti tunayoijadili leo hapa katika shilingi bilioni 40.4 za maendeleo, shilingi 34 bilioni zinatoka nje ni msaada. Kwa utaratibu huu, hatuwezi kukidhi mahitaji ya kujenga Mahakama zetu nchi nzima kwa kuombaomba. Nimetoa rai kwamba, kwa nini tusijitazame ndani na hasa katika maeneo ambayo tunaweza tukaiga mfano tunavyojenga Chuo Kikuu cha Dodoma, tukachukua Mradi wa Kutengeneza Mahakama zetu nchi nzima, kwa utaratibu huo wa Chuo Kikuu cha Dodoma inawezekana.

Nataka nipewe ufanuzi juu ya rai hii kama anaikubali ama ina matatizo gani maana sikusikia chochote alipokuwa anajibu hoja zetu?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kaboyonga ametoa rai hiyo katika mchango wake wa maandishi na mimi nimeisoma. Kama ilivyo kwa wengine wengi, sikuweza kujibu hoja zao zote kutokana na suala la muda. Kwa mawazo yangu na wenzangu pia tulizungumza ya kwamba, ni wazo zuri sana, tutalifuatilia na wenzetu wa Hazina maana ile mikopo inayotoka NSSF na PPF na kwingine, lazima iwe *guaranteed* na Hazina.

Tutaongea nao, wakikubali kutu-*guarantee* ni mradi nzuri sana na mimi ningependa nione *Primary* za *District Courts* nzuri sana za Mkoa na Mahakama Kuu mahali popote, *by the time* naondoka hapa niseme kazi ilikuwa nzuri. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Itapendeza Waziri ukianzia Mahakamu Kuu Tabora, ndiko lilikotoka wazo sasa ndiyo hivyo tena. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Nakushukuru Mwenyekiti. Nilidhani nimerukwa. Katika mchango wangu wa maongezi na wa maandishi, ambao Mheshimiwa Waziri hakutaka kuutambua, nilizungumzia suala la *Organization of Islamic Conference*, lakini katika majibu yake Mheshimiwa Waziri hakuweza kueleza chochote kuhusu Tanzania kuijunga na *Organization of Islamic Conference (OIC)* na nikaeleza na sina haja ya kurudia sana; nchi nyingine zimejiunga na kufaidika na Taasisi hii. Hivi kuna tatizo gani ambalo pengine Serikali na Wizara wanaona kwamba Tanzania haiwezi kuijunga? Tupate ufanuzi tujue ni kwa nini Serikali haitaki au kama nilivyosema kwenye mchango wangu mpaka wenzetu wa upande wa pili wakubali?

**MWENYEKITI:** Nadhani anaeleweka, Mheshimiwa Waziri maelezo.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, Mheshimiwa Alhaj Manju Msambya, aliliandika jambo hili na alizungumza na mimi nimeliona. Nilichelea kulitolea maelezo nikijua kabisa naingia kwenye *area* ya wenzangu wa Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, ambao bado hawajatoa bajeti yao. Ngoja niseme tu na mimi nimeisoma hii *Charter of the Organization of the Islamic Conference* na ina mambo mengi, lakini moja ya *objectives* zao inasema: *to disseminate, promote and preserve the Islamic teachings and values basing on the moderation and tolerance, promote Islamic culture and safeguard Islamic heritage.* Nafikiri Serikali italiangalia, itaamua kama ingependa kujiunga au hapana.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, tusubiri.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 1002 - <i>Finance and Accounts</i>	...	...	Sh.	428,962,000
Kif. 1003 - <i>Policy and Information</i>	...	...	Sh.	618,853,000
Kif. 1004 - <i>Internal Audit Unit</i>	...	...	Sh.	205,911,000
Kif. 1005 - <i>Information Education and Communication</i>	.....	.....	Sh.	174,651,000
Kif. 1006 - <i>Procurement Management Unit</i>	...	Sh.	209,547,000	
Kif. 1007 - <i>Management Information System Unit</i>	.....	.....	Sh.	520,621,000
Kif. 2004 - <i>Public Legal Services Unit Unit</i>	...	Sh.	270,949,000	
Kif. 2005 - <i>Legal Reform Unit</i>	...	...	Sh.	404,775,000

(*Vifungu viliyyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

#### **Fungu 55 - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

Kif. 1001 - <i>Administration and General</i>	...	Sh.	2,811,052,250
Kif. 1002 - <i>Finance and Accounts</i>	...	Sh.	150,738,738,200
Kif. 1003 - <i>Internal Audit Unit</i>	...	Sh.	32,617,000
Kif. 1004 - <i>Legal Services</i>	...	Sh.	157,339,300
Kif. 1005 - <i>Procurement Unit</i>	...	Sh.	41,795,000
Kif. 1006 - <i>Management Information System Unit</i>	.....	Sh.	96,265,000
Kif. 2001 - <i>Administration Justice</i>	...	Sh.	482,723,800
Kif. 2002 - <i>Human Rights</i>	...	Sh.	298,815,400
Kif. 2003 - <i>Research and Documentation</i>	...	Sh.	238,788,600
Kif. 2004 - <i>Public Education and Training</i>	...	Sh.	145,066,650

Kif. 3001 - Zanzibar Office ... ... ... Sh. 148,567,800

(*Vifungu viliyyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

### **Fungu 59 - Tume ya Kurekebisha Sheria**

Kif. 1001 – *Administration and General* ... Sh. 1,314,657,000

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

### **Fungu 60 - Mahakama ya Kazi**

Kif. 1001 - *Administration and General* ... Sh. 986,827,000

Kif. 2001 - *Arusha Zone* ... ... ... Sh. 28,274,000

Kif. 2002 - *Dar es Salaam* ... ... ... Sh. 122,820,000

(*Vifungu viliyyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

### **Fungu 64 - Mahakama ya Biashara**

**MWENYEKITI:** Hapa Waheshimiwa ndiyo muangalie ile karatasi iliyogawiwa, kwa sababu kwenye baadhi ya vitabu hakuna tarakimu zozote, ni makosa ya uchapaji tu.

Kif. 1001 - *Administration and General* ... Sh. 1,176,095,000

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili fungu la 64 la *Commercial Court, sub-vote 220600* wameweka hapo kwa ajili ya *clothing* na *bedding*. Nilitaka kupata maelekezo hapa; kwenye *Commercial Court* vitanda ni kwa ajili ya kitu gani?

**MWENYEKITI:** Ingawa *bedding* siyo lazima iwe ni kitanda. *Bedding* inaweza kuwa ni shuka, *anyway* Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sikutegemea kwamba, Mheshimiwa Serukamba atauliza hilo. Nimfahamishe tu kwamba, katika Mahakama hizi kuna walinzi ambao wanahitaji uniform; walinzi wanahitaji viatu; na pia wakienda kule Majaji wanafikia kwenye *Rest Houses* wanahitaji hizo *bedding* na vitu kama hivyo.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, ni shuka siyo vitanda.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 90 - Mahakama ya Ardhi**

Kif. 1001 - *Administration and General* ... ... Sh. 1,144,353,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **MIPANGO YA MAENDELEO**

#### **Fungu 12 - Tume ya Utumishi wa Mahakama**

Kif. 1001 - *Administration and General* ... ... Sh. 146,789,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

#### **Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

Kif. 1001 - *Administration and Human Resources*

*Manag* ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 200,000,000  
Kif. 1002 - *Finance and Accounts Unit* ... ... Sh. 70,000,000  
Kif. 1003 - *Planning Division* ... ... ... Sh. 863,354,000  
Kif. 1004 - *Internal Audit Unit* ... ... ... ... Sh. 60,000,000  
Kif. 1005 - *Information, Education and Communication* ... ... ... ... Sh. 55,000,000  
Kif. 2002 - *Public Prosecution* ... ... ... Sh. 4,595,589,000  
Kif. 2003 - *Legislative Drafting* ... ... ... Sh. 268,434,000  
Kif. 3001 - *Civil and International Law Division* ... Sh. 1,131,830,000  
Kif. 4001 - *Constitutional Affairs and Human Rights* ... Sh. 144,151,000

*(Vifungu viliyyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

#### **Fungu 18 - Mahakama Kuu**

Kif. 1001 - *Administration and General (RIIC)* ... Sh. 1,655,998,000

Kif. 1016 - *Resident Magistrate Courts* ... ... Sh. 791,704,000

*(Vifungu viliyyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

#### **Fungu 19 - Mahakama za Wilaya na Msingi**

Kif. 1002 - <i>District Courts</i>	...	...	...	Sh.	758,481,000
Kif. 1003 - <i>Primary Courts</i>	...	...	...	Sh.	8,809,926,000

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

#### **Fungu 40 - Mahakama ya Rufaa**

Kif. 1001 - <i>Administration and General</i>	...	...	Sh.	4,894,588,000
Kif. 2001 - <i>High Court</i>	...	...	Sh.	0
Kif. 2002 - <i>Court of Appeal Dar es Salaam</i>	...	...	Sh.	1,137,374,000
Kif. 2011 - <i>Primary Courts</i>	...	...	Sh.	0
Kif. 2012 - <i>District Courts</i>	...	...	Sh.	0

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

#### **Fungu 41 - Wizara ya Katiba na Sheria**

Kif. 1001 - <i>Administration and General</i>	...	...	Sh.	3,464,552,000
Kif. 1002 - <i>Finance and Accounts</i>	...	...	Sh.	66,970,000
Kif. 1003 - <i>Policy and Information</i>	...	...	Sh.	1,053,950,000
Kif. 1004 - <i>Internal Audit Unit</i>	...	...	Sh.	36,028,000
Kif. 1005 - <i>Information Education and Communication</i>	...	...	Sh.	73,675,000.00
Kif. 1006 - <i>Procurement Management Unit</i>	...	...	Sh.	25,600,000.00
Kif. 1007 - <i>Management Information System Unit</i>	...	Sh.	318,976,000	
Kif. 2004 - <i>Public Legal Services Unit</i>	...	...	Sh.	100,000,000
Kif. 2005 - <i>Legal Reform Unit</i>	...	...	Sh.	5,511,545,000

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

#### **Fungu 55 - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

Kif. 1001 - <i>Administration and General</i>	...	...	Sh.	541,054,000
Kif. 1004 - <i>Legal Services</i>	...	...	Sh.	734,080,000

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

#### **Fungu 59 - Tume ya Kurekebisha Sheria**

Kif. 1001 - <i>Administration and General</i>	...	...	Sh.	1,160,473,000
---	-----	-----	-----	---------------

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 60 - Mahakama ya Kazi**

Kif. 1001 – *Administration and General* ... ... Sh. 626,410,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 64 - Mahakama ya Biashara**

Kif. 1001 - *Administration and General* ... ... Sh. 607,576,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 90 - Mahakama ya Ardhi**

Kif. 1001 - *Administration and General* ... ... Sh. 532,727,994

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Kuna ombi la mwongozo, Mheshimiwa Anna Abdallah.

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokuwa tunapitisha Vote 59 - *Law Reform Commission*, mimi kitabu changu hakina jambo lolote kiko *blank* kabisa. Kwa hiyo, hicho kilichosemwa huku sisi hatukupata hata hiyo iliyogawiwa. Kwa hiyo, tungependa tupatiwe.

**MWENYEKITI:** Nadhani ni bahati tu lakini imegawiwa.

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Wengine tumegawiwa ile nyingine tu, lakini hapa hakuna.

**MWENYEKITI:** Ilipaswa zigawiwe zote mbili na hii ya kifungu cha 59 tunayo hapa. Basi ni bahati mbaya, mngetafuta hii ya Kitabu cha Nne, naona sehemu nyingine mmepeleka ya Kitabu cha Pili bila Kitabu cha Nne. Mpatieni Mheshimiwa Anna Abdallah. Haya Bunge linalrudia.

(*Bunge lilirudia*)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka 2009/2010, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila ya mabadiliko. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba, makadirio haya sasa yakubaliwe na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)  
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria  
kwa Mwaka 2009/2010 yalipitishwa na Bunge*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyio mbele yetu ni kukubali kuyapitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Ahsante sana, hoja imepitishwa, walioafiki wameshinda. (*Makofî*)

Kwa hiyo, nafurahi kuliarifu Bunge na kuwaarifu Wananchi kupitia Bunge kwamba, Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka 2009/2010, yamepitishwa rasmi na Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, leo tarehe 30 Juni hapa Dodoma. Tunawatachia wote mnaohusika na matumizi haya, yaweze kutenda kazi ambayo Wananchi wanaitarajia. Tunawatachia kheri katika mwaka wa fedha unaokuja.

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo machache tu. Kwanza, Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameondoka mchana huu kwa ziara Kaskazini ya Nchi na ameniarifu kwamba, Shughuli za Serikali humu Bungeni, ataziongoza kwa niaba yake Mheshimiwa Mohammed Seif Khatib, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano). Tunamtazamia Mheshimiwa Waziri Mkuu, kurejea keshokutwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Khatib atakaa hapo alipo hadi keshokutwa nadhani. Nakutakia kheri katika shughuli hizi.

Nilikuwa namtazamia Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, aliniaga kwamba angerejea leo, lakini hakurejea. Kwa hiyo, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis,

anaendelea kuongoza Kambi ya Upinzani. Naye namtakia kheri, mambo haya ni magumu, basi ye ye ndiyo kama ukiwa na suala lolote linalohusu Kambi ya Upinzani, basi anasimamia. Nakutakia kazi njema. (*Makofi*)

Pamoja na wageni waliotambulishwa, wapo Wawakilishi 50 kutoka Asasi Zisizo za Kiserikali (AZAKI), ambao wameungana nasi jioni hii. Ningombal pale walipo wasimame; tafadhalili wale wa AZAKI. Alaa! kumbe wametoka. Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kwa ajili tu ya kupanga shughuli zenu vyema, nawaarifu kwamba, Siku ya Jumamosi tarehe 4 Julai, 2009, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TICRA), itafanya Semina katika Ukumbi wa Pius Msekwa, kwa ajili ya Wabunge wote. Nakuombeni kwa kuwa hatuna shughuli nydingine ya Bunge siku hiyo, semina itakuwa saa nne asubuhi Ukumbi wa Pius Msekwa. Semina ya Mamlaka ya Mawasiliano kuhusu utekelezaji wa Mpango Mpya wa Kitaifa, Mpango Kabambe wa Kitaifa wa Mawasiliano na pia Mpango wa *Post Code*, nashindwa kutafsiri mpango wa *Post Code*. Kwa hiyo, tutayaona huko na taarifa ya awali tu, Jumamosi inayofuata, EWURA nao watafanya Semina kwa Wabunge wote. Kwa hiyo, Jumamosi hapana, hii itafanyika Jumapili kwa sababu Jumamosi kuna shughuli nydingine. Kwa hiyo, Semina ya EWURA itakuwa Siku ya Jumapili tarehe 12 Julai, hii ya TICRA Mamlaka ya Mawasiliano ndiyo Jumamosi ijayo tarehe 4 Julai, 2009.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, nawatakia jioni njema na kesho tutaanza Wizara ya Miundombinu kwa siku mbili. Kwa hiyo, sasa naliahirisha Bunge hadi hapo kesho saa tatu asubuhi.

(*Saa 01.36 usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumatano,  
Tarehe 1 Julai, 2009 Saa Tatu Asubuhi*)

